

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA SABA

Kikao cha Pili – Tarehe 6 Aprili, 2022

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Mwenyekiti (Mhe. David M. Kihenzile) Alisoma Dua

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Katibu!

NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na: -

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, WENYE ULEMAVU
(MHE. PASCAL P. KATAMBI):**

Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

**MHE. AGNES E. HOKORORO K.n.y. MWENYEKITI WA
KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka wa fedha 2021/2022; pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

MHE. JONAS W. MBUNDA K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022; pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mfuko huo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

MHE. DKT. ALLICE K. KAIJAGE - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MASUALA YA UKIMWI:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu (Tume ya Uratibu na Udhibiti wa UKIMWI) kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022; pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

MWENYEKITI: Ahsante sana. Katibu!

NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tunaingia kwenye hoja ya maswali tutaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Muuliza swali wa kwanza ni Mheshimiwa Joseph Kizito Mhagama Mbunge wa Madaba.

Na. 11

Ujenzi wa Stendi ya Mabasi ya Madaba

MHE. JOSEPH K. MHAGAMA aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itasaidia ujenzi wa Stendi ya Madaba ikizingatiwa kwamba stendi hiyo ipo kwenye eneo la kimkakati?

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais TAMISEMI, Mheshimiwa David Silinde majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE) alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Joseph Kizito Mhagama, Mbunge wa Jimbo la Madaba kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu wa Halmashauri ya Wilaya ya Madaba kuwa na stendi ya mabasi katika Mji wa Madaba ili kuboresha upatikanaji wa huduma na kuongeza mapato ya Halmashauri hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Madaba katika mwaka wa fedha 2018/2019 iliandaa na kuwasilisha Serikali Kuu andiko la Mradi wa Kimkakati kwa ajili ya ujenzi wa stendi ya mabasi ambalo halikukidhi vigezo. Aidha, katika mwaka wa fedha 2022/2023 Halmashauri ya Wilaya ya Madaba imepanga kutumia Shilingi Milioni Tano, kwa ajili ya kukamilisha upembuzi yakinifu (*feasibility study*) kwa ajili maandalizi ya andiko la mradi wa ujenzi wa stendi litakalowasilishwa Serikali Kuu ili iweze kutafuta fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo wa kimkakati.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Dokta Joseph Kizito Mhagama swali la nyongeza.

MHE. JOSEPH K. MHAGAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninaishukuru Serikali kwa majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imepita miaka minne tangu Serikali Kuu ilipobaini kwamba andiko la mradi wa Stendi ya Madaba halikukidhi vigezo. Ni hatua gani za haraka ambazo Serikali Kuu ilizichukua wakati huo ili kuhakikisha kwamba stendi hii inajengwa na inawanufaisha wananchi wa Madaba ili kuongeza mapato kwa Halmashauri ya Wilaya ya Madaba?

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili kama upembuzi yakinifu unakusudiwa kufanya wa kwenye bajeti ya mwaka 2022/2023, ni lini sasa kwa uhakika stendi ya Madaba itajengwa? (*Makof*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri David Silinde majibu kwa ufupi.

NABU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naomba kujibu maswali madogo mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Dkt. Joseph Kizito Mhagama, Mbunge wa Jimbo la Madaba kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge aliuliza tu kwamba andiko la awali ambalo limechukua takribani miaka minne na alichotaka kufahamu ni hatua gani ambazo Serikali ilizichukua baada ya hili andiko kukataliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi ambacho tulikifanya kwa kutumia wataalam wetu tulilirudisha lile andiko katika Halmashauri ya Madaba na baada ya kufanya hivyo waliainishiwa maeneo ya kufanya marekebisho. Kwa hiyo, jukumu la kuandika andiko ni la Halmashauri ya Madaba na ndio maana hata sasa hivi tumewarejea tena ili waandike upya haraka iwezekanavyo ili sisi tutafute fedha hii stendi iweze kukamilika. Kwa hiyo, mara watakapokuwa wamekamilisha kwa wakati basi na sisi tutatafuta fedha ili tuweze kujenga stendi hiyo kwa manufaa ya wananchi wa Madaba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili kuhusu upembuzi yakinifu mara utakapokamilika ameuliza lini, ni kwamba watakavyomaliza andiko na mimi naamini tutajiridhisha kwamba kama andiko linakidhi vigezo likishakamilishwa mara baada tutakapopata fedha tutaanza mara moja kuhakikisha mradi ule unaanza. Ahsante. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante. Nimekuona Mheshimiwa Ndaisaba swali la nyongeza.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

MHE. NDAISABA G. RUHORO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa fursa hii ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuiuliza Serikali ni lini itaisaidia Wilaya ya Ngara kuweza kujenga stendi mpya na ya kisasa? Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

NABU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Ndaisaba George, Mbunge wa Ngara kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, anachotaka kujua tu ni lini tutawasaidia kujenga stendi mpya na naamini kwamba moja ya miradi ya kimkakati katika Halmashauri nyingi ni pamoja na kuwa na stendi mpya. Kwa hiyo, kama Halmashauri yake itakuwa imewasilisha andiko maana yake kazi kubwa ambayo tunaifanya sasa ni kutafuta fedha, mara tutakapopata fedha maana yake ujenzi huo na wenyewe utaanza. Ahsante sana. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Neema Lugangira swali la nyongeza.

MHE. NEEMA K. LUGANGIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kufahamu hivi karibuni Makamu wa Rais alivyokuwa pale Bukoba Mjini aliwasilisha ahadi ya Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan, kwamba Bukoba Mjini sasa tutajengewa stendi kuu ya mabasi. Kwa hiyo, ninataka kufahamu ni lini hiyo ahadi itatekelezwa na Bukoba tutapata stendi kuu ya mabasi ili kufungua Mkoa wetuwa Kagera na nchi za jirani? (*Makofii*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NABU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naomba kujibu swalii dogo la nyongeza la Mheshimiwa Neema Lugangira Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kikubwa ambacho Wabunge wote wanapaswa kufahamu wakiwemo Mheshimiwa Neema Lugangira ni kwamba ahadi zote za Viongozi zipo katika hatua ya utekelezaji. Kikubwa tumeshazainisha, tumeshazipa vipaumbele, jukumu letu sasa hivi ni kutafuta fedha kuhakikisha hizo ahadi zinatekelezeka.

Kwa hiyo, pesa itakapokuwa imepatikana hii ahadi ya Makamu wa Rais na yenyewe itatekelezeka kama ambavyo ameahidi. Kikubwa ni kwamba ahadi zote za viongozi zitatekelezwa. Ahsante. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante. sasa nimemuona Mheshimiwa Kuchauka amesimama muda mrefu swalii la nyongeza la tatu.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, asante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swalii la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Liwale ilikuwa na mradi wa kimkakati wa stendi lakini fedha zililetwa zikarejeshwa baada kukwama kwenye manunu.

Je, fedha zile zitarejeshwa lini ili mradi ule uendeleee?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NABU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naomba kujibu swalii dogo la nyongeza la Mheshimiwa Kuchauka Mbunge wa Jimbo la Liwale kama ifuatavyo:-

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla hatujababidilisha sheria na ninyi mnakumbuka mwaka jana, fedha zote ambazo zilikuwa zinavuka mwaka zilikuwa zinarejeshwa Hazina, maana yake mnatakiwa kuanza kuomba upya.

Kwa hiyo, nimwambie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba nimesikia maombi hapa ambayo ameyainisha na tutakwenda pale Ofisi ya Rais, TAMISEMI ili kuona namna bora ya kusaidia kwa zile fedha ambazo awali zilikuwa zimeshapelekwa. Ahsante sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Tunaendelea na Wizara ya TAMISEMI, sasa namwita Mheshimiwa Emmanuel Peter Cherehani, Mbunge wa Ushetu aulize swali lake.

Na. 12

Ujenzi wa Kituo cha Afya Ulowa-Ushetu

MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi ya Waziri Mkuu aliyoitoa mwaka 2017/2018 ya Ujenzi wa Kituo cha Afya Ulowa katika Jimbo la Ushetu?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri usiondoke mpaka majibu yakamilike, *okaysawa majibu*.

NABU WAZIRI, OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Emmanuel Peter Cherehani, Mbunge wa Jimbo la Ushetu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea kutekeleza ahadi mbalimbali zinazotolewa na viongozi wa Kitaifa kote nchini ikiwemo ahadi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ya ujenzi wa Kituo cha Afya katika jimbo la Ushetu.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali katika mwaka wa fedha 2021/2022 inaendelea na mpango wa kutafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi wa vituo vya afya kwenye maeneo ya kimkakati yenye uhitaji mkubwa nchini kote ikiwemo Kituo cha Afya cha Ulowa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Cherehani swali la nyongeza.

MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, ahadi hii sasa ina miaka Sita na inaenda mwaka wa Saba, ahadi zote zinazotolewa na Viongozi wetu wa Kitaifa wanatoa kwa sababu ya hali ilivyo ngumu kwenye Majimbo yetu yaliyo mengi. Ninavyo jua kwa Viongozi wa Kitaifa ni sehemu ya maelekezo ya Serikali, ahadi hii hata hayati marehemu John Kwandikwa alifuatilia sana lakini utekelezaji wake mpaka leo haujafanyika.

Je, ni nini kauli ya Serikali juu ya ahadi hii na kwa nini Serikali isitafute fedha za ziada kuhakikisha kituo cha afya hiki kinajengwa?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri TAMISEMI, Mheshimiwa David Silinde majibu yanayoashiria ni lini jambo hili litatekelezeka maana hata Kwandikwa alikuwa ameahidiwa, majibu.

NABU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Emmanuel Peter Cherehani, Mbunge wa Jimbo la Ushetu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, alichoeleza ni kwamba hii ilikuwa ni ahadi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, nieleze tu Bunge lako tukufu kwamba moja ya mpango mkubwa wa Serikali ambao ulikuwepo awali ni kuhakikisha kwamba zile Tarafa zote nchini ambazo hazikuwa na vituo vya afya tulikuwa tunapeleka vituo vya afya, ndiyo maana katika mwaka wa fedha huu unaokwenda kuisha Serikali imepeleka fedha

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

zaujenzi wa vituo vya afya 233 ikiwemo katika Jimbo la Ushetu ambapo tumepeleka fedha awamu ya kwanza, fedha za tozo Milioni 250 kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya ambacho wao wamepeleka katika eneo lingine.

Meshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo katika eneo hili ambalo liko katika ahadi baada ya kumaliza huu mkakati ambaao tumeuainisha kumaliza Tarafa zote nchini basi na eneo lako tutaliweka katika kipaumbele kuhakikisha kwamba hii ahadi haichukui muda mrefu ili kuwasaidia wananchi wa Kata ya Ulowa. Ahsante sana. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante. Nimekuona Mheshimiwa Mwakasaka.

MHE. EMMANUEL E. MWAKASAKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo la Tabora Mjini wananchi kwa nguvu zao wamejitahidi sana kujenga vituo vya afya ambavyo vingi viko kwenye maboma lakini wengine wamekusanya mawe na kujitolea nguvu zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina mpango gani wa kusaidia kumalizika kwa hivi vituo vya afya ambavyo wananchi wamejitoa nguvu zao?

MWENYEKITI: Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri TAMISEMI.

NABU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Mwakasaka, Mbunge wa Tabora Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Serikali inatambua maeneo mbalimbali nchini ikiwemo Tabora Mjini wananchi wameshiriki kwa nguvu zao kuchangia ujenzi wa

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

vituo vya afya na maboma yako mengi karibu kila Mbunge hapa anaweza kuyaainisha. Kwa hiyo, wakati wa sasa ukiwa ni mpango wa kuhakikisha kwamba Halmashauri zote zinapata hospitali za Wilaya, ambapo tulikuwa na Halmashauri 28 hazikuwa na hospitali za Halmashauri ambapo mwaka huu wa fedha Serikali imepeleka fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wa pili ilikuwa ni kumaliza Tarafa zote nchini, tulikuwa na Tarafa 570, karibu Tarafa 233 zilikuwa hazina ambapo Serikali tumepeleka fedha kwa ajili ya ujenzi wa maeneo hayo. Kwa hiyo, mpango wa tatu utakuwa sasa ni kwenda kumalizia katika yale maeneo ambayo wananchi wameweka nguvu zao. Kwa hiyo, haya masuala ni yanakwenda kwa mipango na kwa muda kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inalitambua hilo na tutatenga fedha kwa ajili ya kuhakikisha kwamba tunapeleka fedha ku-support wananchi nguvu zao walizozitoa. Ahsante sana.(*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Festo Sanga.

MHE. FESTO R. SANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naomba kuuliza swali dogo la nyongeza kwamba Tarafa ya Matamba kuna kituo cha afya cha Matamba kina takribani miaka 30, hakina jengo la Mama na Mtoto na wala hakina jengo la mochwari. Huduma ya mochwari tunaenda kupata kwenye Wilaya ya jirani inaitwa Chimala. Sasa tunaomba ni lini Serikali itatupatia fedha tuweze kujenga jingo la mama na mtoto lakini eneo la kuhifadhi wenzenetu kwa maana ya mochwari, kwa sababu ni umbali mrefu tunaenda kuhudumiwa kutoka kwa Jirani?

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge maswali yetu yatakuwa ni mafupi na Mheshimiwa Naibu Waziri ataendelea kujibu kwa ufupi zaidi ili kutoa fursa kwa Wabunge wengi kuweza kuuliza maswali, majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

NABU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naomba kujibu swali dogo la

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

nyongeza la Mheshimiwa Festo Sanga Mbunge wa Jimbo la Makete kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ameainisha kwamba Tarafa ya Matamba ina kituo cha afya lakini hakina huduma ya mochwari pamoja na mama na mtoto, kwa hiyo alichoomba tu ni kwamba Serikali lini tutapeleka fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwambie tu kwamba tumelipokea hili ombi na tutaliweka katika mipango yetu ya baadaye ili tuhakikishe kwamba hizi huduma mbili ambazo ameziainisha Mheshimiwa Mbunge zinapatikana. Ahsante. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Nimekuona Mheshimiwa Paresso.

MHE. CECILIA D. PARESSO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mipango ambayo Serikali imeainisha hapa ya ujenzi ya vituo vya afya lakini hakuna mpango wa wazi wa kuonesha namna gani sasa tunajenga vituo vya afya lakini tunaajiri watumishi wa sekta ya afya tukizingatia kwamba tuna upungufu wa takribani asilimia 50 ya watumishi wa afya kwenye sekta zetu za afya? (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

NABU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Cecilia Paresso Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Serikali inajenga na moja ya mkakati tulionao ni kuajiri na hata katika mwaka huu wa fedha nafikiri kama wiki ijayo Mheshimiwa Waziri wa Nchi atatangaza nafasi za ajira ambazo tutakwenda kuajiri

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

katika maeneo haya ya afya pamoja na elimu. Kwa hiyo, nimhakikishie tu kwamba Serikali imejipanga kuajiri na Waziri wa Nchi atatangaza hilo. A sana. (*Makof*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Dkt. Chaya swali la nyongeza.

MHE. DKT. PIUS S. CHAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa hii nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo la Manyoni Mashariki tuna Kituo cha Afya cha Kintiku ambacho tayari Serikali ilishajenga jengo la maabara, jengo la x-ray, wodi ya mama na mtoto na mochwari, lakini hatuna jengo la *OPD*. Ni nini kauli ya Serikali kuhakikisha kwamba wanatupatia jengo la *OPD*?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri endapo kama utakuwa na majibu unawenza kujibu swali la nyongeza kutoka kwa Daktari Chaya.

NABU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dokta Chaya Mbunge wa Jimbo la Manyoni Mashariki kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ameainisha kwamba katika Kituo cha Afya cha Kintiku kinachokosa tu ni jengo la *OPD* na nimhakikishie tu kwamba maeneo yote ambayo yana mapungufu na sisi tulipeleka fedha tutamaliza majengo, kwa sababu maeneo mengine yanakosa mochwari, maeneo mengine yanakosa maabara, mengine yanakosa wodi za akina mama, kwa hiyo lipo katika mpango ikiwemo katika eneo hili la Kintiku ambalo Mheshimiwa Mbunge ameliaainisha. Ahsante.

MWENYEKITI: Maswali bado ni mengi na muda wetu unakimbia. Mheshimiwa Almas Maige nakupa fursa uulize swali lako la nyongeza.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

MHE. ATHUMAN A. MAIGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Katika Kituo cha Afya cha Ukuge ulijengwa mtambo mkubwa uliokusudiwa kutengeneza *oxygen* kwa ajili ya Kanda yote ya Magharibi, lakini bahati mbaya mtambo ulipowashwa, ukawa unatengeneza *nitrogen*.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuchukua mpango huo unaotengeza *nitrogen* ili watuletee unaotengeneza *oxygen*?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, haya maswali ya nyongeza kama una majibu unaweza kutoa, lakini pia anaweza kuleta kama swali la msingi, kama huna majibu kwa sasa.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Almas Maige, Mbunge wa Tabora Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, alichokielezea kuhusu huo mtambo ili Serikali ichukue najua suala hili linahusu zaidi Wizara ya Afya. Kwa hiyo, kwa niaba ya Wizara ya Afya, tuseme tumelipokea hilo na Serikali italifanyia kazi. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Tunaendelea na Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Sasa namwita Mheshimiwa Aloyce John Kamamba, Mbunge wa Buyungu, aulize swali lake.

Na. 13

Hitaji la Watumishi wa Afya - Kakonko

MHE. ALOYCE J. KAMAMBA aliliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka Watumishi wa Afya wa Kada mbalimbali katika Wilaya ya Kakonko?

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI Mheshimiwa Silinde, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Aloyce John Kamamba, Mbunge wa Jimbo la Buyungu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2020/2021 Serikali iliajiri Watumishi wa kada za afya 2,726 ambapo Halmashauri ya Wilaya ya Kakonko ilipelekewa watumishi 24 waliopangwa kwenye vituo vya kutolea huduma za afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali katika mwaka wa fedha 2021/2022 imepanga kuajiri watumishi wa kada mbalimbali za afya kwa ajili ya kuboresha hali ya utoaji huduma za afya nchini kote ikiwemo Halmashauri ya Wilaya ya Kakonko. Aidha, Serikali kwa kushirikiana na wadau itaendelea na mpango wa kuajiri watumishi wa kada za afya kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha. (Makofii)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Aloyce John Kamamba, swali la nyongeza.

MHE. ALOYCE J. KAMAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Pamoja na majibu ambayo yametolewa na Serikali na mpango mzuri wa Serikali katika kupeleka watumishi katika maeneo mbalimbali hasa Wilaya ya Kakonko, bado watumishi hawa wamekuwa wakihama kutokana na upungufu wa miundombinu hasa nyumba za watumishi katika maeneo hayo.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba watumishi hawa wa kada ya afya wanabaki katika

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

maeneo hayo hasa kwa kujenga nyumba za watumishi hao?
(Makof)

(b) Kutokana na changamoto hiyo: Je, Mheshimiwa Waziri yupo tayari kufuatana nami kwenda Wilaya ya Kakonko ili hiki ambacho nakieleza kama changamoto aweze kuona na hatimaye aweze kutafuta njia sahihi za kuweza kumaliza changamoto hiyo? Nashukuru. *(Makof)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba kujibu maswali madogo mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Aloyce John Kamamba, Mbunge wa Jimbo la Buyungu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza Mheshimiwa Mbunge ameainisha kwamba tunapeleka watumishi katika maeneo kama Buyungu, Halmashauri ya Kakonko, lakini asilimia kubwa ya hawa watumishi wamekuwa wakihamia.

Kwa hiyo, alichokuwa anaainisha Mheshimiwa Mbunge ni kutaka Serikali moja, tujenge nyumba za watumishi ili watu wabaki; nafikiri kuongeza zile *incentives* kwa ajili ya watumishi wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya mkakati wa Serikali sasa hivi ni kuhakikisha watumishi wote wapya tunaowaajiri hawaruhuswi kuhama katika maeneo yao, walau siyo chini ya miaka mitatu. Hiyo ni moja ya sehemu ya mikataba ambayo tumeiweka. Kwa hiyo, tutaendelea kuboresha mazingira kwa kutenga fedha ili kujenga nyumba za watumishi na kuongeza mahitaji mengine ambayo wanayahitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili la kwenda Kakonko, niko tayari, hiyo nguvu ninayo na uwezo ninao na tuko tayari kwa ajili ya kuwatumikia. Ahsante sana.
(Makof)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

MWENYEKITI: Ahsante, nimekuona Mheshimiwa Sanga Mbunge wa Makambako.

MHE. DEO K. SANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa Serikali ya Awamu ya Sita imefanya kazi nzuri ya kutuletea fedha za kujenga vituo vya afya na hospitali za Halmashauri: Je, katika Kituo cha Afya cha Lyamkena na Hospitali iliyoko Mlowa katika Mji wa Makambako, inafanya kazi na inahudumia wagonjwa asubuhi mpaka jioni; ni lini Serikali italeta watumishi ili kiweze kuhudumia masaa 24? (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, kama una majibu kwa Mheshimiwa Sanga.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba kujibu swali la Mheshimiwa Deo Sanga, Mbunge wa Makambako, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ambacho ameomba tu ni watumishi na katika jibu la msingi nililolijibu awali ni kwamba Serikali inatarajia kuajiri na tangazo la ajira litatolewa na Waziri wa Nchi na nafikiri inawezekana ikawa kabla ya wiki ijayo. Mara atakapolitoa, ajira zitakavyoombwa, sehemu ya watumishi tutakaowaajiri, baadhi tutawapeleka katika eneo hilo ili kuweza kusaidia. Ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante, naamini mtawapeleka na Mufindi Kusini pia. Bado niko upande huu, nimekuona Mheshimiwa Lucy Sabu, Mbunge wa Viti Maalum kutoka Mkoa wa Simiyu. (*Kicheko*)

MHE. LUCY J. SABU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naomba niulize swali dogo la nyongeza.

Je, ni lini Serikali itapeleka mtaalam wa meno katika Hospitali ya Somanda Wilaya ya Bariadi kwa kuwa aliyejukwepo amestaafu? Ahsante.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

MWENYEKITI: Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri, kuhusu mtaalam wa meno.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE): Mheshimiwa Mwenyeekiti, ahsante sana. Naomba kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Sabu, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyeekiti, anachohitaji ni mtaalam wa meno na ninaamini tunapokuwa tunaajiri, tunazingatia maeneo yenye upungufu. Kwa hiyo, ninaamini pamoja na eneo analolitaja, litakuwa katika hizo sehemu za ajira ambazo zitatangazwa. Ahsante sana. (Makofii)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Florent Kyombo, Mbunge wa Nkenge.

MHE. FLORENT L. KYOMBO: Mheshimiwa Mwenyeekiti, ahsante. Pamoja na pongezi kubwa kwa Serikari kwa ujenzi wa vituo vya afya unaoendelea sasa, vipo vituo vya afya ambavyo vimejengwa kipindi cha nyumba lakini mpaka sasa havina watumishi wa kada ya afya wa kutosha:-

Je, ni lini sasa Serikali itapeleka watumishi hao ili wananchi wapate huduma inayostahili? Ahsante.

MWENYEKITI: Naona suala la watumishi limerudiwa sana. Mheshimiwa Naibu Waziri unaweza ukalijibu kwa jumla kwa ajili ya Wabunge wote ili lisijirudie tena kwenye *section* hii?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE): Mheshimiwa Mwenyeekiti, ahsante sana. Naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Kyombo, Mbunge wa Nkenge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyeekiti, naomba nilijibu swalii hili kama ulivyoelekeza. Tunatambua kwamba kuna changamoto ya ubaha wa watumishi katika kada ya Afya.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Moja ya mikakati ni pamoja na Serikali kuajiri. Katika mwaka wa huu wa fedha 2021/2022 Serikali inatarajia kuajiri. Waziri wa Nchi atakapokuwa ametangaza ajira hizi, maana yake tutaainisha na kupeleka maeneo yale ambayo yana uhaba mkubwa wa watumishi kuhakikisha kwamba huduma za afya huduma za Afya zinaanza. Kwa hiyo, hilo ndilo jibu la msingi na niwahakikishie tu Waheshimiwa Wabunge kwamba tutazingatia maeneo yote ambayo hayana watumishi. Ahsante sana. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante. Nimekuona Mhesimiwa Dkt. Kimei.

MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI: Mhesimiwa Mwenyekiti, namshukuru Waziri kwa kuwa muwazi na kuwa mtu mzuri. Alitembelea Vunjo baada ya kuahidi hapa.

Mhesimiwa Mwenyekiti, swali langu ni hivi, je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi yake ya kuinua hadhi ya *OPD* Himo kuwa Kituo cha Afya kwa kutekeleza majengo matatu yanayostahili pale, pamoja na watumishi wanaohitajika?

MWENYEKITI: Mhesimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE): Mhesimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba kujibu swali la Mhesimiwa Dkt. Kimei, Mbunge wa Vunjo, kama ifuatavyo:-

Mhesimiwa Mwenyekiti, ambacho anahitaji tu ni kwamba kwenye eneo hilo la Himo tupandishe hadhi, tuongeze watumishi, tujenge jengo la *OPD* na anachotaka kufahamu tu, ni lini sasa ile huduma ambayo ameikusudia Mhesimiwa Mbunge itatekelezeka?

Mhesimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba Serikali imelipokea na tutalifanya kazi kwa sababu Serikali ya Awamu ya Sita moja ya ajenda yake kubwa kabisa ni kuhakikisha tunaboresha huduma za afya nchini. Ahsante sana.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, naona umesimama.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naomba nimpongeze sana Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Nimesikiliza hapa maswali kwenye Ofisi ya Rais, TAMISEMI takribani Wabunge wengi ambao wamekuwa wakiuliza maswali ya nyongeza wamekuwa na hofu ya uhaba wa watumishi na hasa kwenye sekta ya elimu na sekta ya afya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasimama hapa kwa heshima kubwa ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, naomba niwaarifu Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Rais na Serikali yake wametambua tatizo hilli la uhaba wa watumishi na hasa kwenye miradi ya sekta ya afya na sekta ya elimu. Hivyo basi, Mheshimiwa Rais ametoa kibali. Ahadi ya Serikali kwa mwaka huu wa fedha ilikuwa tuajiri watumishi 44,000; tayari Serikali ilishaajiri watumishi wapya na wa ajira mbadala 12,000. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwathibitishie Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Rais ameridhia na wiki ijayo nitatoa tangazo rasmi la ajira 32,000 na utaratibu wa ajira hizo na mgawanyo wake katika sekta ambazo zinaongoza kwa uhaba wa watumishi, maelezo yote nitayatoa wiki ijayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge, Serikali ya Awamu ya Sita inajali tatizo la uhaba wa watumishi nchini. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Jenista Mhagama kwa kauli hiyo ya Serikali, kwa sababu kuna changamoto kubwa sana ya watumishi. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Nakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri Silinde kwa majibu mazuri sana. Ahsante sana. Unaweza kwenda kuketi sasa. (*Makof*)

Tunakwenda Wizara ya Mifugo na Uvuvi, namwita Mheshimiwa Regina Ndege Qwaray, Mbunge wa Viti Maalum kutoka Manyara, aulize swali lake. Mheshimiwa Flatei Massay atauliza swali kwa niaba yake. (*Makof*)

Na. 14

Kujenga mabwawa ya kunyweshea mifugo katika kila Kijiji nchini

MHE. REGINA N. QWARAY aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuchimba mabwawa ya kuhifadhi maji kwa ajili ya kunyweshea mifugo katika kila Kijiji nchini?

MWENYEKITI: Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Abdallah Ulega, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Regina Ndege Qwaray, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkakati wa Serikali ni kuhakikisha maeneo yenye mifugo mingi na yale yaliyoathirika na ukame mara kwa mara yanakuwa na miundombinu ya maji yakiwemo mabwawa kwa ajili ya maji ya mifugo. Katika kutekeleza mkakati huo, mwaka wa fedha 2021/2022 Serikali imetenga shilingi bilioni 2.146 kwa ajili ya uchimbaji na ujenzi wa mabwawa au malambo na visima virefu vya maji kwa ajili ya mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kutenga fedha za kuchimba, kujenga na kukarabati mabwawa ama

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

malambo na visima virefu kulingana na upatikanaji wa fedha. Aidha, napenda kutoa wito kwa Halmashauri za Wilaya, wafugaji na wadau wengine kuchimba na kujenga malambo au mabwawa, visima virefu kwa ajili ya maji ya mifugo. Pia, nahimiza wafugaji kuwa na vyanzo vyao binafsi nya maji kwa ajili ya mifugo yao.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Flatei Massay, swali la nyongeza.

MHE. FLATEI G. MASSAY: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na majibu haya ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shilingi bilioni mbili aliyoisema kwenye majibu yake ya msingi, ni ndogo sana kutokana na swali lilivyoullizwa wa kila Kijiji kuchimbwa mabwawa.

Je, Serikali ina mpango gani sasa kuongeza bajeti ili maeneo haya anayoyasema yaweze kuchimbwa mabwawa? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; tumeleta maombi ya Mbulu Vijijini kuchimbiwa mabwana katika vijiji nya Gidihim, Eshkesh, Yaeda, Masieda na Endagichan na wewe Naibu Waziri unafahamu: Lini mtatuchimbia hayo mabwawa kama tulivyoomba?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Flatei Massay. La kwanza ni juu ya kuongezwa kwa bajeti. Nimelipokea jambo hili na kwa kuwa sasa ndo tuko kwenye Bunge la Bajeti, namwomba Mheshimiwa Flatei Massay na Waheshimiwa Wabunge wengine, tusiwhishe shughuli; tusubiri, nina imani mambo mazuri yanakuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni hivi vijiji vyake alivyovitaja. Naomba mimi na yeche tuzungumze mara baada

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

ya hapa kuona namna ambavyo tunaweza kujipanga kwa ajili ya kutekeleza kile alichokiomba. Ahsante. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Rashid Shangazi, Mbunge wa Mlalo.

MHE. RASHID A. SHANGAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa nafasi hii. Serikali iliwaahidi wananchi wa Kijiji cha Kivingo Kata ya Lunguza amba wako pembezoni mwa hifadhi ya Taifa Mkomazi, kuwajengea bwawa kwa ajili ya shughuli za kilimo na lambo kwa ajili ya shughuli za ufugaji; na Mamlaka ya Hifadhi Tanzania (*TANAPA*) ilikuwa imeanza huo mchakato. Sasa ni lini Serikali itahakikisha kwamba bwawa hili linachimbwa na lambo kwa ajili ya mifugo linapatikana?

MWENYEKITI: Naibu Waziri, Mheshimiwa Abdallah Ulega, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swalii zuri la Mheshimiwa Rashid Shangazi, Mbunge wa Mlalo juu ya ahadi iliyotolewa na Shirika letu la *TANAPA* kuhusu kujenga lambo katika Kijiji cha Kizingo pembedi ya hifadhi ya Taifa ya Mkomazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Serikali tunafanya kazi kwa pamoja na *TANAPA* ni chombo chetu, naomba nimwahidi Mheshimiwa Mbunge ya kwamba nitazungumza na Mheshimiwa Waziri wa Maliasiri na Utalii tuwakumbushe *TANAPA* tuweze kuifanya kazi hii ya wananchi. Ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Boniphace Getere, Mbunge wa Bunda.

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swalii la nyongeza. Naishukuru Wizara ya Mifugo na Uvuuvi. Miezi michache iliyopita Waziri wake alifika kwenye Jimbo langu akaangalia hatari kubwa ya lambo la Salamakati ambalo bado kidogo sana kutoweka. Kutokana na mvua zilizonyesha, lambo lile

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

lina hatari kubwa sana ya kubomoka lote. Mheshimiwa Waziri aliahidi kuweka mikakati ya dharura ya kuziba lile lambo kabla halijabomoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kupata majibu kuna mikakati gani ya kuziba lambo la Salama ambalo liko hatarini kubomoka?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Naibu Waziri anaweza kunieleza nini kuhusu namna gani anaweza kwenda kuziba hilo lambo au kulijenga upya au kuliziba ile nyufa inayotaka kubomoka?

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza tumepokea shukrani kutoka kwa Mheshimiwa Boniphace Getere. Pili ni juu ya ukarabati wa hili lambo. Naomba nilichukue jambo hili na kwenda kulisukuma ili liweze kufanyika sawa na ahadi ya Mheshimiwa Waziri.

MWENYEKITI: Nimekuona Mheshimiwa Jackson Kiswaga, Mbunge wa Kalenga.

MHE. JACKSON G. KISWAGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swalii la nyongeza. Katika Bwawa la Mtera lilioko Halmashauri ya Iringa Vijiji kumekuwa na upungufu mkubwa wa Samaki na hivyo kuathiri biashara ya samaki katika Nyanda za Juu Kusini na masoko mengine.

Je, Serikali ina mpango gani sasa wa kujenga mashamba darasa ya samaki hasa Jimbo la Kalenga ili sasa tuweze kufundisha vijana wengi kufuga samaki na hivyo kufufua uchumi wa vijana kwa namna hiyo? Ahsante sana. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Kiswaga, Mbunge wa Kalenga, juu ya mashamba darasa ya kufugia samaki kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo *program* ambayo itakwenda katika baadhi ya Halmashauri zetu na yawezekana kabisa moja ya Halmashauri itakayofaidika na *program* hii ya mashamba darasa ya samaki ikawa ni Halmashauri ya Kalenga.

Kwa hiyo, naomba nilichukue jambo hili la Mheshimiwa Mbunge ili tuweze kulifanya kazi na wananchi wa Kalenga waweze kufaidika. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Yahaya Massare, Mbunge wa Itigi, swalii la nyongeza.

MHE. YAHAYA O. MASSARE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa nafasi. Serikali iliahidi Bwawa la Mhanga katika Halmashauri ya Itigi na wakaanza ujenzi, lakini ukasimama: Je, Waziri yuko tayari kwenda nami kuona utekelezaji wa ahadi hii nzuri ya Serikali ili wananchi wawaonee aweze kusukuma malizio lile lambo ambalo linajengwa pale Muhamanga?

MWENYEKITI: Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri kwa ufupi.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimhakikishe kaka yangu Mheshimiwa Massare, niko tayari kwenda Itigi. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Tunaendelea na Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Sasa namwita Mheshimiwa Halima James Mdee Mbunge wa Viti Maalum, aulize swalii lake.

MWENYEKITI: Tunaendelea na Wizara ya Mifugo na Uvuvi sasa namwita Mheshimiwa Halima James Mdee, Mbunge wa Viti Maalum, aulize swalii lake.

Na. 15

Malalamiko ya Wadau wa Ngozi

MHE. HALIMA J. MDEE aliuliza:-

Je, Serikali ina kauli gani juu ya ushuru mkubwa wa bidhaa za ngozi unaotozwa bandarini na vikwazo vyatya kusafirisha bidhaa hiyo nje ya nchi?

MWENYEKITI: Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri Mifugo na Uvumi.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvumi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Halima James Mdee, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwango vyatya ushuru wa kusafirisha ngozi ghafi na ngozi iliyosindikwa kiwango cha kati kwa maana ya *Wet blue* nje ya nchi ni makubaliano ya Nchi Wanachama za Jumuiya ya Afrika Mashariki waliokubaliana kuainisha viwango vyatya ushuru kwa lengo la kuhakikisha viwanda vyatya ndani vinapata malighafi ya kutosha na kuzalisha bidhaa za ngozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushuru wa kusafirisha ngozi ghafi nje ya nchi kwa maana *export levy* ni asilimia 80 ya mzigo ukiwa bandarini kwa maana *FOB* au Dola za kimarekani 0.52 kwa kilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, ngozi zilizosindikwa kwa kiwango cha kati kwa maana ya *Wet blue* zinatozwa ushuru wa asilimia 10 ya *FOB* ili kutoa motisha kwa wasindikaji. Ngozi zilizosindikwa hadi kufikia hatua ya mwisho kwa maana ya *finished leather* hazitozwi ushuru wowote ule, ni 0%. Jithada hizo zimesaidia kuvutia uwekezaji katika viwanda vyatya kusindika ngozi na kuzalisha bidhaa za ngozi.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna vikwazo vyovoyote katika kusafirisha zao la ngozi, kwa kuwa takwimu zinaonyesha kiwango cha usafirishaji wa ngozi ghafi kimeendelea kupanda kutoka kilo 513,201 mwaka 2015/2016 hadi kufikia kilo 7,370,533 mwaka 2020/2021.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Halima James Mdee, swali la nyongeza.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa majibu ya Waziri yanakiri kwamba ushuru mkubwa ulilenga kulinda viwanda vya ndani na ni asilimia 80 ya thamani ya mzigo ukiwa bandarini, sasa kuna ushahidi ulio dhahiri kwamba viwanda vya ndani viliviyokuwa vikilindwa vingi vimekufa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna kiwanda cha Himo ambacho na chenyewe kiko hai, lakini ngozi inayohitajika ni ya *kilogram* 12 ambayo inapatikana Bukoba. Sasa swali langu kwa Serikali, wafanyabiashara wa ngozi wamekwama ushuru mkubwa, viwanda vya ndani vimekufa, Serikali haipati mapato ya kutosha. Sasa, je, kwa kuzingatia kwamba hata Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki linapokuja suala la masilahi ya ndani na yenyewe wala haitekelezi makubaliano yenu, kwa nini Serikali isifanye tathmini upya, kuangalia uamuizi wake ili kulinda wafanyabiashara wa ndani wa Ngozi na kulinda nchi? Hilo swali langu la kwanza. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa makubaliano ya Jumuiya tusitumie kama kigezo maana kuna ushahidi yanakiukwa na...

MWENYEKITI: Uliza swali la pili, uliza swali la nyongeza.

MHE. HALIMA J. MDEE: kwa nini tusitathini kwa maslahi ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, tunaingia mwaka mpya wa fedha, tunaamini Wizara ya Mifugo chini ya Mawaziri akiwemo kijana makini, hivi bado hawajafikiria

mwaka huu wa kikodi kuangalia hili eneo muhimu? Kwa sababu ni dhahiri shahiri kuna ngozi zinaoza huko mtaani kwa maelfu, hawaajaangalia hili eneo ili wasaidie nchi? (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri Mifugo na Uvubi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Halima James Mdee, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza ni juu ya tathmini Serikali kutazama kulingana na hali halisi ya biashara ya Ngozi. Nimelipokea jambo lake hili la kusema tufanye tathmini ni jambo jema.

Vilevile nimirshukuru amekiri na ndio ukweli wenyewe kwamba tumeweka viwango hivi vya kikodi ndani ya Jumuiya yetu ya Afrika Mashariki kwa lengo la kulinda viwanda vyetu vya ndani. Hii *80 percent* tuliyoiweka imewekwa makusudi kwa ajili ya ku-*discourage* kutoa ngozi ikiwa ghafi kwenda nje ya mipaka ya Taifa letu ili kulinda ajira na kupata kipato zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, niseme ukweli bado ngozi nydingi inakwenda nje ikiwa ghafi, pamoja na ushuru huo mkubwa inakwenda Nigeria, Ghana ambako huko wanaitumia kama chakula, kwa hiyo hili lifahamike. Hii ngozi tunayosema kwamba iko vijiji inaharibika, inawezekana lakini kwa uhitaji wa ngozi wa sasa jambo la ngozi kuharibika ni kiasi kidogo sana, yawezekana wahitaji wanaohitaji hizi ngozi hawajaweza kuviflikia vile vijiji ambavyo vina hiyo ngozi inayoharibika. Hata hivyo, niseme tu kwamba tutaimarisha sasa mfumo wetu ili hata ile iliyoko kule vijiji inaweze kapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, amezungumza juu ya maboresho ya kikodi. Hili jambo pia vilevile nimelichukua, kwa ajili ya kuweza kuangalia maslahi mapana ya sekta hii ya ngozi.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

MWENYEKITI: Tunakushukuru kwa majibu Mheshimiwa Naibu Waziri, sasa unaweza kwenda kuketi.

Waheshimiwa Wabunge, sasa tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, namwita Mheshimiwa Joseph Michael Mkundi, aulize swali lake.

Na. 16

Ukarabati wa Kituo cha Polisi cha Nansio

MHE. JOSEPH M. MKUNDI aliuliza:-

Je, nini mkakati wa Serikali kukifanya ukarabati Kituo cha Polisi cha Nansio?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Joseph Michael Mkundi, Mbunge wa Ukerewe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua uchakavu wa Kituo cha Polisi Nansio kilichopo Ukerewe. Tathmini kwa ajili ya ukarabati imeshafanyika mwaka huu wa 2022 na kubaini kuwa kiasi cha shilingi 68,000,000 zinahitajika ili kugharamia ubadilishaji paa, dari, mfumo wa maji na maji taka, pamoja na kuziba nyufa, kurekebisha sakafu pamoja na kupaka rangi. Ukarabati huu utafanyika kulingana na upatikanaji wa fedha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Joseph Michael Mkundi, swali la nyongeza.

MHE. JOSEPH M. MKUNDI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kwanza nitumie fursa hii kutoa pole kwa Mkuu wa Polisi wa Wilaya ya Ukerewe, kwa msiba wa askari uliopatikana jana.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada hayo, nina maswali mawili ya nyongeza, la kwanza; kwa kuwa tathimini tayari imeshafanyika, lakini miundombinu iliyoko pale hasa mifumo ya maji safi na maji taka pamoja na mapaa ya kituo chenyewe na nyumba za watumishi ni mbovu sana, sasa Serikali haioni sababu kuchukua jambo hili kama la dharura na ikalifanya kazi kwa haraka kadri inavyowezekana ili kujenga mazingira mazuri ya utendaji kwa watumishi wetu pale?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalii la pili, je, Mheshimiwa Waziri haoni sababu, namwomba ikiwezekana twende naye pale ili aangalie mazingira kwa uhalisia tuweze kujadiliana tuone namna njema ya kuboresha mazingira ya utendaji kwa watumishi wetu wa Ukerewe? Nashukuru sana. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Waziri majibu.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Joseph Michael Mkundi, Mbunge wa Ukerewe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalii lake la kwanza alikuwa anaomba tuchukue jambo hili kama dharura; basi kwa sababu Mheshimiwa Mbunge anakifahamu vizuri kituo hiki naomba nikubaliane naye kwamba tunalichukulia hili jambo kama la dharura. Kwa hiyo nitatoa maelekezo kufuatilia, kuona jinsi gani ambavyo tunaweza tukafanya ili yale mambo ya dharura tuweze kuyafanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, kuhusu suala la mimi kwenda kwenye Jimbo lake, hilo halina tatizo, tutapanga ratiba baada ya Bunge hili kumalizika ili tuweze kwenda kutembelea jimbo lake kuona wenyewe jinsi ambavyo tunaweza kusaidiana kutatua changamoto za kidharura ambazo Mheshimiwa Mbunge amezieleza.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Iddi Kassim, Mbunge wa Msalala, swalii la nyongeza.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

MHE. IDDI K. IDDI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kumekuwa na ukosefu wa amani katika baadhi ya maeneo hasa katika Kata ya Ngaya na kata ya Buriye na kupelekeea wananchi sasa kuweza ku-share na Mbunge wao ambaye ni mimi kujenga Kituo cha Polisi na sasa kimefikia kwenye hatua ya lenta. Sasa swali langu ni lini Mheshimiwa Waziri atafika kuja kuweka jiwe la msingi sambamba na kutenga fedha kuja kumalizia Kituo hicho cha Polisi? Ahsante. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante kwa swali lako fupi. Mheshimiwa Waziri, majibu.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Iddi, Mbunge wa Msalala, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge na wananchi wake kujitolea kujenga kituo hiki na kama ambavyo nilivyokuwa nimejibu jana kwa zile jitihada ambazo zimeanzishwa na wananchi, tumeshajitahidi kuziendeleza. Tuna mfuko wetu wa tozo na tozo, japokuwa hauwezi kukidhi maeneo yote, lakini tutajitahidi kuangalia tutakachoweza kufanya ili tuongeze jitihada hizo ambazo Mheshimiwa Mbunge na wananchi wake wamezifikia. Nitakuwa tayari kwenda kuweka jiwe la msingi wakati wowote ambapo Mheshimiwa Mbunge mimi na yeye tutashauriana yaani muda muafaka wa kuweza kufanya kazi hiyo.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Justine Nyamoga, swali la nyongeza.

MHE. JUSTIN L. NYAMOGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona, kwa miaka 20 sasa Wilaya ya Kilolo haina Makao Makuu ya Polisi na wala kwenye Wilaya penyewe hakuna Kituo cha Polisi.

Je, ni lini Serikali itatimiza ahadi za viongozi mbalimbali kujenga Makao Makuu ya Polisi katika Wilaya ya Kilolo kwenye Mji wa Kilolo?

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiri kwamba Mheshimiwa kwenye Jimbo lake la Kilolo kama ambavyo Wilaya kadhaa zimekuwa zina ukosefu wa Vituo vya Polisi vya Wilaya na hii ni moja kati ya mambo ambayo jana niliyazungumza na mikakati ya Kiserikali ya kiujumla ya kukabiliana na tatizo hili, hivyo nimwombe Mheshimiwa Mbunge avute Subira, lakini suala hili tumelichukua kwa uzito wake.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Furaha Matondo swali la nyongeza.

MHE. FURAHA N. MATONDO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali la nyongeza msitu wa Rubya umetoa milioni 50 kwa ajili ya kujenga Kituo cha Polisi, pale Rubya.

Je, Serikali ipo tayari kuwaongezea fedha ili kituo hicho kiweze kukamilika pamoja na nyumba za maaskari?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani kasema kituo gani?

MWENYEKITI: Hebu rudia, swali lako Mheshimiwa Matondo.

MHE. FURAHA N. MATONDO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali. Msitu wa Rubya katika Wilaya ya Ukerewe umetoa milioni 50 kujenga Kituo cha Polisi pale Rubya.

Je, Serikali ipo tayari kuongezea fedha ili kituo hicho kiweze kukamilika pamoja na nyumba za maaskari?

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Waziri, majibu.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli fedha hizo zimetolewa, lakini mpaka sasa taarifa nilizokuwa nazo ni kwamba kazi hizi zinaendelea vizuri na hakujaonekana dalili za kushindwa kukamilika wala wafadhili hawajaonesha dalili ya kushindwa kuendelea kukamilisha kituo hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naomba tuwape muda wakamilishe tuone watafikia wapi, kama kutatokea changamoto baadaye, basi tutaangalia namna gani ya kuweza kulikabili.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiswa Ester Bulaya, swalii la nyongeza.

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Kituo cha Polisi cha Wilaya Bunda ni chakavu sana na Mheshimiwa Waziri anakijua, amefika pale na kinahudumia Majimbo matatu Mwibara, Bunda Mjini na Bunda. Je, ni lini Mheshimiwa Wizara atakikarabati kituo hicho ili kiendane na hadhi ya Wilaya?

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani Nchi, majibu.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Kituo cha Bunda kiko chakavu na binafsi nakumbuka niliwahi kutembelea kituo hiki na hata Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo hili naye vilevile alinikumbushia juu ya ukubwa wa changamoto hii. Hivyo basi, nimhakikishie Mheshimiwa Ester Bulaya kwamba tunafahamu

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

na pale ambapo hali ya kibajeti itakapokaa vizuri, basi tutakifanyia kazi kituo hiki.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Janejelly, swali la nyongeza.

MHE. JANEJELLY J. NTATE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Kata ya Kilungule, Jimbo la Mbagala wananchi wamejenga Kituo cha Polisi kwa nguvu zao, lakini sasa ni mwaka wa tatu Serikali haijafanya juhudii ya kufungua kituo hicho. Je, ni lini Wizara italeta watumishi ili kituo hicho kifanye kazi?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Waziri Mambo ya Ndani ya Nchi.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Janejelly, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kituo hiki vilevile nakifahamu nakumbuka wakati ambapo tunaanza jitihada za kujenga hiki tulishiriki kufanya harambee. Niwapongeze sana wananchi walioshiriki lakini niwahakikishie kwamba juhudii hizo za wananchi hazitapotea bure kwa vituo vyote ambavyo wananchi wametoa nguvu zao, basi Serikali tutaangalia kadri itakavyowezekana, hali itakaporuhusu tuweze kuvikamilisha.

MWENYEKITI: Ahsante. Nimekuona Mheshimiwa Chikota, Mbunge wa Nanyamba.

MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Napenda kuuliza kwamba, je, Serikali ina mpango gani wa kujenga kituo cha Polisi Nanyamba kwa sababu sasa hivi Nanyamba ni Makao Makuu ya Halmashauri ya Mji wa Nanyamba na kuna changamoto za kiulinzi kule mpakani? Nakushukuru.

MWENYEKITI: Majibu Mheshimiwa Waziri.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naona kuna changamoto ya sauti kidogo, anaweza akarudia.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Chikokota ebu uliza swalilako vizuri.

MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Naitwa Chikota.

MWENYEKITI: Sawa Mheshimiwa Mbunge wa Nanyamba, swalilako nyongeza.

MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuiuliza Serikali kwamba ina mpango gani wa kujenga Kituo cha Polisi Nanyamba kwa sababu kilichopo sasa hivi ni kidogo, lakini pia kule mpakani kuna changamoto ya kiulinzi na sasa hivi Nanyamba ni Makao Makuu ya Halmashauri ya Mji wa Nanyamba?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, kama una majibu au kama utahitaji *details* pia una nafasi.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swalilako nyongeza la Mheshimiwa Chikota, Mbunge wa Nanyamba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna mpango wa kujenga vituo vikubwa zaidi, kukarabati, kujenga vipyta katika maeneo ambayo hakuna, lakini mambo haya hatuwezi kuyakamilisha kwa wakati mmoja na ndio maana hata ukiangalia bajeti inayokuja mwaka huu tunatarajia kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa Makao Makuu ya Polisi Mtwara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mnaona jitihada ya Serikali tunaenda hatua kwa hatua. Kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa kuwa hata Makao Makuu ya Mtwara tunataka kujenga, ina maana hata changamoto za Wilaya nazo tutazifanya kazi hatua kwa hatua. Kwa hiyo nimwombe mvute Subira.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, sasa namwita Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq, aulize swali lake.

Na. 17

Wahanga wa Vitendo vya Ukatili Nchini

MHE. FATMA H. TOUFIQ aliuliza:-

Je, kuna wahanga wangapi wa vitendo vya ukatili nchini kuanzia mwaka 2019 hadi 2022?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu za matukio ya vitendo vya ukatili nchini vilivyoripotiwa kwenye Vituo vya Polisi kuanzia mwaka 2019 hadi Machi, 2022 ni 27,838 kwa mchanganuo ufuatao:-

Matukio ya kubaka ni 19,726; kulawiti ni 3,260 ambaao kati ya hao wanaume ni 3,077 na wanawake ni 183; kuunguzwa kwa moto ni 198 kati ya hao wanaume ni 73 na wanawake ni 125; kutupa watoto wachanga ni 443 kati yao wanaume ni 177 na wanawake ni 266; kipigo ni 4,211 ambaao kati ya hao wanaume ni 16 na wanawake ni 4,195.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jumla ya kesi zilizofikishwa Mahakamani ni 21,063 na watuhumiwa ambaao wamehukumiwa 14,278. Mashauri mengine yako kwenye hatua mbalimbali za upelelezi pamoja na Mahakamani. Aidha, Serikali inaendela kuiasa jamii kutumia vema taasisi za familia kaya, jumuia za kidini kuanzia ngazi za vitongoji, vijiji na mitaa ili kudhibiti vitendo vya ukatili katika jamii.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq swali la nyongeza.

MHE. FATMA H. TOUFIQ: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, ninamshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu mazuri lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa idadi kubwa ya waathirika wa ukatili ni wanawake na watoto.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuzuia idadi kubwa ya takwimu tunazoletewa hapa ili kupunguza ukatili huo? (*Makof*)

Swali la pili, pamoja na kuwa Serikali imetoa taarifa kuwa wanaume 3,077 ndiyo waliofanyiwa ukatili wa kulawitiwa, sina shaka idadi kubwa itakuwa ni watoto wa kiume.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwalinda watoto wa kiume ili kusudi wasifanyiwe ukatili? (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq kwa swali hili la nyongeza sasa Mheshimiwa Waziri unaweza kujibu.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq, Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Dodoma kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la takwimu linaweza kuonekana kwamba ni nyingi kwa sababu ya jitihada ambazo Serikali imechukua kupitia Jeshi la Polisi la kuanzisha Dawati la Kijinsia, ambapo hapo zamani watu wengi ilikuwa wanapata shida au wanaona aibu kuripoti matukio kama haya kwenye *counter* ya polisi. Kupitia uendeshwaji wa dawati hili watu wengi zaidi wamekuwa wakijitokeza na kutoa taarifa na hivyo basi kufanya sasa yale matukio ambayo hayatolewi taarifa zamani sasa yanaweza kutambulika.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na suala la mikakati ya kuwalinda. Suala la kuwalinda watoto wetu si jukumu la Serikali peke yake, hili ni suala la kila mmoja wetu tukianzia wazazi. Kwa hiyo, niseme wakati Serikali inafanya kila jitihada kuhakikisha kwamba inaweka mazingira mazuri ya ulinzi ikiwemo kuhakikisha kwamba inachukua hatua kali kwa wale wote ambao wanahusika na vitendo vya kuzalilisha Watoto wetu naomba sana wazazi na wenyewe wachukue majukumu yao ipasavyo, kwa maana ya kuangalia kuhakikisha wanafuatisilia nyendo za watoto wao na kuhakikisha kwamba wanawalinda na kuwasimamia. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Tunza Malapo swalii la nyongeza.

MHE. TUNZA I. MALAPO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru.

Kwa kuwa vitendo vya ukatili vimezidi kuongezeka kila siku tunasikia matukio mbalimbali, na kwa kuwa adhabu mbalimbali zinatolewa lakini vitendo vinazidi kuongezeka.

Je, Serikali sasa haioni ni wakati muafaka wa ku-review hizi adhabu ili ziwe kali zaidi watu wasiendelee kufanya hivi vitendo vya ukatili? (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi majibu.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Tunza Malapo, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ametoa wazo zuri nadhani ni jambo la kulichukua na kulitafakari na kulifanyia kazi. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Sophia Mwakagenda.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri kumekuwa na mauaji na vipigo vingi sana kisa wivu wa kimapenzi. Serikali inachukua jukumu gani la kuhakikisha wale wanaofanya vitendo hivyo wanachukuliwa hatua kali na za haraka ili mambo hayo yasiendelee kutokea katika jamii ya kitanzania. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Waziri majibu.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Sophia Mwakagenda kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli yametokea matukio ya mauaji yenye vyanzo mbalimbali ikiwemo chanzo ambacho amekizungumza Mheshimiwa Mbunge. Mheshimiwa Mbunge anasema kwamba adhabu hizo hazijasaidia. Lakini labda nieleze kwa ufupi kwamba, ukiangalia katika kipindi cha mwezi Januari mpaka Februari tulishuhudia matukio mengi sana ya mauaji ya vyanzo mbalimbali kwenye jamii, ikiwemo vyanzo hivyo vya wivu wa mapenzi, ushirikina, ulevi uliokithiri, kugombania mali, urithi na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumechukua hatua ya kuunda Tume, Tume imefanya kazi yake vizuri imetuletea mapendekezo mengi, lakini katika mambo makubwa na ya msingi ambayo nimetaka nilizungumze hapa kwamba mbali ya kuchukua hatua jambo kubwa la msingi ni kuhakikisha kwamba tunadhibiti matukio kama haya yasijitokezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia taarifa ambayo tumepewa na Tume kuna hatua mbalimbali ambazo tumezichukua za kuhakikisha tunadhibiti. Moja katika hatua muhimu sana ambayo tumechukua ni kuhakikisha kwamba tunaimarisha mifumo katika ngazi za Kata.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Jeshi la Polisi mtakumbuka hivi karibuni walihitimu askari zaidi ya zaidi ya 4,200 na zaidi, hao wote tumewapeleka kwenye kata kuhakikisha kwamba kwenye kata tuna askari wa kutosha ambao wana weledi wa kusimamia masuala ya usalama katika ngazi husika na kushirikiana na Kamati za Ulinzi za Kata pamoja na wadau mbalimbali ikiwemo wananchi kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, mbali ya kuchukua hatua lakini jitihada kubwa vilevile tunazielekeza katika kudhibiti matukio kama haya yasiweze kujitokeza.

MWENYEKITI: Ahsante. Sasa ninamuita Mheshimiwa Jerry William Silaa Mbunge wa Ukonga aulize swali lake.

Na. 18

**Sheria inayosimamia Wanaostahili kutumia
Ving'ora na Vimulimuli**

MHE. JERRY W. SILAA aliuliza:-

Je, ni Sheria gani inasimamia orodha ya wanaostahili kutumia ving'ora na vimulimuli kwa misafara ya Viongozi na Wananchi wa kawaida.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jerry William Silaa Mbunge wa Ukonga, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Usalama Barabarani Sura ya 168 ya mwaka 1973 kama ilivyofanyiwa marejeo mwaka 2002, ndiyo sheria inayosimamia matumizi ya ving'ora na vimulimuli barabarani. Kifungu 39(b) kifungu kidogo cha (1) na (2) cha sheria, kinaelekeza matumizi ya ving'ora na vimulimuli barabarani ambayo ni kutoa ishara kwa watumiaji wengine wa barabara kuchukua tahadhari kuwa kuna

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

dharura. Kifungu cha 54 kifungu kidogo cha (1) hadi cha (5) kinæleza utaratibu na mazingira ya matumizi ya ving'ora na vimulimuli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, magari yanayostahii kutumia ving'ora na vimulimuli kwa mujibu wa sheria ni magari ya polisi, zimamoto, magari ya wagonjwa (*ambulance*), magari ya vikosi vyta ulinzi na usalama pamoja na magari yaliyopata kibali maalumu kutoka kwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi na kutangazwa katika Gazeti la Serikali.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Jerry Silaa swali la nyongeza.

MHE. JERRY W. SILAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Niishukuru Serikali kwa majibu mazuri na kwa operesheni inayoendelea maana Dar es Salaam ilikuwa kila ukikaa unasikia koro koro nyuma ya gari yako, kitu ambacho ni kinyume cha sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza:

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia Kifungu cha 54 cha Sheria, Sura ya 168 ya Usalama Barabarani; je, Waziri ameshatoa vibali vingapi mpaka sasa vya utumiaji wa ving'ora ukiondoa magari yaliyoorodheshwa?

Swali la pili; je, Serikali ina mpango gani wa kufanya marekebisho ya sheria hii ambayo ni ya muda mrefu ili kuweza kutoa adhabu stahiki kwa watu wanaovunja sheria hii, vilevile kuweza kuona namna ya kuongeza viongozi wenye kustahili heshima hii na kuweza kuwaondolea tataruki wananchi. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi majibu.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Jerry Silaa kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka sasa tokea nimepewa dhamana hii sjawahi kutoa kibali hata kimoja.

Pili, kuhusu mabadiliko ya sheria tunao mchakato ambaa unaendelea wa mabadiliko ya sheria ya usalama barabarani, kwa hiyo kwa kuwa mchakato huu hatma yake ni hapa Bungeni, basi Mheshimiwa Mbunge naomba hoja zake aziandae vizuri ili kuweza kuhakikisha mchakato huu utakapofika Bungeni aweze kusaidia kutoa hoja za kuongeza yale ambayo anahisi yanafaa katika marekebisho hayo ya sheria itakapokuja.(Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nchi, Mheshimiwa Hamad Yussuf Masauni kwa majibu mazuri. Sasa tunakwenda Wizara ya Afya namuita Mheshimiwa Dennis Lazaro Londo, Mbunge wa Mikumi, aulize swalii lake.

Na. 19

Idadi ya *Physiotherapist* Mkoa wa Morogoro

MHE. DENNIS L. LONDO aliuliza: -

Je, kuna Wataalam wangapi wa huduma za utengamano na mazoezi ya viungo *physiotherapist* katika Mkoa wa Morogoro?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Mheshimiwa Mollel majibu.

NAIBU WAZIRI WA AFYA alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Afya naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Dennis Lazaro Londo Mbunge wa Mikumi, kama ifuatavyo: -

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Morogoro una jumla ya wataalam 15 kati ya 30 wanaohitajika wa huduma za utengamao na mazoezi ya viungo ambapo Kilosa kuna mtaalam mmoja, Hospitali ya Rufaa Morogoro kuna wataalam wanne, Mvomero mtalaam mmoja, Ifakara Hospitali wanne na Mzinga Hospitali wataalam watano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha watalaam tisa wa huduma za utengamao wameombewa kibali cha ajira katika bajeti ya mwaka wa fedha 2022/2023. Ahsante. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Dennis Londo swali la nyongeza.

MHE. DENNIS L. LONDO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umbali wa kutoka Morogoro Mjini mpaka Mikumi ni kilometra 120 na kutoka Mikumi mpaka Iringa ni kilometra 190, kuna ajali nyingi sana ambazo zinatokea katika kipande hiki na wanategemea sana huduma katika Kituo cha Afya na Hospitali hiⁱ ya Mtakatifu Kizito pale Mikumi.

(a) Je, Serikali haioni umuhimu wa kupeleka watalaam wa huduma wa utengamao na *physiotherapy* pale Mikumi? (*Makofi*)

(b) Je, Serikali haioni wakati umefika sasa kuokoa maisha ya Watanzania wengi kuanzisha *centre of excellence* ya wataalam wa mifupa kwa ajili ya kujifunza pale Mikumi? Naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya.

NAIBU WAZIRI WA AFYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, maswali yake mawili moja la kuongeza watalaan. Moja, kwenye eneo la kuongeza watalaan suala tu siyo kuongeza watalaan lakini ni kushirikiana na wenzetu wa Wizara ya Mambo ya Ndani, lakini uchukuzi kwa ajili ya kuhakikisha kwamba tunapunguza mambo ambayo yanapelekea ajali zitokee kwenye maeneo hayo, pia kuhamasisha elimu ya magonjwa yasiyoambukiza ili kupunguza idadi ya watu hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na yeze kwamba Mkoa wa Morogoro ukiangalia wanahitajika watalaan 30 na kwa mwaka huu wanaenda kuongezwa watalaan tisa maana yake katika hawa tisa tutaona ni namna gani tunaweza kuhakikisha tunaongeza watalaan kwenye eneo ambalo yeze amelitaja. Lakini kuangalia vizuri zaidi *data* zilizotumika kuamua wanahitajika Mkoa wa Morogoro hawa 30 kuangalia kama illumika *data* za wakati gani ili kama kunahitajika kuongeza basi tuwaongeze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine la wataalam wa mifupa na vitu vingine tunaenda kufikiria kwenye ajira ambazo amesema Mheshimiwa Waziri wa Utumishi ni 32,000 basi tutaenda kulizingatia eneo hilo wakati tukipata hivyo vibali. Ahsante sana. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Tadayo Joseph Mbunge wa Mwanga swali la nyongeza.

MHE. JOSEPH A. TADAYO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kupata nafasi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa huduma ya utengemao na mazoezi ya viungo ni muhimu sana kwa wagonjwa wanaopata matatizo yanayohusika na viungo, na kwakuwa Wilaya nzima ya Mwanga kuanzia Hospitali ya Wilaya mpaka vituo vyake vya afya hatuna matalaan hata mmoja wa huduma hiyo.

Je, Serikali inatoa kauli gani juu ya kutupatia *physiotherapist* katika Wilaya ya Mwanga hasa ukizingatia

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

ahadi ya Mheshimiwa Waziri wa Utumishi juu ya ajira lukuki zinazokuja kwa ajili ya afya. Ahsante. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa ufupi.

NAIBU WAZIRI WA AFYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa kuwapigania wananchi wa Mwanga, lakini ye ye mwenyewe anajua sasa Rais wetu amepeleka fedha pale Mwanga kwa ajili ya kujenga Idara ya Dharura na ujenzi unaendelea. Wakati ujenzi unakamilika na kuweka vifaa na ajira 32,000 ambazo zimetokea hayo mambo yatakwenda kuzingatiwa kuhakikisha tunapomaliza huduma ya magonjwa ya dharura na watalaan wa aina hiyo uliowasema wanakuwepo vilevile kwenye eneo hilo. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Esther Matiko swali la nyongeza.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru, hospitali ya Mji wa Tarime inahudumia zaidi ya wananchi wa Wilaya tatu na imekuwa ina uhaba wa watumishi wa afya wakiwemo watalaan wa utengamao na mazoezi ya viungo.

Je, ni lini sasa Serikali itatuletea watalaan hawa wa utengemao na mazoezi ya viungo? (*Makofii*)

MWENYEKITI: Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA AFYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa swali lake zuri, lakini nitamuomba Mheshimiwa Mbunge mimi na ye ye tutashirikiana kuangalia kwa maana ya *data* za Wilaya hiyo na sehemu hizo, kwanza kwasababu amesema hospitali inatumia na Wilaya tatu, tutaangalia kuona tatizo lipo wapi.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Moja; kama kuna maeneo ambayo inaweza ikafanyika kwenye Wilaya husika wapelekwe kwenye Wilaya husika, lakini kwenye ajira ambazo zinakwenda kutokea tutaenda kuzingatia kwa kuangalia *data* za eneo husika na utumishi watakapotuleta kibali hayo yatazingatiwa. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Judith Kapinga swali la nyongeza.

MHE. JUDITH S. KAPINGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Mbanga siyo tu kwamba haina Daktari hata mmoja wa masuala ya viungo, lakini haina Daktari hata mmoja wa macho, meno na *radiojia* na anesthesia.

Je, Serikali inatuahidi nini katika kupata watalaamu hawa.

MWENYEKITI: Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA AFYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Mbunge nampongeza sana jinsi ambavyo amekuwa na mchango mzuri sana hasa kwenye eneo la lishe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuambie majibu ni yale yale kwamba kwenye ajira 32,000 pia tutachukua kwa kushirikiana na yeye lakini tutawauliza watalaam wa eneo husika kwa kuangalia *load* ya wagonjwa wanaohitaji huduma ya mtengamao kwenye eneo alilotaja ili tuweze kuamua mapema na kupeleka mahitaji Utumishi ili kuweza kupata hao watalaamu ambao Mheshimiwa anawataja.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Tabasam swali la nyongeza.

MHE. TABASAM H. MWAGAO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naomba kuuliza swali la nyongeza kwa Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Naibu Waziri ulikuja Sengerema nikaalika mukutano mkubwa sana na ukaahidi katika kituo cha Busisi kukipa vifaa, leo mwaka unakwisha unaniandalia kitu gani huko Jimboni kwangu. Ahsante. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA AFYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimjibu Kaka yangu Mheshimiwa Tabasam ni kweli nimekwenda kwenye eneo husika, tulifanya pamoja naye mukutano wa wananchi na tuliahidi mbele ya wananchi, nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa kushirikiana na wenzangu wa TAMISEMI, tayari Kituo cha Afya cha Busisi kipo kwenye maombi ya dharura ambayo sasa yanaenda kutekelezwa mwaka huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tayari imeshaingizwa kwenye mpango na fedha zinaenda kupelekwa kwa ajili ya kufanya kazi tuliyokubaliana siku ile kwenye mukutano. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Tunashukuru Mheshimiwa Naibu Waziri Wizara ya Afya. Sasa namuita Mheshimiwa Dkt. Paulina Daniel Nahato, Mbunge wa Viti Maalumu aulize swali lake Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia.

Na. 20

Upungufu wa Wahadhiri wa Vyuo Vikuu Nchini

MHE. DKT. PAULINA D. NAHATO aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itatoa vibali kwa Vyuo Vikuu vyenye upungufu wa Wahadhiri ili viweze kuajiri Wahadhiri wapya?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu Sayansi na Teknolojia Mheshimiwa Kipanga.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Elimu Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Dkt. Paulina Daniel Nahato Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua changamoto ya upungufu wa Wahadhiri katika Vyuo Vikuu vya Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekua ikitoa vibali vya ajira kila mwaka ambapo katika mwaka wa fedha 2018/2019 hadi 2020/2021, Serikali ilitoa vibali vya nafasi za ajira mpya za Wakufunzi na Wahadhiri Wasaidizi 333 katika Vyuo Vikuu vya Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kukabiliana na changamoto ya upungufu wa Wahadhiri Vyuo, Wizara yangu inaendelea na jitihada za kuomba vibali vya ajira za Wahadhiri kutoka Wizara yenye dhamana na Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Sambamba na hilo, pia upo utaratibu wa kuwahamisha watumishi wenye sifa kutoka Taasisi mbalimbali za Serikali kwenda Vyuo Vikuu na kuwajengea uwezo ikiwa ni pamoja na kuwasomesha kozi za muda mfupi na mrefu. Nakushukuru sana.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Paulina Nahato, swalii la nyongeza.

MHE. DKT. PAULINA D. NAHATO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, namshukuru Waziri kwa majibu mazuri, lakini naomba kumuuliza maswali mawili.

Tunafahamu Serikali inaenda kutekeleza Mradi wa *High Education for Economic Transformation (HEET)*; sasa namuuliza swalii; je, mradi huo unatarajia kusomesha wahadhiri wangapi?

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Je, Serikali inatuhakikisha kuwa Mradi huu wa *HEET* utapunguza ubaha wa Wahadhiri katika vyuo vikuu kwa kiasi gani? Ahsante.

MWENYEKITI: Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, naomba sasa kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Dkt. Nahato kwa pamoja kama ifutavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Serikali yetu ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais wetu, Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan, tumepata mkopo wa jumla ya dola za Kimarekani milioni 425, sawa na shilingi bilioni 972.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mradi huu, pamoja na mambo mengine utakwenda kuimarisha miundombini kwenye vyuo vyetu vya Umma karibu 14, vilevile utashughulikia masuala ya Wahadhiri pamoja na watafiti katika nchi yetu. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu, katika mradi huu tunatarajia kufanya maendelezo ya Wahadhiri wetu katika Vyuo Vikuu wapatao 831, ambapo katika kada ile ya *PhD.*, ambayo tunaita Uzamivu, ni wahadhiri 444 na wale wa *Masters* yaani Uzamili ni 387.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimwondoe wasiwasi, jambo hili tutakwenda kulifanya na kuhakikisha tunataondoa changamoto hii ya wahadhiri katika vyuo vyetu. Nakushukuru. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante. Nimekuona Mheshimiwa Issa Mtemvu, Mbunge wa Kibamba.

MHE. ISSA J. MTEMVU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Nimesikia majibu ya Serikali ni mazuri na yanaleta moyo katika kupunguza changamoto ya upungufu wa Wahadhiri na hasa Wahadhiri Wabobezi

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

katika Vyuo Vikuu vyetu. Pamekuwa na tafiti chini ya Chama cha Wafanyakazi wa Vyuo Vikuu (*THTU*) kwamba kuna upungufu mkubwa sana; utafiti wa 2017, lakini sababu kubwa waliyotoa ni Serikali kutumia sana wataalamu wao katika kujaza nafasi mbalimbali Serikalini:-

Je, Serikali haioni sasa ni wakati mzuri wa kushauri mamlaka za uteuzi kuacha kutumia wataalam hawa, hasa Wahadhiri Wabobezi katika nafasi mbalimbali Serikalini?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri Kipanga, majibu.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Mtemvu, Mbunge wa Kibamba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile Mbunge ametoa wazo na Mamlaka za Uteuzi zipo, namwomba Mheshimiwa Mbunge tuichukue hoja yake hii ili tuweze kuifikisha kwenye vyombo hivi nya uteuzi ili waweze kufanya *evaluation* au tathmini toshelezi kabisa iwapo kama wanaona inafaa kufanya hivyo, basi liweze kufanyiwa kazi. Nakushukuru sana.

MWENYEKITI: Profesa Ndakidemi, swali la nyongeza.

MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kumekuwa na uhaba mkubwa sana wa Maprofesa katika Vyuo Vikuu nya Dar es Salaam, Sokoine, Mandela, Ardhi na Chuo cha Muhimbili. Baada ya kustaifu wakiwa na miaka 65 wanaambiwa waende nyumbani na biashara imeishia hapo, lakini kuna uhaba mkubwa.

Kipi bora, je, tuongeze miaka yao ifike angalau 70 waendelee kuhudumia nchi yetu? Kwa sababu kuna ombwe kubwa sana la ngazi hizi kwenye Vyuo Vikuu. Naomba Serikali ifikirie hawa watu waendelee mpaka miaka fulani hivi ili vijana wetu wapate elimu ya uhakika. Ahsante sana.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

MBUNGE FULANI: Unatetea unga!

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri Kipanga, majibu.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, naomba kujibu swalii dogo la nyongeza la Mheshimiwa Profesa Ndakidemi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli anayozungumza Mbunge kwamba tumekuwa na changamoto sana ya Wahadhiri katika kada hii ya Maprofesa kutohana na wao kustaaifu. Naomba nimweleze tu Mheshimiwa Mbunge kwamba kustaaifu kwa upande wa Utumishi wa Umma ilikuwa ni miaka 60 kwenye maeneo mengine yote, lakini kwa upande wa wenzetu hawa Maprofesa au Wahadhiri wa Vyuo Vikuu ilipandishwa kutoka miaka 60 kwenda miaka 65. Sasa hivi Mheshimiwa Profesa Ndakidemi anasema kwamba angalau tungeongeza ifike miaka 70.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba tulibebe wazo hilli, ingawa vilevile nimeeleza kwenye majibu yangu ya msingi kwamba katika mradi wetu wa *HEET*, unakwenda kufundisha katika *level/ile* ya *Ph.D* ambapo tunaamini wengi sasa wataenda kuwa Maprofesa, ambao tutahakkisha katika eneo hili tunaenda kufanya *coverage* kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuchukue wazo lake Mheshimiwa Prof. Ndakidemi twende tukalifanyie kazi ili tuweze kuona mtu akifikisha miaka 70 atakuwa na uwezo wa kusimama darasani akafundisha au akasimamia watu kwenye kazi zao? Nakushukuru sana. (*Makof!*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa majibu yako mazuri.

Waheshimiwa Wabunge...

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

MHE. AGNESTA L. KAIZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo wa Spika.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tumefika tamati ya kikao chetu cha maswali na majibu. Tunaishukuru Serikali kwa majibu mazuri, lakini hususan kwa ile ahadi ya kuajiri watumishi zaidi 32,000 ambayo itakwenda kujibu maswali mengi sana ya wananchi wetu kule majimboni. (*Makofii*)

Naomba kutambulisha wageni; wageni waliopo Bungeni asubuhi ya leo; kwanza waliopo kwenye Jukwaa la Spika ni wageni 29 wa Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu, ambao ni viongozi na watendaji wa Ofisi ya Waziri Mkuu; tunaye Dkt. John Kiang'u Jingu, Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu), sijui yupo hapa; Nafikiri yupo pale, tunamwona. (*Makofii*)

Tunaye Profesa Jamali Adam Katundu, Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu, (Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu). Yuko wapi? Okay, nafiki mnawona pale; tunaye Ndugu Caspary Muya, Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu, ahsante. (*Makofii*)

Vilevile tunaye Jaji Francis Mtungi, Msajili wa Vyama vya Siasa. Yuko wapi? Hayupo eeh, haya. Tunaye Ndugu Wilson Charles Mahera, Mkurugenzi wa Tume ya Uchaguzi; nafikiri hayupo.

Tunaye Ndugu Gerald Musabila Kusaya, Kamishna Jeneral, Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevyta, ahsante sana. (*Makofii*)

Aidha, wameambatana na Wakurugenzi wa Taasisi zilizopo chini ya Ofisi hiyo na Wawakilishi kutoka Mashirika ya Kimataifa, naomba kwa umoja wao wasimame wote. Ahsanteni sana. (*Makofii*)

Matangazo ya wageni wa Waheshimiwa Wabunge; wapo wageni sita wa Mheshimiwa David Kihenzile ambao ni

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

wafanyakazi wa *Nourish Africa Management* wakiongozwa na Mkurugenzi Mtendaji *Engineer* Balbina Andrew, karibuni sana. Hawa wanahusika na masuala ya mazingira pia. (*Makofii*)

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Daniel Sillo ambaye ni mpigakura wake kutoka Jimboni Babati Vijijiini, Mkoa wa Manyara, Ndugu John Pius, karibu sana Ndugu John Pius mgeni wa Mheshimiwa Sillo; pia tunao wageni watano wa Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, Mbunge ambaao ni mtoto wake na Wapigakura wake kutoka Jijini Mbeya, ahsante. (*Makofii*)

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Josephine Genzabuke, Mbunge, ambaao ni Madiwani kutoka Kasulu Mkoa wa Kigoma, ahsanteni sana Waheshimiwa Madiwani. (*Makofii*)

Wapo wageni wawili wa Mheshimiwa Festo Sanga, Mbunge, ambaao ni Wapigakura wake kutoka Makete kutoka Mkoa wa Njombe, Ndugu Panola Fungo na Ndugu Oportuna Mwitile, wasimame, ahsante. (*Makofii*)

Wageni wawili wa Mheshimiwa Simon Songe, Mbunge, ambaao ni Mwenyekiti wa Halmashauri ya Busega, Mheshimiwa Sundi Mniwe pamoja na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Busega, Ndugu Veronica Sayore kutoka Mkoa wa Simiyu. (*Makofii*)

Wageni walitembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; wanachuo 30 wa Bunge la Chuo Kikuu cha Kikatoliki cha Ruaha Mkoani Iringa, karibu sana wanachuo kwa kuendelea kuja kujifunza shughuli zetu za Bunge.

Pia tunao wawakilishi kutoka Vyama vya Wafanyakazi, ahsante; tuna wawakilishi kutoka Vyama vya Waajiri, yupo mmoja, ahsante; tuna wawakilishi kutoka Vyama vya Watu wenye Ulemavu, ahsante; tuna wawakilishi kutoka Mashirika ya Umoja wa Mataifa; mwakilishi wa *ILO*, ahsante, mwakilishi wa *UNICEF*, ahsante; wawakilishi wa *NFPA*,

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

ahsante, wawakilishi wa *UNDP*, ahsante na wawakilishi wa *Jiz*, ahsante. (*Makofii*)

Tunaye Mwenyekiti wa Bodi ya Sekta ya Mishahara Binafsi, ahsante sana; pia tunaye Bwana Meshack Bandawe, Katibu wa Kikosi Kazi cha Taifa cha Kuratibu Serikali cha Kuhamia Dodoma na Ujenzi wa Mji wa Serikali, ahsante sana. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, sasa nitampisha Mheshimiwa Naibu Spika kwa ajili ya kuja kuendelea baada ya hapa. (*Makofii*)

Hapa Naibu Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alikalia Kitit

NAIBU SPIKA: Ahsanteni. Tuna kazi kubwa mbele yetu, Katibu.

NDG. NENELWA MWIHAMBI, ndc – KATIBU WA BUNGE:

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 - Ofisi ya Waziri Mkuu

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri Mkuu. (*Makofii*)

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja kwamba kutokana na taarifa zilizowasilishwa leo ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti zilizochambua Bajeti ya Mfuko wa Bunge na Ofisi ya Waziri Mkuu, Bunge lako sasa lipokee na kujadili Taarifa ya Mapitio ya Utekelezaji wa Kazi za Serikali kwa mwaka wa fedha 2021/2022 na Mwelekeo wa Kazi za Serikali kwa mwaka 2022/2023.

Aidha, naliomba Bunge lako tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Ofisi ya Waziri

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mkuu na Taasisi zilizo chini yake pamoja na Ofisi ya Bunge kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kukutana hapa leo kwa ajili ya kujadili Taarifa ya Mapitio ya Utekelezaji wa Kazi za Serikali kwa mwaka wa fedha 2021/2022 na mwelekeo wake wa mwaka 2022/2023. Aidha, naomba kuwatakia heri ya Mfungo wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani kwa Waislamu na Kwaresma njema kwa Wakristu. Pia, nitumie fursa hii kuwatakia waumini wote sherehe njema za Sikuu za Pasaka na Eid. *Inshallah*, Mwenyezi Mungu atujaalie kwetu sote tukamilishe funga zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, salamu za pole; tangu tulipohitimisha Mkutano wa Bajeti wa Bunge hili mwaka 2021, nchi yetu ilikumbwa na majanga na matukio mbalimbali yaliyosababisha vifo na uharibifu wa mali. Nitumie fursa hii kutoa pole kwa wote waliofiwa na ndugu, jamaa na marafiki. Mungu azilaze roho za Marehemu mahali pema peponi, Amina. Kwa ndugu zetu walioumia na bado wanajiuguza, tumwombe Mwenyezi Mungu awasaidie kupona haraka na kurejea katika shughuli za ujenzi wa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, salamu za pongezi; kwa namna ya pekee, naomba nimpongeze Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutimiza mwaka mmoja tangu ashike nafasi ya kuongoza nchi yetu akiwa Rais wa Awamu ya Sita wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Katika kipindi hicho, tumeshuhudia mafanikio makubwa katika kuimarisha miundombinu hususan barabara, reli, viwanja vya ndege, bandari, huduma za kiuchumi na kijamii kama vile ujenzi wa madarasa, hospitali, zahanati na vituo vya afya, huduma za maji, utawala bora, mapambano dhidi ya rushwa na ujisadi, pamoja na kuhamasisha uwekezaji na utalii. Nami niungane na Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wenzangu kuendelea kumwombea kwa Mwenyezi Mungu aendelee kumpa nguvu, ulinzi, afya na kila liliilo la heri katika kuwatumikia Watanzania.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii pia kuwapongeza Mheshimiwa Dkt. Philip Isidor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kutokana na fikra na uongozi wao makini katika ujenzi wa Taifa letu. Ni dhahiri kuwa juhudzi zao za kuongoza na kusimamia utekelezaji wa Mpango ya Serikali zinaendelea kuleta manufaa makubwa kwa wananchi wa Taifa letu kwa ujumla. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee, nimpongeze Mheshimiwa Spika ambaye pia leo yupo safarini Uganda, kwanza kwa kuchaguliwa kwake na Bunge na kupata ushindi wa asilimia mia moja. Ushindi huo umetokana na imani kubwa waliyonayo kwako na ni matokeo ya kuliongoza Bunge hili kwa umahiri na weledi mkubwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, niwapongeze Waheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Mbunge na Naibu Spika ambaye leo upo kwenye Kiti pamoja na Wenyeviti wa Bunge; Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, Mbunge, na Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile, Mbunge kwa kuendelea kukusaidia kikamilifu katika kutekeleza majukumu ya kuliongoza Bunge letu Tukufu. Nawapongeza pia Wenyeviti na Makamu Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge kwa kuendelea kutekeleza majukumu yao kikamilifu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi karibuni Bunge lako Tukufu limepata Wabunge wapya. Hivyo, nitumie fursa hii kuwapongeza sana Mheshimiwa Emmanuel Lekishon Shangai kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Jimbo la Ngorongoro na Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha kwa kuteuliwa kuwa Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ni matumaini yangu kuwa Bunge lako Tukufu litaendelea kuwapatia ushirikiano wa kutosha ili waweze kutekeleza majukumu yao ipasavyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii pia kuwashukuru Wajumbe wa Kamati za Kudumu za Bunge kwa ushauri walioutoa wakati wa kupitia Makadirio ya Mapato

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

na Matumizi ya Wizara, Mikoa, Wakala, Idara za Serikali zinazojitegemea na Serikali za Mitaa. Kwa namna ya pekee nawashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Joseph Kizito Mhagama, Mbunge wa Madaba; Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI inayoongozwa na Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq, Mbunge wa Viti Maalum; na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Sillo Daniel Baran, Mbunge wa Babati Vijijini kwa kutoa mchango mkubwa wakati wa uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha za mafungu ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Mfuko wa Bunge. Maoni na ushauri wao utazingatiwa wakati wa utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2022/2023. (Makofi)

Mheshimiwa Nailbu Spika, napenda kutoa shukrani zangu kwa dhati kabisa kwa Mheshimiwa George Boniface Simbachawene, Mbunge wa Kibakwe na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu; Mheshimiwa Profesa Joyce Lazaro Ndalichako, Mbunge wa Kasulu Mjini na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu; lakini pia tunaye Mheshimiwa Ummu Hamisi Nderiananga, Mbunge wa Viti Maalum na Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu; na Mheshimiwa Patrobas Paschal Katambi, Mbunge wa Shinyanga Mjini na Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sitawashukuru Waheshimiwa Balozi Dkt. Pindi Hazara Chana, Waziri wa Maliasili na Utalii na Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa ushirikiano wao mkubwa walionipa pamoja na kazi nzuri waliyofanya wakati wote walipokuwa wanatumikia nafasi ya Waziri wa Nchi, ndani ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile niwashukuru sana Dkt. John Antony Kiang'u Jingu, Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mkuu anayeshughulikia Sera, Bunge na Uratibu; Profesa Jamal Adam Katundu, Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu na Ndugu Kaspar Kaspar Mmuya, Naibu Katibu Mkuu anayeshughulikia Sera, Bunge na Uratibu; Wakurugenzi na Wakuu wa Vitengo, Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Ofisi Binafsi ya Waziri Mkuu na wafanyakazi wote kwa ushirikiano mkubwa wanaonipa wakati ninapotekeleza majukumu yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii pia kuwashukuru washirika wa maendeleo zikiwemo nchi rafiki, taasisi na mashirika ya kimataifa, madhehebu ya dini na mashirika yasiyo ya kiserikali kwa kuendelea kuunga mkono juhudzi za Serikali, kujenga uchumi shindani na viwanda na kuiletea nchi yetu maendeleo. Mchango wao umekuwa muhimu katika kuiwezesha nchi yetu kupiga hatua kubwa kimaendeleo kulingana na mipango tuliojiwekea.

Mheshimiwa Naibu Spika, makadirio ya bajeti ninayowasilisha leo ni sehemu ya utekelezaji wa maelekezo ya llani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya Mwaka 2020 pamoja na ahadi zilizotolewa wakati wa kampeni za Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020. Vilevile, makadirio hayo ya mapato na matumizi yamezingatia vipaumbele vya Mpango wa Tatoo wa Maendeleo wa Miaka Mitano katika kutekeleza Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2025 na Mapendekezo ya Mpango na Bajeti kwa mwaka 2022/2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya mwaka 2021/2022. Mwaka 2021/2022, Serikali ilianza utekelezaji wa Mpango wa Tatoo wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano ulioanza mwaka 2021/2022 - 2025/2026 ukiwa na dhima ya Kujenga Uchumi Shindani wa Viwanda kwa Maendeleo ya Watu. Aidha, Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2021/2022 uliandaliwa kwa ajili ya kuanza utekelezaji wa mpango huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi Februari, 2022, mafanikio yaliyopatikana kutokana na utekelezaji wa

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

mpango huo ni pamoja na: Ujenzi wa Reli ya Kisasa unaoendelea kwa Kiwango cha Kimataifa ambapo ujenzi wa kipande cha Dar es Salaam - Morogoro (kilomita 300) umefikia asilimia 95.3; 9 kipande cha Morogoro - Makutupora (kilomita 422) asilimia 81.1; na Mwanza - Isaka (kilomita 341) umefikia asilimia 3.9. Aidha, tarehe 28 Desemba, 2021, Serikali illingia Mkataba na Kampuni ya Yapi Merkezi ya nchini Uturuki kwa ajili ya ujenzi wa njia ya reli kwa kipande cha Makutupora - Tabora (kilomita 368). Taratibu za kumpata mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa kipande cha Tabora - Isaka ambapo hivi karibuni zimashakamilika kilomita 165 zinaendelea ili kuimarishwa ili ujenzi huo uweze kuanza mara moja. Reli hii inayojengwa kwa awamu ya kwanza ya ujenzi wa reli hiyo kutoka Dar es Salaam hadi Mwanza itakuwa na urefu wa kilomita 1,219.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbili; Utekelezaji wa Mradi wa Kufua Umeme wa Maji wa Julius Nyerere (megawati 2,115) umefikia asilimia 56.79, ambapo ujenzi wa handaki la kuchepushia maji umekamilika. Kazi zinazoendelea kutekelezwa ni pamoja na ujenzi wa kituo cha kupokea na kusafirisha umeme kilovoti 400, njia za kupitisha maji ya kufua umeme, nyumba ya mitambo ya kufua umeme, ujenzi wa tuta kuu la bwawa na utengenezaji wa mitambo tisa ya kuzalisha umeme yenye uwezo wa kuzalisha Megawati 235 kila moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu; Kukamilika kwa ulipaji wa fidia katika maeneo ya kipaumbele ya Mradi wa Ujenzi wa Bomba la Mafuta Ghafi kutoka Hoima, Uganda hadi Chongoleani – Tanga, Tanzania pamoja na kusaini Mkataba kati ya Nchi Hodhi na Wawekezaji na Mkataba wa Ubia umekamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne; ujenzi wa Barabara na Madaraja Makubwa ambapo ujenzi wa barabara ya mzunguko katika Jiji la Dodoma yenye urefu wa kilomita 112.3 umeanza. Aidha, ujenzi wa Daraja la Kigongo - Busisi (Mwanza), daraja la Tanzanite, Dar es Salaam umekamilika na sote tumeshuhudia Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akizindua daraja hilo tarehe 24 Machi, 2022. Madaraja mengine yaliyokamilika ujenzi wake ni Kitengule, Kagera; Kiegeya, Morogoro; na Ruhuhu, Ruvuma. Ujenzi na ukarabati wa madaraja makubwa tisa ya Gerezani, Dar es Salaam; Msingi, Singida; Wami, Pwani; Sukuma, Mwanza; Sanza, Singida; Mteria, Dodoma/Iringa; Godegode, Mkoani Morogoro; Mitomoni, Ruvuma na Mkenda, Ruvuma unaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, tano; ni kuboresha Usafiri wa Abiria na Mizigo katika Maziwa Makuu. Ziwa Victoria Ujenzi wa gati la Nyamirembe, Magarine, Lushamba, Bukoba, Ntama, Chato, Muleba, pamoja na gati mbili za majahazi katika Bandari ya Mwigobero umekamilika. Aidha, ujenzi wa meli mpya ya *MV Mwanza Hapa Kazi Tu* umefikia asilimia 65 na kwa sasa ujenzi unaendelea katika ghorofa ya tatu. Ziwa Tanganyika: Ujenzi wa gati la Kagunga, Sibwesa na Kabwe (Nkasi) na Bandari ya Lagosa umekamilika. Aidha, ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya Bandari za Kigoma, Kibirizi na Ujiji pamoja na upanuzi wa Bandari ya Kasanga unaendelea. Ziwa Nyasa: Ujenzi wa sakafu ngumu katika bandari za Kiwira na Itungi umekamilika na ujenzi wa sehemu ya kuegesha meli katika Bandari ya Kiwira unaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, sita; Viwanja vya Ndege. Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Songea umefikia asilimia 96 na Kiwanja cha Ndege cha Mtwara umefikia asilimia 86. Aidha, mkandarasi wa ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Msalato kutoka China *M/s Sinohydro Corporation Limited* na wenzake wamekabidhiwa mradi tayari na kuanza ujenzi. Vilevile, maandalizi ya ujenzi wa viwanja vya ndege vya Mikoa ya Shinyanga, Kigoma, Tabora na Rukwa yanaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, saba: Uendelezaji wa Mji wa Serikali – Mtumba. Awamu ya pili ya ujenzi wa majengo 24 ya Wizara ikiwemo Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali yatakayotosheleza mahitaji ya watumishi wote ulianza Desemba, 2021 na unatarajija kukamilika Desemba, 2023. Aidha, ujenzi wa miundombinu ya maji, umeme na

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

mawasiliano unaendelea zikiwemo barabara zenye urefu wa kilomita 51.2 ambazo ujenzi wake umekamilika kwa zaidi ya asilimia 97.

Mheshimiwa Naibu Spika, nane; Sekta ya Elimu. Serikali imeendelea kujenga miundombinu ya elimu kwa lengo la kuhakikisha kuwa watoto wanapata elimu katika mazingira bora na yenye staha. Kupitia utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano Dhidi ya UVIKO-19, tumefanikiwa kupunguza msongamano wa wanafunzi kwa kuongeza madarasa 12,000 katika shule za sekondari, madarasa 3,000 katika vituo shikizi na mabweni 50 kwa wanafunzi wenyewe ulemavu. Ujenzi huo wa vyumba vya madarasa umewezesha wanafunzi wote waliochaguliwa katika mwaka wa masomo 2022 kuijunga na kidato cha kwanza kwa mkupuo mmoja. Kitendo hiki ni utekelezaji wa llani ya CCM ya Mwaka 2020 inayotaka upatikanaji wa elimu hapa nchini uimarishwe kwa kujenga miundombinu ya kutosha na usawa katika utoaji wa elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tisa; Sekta ya Afya. Ukarabati wa miundombinu ya kutolea huduma za afya nchini umefanyika. Miundombinu hiyo, inahusisha hospitali za rufaa za kanda, hospitali za rufaa za mikoa, hospitali za halmashauri, vituo vya afya na zahanati.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mafanikio yaliyopatikana, utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2021/2022 ulikabiliwa na changamoto mbalimbali, ikiwemo: athari za UVIKO-19 zilizosababisha kuchelewa kwa utekelezaji wa baadhi ya miradi ya maendeleo; kuvurugika kwa mnyororo wa uzalishaji na usambazaji wa bidhaa na huduma katika soko la dunia na hivyo kusababisha ongezeko la gharama za vifaa vya ujenzi; kupungua kwa mapato yatokanayo na shughuli za kiuchumi, misaada na mikopo nafuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kukabiliana na changamoto hizo, Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali ili kuimarisha shughuli za kiuchumi na kijamii

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

zilizoathirika na UVIKO-19. Pia, Serikali imeendelea kuhamasisha wananchi kupata chanjo na kufuata miongozo mbalimbali ya wataalam wa afya ili kujikinga na viashiria vya UVIKO - 19.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2022/2023, Serikali itajikita katika utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2022/2023 ambao ni wa pili katika utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano ilioanza 2021/2022 - 2025/2026. Mpango huo utawezesha kufikia malengo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuimarisha ukuaji wa Pato la Taifa; kudhibiti kasi ya mfumuko wa bei; kuimarisha mazingira ya uwekezaji na biashara hususan ushiriki wa sekta binafsi; kuboresha miundombinu ya huduma za kiuchumi na kijamii kama vile afya, elimu, maji, umeme vijijini pamoja na kuimarisha ustawi wa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2022/2023, Serikali itahakikisha sera za mapato na matumizi katika muda wa kati zinajikita katika kutekeleza vipaumbele vilivyoainishwa. Msukumo mkubwa utakuwa kuhakikisha usimamizi madhubuti wa fedha za umma na kuzielekeza kwenye maeneo yatakayoongeza tija, ajira na kuinua uchumi wa mwananchi mmoja mmoja. Aidha, Serikali itahakikisha miradi ya kipaumbele na kimkakati inayoendelea kutekelezwa, inakamilika kwa wakati ikiwa ni pamoja na utekelezaji wa miradi mipyta.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hali ya Uchumi; kwa mujibu wa Taarifa ya Shirika la Fedha la Kimataifa ya Januari, 2022, kasi ya ukuaji wa uchumi wa dunia inatarajiwa kupungua hadi kufikia asilimia 4.4 ya mwaka 2022 ikilinganishwa na asilimia 5.9 ya mwaka 2021. Kupungua kwa kasi ya ukuaji wa uchumi wa dunia kutachangiwa na sababu mbalimbali ikiwemo athari za UVIKO-19. Hali hiyo inatarajiwa kusababisha kuvurugika kwa mnyororo wa uzalishaji na usambazaji wa bidhaa na huduma kwa ujumla.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukuaji wa uchumi katika nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara unatarajiwa kukua kwa asilimia 3.7 wa mwaka 2022 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia nne wa mwaka 2021.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha Januari hadi Septemba, 2021, uchumi wa Taifa letu ulikuwa kwa asilimia 4.9 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 4.8 katika kipindi kama hicho mwaka 2020. Kuongezeka kwa kasi ya ukuaji kumetokana na jitihada mbalimbali zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali ikiwemo utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano Dhidi ya UVIKO - 19 na miradi mbalimbali ya maendeleo inayoendelea kutekelezwa maeneo yote nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2021, kumekuwa na mfumuko wa bei uliokua kwa wastani wa asilimia 3.7 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 3.3 ya mwaka 2020. Mfumuko huo ulikuwa ndani ya lengo la muda wa kati ya asilimia tatu mpaka tano, wigo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki usiozidi asilimia nane na ndani ya wigo wa Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika wa kati ya asilimia tatu mpaka saba. Kuongezeka kwa mfumuko wa bei kulichangiwa na sababu mbalimbali zikiwemo athari za UVIKO-19; kuongezeka kwa ghamama za uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa bidhaa na huduma; na kupungua kwa upatikanaji wa mazao ya chakula katika baadhi ya masoko ya ndani kutokana na mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ili kuhakikisha kuwa kunakuwa na ukuaji wa uchumi shirkishi na endelevu na viashiria vingine vyta uchumi vinaendelea kuwa imara ikiwa ni pamoja na kutoa msukumo katika kutekeleza vipaumbele vyta Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2022/2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uwekezaji; Serikali imeendelea kutekeleza mikakati ya kuvutia na kutangaza fursa za uwekezaji zilizopo nchini. Mikakati hiyo ni pamoja na kuhamasisha ushiriki wa sekta binafsi katika uwekezaji,

kufanya mapitio ya sera, sheria na kanuni zinazosimamia uwekezaji pamoja na kutenga hekta milioni 1.6 kwa ajili ya uwekezaji. Aidha, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amekuwa chachu ya mafanikio hayo hususan kuititia ziara mbalimbali alizozifanya nje ya nchi. Hadi Februari, 2022, Serikali imefanikiwa kuvutia uwekezaji na kusajili jumla ya miradi ya uwekezaji 294 yenye thamani ya dola za Marekani bilioni 8.04 ambazo ni sawa na shilingi trillioni 18.58 ikilinganishwa na dola za Marekani bilioni moja mwaka 2020/2021. Miradi hiyo inatarajiwa kuzalisha ajira takriban 62,301.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2022/2023, Serikali itaendelea kufanya mapitio ya Sera ya Taifa ya Uwekezaji ya mwaka 1996 ili iendane na mazingira ya sasa ya uwekezaji ikiwa ni pamoja na kujumuisha vipaumbele vivilivoainishwa katika Mpango ya Maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Serikali itaendelea kutekeleza Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Kufanya Biashara ikiwa ni pamoja na kuendelea kuondoa muingiliano wa majukumu kwa taasisi za udhibiti, kuondoa tozo sumbufo na kuimarisha ushirikiano wa sekta ya umma na sekta binafsi. Aidha, itaimarisha majadiliano na utatuzi wa changamoto zinazoikabili sekta binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwenendo wa Siasa Nchini; dhamira ya Serikali ni kuendelea kukuza na kuimarisha demokrasia ya vyama vyaa siasa nchini, sambamba na kudumisha maridhiano, amani, utulivu na umoja wa kitaifa tulionao Tanzania.

Katika kuhakikisha dhamira hiyo inatimia, Serikali iliandaa Mkutano wa Wadau wa Demokrasia ya Vyama vyaa Siasa ambaao ulifanyika tarehe 15 na 16 Desemba, 2021, Jijini Dodoma. Katika Mkutano huo, wadau walijadili hali ya mfumo wa demokrasia ya vyama vyaa siasa hapa nchini na kutoa maoni na mapendekezo ambayo yaliwasilishwa Serikalini kwa ajili ya kufanyiwa kazi.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kupokea mapendekezo hayo, Serikali iliridhia kuundwa kwa Kikosi Kazi kilicho jumuisha wawakilishi kutoka vyama mbalimbali nya siasa nchini. Jukumu kubwa la kikosi kazi hicho ilikuwa ni kuchambua maoni na mapendekezo ya washiriki wa Mkutano wa Wadau wa Demokrasia ya Vyama nya Siasa na kuandaa mapendekezo na kuwasilisha kwa Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutumia fursa hii kwanza kumshukuru sana na kumpongeza Rais wetu, kwa maelekezo aliyotoa baada ya kupokea taarifa ya awali ya Kikosi Kazi. Lengo la Mheshimiwa Rais ni kuhakikisha vyama nya siasa vinatumia haki yao ya kufanya shughuli za siasa kwa mujibu wa Katiba zao, huku vikiheshimu sheria za nchi na kudumisha uzalendo, amani, utulivu, umoja wa kitaifa na kutozuia shughuli za maendeleo. Ni imani yetu kwamba, hatua hizi zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali zitadumisha uhusiano mzuri kati ya wadau na Serikali katika kukuza na kudumisha demokrasia ya vyama vingi nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi karibuni zimefanyika chaguzi ndogo tatu katika Majimbo ya Konde, Ushetu na Ngorongoro pamoja na Kata 16. Nitumie fursa hii kuvipongeza Vyama vyote vilivyoshiriki katika chaguzi hizo ambazo zilifanyika kwa amani na utulivu. Kipekee nikipongeze Chama Cha Mapinduzi kwa ushindi mkubwa kilichoupata katika Majimbo ya Ushetu na Ngorongoro pamoja na kata zote 16. Aidha, nikipongeze chama cha ACT – Wazalendo kwa kushinda kiti kimoja cha Ubunge katika Jimbo la Konde. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kuhusu Bunge; Bunge lako Tukufu limeendelea kutekeleza kwa ufanisi majukumu yake ya msingi ya kutunga sheria, kushauri na kuisimamia Serikali. Katika mwaka 2021/2022, Bunge limefanya Mikutano yake kwa mujibu wa sheria ikiwemo Bunge kukaa kama Kamati ya Mipango kwa ajili ya kupokea, kujadili na kushauri kuhusu mapendekezo ya Mpango wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali pamoja na Mwongozo wa Kuandaa Mpango na Bajeti ya Serikali katika mwaka 2022/2023. Vilevile

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Bunge limeratibu shughuli mbalimbali za Kamati za Kudumu za Bunge zikiwemo semina na ziara za kukagua miradi ya maendeleo na kuishauri Serikali. Aidha, mfumo wa Bunge mtandao umeendelea kuboreshwa ili kuuwezesha kufanya kazi kwa ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2022/2023 Ofisi ya Bunge inaratibu na kuwezesha ushiriki wa Wabunge na Kamati za Kudumu za Bunge katika shughuli mbalimbali za ndani ya nchi, kikanda lakini pia kimataifa pamoja na kushiriki katika michezo ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Aidha, uendeshaji na usimamizi wa ukumbi wa Bunge utaboreshwili ili kuimarisha usalama katika maeneo na majengo ya Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ya Mahakama, ili kulinda haki na maslahi ya Watanzania, Serikali imeendelea kutekeleza miradi ya ujenzi wa Mahakama katika ngazi mbalimbali nchini na kuimarisha miundombinu ya utoaji haki na huduma.

Miradi inayokamilishwa ni ujenzi wa vituo jumuishi vitano vya utoaji haki katika Mikoa ya Dar es Salaam ambako pia Wilaya za Temeke na Kinondoni zimepata majengo, Dodoma, Arusha na Morogoro. Ujenzi wa kituo jumuishi katika Mkoa wa Mwanza unaendelea na upo katika hatua ya kukamilishwa. Ujenzi wa Mahakama mbili za Hakimu Mkazi wa Katavi na Lindi, Mahakama za Wilaya nne za Bunda, Chemba, Rungwe na Bahi na Mahakama za Mwanzo tatu katika maeneo ya Matiri kule Wilayani Mbanga Mkoani Ruvuma, Haydom Wilayani Mbulu na Kibaigwa Kongwa umekamilishwa. Pia Serikali imekamilisha ujenzi wa jengo la kuhifadhi kumbukumbu liliopo Jijini Tanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2021/2022 Serikali imeendelea na utekelezaji wa mradi wa Mahakama maalum zinazotembea katika Wilaya za Kinondoni eneo la Bunju, Ilala kule eneo la Chanika, Temeke kule Buza, Ubungo pale Kibamba na Illemela Mkoani Mwanza. Kupitia Mahakama hizo jumla ya mashauri 692 yameshasikilizwa na kuhitimishwa.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2022/2023, Serikali itaendelea kukamilisha ujenzi wa majengo mbalimbali yakiwemo kituo Jumuishi cha Utoaji Haki cha Mwanza, Mahakama ya Hakimu Mkazi ya Songwe, Mahakama za Wilaya Nane za Kilindi, Sikonge, Same, Tandahimba, Mwanga, Ngara, Namtumbo na Nanyumbu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile itaendelea na ujenzi wa Mahakama za Wilaya 18 katika Wilaya za Kakonko, Buhigwe na Uvinza Mkoani Kigoma, Butiama na Rarya Mkoani Mara, Itlima na Busega Mkoani Simiyu, Songwe, Mbogwe na Nyang'wale Mkoani Geita, Kyerwa na Misenyi Mkoani Kagera, Gairo, Mvomero na Kilombero Mkoani Morogoro, Mkinga Mkoani Tanga, Tanganyika Mkoani Katavi na Kaliua Mkoani Tabora.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali pia itakamilisha ujenzi wa Mahakama za Mwanzo Sita za Mlimba na Mang'ula Mkoani Morogoro, Kabanga kule Ngara, Kimbe kule Kilindi, Chanika - Ilala na Nyakibimbili - Bukoba na mradi wa ukarabati wa upanuzi wa Mahakama Kuu iliyopo Tabora na Mahakama ya Hakimu Mkazi kule Moshi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ya uzalishaji nianze na kilimo; sekta ya kilimo ni muhimu katika ukuaji wa uchumi wa Taifa letu na maendeleo ya wananchi wake. Kwa mujibu wa takwimu zillzopo, sekta ya kilimo inatoa ajira kwa wastani wa asilimia 65 ya Watanzania wote na inaendelea kuchangia malighafi za viwanda. Serikali kwa kutambua umuhimu huo, katika kipindi cha mwaka 2021/2022 imeendelea kutoa kipaumbele kwenye sekta ya kilimo ili kuinua Pato la Taifa na la mtu mmoja mmoja, kuimarisha usalama wa chakula na kuongeza ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, licha ya hayo, imeendelea kuchukua hatua kadhaa katika kuhakikisha pembejeo za kilimo hususan mbolea zinapatikana kwa bei nafuu, kwa wakati na kiwango cha kutosha pamoja na kuimarisha upatikanaji wa masoko ya uhakika ya mazao ya wakulima. Ni dhahiri kuwa matumizi ya mbolea, mbegu bora na viuatilifu

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

yatasaidia sana kuongeza tija na uzalishaji wa mazao ya kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya upatikanaji wa chakula. Hali ya uzalishaji, usalama na upatikanaji wa chakula hapa nchini imeendelea kuimarka. Katika msimu wa kilimo wa mwaka 2020/2021, uzalishaji wa mazao ya chakula Kitaifa ulikuwa tani milioni 18.8 ikilinganishwa na mahitaji halisi ya tani milioni 14.8. Kutokana na uzalishaji huo, nchi yetu ina ziada ya tani milioni 3.8 za chakula. Uzalishaji huo umeihakikisha nchi utoshelevu wa chakula kwa asilimia 125 kwa msimu wa kilimo wa mwaka huu tunaomaliza wa 2021/2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, ongezeko hilo linatokana na mtawanyiko mzuri wa mvua katika msimu wa mwaka 2020/2021, matumizi mazuri ya mbegu bora, mbolea, huduma za ugani zinazoendelea kutolewa na Wataalam pamoja na mipango madhubuti inayotekelizwa na Serikali. Pamoja na uwepo wa ziada hiyo, Serikali imeendelea kuimarisha usalama wa chakula nchini kwa kununua na kuhifadhi nafaka, kuititia Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula ambapo hadi mwishoni mwa Februari, 2022 akiba ghalani kwetu ilikuwa tani 199,793.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hatua za kuimarisha uzalishaji na usalama wa chakula, Serikali imeendelea kuimarisha miundombinu ya uhifadhi chakula kwa kujenga maghala na vihenge vya kisasa. Ujenzi wa vihenge vya kisasa katika maeneo ya Babati, Mpanda na Sumbawanga umekamilika. Aidha, ujenzi katika maeneo ya Dodoma, Mbozi, Makambako na Songea umefikia asilimia 80. Vilevile, Serikali imekamilisha ujenzi wa maghala katika Miji ya Babati, Mpanda na Sumbawanga, tena Ujenzi katika maeneo ya Songea, Makambako na Shinyanga unaendelea. Kukamilika kwa miundombinu hiyo kutaongeza uwezo wa kuhifadhi chakula kutoka tani 341,000 za sasa hadi tani 501,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya upatikanaji wa pembejeo za kilimo; kwa takribani miaka mitatu sasa, dunia

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

imekumbwa na janga hili la UVIKO-19 na nchi nyingi zikiwemo wazalishaji wakubwa wa mbolea duniani ziliweka amri ya watu wao kusalia majumbani mwao. Hali hiyo, imesababisha kusimama kwa uzalishaji na kuathiri upatikanaji wa mbolea duniani kote. Mahitaji ya mbolea hapa nchini kwa msimu wa 2021/2022 ni tani 698,260.

Hadi kufikia Februari, 2022 upatikanaji wa mbolea ulifika tani 436,452 sawa na asilimia 63 ya mahitaji na kuhamasisha matumizi ya mbolea zinazozalishwa hapa nchini na kuratibu uagizaji wa pamoja kutoka kwa wazalishaji wa nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali katika mwaka 2022/2023, itaendelea kuhamasisha uwekezaji wa ujenzi wa viwanda vya ndani vya kuzalisha mbolea, kuhimiza viwanda viliivypo kuongeza uzalishaji, kuongeza matumizi ya mbolea zinazozalishwa nchini na matumizi ya mbolea mbadala, lakini pia, Serikali itaendelea kushirikiana na sekta binafsi katika kuzalisha, kuagiza na kusambaza pembejeo kwa wakulima kote nchini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuimarisha huduma za ugani; kilimo bora na chenye tija kwa sehemu kubwa hutegemea huduma za ugani. Huduma za ugani zinahusisha utoaji wa elimu na teknolojia bora za uzalishaji wa mazao kwa wakulima, matumizi sahihi ya pembejeo, zana bora za kilimo na upatikanaji wa masoko ya mazao ya kilimo na mtaji. Kwa kutambua hilo Serikali imeendelea kuimarisha huduma za ugani nchini kwa kuhakikisha kuwa, Maafisa Ugani wanawafikia wakulima na kutoa huduma stahiki kwa wakati. Ili kutimiza azma hiyo Serikali imeshagawa pikipiki 6,704 kwa Maafisa Ugani wote nchini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sote tumeshuhudia Mama yetu mpendwa, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania siku ya tarehe 4 Aprili, 2022 akigawa pikipiki hizo kwa ajili ya Maafisa Ugani kilimo, vifaa vya kupimia afya ya udongo 3,483 kwa Halmashauri 143 na simu janja 367. Kitendo hicho kinathibitisha kuwa

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Serikali ya Awamu ya Sita inaiangalia vizuri tena kwa jicho la karibu sekta ya kilimo ili iendelee kuleta tija kwa Watanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2022/2023 Serikali itaendelea kuimarisha huduma za ugani kwa kutoa vitendea kazi zaidi kwa Maafisa Ugani Kilimo, kununua na kusambaza visanduku vya ugani, kutoa mafunzo rejea kuhusu uzalishaji bora wa mazao, matumizi ya mfumo ya M-Kilimo na kukarabati na kuanzisha Kituo cha Mawasiliano ya Kilimo kwa ajili ya mawasiliano kwa Maafisa Ugani na Wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, uzalishaji wa mazao ya kimkakati; Serikali imeendelea kufuatilia na kuimarisha uzalishaji wa mazao ya kimkakati kwa lengo la kuleta tija zaidi na manufaa kwa mkulima mmoja mmoja na kuinua Pato la Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2022/2023 Serikali itaendelea kusimamia mkakati wa kuongeza uzalishaji wa masoko ya mazao ya mkonge, pamba, kahawa, korosho, tumbaku, chikichi, chai, alizeti, zabibu, pamoja na mazao ya ufuta, choroko, mbaazi na ngano.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa mazao mengine, Serikali itaongeza uzalishaji wa chikichi na alizeti ili kuongeza mafuta ya kula. Vilevile itahamasisha uanzishaji wa mashamba mapya ya mazao yote ya kimkakati ikiwemo zao la korosho, pamba, tumbaku, kahawa na chikichi na mazao mengine, kukamilisha ujenzi wa ghala za kuhifadhi na kuanzisha kituo cha mafunzo ya usindikaji ili kutoa huduma bora kwa wakulima. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuimarisha ushirika; Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali ili kuimarisha Vyama vya Ushirika hapa nchini. Hatua hizo ni pamoja na kuwezesha upatikanaji wa vitendea kazi, kuhamasisha ushirika na kufanya kaguzi za mara kwa mara ili kuhakikisha kwamba vyama hivyo vinaendeshwa kwa mujibu wa sheria. Hadi Februari, 2022 Serikali imekagua Vyama vya Ushirika 6,013

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

ambapo ilibainika kuwa baadhi ya vyama vimekiuka taratibu za uendeshaji wa Vyama vya Ushirika hapa nchini. Kati ya hivyo, vyama 357 vilipata hati inayoridhisha, vyama 2,674 Hati yenye Shaka, vyama 1,253 Hati Isiyoridhisha na vyama 1,729 Hati Mbaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, hatua mbalimbali za kisheria zimechukuliwa dhidi ya wote waliohusika na ukiukwaji wa taratibu za uendeshaji wa Vyama vya Ushirika, ikiwemo vitendo vya wizi wa mali na fedha za ushirika. Katika kuimarisha Vyama vya Ushirika, Serikali immeanzisha Mfumo wa Kielektroniki wa Usimamizi na Ukaguzi wa Vyama vya Ushirika pamoja na kuanzisha Benki ya Taifa ya Ushirika Tanzania (*National Cooperative Bank - NCB*). (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kupitia uhamasishaji wa masoko na uwekezaji katika Vyama vya Ushirika, jumla ya tani 575,295.74 za mazao mbalimbali yenye thamani ya Shilingi Trilioni 1.52 yaliuzwa. Serikali katika mwaka wa fedha 2022/2023, itaendelea kuelimisha umma kuhusu umuhimu wa ushirika na kuimarisha mifumo ya udhibiti na ukaguzi wa Vyama vya Ushirika. Nitumie fursa hii kuwataka viongozi wote wa Vyama vya Ushirika walioomba ridhaa ya kuwaongoza wanaushirika wenzao kufuata taratibu zilizowekwa ili Wanaushirika waweze kuona tija ya uwepo wa vyama hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mnamo mwezi Desemba, 2021 Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi wa Rais wetu, iliipatia Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania mtaji wa Shilingi Bilioni 208 ikiwa ni nyongeza kwenye mtaji wa awali wa Shilingi Bilioni 60 uliowekwa na Serikali wakati wa uanzishwaji wa benki mwaka 2012. Mtaji huo wa Shilingi Bilioni 208 ni mkubwa kuwahi kuongezwa kwa mkupuo kwa taasisi ya fedha katika historia ya nchi yetu. Vile vile, Serikali kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Ufaransa (*AfD*) imetoa Shilingi Bilioni 210 kwa Benki yetu ya Kilimo ili kutoa huduma za kifedha kupitia kongani na minyororo ya thamani kwa nia ya kuleta mapinduzi ya kimkakati katika kilimo na kwa wakulima wadogo. (*Makofii*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, kufikia Februari, 2022 Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania imefanikiwa kutoa mikopo yenye thamani ya zaidi ya Shilingi Bilioni 354.64 ambayo imewanufaisha wakulima wadogo, wakulima wa kati na wakulima wakubwa wapatao 1,522,751 katika Mikoa ya Tanzania Bara na Zanzibar. Aidha, kupitia Mfuko wa Dhamana kwa wakulima wadogo imetoa jumla ya mikopo ya Shilingi Bilioni 129.39 tangu Mfuko huo ulipoanza rasmi udhamini wa mikopo mwaka 2018.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2022/2023, Serikali kupitia Benki ya Maendeleo ya Kilimo itaendelea kuwawezesha wakulima wadogo kupata mikopo ya dhamana kwa ajili ya kuboresha uzalishaji, uchakataji, uhifadhi, usafirishaji pamoja na upatikanaji wa masoko. Ni imani ya Serikali kuwa jitihada hizi zitasaidia sana kukuza uchumi, kuongeza usalama wa chakula sambamba na kupunguza umaskini wa kipato.

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ya mifugo; Serikali imeendelea kutoa elimu kuhusu ufugaji bora wa kibashara kwa wadau mbalimbali waliopo kwenye mnyororo wa thamani. Hatua hii imeongeza kiwango cha uzalishaji na usindikaji wa mazao ya mifugo kama vile nyama, maziwa na ngozi. Katika mwaka 2021/2022, uzalishaji wa maziwa umeongezeka kwa asilimia 9.67 kutoka lita Bilioni 3.1 zilizozalishwa mwaka 2020/2021 hadi kufikia lita Bilioni 3.4. Aidha, uzalishaji wa nyama zinazouzwa nje ya nchi umeongezeka kutoka tani 1,774.29 mwaka 2020/2021 hadi kufikia tani 5,362.9 zenye thamani ya dola za Marekani Milioni 22.44.

Mheshimiwa Naibu Spika, ongezeko hili limesababishwa na kukua kwa soko la nyama hususan katika nchi za Oman, Kuwait, Bahrain, Saudi Arabia, Qatar, Vietnam, Comoro na Mji wa Hong Kong. Serikali katika mwaka 2022/2023 itaimarisha huduma za ugani katika ngazi za Kata na Vijiiji, kutoa vitendea kazi zikiwemo pikipiki kwa Maafisa Ugani wa Mifugo na upatikanaji wa dawa za chanjo. Lakini Serikali

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

kupitia Wizara itaananza mashamba darasa ya malisho na tumeanza na eneo la Loliondo na Handeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha Serikali itaendelea kuboresha mazingira ya kibiashara, kuvutia uwekezaji mpya pamoja na kufanya majadiliano na wadau kutoka nchi mbalimbali ili kufungua masoko mapya ya mazao ya mifugo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ya uvuvi; Serikali katika mwaka 2021/2022 imeendelea kuboresha sekta ya uvuvi ili iweze kuchangia kikamilifu katika Pato la Taifa. Hatua zilizochukuliwa ni pamoja na kuandaa na kutekeleza mfumo shirikishi wa usimamizi wa rasilimali za uvuvi katika Mikoa ya Kanda ya Ziwa Victoria, kwa lengo la kuwa na uvuvi endelevu, kupunguza kero za wananchi, kudhibiti uvuvi na biashara haramu za mazao ya uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali katika mwaka 2022/2023 itaendelea kuimarisha miundombini wezeshi ya uvuvi ikiwemo kununua meli mbili za uvuvi, ujenzi wa Kituo cha Ukuzaaji Viumbe Maji Rubambagwe - Geita, ujenzi wa Bandari ya Uvuuvi - Kilwa Masoko Mkoani Lindi na kuimarisha usimamizi wa rasilimali katika Ukanda wa Uchumi wa Bahari na Bahari Kuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, maliasili na utalii; utalii ni sekta muhimu yenye mchango mkubwa katika Pato la Taifa. Kutokana na umuhimu huo, Serikali imeendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ya kulinda na kuhifadhi rasilimali za maliasili na malikale pamoja na kuendeleza utalii hapa nchini. Aidha, Serikali imeongeza kasi ya utangazaji utalii Kitaifa na Kimataifa, kuboresha ulinzi na usalama wa rasilimali za maliasili na malikale na kushirikisha jamii katika kutekeleza mipango ya uhifadhi wa ikolojia.

Mheshimiwa Naibu Spika, idadi ya watalii walioingia nchini iliongezeka kwa asilimia 48.6 kutoka watalii 620,867 mwaka 2020 hadi watalii 922,692 kwa mwaka 2021. Utalii wa ndani pia umeendelea kuimarika ambapo idadi ya watalii

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

wa ndani walitembelea maeneo ya hifadhi iliongezeka kutoka 562,549 mwaka 2020 hadi 788,933 mwaka 2021, ongezeko hili ni sawa na ongezeko la asilimia 40.2.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile mapato yatokanayo na watalii wa Kimataifa yaliongezeka kutoka dola za Marekani milioni 714.59 mwaka 2020 hadi dola za Marekani bilioni 1.25 mwaka 2021 sawa na ongezeko la asilimia 76.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuimarika kwa utalii nchini kumetokana na mwelekeo wa jitihada za Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, katika kuanzisha na kutekeleza Mpango wa Kitaifa wa kukabiliana na janga la UVIKO-19 hapa nchini. Hii ni pamoja na kutekeleza mkakati wa kuinua sekta ya utalii nchini na kutekeleza mpango wa chanjo ya UVIKO-19 Kitaifa. Mpango huo wa Kitaifa umeleta taswira mpya kiutalii ambapo Tanzania imekuwa ni eneo salama zaidi kutembelewa na watalii kuliko maeneo mengine. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na utekelezaji wa mipango hiyo, kumekuwa na jitihada mahsus za Mheshimiwa Rais katika kuitangaza Tanzania Kimataifa kupitia programu yake maalum ya *Royal Tour*. Kupitia programu hiyo, mtando maarufu wa habari nchini Marekani wa '*TheGrio*' umetambua juhudzi za Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan katika kuiongoza vyema sekta ya utalii nchini na kuifanya Tanzania kuwa kivutio cha kwanza cha utalii Barani Afrika kwa mwaka 2022. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande mwingine Serikali kwa kushirikiana na Wananchi inaendelea kuimarisha usimamizi wa mapori na vyanzo vya maji na maeneo ya mazalia ya Wanyama hasa eneo la Loliondo ili kulinda uhai wa ikolojia hiyo. Serikali inaimarisha huduma za jamii ikiwemo maji yatakayotumika kunyweshea mifugo, tumeshachimba visima Vinne kati ya 13 vinavyotakiwa kuchimbwa maeneo ya wananchi. Aidha, katika Kijiji cha Msomera, Wilayani Handeni Serikali inaendelea na ujenzi wa nyumba 101 kwa

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

ajili ya wananchi wanaotaka kuhamia eneo hilo kwa hiari yao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2022/2023 Serikali itaendelea kuongeza juhudini katika kulinda na kuhifadhi rasilimali za maliasili na malikale, kukuza utalii wa ndani, kuongeza kasi ya utangazaji utalii Kitaifa na Kimataifa na kuibua masoko mapya ya utalii. Aidha, Serikali itaendelea kukarabati na kuimarishe miundombinu katika maeneo ya hifadhi, kuibua na kuendezea mazao ya utalii kimkakati. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kusimamia kikamilifu sekta ya madini na kuhakikisha inakuwa na mchango mkubwa kwenye pato la Taifa. Mchango wa sekta ya madini katika kipindi cha Januari hadi Septemba umeongezeka kutoka asilimia 6.5 mwaka 2020 hadi kufikia asilimia 7.3 ya mwaka 2021. Aidha, hadi Februari, 2022, kiasi cha shilingi bilioni 406.6 za maduhuli kimekusanya sawa na asilimia 62.6 ya lengo la kukusanya shilingi bilioni 650 kwa mwaka. Mafanikio hayo ni kielelezo tosha cha kuendelea kuimarike kwa sekta hii kufuatia usimamizi thabiti unaowekwa na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kuimarishe usimamizi na kuanzisha masoko mapya ya madini na vituo vya ununuzi nchini kwa lengo la kupata takwimu sahihi za mauzo ya madini, lakini pia kuongeza ukusanyaji wa maduhuli na kusaidia wananchi wadogo kupata soko la uhakika na kupata bei stahiki kwa bidhaa za madini. Hadi Februari, 2022, jumla ya masoko ya madini 44 na vituo vidogo vya ununuzi wa madini 70 vimeanzishwa hapa nchini. Kupitia masoko na vituo hivyo kwa kipindi cha Julai, 2021 hadi Januari, 2022, mauzo ya madini yalionegezeka kwa asilimia 12.4 ikilinganishwa na kipindi kama hicho kwa mwaka 2020/2021.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhamasisha na kutangaza fursa za uwekezaji zilizopo kwenye Sekta ya Madini, Serikali iliandaa na kushiriki katika maonesho, makongamano,

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

mikutano ya kikanda na kimataifa na majukwaa mbalimbali. Kupitia hatua hizo, wawekezaji wameendelea kuiamini nchi yetu kama mahali salama na penye mazingira rafiki ya uwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2021/2022, Serikali imetoa leseni tatu za uchimbaji mkubwa sana wa madini kwa kampuni ya *Nyanzaga Mining Company Limited*, *Williamson Diamond Limited* na *Tembo Nickel Corporation Limited*. Aidha, Serikali ilitoa leseni mbili za uchimbaji wa kat i kwa kampuni za *Mahenge Resources Limited* na *Jacana Resources Limited*. Vilevile jumla ya leseni 6,382 za wachimbaji wadogo zimetolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2022/2023 Serikali itaendelea kuimarisha usimamizi wa uchimbaji mkubwa na wa kat i wa madini ili uweze kuleta tija kwa Taifa letu, kubuni na kuimarisha utekelezaji wa mipango ya kuwawezesha wachimbaji wadogo ili waweze kufanya shughuli zao kwa tija, kuimarisha na kuhimiza uanzishwaji wa masoko kwenye maeneo mbalimbali kunakofanyika shughuli za madini, kuimarisha udhibiti wa vitendo vya utoroshaji wa madini na kuhamasisha shughuli za uongezaji thamani ya madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Nishati. Dhamira ya Serikali ni kuhakikisha kwamba, kunakuwa na upatikanaji wa kutosha na wa uhakika na unafuu wa nishati ya umeme, mafuta na gesi ili kuimarisha shughuli za kiuchumi na kijamii. Katika kufanikisha dhamira hiyo, Serikali imeendelea kutekeleza miradi mikubwa ya umeme ikiwa ni pamoja na ujenzi wa mradi wa Kufua Umeme wa Julius Nyerere weny e Megawati 2,115. Mradi wa Kufua Umeme kwa Kutumia Gesi wa *Kinyerezi I - Extension* Megawati 185 na Mradi wa Kuzalisha Umeme wa Maji wa Rusumo Megawati 80. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Kufua Umeme kwa kutumia Gesi wa *Kinyerezi I - Extension* unatarajia kuongeza MW 185 katika mradi wa sasa unaozalisha MW 150 na hivyo kufanya kituo hicho kuzalisha jumla ya MW 335.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Utekelezaji wa mradi huu, umefikia asilimia 86 na unatarajiwa kukamilika Novemba, 2022. Vilevile, Mradi wa Kuzalisha Umeme wa Maji wa Rusumo, MW 80, unaohusisha ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme kwa kutumia maporomoko ya maji ya Mto Kagera, nao umefikia asilimia 86.7. Kukamilika kwa miradi hii na mingine mgingi itakayoanza kutekelezwa kutachochaea kasi ya uzalishaji na usambazaji wa umeme vijiji mpaka mijini na hivyo kuongeza hali ya upatikanaji wa umeme hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea na uimarishaji wa njia za kusafirisha umeme ili kuhakikisha kuwa maeneo yote ya nchi yanafikiwa na umeme nafuu na wa uhakika ikiwa ni pamoja na kuiunganisha kwenye Gridi ya Taifa mikoa minne iliyosalia. Katika mwaka wa fedha 2021/2022, Serikali imeendelea na ujenzi wa njia za kusafirisha umeme za msongo wa KV 400 Iringa - Singida mpaka Shinyanga, njia ya kusafirisha umeme KV 400 kutoka Singida - Arusha mpaka Namanga, njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa KV 220 kutoka Geita mpaka Nyakanazi, njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa KV 220 kutoka Rusumo mpaka Nyakanazi na njia ya kusafirisha umeme msongo wa KV 400 kutoka Rufiji - Chalinze-Kinyerezi hadi hapa Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea na utekelezaji wa mradi wa Kusambaza Umeme Vijiini Awamu ya Tatu Mzunguko wa Pili kwa maana ya *REA III Round 2*, ambapo lengo lake ni kuunganisha vijiji vyote vya Tanzania Bara. Kutokana na kazi kubwa ya usambazaji wa umeme vijiji uliofanyika, kiwango cha upatikanaji wa umeme maeneo ya vijiji kimefikia asilimia 69.8. Katika mwaka 2022/2023, Serikali itaendelea kutunisha Mfuko wa *REA* ili kuhakikisha vijiji vilivyosalia pamoja na taasisi zinazotoa huduma za kijamii vijiji zinapata umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea na shughuli za utafutaji wa mafuta na gesi nchini ambapo hadi Februari, 2022, kiasi cha futi za ujazo triliioni 57.54 za gesi asilia kiligundulika katika vitalu vya *Mnazi Bay* Kaskazini na Eyasi, Wembere. Aidha, matumizi ya gesi asilia nchini yameendelea

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

kuhamashishwa ambapo magari zaidi ya 750 yameunganishwa na mfumo wa matumizi ya gesi asilia na ujenzi wa miundombinu ya kuunganisha nyumba 300 za Mtwara na nyumba 506 za Dar es Salaam unaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2022/2023, Serikali itaendelea na shughuli za utafutaji, ugunduzi na kuhamasisha matumizi ya gesi asilia ili kuhakikisha kwamba, sekta hiyo inakuwa na mchango mkubwa katika pato la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ardhi ni rasilimali muhimu katika kukuza uchumi na kuondoa umaskini. Ili nchi yetu iweze kunufaika na rasilimali hiyo muhimu, ni vema kuwa na mipango endelevu ya matumizi bora ya ardhi sambamba na upimaji wa ardhi hiyo. Kwa kutambua umuhimu huo, Serikali imewezesha uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji 217 katika Halmashauri 29 na hivyo kuwa na vijiji 2,556 vyenye mpango wa matumizi ya ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, imeendelea kuboresha makazi katika maeneo yasiyopangwa ambapo hadi Machi, 2022 makazi 555,285 yalirasimishwa na kufanya idadi ya makazi yaliyorasimishwa nchini kuwa 2,094,879. Vilevile, Serikali imeandaa mipango ya matumizi ya ardhi katika maeneo ya miradi ya kimkakati kwa lengo la kulinda ikolojia na kuwezesha matumizi bora ya ardhi yasiyoleta athari katika mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mipango hiyo, Serikali inaendelea na zoezi la kubadilisha ramani na michoro ya mipango miji kutoka mfumo wa analogia kwenda mfumo wa dijitali. Hadi Machi, 2022, ramani za viwanja 598,000 katika halmashauri 38 tayari zimewekwa katika mfumo wa kidijitali. Matumizi ya mfumo huo yatarahisisha usimamizi, utoaji wa huduma za ardhi na ukusanyaji wa mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, miundombinu ya usafiri na usafirishaji ni kichocheo muhimu katika ukuaji wa uchumi. Kwa msingi huo, Serikali imeendelea kuimarisha miundombinu na

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

huduma za usafirishaji ili kupunguza gharama za uzalishaji na kufanikisha maendeleo ya nchi kwa haraka sambamba na kutumia fursa ya klijografia kuinua uchumi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2021/2022, Serikali imejenga jumla ya kilomita 251.9 za barabara kwa kiwango cha lami ambazo zimehusisha barabara kuu, barabara za mikoa na wilaya. Lengo ni kuhakikisha kuwa Makao Makuu ya mikoa yote na nchi jirani yanaunganishwa kwa mtandao wa lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeanza awamu ya pili ya ujenzi wa barabara na miundombinu ya mabasi yaendayo haraka katika Jiji la Dar es Salaam na ujenzi wa barabara za mchepuo (*bypass*) katika Jiji la Mbeya, Dodoma na Mji wa Iringa. Aidha, ujenzi wa barabara za mchepuo katika Jiji la Mwanza na Arusha umekamilika. Vilevile, Serikali inaendelea na ujenzi wa barabara ya njia nane kutoka Kimara hadi Kibaha yenye urefu wa kilomita 19.2 ambayo imekamilika kwa asilimia 86 baada ya nyongeza ya kazi za mkataba na barabara za juu katika eneo la Keko na Kurasini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie viwanja vya ndege na usafiri wa anga. Usafiri wa anga ni muhimu katika kuongeza tija na ufanisi katika sekta zinazotegemea usafiri huo ili kuchochaea ukuaji wa uchumi. Kwa kutambua umuhimu huo, Serikali imeendelea kuimarisha usafiri wa anga kwa kukarabati viwanja vya ndege, ujenzi wa viwanja vipya vya ndege pamoja na ununuzi wa ndege mpya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali katika mwaka wa fedha 2021/2022 imeendelea kulimariisha Shirika letu la Ndege (*ATCL*) ili liweze kutoa huduma bora za usafiri wa anga ndani na nje ya nchi. Hadi Februari, 2022, Serikali imefanya malipo ya awali ya ununuzi wa ndege tano mpya. Kati ya hizo, ndege moja ni aina ya *Boeing 787-8 Dreamliner*, ndege mbili aina ya *Boeing 737-9*, ndege moja aina ya *De Havilland Dash 8-Q400* na ndege moja ya mizigo aina ya *Boeing 767-*

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

300F. Kukamilika kwa ununuzi wa ndege hizo, kutaiwezesha Serikali kuwa na jumla ya ndege mpya 16. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na kuendelea kuimarika kwa Shirika letu la Ndege, hivi karibuni limefanikiwa kuanza safari katika vituo vya Arusha, Geita, na kurejesha safari za Mtwara na Songea. Aidha, limerudisha safari za kikanda katika vituo vya Bujumbura, Entebbe, Harare, Lusaka na Hahaya pamoja na kuanzisha vituo vipyta vitatu katika Miji ya Lubumbashi, Nairobi na Ndola. Vilevile, Shirika limefanikiwa kurejesha safari ya kimataifa kwenda Mumbai, India, pamoja na kuanzisha safari za mizigo kuelekea Guangzhou nchini China. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu reli pamoja na ujenzi wa reli ya kisasa (*SGR*); katika mwaka 2021/2022, Serikali imeendelea na ukarabati wa njia ya Reli ya Kati kutoka Dar es Salaam hadi Mwanza na Kigoma sambamba na ununuzi wa vichwa vya treni vitatu, mabehewa 44 ya mizigo na mtambo wa kupima ubora wa njia ya reli. Katika mwaka 2022/2023, kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na kuendelea kutafuta mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa njia ya reli kwa kipande cha Tabora - Isaka Kilometra 165 na ujenzi wa njia za reli kwa vipande vya Uvinza - Musongati - Gitega (Burundi) yenye urefu wa Kilometra 282 na Kaliua - Mpanda - Karema Kilometra 321 kwa kiwango cha *SGR*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatekeleza mpango wa uboreshaji wa bandari nchini kwa kufanya upanuzi na kuimarisha miundombinu ya Bandari za Dar es Salaam, Tanga na Mtwara. Katika mwaka 2021/2022, Serikali imekamilisha ukarabati wa gati Na. 1 - 7 kwenye Bandari ya Dar es Salaam kwa kuongeza kina hadi kufikia mita 14.5. Aidha, gati maalum la kuhudumia meli za magari limeanza kutumika na kazi ya kuchimba na kupanua lango la kuingilia meli bandarini na sehemu ya kugeuzia meli inaendelea na ujenzi wake umefikia asilimia 15.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, Serikali imeendelea kuboresha Bandari za Tanga na Mtwara ambapo kazi ya

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

uongezaji wa kina cha lango la kuingilia meli kutoka mita nne hadi mita 13 pamoja na kuweka vifaa vya kuongozea meli katika Bandari ya Tanga umekamilika. Utekelezaji wa awamu ya pili ya uboreshaji wa Bandari ya Tanga umefikia asilimia 25.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2022/2023, Serikali itanunua vivuko vipyta vitano vitakavyotoa huduma katika maeneo ya Kisorya - Rugezi, Ijinga - Kahangala, Bwiro - Bukondo, Nyakarilo - Kome, Nyamisati - Mafia na kivuko kipyta cha Magogoni - Kigamboni pamoja na kuendelea na ujenzi na ukarabati wa miundombinu muhimu ya usafiri na usafirishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kuimarisha miundombinu ya mawasiliano kwa kupanua mtandao na mkongo wa Taifa wa mawasiliano nchini na katika nchi jirani ili kurahisisha upatikanaji wa huduma za kijamii na kiuchumi kwa njia ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA).

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2021/2022, Serikali imejenga kilomita 409 za Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano na kufikia urefu wa kilomita 8,319 sawa na asilimia 55 ya lengo la kufikia kilomita 15,000 ifikapo mwaka 2025. Aidha, Serikali imefanikiwa kuunganisha Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano na nchi ya Msumbiji kutokea eneo la Mangaka hadi Mtambaswala.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua hii imefanya nchi zilizounganishwa na Mkongo wa Taifa kufikia saba ambazo ni Burundi, Kenya, Rwanda, Uganda, Msumbiji, Malawi na Zambia. Lengo la Serikali ni kuhakikisha kuwa nchi ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo inaunganishwa kuititia Ziwa Tanganyika na hivyo kufanya nchi yetu kuwa kitovu cha mawasiliano katika ukanda wa maziwa makuu kuelekea uchumi wa kidijitali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua umuhimu wa elimu kama nyenzo imara kwa maendeleo ya kiuchumi

na kijamii, Serikali imeendelea kuboresha na kuimarisha elimumsingi, ufundi na elimu ya juu. Katika mwaka 2021/2022, Serikali imeendelea kutekeleza mpango wa Elimumsingi Bila Ada kwa mafanikio makubwa ambapo hadi kufikia Februari, 2022, shilingi bilioni 192.4 zimetumika kutekeleza mpango huo katika shule za msingi na sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, kupitia Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano Dhidi ya UVIKO-19, Serikali imetumia shilingi bilioni 304 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vyta madarasa 12,000 vyta shule za sekondari, vyumba vyta madarasa 3,000 vyta vituo shikizi na ujenzi wa mabweni 50.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kuimarisha Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi ambapo katika mwaka 2021/2022, imekamilisha ujenzi na ukarabati wa vyuo 14 vyta Maendeleo ya Wananchi na ujenzi wa vyuo vipyta 25 vyta ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (*VETA*) vyta Wilaya. Vilevile, Serikali imeendelea na ujenzi wa vyuo vipyta vinne vyta ufundi na mafunzo ya Ufundi Stadi (*VETA*) vyta Mikoa ya Njombe, Simiyu, Geita na Rukwa. Aidha, ukarabati na ujenzi wa vyuo vitatu vyta ualimu vyta Sumbawanga (Rukwa), Dakawa na Mhonda (Morogoro) unaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kuimarisha upatikanaji wa elimu ya juu kwa kuongeza fedha za mikopo kwa ajili ya wanafunzi ambapo katika mwaka wa fedha 2021/2022, jumla ya shilingi bilioni 570 zimetumika ikililinganishwa na shilingi bilioni 464 zilizotumika mwaka 2020/2021. Vilevile, idadi ya wanufaika imeongezeka kutoka 149,398 mwaka 2020/2021 hadi wanafunzi 177,605 mwaka 2021/2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa huduma za maji, Serikali imeendelea kutoa kipaumbele katika kusimamia na kuendeleza rasilimali za maji ikiwa ni pamoja na kuhakikisha upatikanaji wa maji pamoja na usafi wa mazingira vijiji na mijini.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ina dhamira ya dhati kuhakikisha upatikanaji wa huduma ya maji mijini na vijiji ni unafika zaidi ya wastani wa asilimia 95 na 85 mtawalia ifikapo mwaka 2025. Hadi Februari, 2022, hali ya upatikanaji wa maji safi maeneo ya mijini imefikia asilimia 86. Aidha, katika miradi 114 inayotekelawa katika maeneo mbalimbali, miradi 40 imekamilika na kuanza kutoa huduma kwa wananchi wapatao 1,978,730 na miradi 74 ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa maeneo ya vijiji ni, upatikanaji wa maji umefikia asilimia 72.3. Aidha, utekelezaji wa miradi 265 umekamilika na imeanza kutoa huduma ya maji safi kwa wananchi wapatao 1,336,856. Katika mwaka 2022/2023, Serikali itaendelea kutekeleza miradi ya maji katika miji 28 pamoja na mradi wa kutoa maji kutoka Ziwa Victoria hadi Dodoma. Aidha, Serikali itaendelea kuimarisha usimamizi na utunzaji wa vyanzo vya maji ili kuhakikisha upatikanaji endelevu wa maji safi unakuwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kuboresha upatikanaji wa huduma za afya nchini kwa kujenga vituo vya kutoa huduma za afya pamoja na upatikanaji wa dawa na vifaa tiba. Katika mwaka 2021/2022, Serikali imekamilisha ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Kusini Mtwara na Hospitali ya Rufaa ya Kanda Chato ambapo tayari zimeanza kutoa huduma kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, upanuzi wa ukarabati wa majengo katika hospitali za Rufaa za Mikoa 13 umefanyika katika Hospitali za Mwananyamala, Iringa, Mawenzi (Kilimanjaro), Ligula (Mtwara), Bombo (Tanga), Manyara, Maweni (Kigoma), Mbeya, Sekou Toure (Mwanza), Songea, Sumbawanga (Rukwa), Kitete (Tabora) na Tumbi (Kibaha Pwani). Ukarabati na upanuzi huo umewezesha kupatikana kwa huduma za kibingwa ambazo awali ziliikuwa hazipatikani katika hospitali hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kuimarisha upatikanaji wa huduma za kibingwa na ubingwa

bobezi nchini. Huduma hizo ni pamoja na upandikizaji wa uloto (*bone 52 marrow transplant*) katika Hospitali ya Taifa Muhimbili, upasuaji wa kuondoa uvimbe kwenye sakafu ya ubongo kuititia tundu la pua katika Taasisi ya Mifupa – *MOI* na upasuaji mgumu wa moyo kwa kutumia tundu dogo katika Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete. Hatua hizo zimesaidia sana kuwapunguzia gharama Watanzania na adha kwa wananchi na Serikali kwa kutafuta huduma hizo nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango wa Maendeleo na Ustawi wa Taifa na Mapambano Dhidi ya UVIKO-19; Serikali imeendelea kudhibiti maambukizi ya ugonjwa huo kwa kuanzisha rasmi utekelezaji wa afua ya chanjo ya UVIKO 19 na kuratibu upatikanaji wa chanjo hizo. Hadi tarehe 28 Februari, 2022, jumla ya dozi 9,845,774 zimepokelewa nchini, dozi 5,426,840 sawa na asilimia 55 zimesambazwa mikoani na watu 2,664,373 waliochanjwa dozi kamili imekamilika. Nitoe wito kwa Watanzania wote kuendelea kupata chanjo hizo ambazo ni za bure na zinapatikana katika maeneo yote nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kupunguza athari za UVIKO -19 nchini, Serikali ilipatiwa mkopo wa shilingi triliioni 1.3 na Shirika la Fedha Duniani kwa ajili ya kutekeleza Mpango wa Maendeleo na Ustawi wa Taifa na Mapambano Dhidi ya UVIKO-19. Sekta zilizonufaika na Mpango huo ni sekta ya maji imepata mgao wa (shilingi bilioni 139.4), sekta ya elimu (shilingi bilioni 368.9), sekta ya afya (shilingi bilioni 466.9), sekta ya utalii (shilingi bilioni 90.2), jamii inayoishi kwenye mazingira magumu (shilingi bilioni 5.5), na kundi la vijana, wanawake na watu wenye ulemavu (shilingi bilioni 5). Aidha, shilingi bilioni 231 zilielekezwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na shilingi bilioni 5.0 kwa ajili ya shughuli mbalimbali ikiwemo uratibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Huduma kwa Makundi Maalum; Serikali imeendelea kuboresha huduma kwa watu wenye ulemavu kwa kutenga kiasi cha shilingi bilioni 3.46 kwa ajili ya ukarabati wa vyuo vya watu wenye ulemavu nchini. Katika mwaka 2021/2022 ukarabati wa Vyuo vya Ufundis Stadi na Marekebisho kwa Watu wenye Ulemavu vya Luanzari

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

(Tabora) na Masiwani (Tanga) umekamilika. Aidha, ukarabati wa vyuo vinne katika Mikoa ya Dar es Salaam, Mtwara, Singida na Tabora unaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imezindua pia Mwongozo wa Utambuzi wa Mapema na Afua Stahiki kwa Watoto wenye Ulemavu wa Mwaka 2021. Mwongozo huu utawezesha utambuzi wa mapema wa watoto wenye ulemavu ili kupunguza makali ya ulemavu ukubwani. Vilevile, Serikaliimeendelea kuzisimamia mamlaka za ajira kuhakikisha kwamba watu wenye ulemavu wanapata fursa ya ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2022/2023, Serikali itaifanya maboresho ya Sera ya Taifa ya Huduma na Maendeleo ya Watu Wenye Ulemavu, kuhakikisha upatikanaji wa vifaa saidizi na kuendelea kuhamasisha jamii kuondokana na unyanyapaa dhidi ya watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kujenga kizazi chenye usawa wa kijinsia, nchi yetu inatekeleza eneo la pili kati ya maeneo sita ya ajenda ya haki za wanawake, usawa wa kijinsia na malengo ya Jukwaa la Kimataifa la Kizazi Chenye Usawa la Umoja wa Mataifa linalohusu haki na usawa wa kiuchumi kwa wanawake. Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mnamo Desemba, 2021 alizindua Kamati ya Ushauri ya Kitaifa ya Utekelezaji wa Ahadi za Nchi kuhusu Kizazi Chenye Usawa ili kuhakikisha kwamba eneo hilo linaratibiwa kikamilifu. Aidha, Tanzania imeungana na mataifa mengine katika kampeni ya siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia sambamba na maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe pongezi nyingi sana kwa Rais wetu kwa kusimamia vema masuala ya usawa wa kijinsia. Kutokana na jitihada zake katika kuimarisha na kutoa kipaumbele katika masuala ya usawa wa kijinsia nchini, aliombwa na akaridhia kuwa kinara wa Jukwaa la Kimataifa la Kizazi Chenye Usawa la Umoja wa Mataifa linalohusu haki na usawa wa kiuchumi kwa wanawake. Hii imedhihirisha kwamba dunia imetambua kazi njema inayofanywa na

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

jemedari wetu, mama yetu mpendwa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kutekeleza azma yake ya kujenga mazingira bora kwa kundi maalum la wafanyabiashara wadogo maarufu kama Wamachinga. Katika mwaka 2021/2022, Serikali kuitia Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano Dhidi ya UVICO-19 imetoa shilingi bilioni 5.0 kwa ajili ya kuboresha miudombinu ya kufanya biashara kwa 56 wafanyabiashara wadogo katika Halmashauri 11 za Dodoma, Mwanza, Arusha, Tanga, Mbeya, Dar es Salaam, lakini pia Dar es Salaam eneo la Kinondoni, Temeke, Ubungo, lakini Mkoani Morogoro na Mji wa Tunduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2022/2023, Serikali itaendelea kutekeleza afua mbalimbali za kuimarisha ustawi wa makundi maalum ikiwa ni pamoja na kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake, watoto na wazee; kuratibu wafanyabiashara wadogo ili kuboresha mazingira ya biashara na kuimarisha uwezeshaji wanawake kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ulinzi na Usalama; hali ya ulinzi na usalama katika nchi yetu imeendelea kuwa shwari kutokana na kazi kubwa inayofanywa na vyombo vyetu vya ulinzi na usalama katika kulinda mipaka yetu pamoja na usalama wa raia na mali zao. Katika kuhakikisha kwamba Taifa letu lina usalama wa kutosha na kuchangia usalama wa Mataifa mengine, Jeshi letu limeendelea kushirikiana na vyombo vingine vya ulinzi na usalama vya Umoja wa Mataifa, Umoja wa Afrika na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika katika operesheni mbalimbali za ulinzi wa amani. Katika mwaka 2021/2022, nchi yetu imepeleka vikosi, waangalizi wa kijeshi, wanadhimu na makamanda katika nchi za Lebanon, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Jamhuri ya Afrika ya Kati na Msumbiji. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi letu la Kujenga Taifa limeendelea kushiriki katika shughuli mbalimbali za kiuchumi

hususan ujenzi, uendeshaji wa viwanda, ufanyaji tafiti, uhawilishaji wa teknolojia pamoja na kushiriki katika kandarasi mbalimbali kupitia Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Kujenga Taifa (SUMAJKT). Katika mwaka 2021/2022, SUMAJKT ilishiriki kikamilifu katika ujenzi unaoendelea wa majengo ya Ofisi za Wizara na Taasisi zilizopo Mji wa Serikali - Mtumba Mkoani Dodoma. Aidha, kupitia mradi huo na miradi mingine Shirika limefanikiwa kuzalisha ajira zaidi ya 9,341 kwa vijana ambapo kati ya ajira hizo za kudumu ni 145 na za muda ni 9,196. Kupitia ushiriki wa JKT kwenye miradi hiyo, Serikali imepunguza gharama za uendeshaji wa mafunzo ya vijana wa mujibu wa Sheria na wa kujitolea kwa kushiriki katika shughuli za ujenzi, viwanda, kilimo na mifugo, ulinzi na mradi wa matrekta na zana za kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Masuala ya Kazi na Wafanyakazi; Serikali Imeendelea kusimamia utekelezaji wa sheria na viwango vya kazi kwa kufanya kaguzi ili kuhakikisha waajiri wanazingatia mikataba ya ajira, saa za kazi, ujira kwa lengo la kupunguza migororo na kuongeza tija. Hadi Februari, 2022, jumla ya kaguzi 3,629 za viwango vya kazi zillifanyika sawa na asilimia 76 ya kaguzi 4,800 zilizopangwa kufanyika. Aidha, kaguzi 96,693 za afya na usalama mahali pa kazi zillifanyika ambapo kumekuwa na ongezeko la upimaji afya mahali pa kazi kutoka Wafanyakazi 125,616 hadi Wafanyakazi 169,735. Kufuatia kaguzi hizo, waajiri 2,114 waliobainika kukiuka Sheria za kazi walichukuliwa hatua mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Rais wetu imeendelea kutekeleza kwa vitendo azma ya kumarisha mazingira na kuvutia uwekezaji hapa nchini. Katika mwaka 2021/2022, Serikali imekamilisha Mfumo wa Kielektroniki wa Utoaji wa Vibali vya Kazi kwa Wageni na Wawekezaji. Mfumo huu umepunguza muda wa kushughulikia maombi ya vibali vya kazi kutoka siku za kazi 14 hadi saba na kupunguza hatua za uchakataji wa kibali kutoka hatua 33 hadi saba. Ni imani ya Serikali kuwa hatua zote hizi muhimu zinazofanyika zitapunguza malalamiko ya muda mrefu ya wadau na hivyo kurahisisha ajira za raia wa kigeni na shughuli za uwekezaji.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2022/2023, Serikali itaendelea kuimarisha usimamizi na utekelezaji wa Sheria za kazi na uratibu wa ajira za wageni nchini kwa kufanya kaguzi katika maeneo ya kazi na kutoa elimu na ushauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, hifadhi ya jamii; sekta ya hifadhi ya jamii imekuwa na mchango mkubwa kwenye uchumi wetu pamoja na ustawi kwa wananchi. Katika mwaka 2021/2022, Serikali iliridhia kulipa deni la shilingi triliioni 2.17 katika Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (*PSSSF*) ambazo ni stahili ya mafao kwa wanachama waliorithiwa kutoka uliokuwa Mfuko wa *PSPF* mwaka 1999.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (*PSSSF*) umelipa mafao kwa wanufaika, wastaafu na wategemezi wapatao 32,467 yenye thamani ya shilingi triliioni 1.05. Aidha, Mfuko umelipa kiasi cha shilingi bilioni 352.51 ikiwa ni pensheni ya kila mwezi kiasi ambacho ni sawa na wastani wa shilingi bilioni 58.75 kila mwezi kwa wastaafu 148,866.

Vilevile Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (*NSSF*) umelipa mafao kwa wanufaika, wastaafu na wategemezi wapatao 98,202 yenye thamani ya shilingi bilioni 363.7. Pia, Mfuko umelipa kiasi cha shilingi bilioni 64.9 ikiwa ni pensheni ya kila mwezi kwa wastaafu 24,881.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kujenga mazingira wezeshi kwa waajiri na kupunguza gharama za uendeshaji, Serikali kuititia Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi imepunguza kiwango cha uchangiaji kwa waajiri wa sekta binafsi kutoka asilimia 1.0 hadi asilimia 0.6. Uamuzi wa kupunguza kiwango hicho cha uchangiaji, umetokana na utekelezaji wa maelekezo ya Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, kuhusu taasisi za Serikali kuhakikisha kwamba zinaweka mazingira bora ya ufanyaji biashara na uwekezaji nchini ili kukuza uchumi wa nchi na kulinda rasilimali watu.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, uwezeshaji wananchi kiuchumi; Serikali imeendelea kutekeleza azma ya kuwawezesha wananchi kiuchumi kwa kuanzisha vituo maalum vya uwezeshaji wananchi kiuchumi, utoaji wa mikopo yenye masharti nafuu kwa vikundi mbalimbali na kutekeleza mpango wa kunusuru kaya maskini. Hadi Februari, 2022, Serikali kupitia Mifuko ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi imewezesha utoaji wa mikopo ya masharti nafuu yenye thamani ya shilingi bilioni 631 kwa wanufaika 1,194,155. Aidha, imeanzisha vituo 17 vya uwezeshaji wananchi kiuchumi katika Mikoa ya Shinyanga, Geita, Singida, Rukwa, Kigoma na Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea na utekelezaji wa kipindi cha pili cha Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini katika Awamu ya Tatu ya TASAF kwa Tanzania Bara na Zanzibar. Kwa mwaka 2021/2022, ruzuku ya shilingi bilioni 117.91 ilihawilishwa kwa kaya 1,279,325 zilizokidhi vigezo vya kuingia katika kipindi cha pili cha mpango kutoka halmashauri 184 kwa Tanzania Bara na Zanzibar. Aidha, Serikali imeendelea kutenga asilimia 10 ya makusanyo ya halmashauri kwa ajili ya uwezeshaji wa wanawake, vijana na wenye ulemavu. Hadi Desemba, 2021, halmashauri zilitenga jumla ya bilioni 35.7 kwa ajili ya uwezeshaji wa wanawake, vijana na wenye ulemavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ukuzaji wa Fursa za Ajira na Ujuzi; katika mwaka 2021/2022, Serikali imechukua hatua za makusudi hususan utekelezaji wa miradi ya kielelezo, ujenzi wa viwanda, sambamba na kuimarisha sekta binafsi kwa ajili ya kuongeza fursa za ajira na ujuzi kwa Watanzania. Kutokana na juhudhi hizo, idadi ya ajira (kujajiri na kuajiriwa) zilizozalishwa ni 584,333.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imefanya utafiti wa hali ya nguvukazi nchini ili kupata viashiria muhimu vitakavyotumika katika kuhuisha, kutunga, kufuatilia na kutathmini sera, mikakati na programu za soko la ajira nchini. Utafiti huo umeonesha kwamba kiwango cha ukosefu wa ajira nchini kimepungua kutoka asilimia 10.3 mwaka 2014 hadi

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

asilimia 9.0 mwaka 2021. Aidha, nguvukazi ya vijana ni watu milioni 14.2 sawa na asilimia 55 ya nguvukazi yote nchini. Vijana milioni 12.5 sawa na asilimia 87.8 ya nguvukazi ya vijana nchini wameajiriwa au kujajiri. Sekta ya kilimo imeendelea kuongoza kwa kutoa zaidi ya asilimia 63 ya ajira kwa vijana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia utekelezaji wa Programu ya Kitaifa ya Kukuza Ujuzi Nchini, vijana 22,899 wamepatiwa ujuzi unaowawezesha kujajiri au kuajiriwa. Kati ya hao, vijana 14,440 wakiwemo vijana wenye ulemavu 349 wamepatiwa mafunzo ya uanagenzi katika fani za ufundi stadi katika vyuo na taasisi 72 nchini. Vijana 3,600 wamewezeshwa kupata mafunzo ya kilimo cha kisasa kwa kutumia teknolojia ya kitalu nyumba na vijana 2,644 wamepewa mafunzo ya kurasimishiwa ujuzi walioupata kupitia mfumo usio rasmi. Vilevile, Serikali imewezesha wahitimu 2,215 kupata mafunzo ya uzoefu kazini katika taasisi binafsi na umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Masuala Mtambuka; nianze na Sensa ya Watu na Makazi. Sensa ya Watu na Makazi ni muhimu katika kupanga na kutekeleza mipango ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii kwa Taifa letu. Hivyo, ifikapo Agosti mwaka huu nchi yetu itaendesha zoezi la sensa ya watu na makazi lenye lengo la kukusanya, kuchakata, kuchambua na kusambaza taarifa za kidemografia, lakini pia kiuchumi, mazingira na kijamii za watu wote na makazi yao katika nchi kwa kipindi maalum.

Mheshimiwa Naibu Spika, sensa ya mwaka huu ni ya kipekee kwa kuwa imeunganishwa na mazoezi mawili makubwa ya kitaifa ambayo ni Sensa ya Anwani za Makazi na Sensa ya Majengo.

Aidha, sensa ya majoribio iliyofanyika katika mikoa 13 ya Tanzania Bara na Zanzibar kufikia Agosti, 2021 imekamilika kwa ufanisi wa hali ya juu pamoja na mfumo wa kuchakata takwimu husika. Hii ni kwa sababu sensa ya mwaka 2022 ni ya kidijitali katika hatua zote za matayarisho, kuhesabu na kuchapisha takwimu zenyewe.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla, hadi tarehe 18 Machi, 2022, maandalizi ya Sensa ya Watu na Makazi yamefikia zaidi ya asilimia 76. Naomba viongozi wote tusaidiane kuhamasisha na kusimamia utekelezaji wa zoezi la Sensa katika maeneo yetu. Aidha, nitoe wito kwa Viongozi wa Dini kuwaelimisha waumini wao kuhusu umuhimu wa kuhesabiwa. Vilevile, niwaombe wananchi wote washiriki katika zoezi la Sensa ya Watu na Makazi kwa kutoa ushirikiano na taarifa sahihi kwa Makarani wa Sensa na Wasimamizi watakaotembelea kwenye kaya zetu. Niwahakikishie wananchi wote, kuwa taarifa zote zinazokusanywa wakati wa sensa ni siri na zitatumika kwa shughuli za kitakwimu tu. Takwimu hizo hazina uhusiano na dini, kodi, siasa, kabilia au mambo mengine kama hayo ambayo hayakukusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Vita Dhidi ya Rushwa; Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais wetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan inaendelea kupambana na vitendo vya rushwa na ufisadi. Hadi Februari, 2022, kesi 715 zikiwemo kesi mpya 204 zimeendeshwa katika mahakama mbalimbali. Kesi 287 ziliamuliwa mahakamani na watuhumiwa 155 walikutwa na hatia.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Shilingi Bilioni 1.39 ziliokolewa kutokana na operesheni za uchunguzi zilizofanyika katika maeneo mbalimbali nchini. Vilevile, katika kuhakikisha miradi inayotekelawa inalingana na thamani ya fedha, ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo 370 yenye thamani ya Shilingi Trilioni 4.6 umefanyika katika sekta za afya, maji, fedha, elimu, kilimo, ujenzi na viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, mikakati iliyotekelawa na Serikali katika kupambana na rushwa imeleta nidhamu, uadilifu na uwajibikaji na kuilettea sifa nchi yetu nzuri kimataifa. Kwa mujibu wa Taarifa za *Transparency International* ya mwaka 2021, Tanzania kwa kuititia kiashiria cha *Corruption Perception Index* imeendelea kufanya kazi vizuri kwa kushika ya 87 kati ya nchi 180 ikiwa imepata nafasi ya Saba (7) ikilinganishwa na nafasi ya 94 kwa mwaka 2020. Aidha, katika mwaka 2022/2023 Serikali itaendeleza mapambano dhidi ya

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

rushwa na ujisadi kwa kuweka kipaumbele kwenye utoji wa elimu kwa umma kuhusu madhara ya vitendo hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapambano dhidi ya UKIMWI; katika mwaka 2021/2022, Serikali imeweka jitihada za kuendelea kupunguza maambukizi mapya, vifo, unyanyapaa na kuimarisha huduma za msingi kwa WAVIU. Kwa mujibu wa takwimu zilizopo hadi Desemba 2020, idadi ya watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI nchini imefika milioni 1.7. Takwimu zinaonesha maambukizi mapya ya VVU kwa wenyе umri kuanzia miaka 15 na zaidi yameshuka kutoka watu 110,000 mwaka 2010 hadi 68,000 mwaka 2020. Idadi ya vifo vitokanavyo na UKIMWI vimepungua kwa asilimia 50 kutoka vifo 64,000 mwaka 2010 hadi 32,000 mwaka 2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, idadi ya WAVIU wanaopata dawa za kufubaza VVU imeongezeka kutoka asilimia 95 mwaka 2016 hadi asilimia 98.3 mwaka 2020, nitoe wito kwa Watanzania wenzangu hususani wanaume tujitokeze kupima ili tuchukue hatua za mapema kutokana na hali zetu. Katika mwaka 2022/2023 Serikali kwa kushirikiana na wadau itaendelea kutekeleza programu mbalimbali ili kuzuia maambukizi mapya ya VVU kwa makundi yote ili kuwezesha nchi kufikia lengo la Kimataifa la kutokomeza UKIMWI ifikapo mwaka 2030. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mapambano dhidi ya dawa za kulevyia; Serikali imeendelea kupambana na dawa za kulevyia kwa kutoa elimu kwa umma kuhusu madhara ya matumizi ya dawa hizo. Hadi Februari mwaka 2022, jumla ya watuhumiwa 11,716 walikamatwa na kilo 35,227.25 za dawa za kulevyia zikiwemo kilogramu 1,124.52 za *heroin*, gramu 811.3 za *cocaine*, tani 22.74 za bangi, tani 10.93 za mirungi na kemikali bashirifu zaidi ya kilogramu 432. Aidha, ekari 185 za bangi na ekari 10 za mirungi zilitketezwa katika maeneo mbalimbali nchini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeimarisha huduma za matibabu kwa watumiaji wa dawa za kulevyia kwa kuongeza idadi ya kliniki zinazotoa huduma kwa waathirika

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

wa dawa za kulevya kutoka tisa mwaka 2020/2021 hadi kliniki 15 zinazohudumia waathirika zaidi ya 10,600 mwaka 2021/2022. Licha ya hayo, Serikali kupitia programu ya kukuza ujuzi imewezesha Waraibu wa Dawa za Kulevya waliopata nafuu wapatao 200 kupata mafunzo ya ujuzi kupitia vyuo nya VETA na SIDO. Nitoe wito kwa wadau wote mkiwemo Waheshimiwa Wabunge wenzangu, asasi za kiraia, viongozi wa dini, vyombo nya habari na jamii nzima kushirikiana na Serikali kutoa elimu kuhusu madhara ya dawa za kulevya. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, uratibu wa masuala ya lishe; maendeleo ya Taifa yanahitaji uwepo wa nguvu kazi yenye afya njema na inayopata lishe bora ili kuimarisha uwezo wa kufanya kazi. Serikali imeendelea kutekeleza mikakati kuhusu lishe ukiwemo Mpango Jumuishi wa Kitaifa wa Masuala ya Lishe wa mwaka 2016/2017 hadi mwaka 2020/2021. Mafanikio yaliyopatikana katika kipindi hicho ni pamoja na:-

Kupunguza udumavu kutoka asilimia 34.7 hadi asilimia 31.8; kupunguza kiwango cha ukondefu kutoka asilimia 3.8 hadi asilimia 3.5, kupunguza upungufu wa wekundu wa damu kwa wanawake wenyewe umri wa miaka 15 - 49 wasio wajawazito kutoka asilimia 44.8 hadi asilimia 28.8, na kuongeza kiwango cha unyonyeshaji wa maziwa ya mama pekee kwa watoto wachanga kutoka asilimia 41.1 hadi asilimia 58.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatekeleza Mpango Jumuishi wa Pili wa Kitaifa wa Masuala ya Lishe wa mwaka 2020/2021 unaokwenda mpaka mwaka 2025/2026 sambamba na mkakati wake wa utafutaji fedha. Jumla ya shilingi bilioni 642.3 zitahitajika katika kipindi cha miaka mitano ili kuwezesha utekelezaji wa Mpango huo. Serikali itaendelea kutenga fedha za kugharimia utekelezaji wa mpango huo ili kuhakikisha kwamba jamii inakuwa na afya bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe wito kwa wadau wa maendeleo na sekta binafsi kuendelea kuunga mkono juhudzi za Serikali katika kuimarisha hali ya lishe hapa nchini kwetu.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, uratibu wa maafa; Serikali imeendelea kuratibu shughuli za usimamizi wa maafa nchini kwa kuzuia, kupunguza madhara na kujiandaa kukabiliana na maafa yanapotokea. Katika mwaka 2021/2022 Serikali imefanya maboresho ya mfumo wa utendaji wa shughuli za maafa ambapo Muswada wa Sheria ya Usimamizi wa Maafa ya mwaka 2022 umeandaliwa. Kutungwa kwa Sheria hii kutaimarisha mfumo wa kitaasisi wa usimamizi na uratibu wa shughuli za maafa nchini kwa kuzingatia wajibu wa sekta na taasisi za mujibu wa Sheria zilizopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2022/2023 Serikali itaendelea kuzijengea uwezo Kamati za Usimamizi wa Maafa za Mikoa na Wilaya, kuimarisha mifumo ya kielektroniki ya usimamizi wa maafa, kuhakikisha uwepo wa vifaa vyta kukabiliana na maafa na misaada ya huduma za kibinadamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la mazingira; Serikali imeendelea kushughulikia changamoto za uharibifu wa mazingira kwa kusimamia na kutekeleza sera, sheria, kanuni, mikakati, mipango na miongozo ya hifadhi na usimamizi wa mazingira na kuratibu utekelezaji wa Mikataba ya Kimataifa ya Mazingira na miradi mbalimbali ya hifadhi ya mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, mionganoni mwa kazi zilizotekelawa katika mwaka 2021/2022 ni kutunga Sera mpya ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 2021 na mkakati wake wa utekelezaji pamoja na kuboresha Sheria ya Usimamizi wa Mazingira na Kanuni zake. Aidha, Serikali imeandaa Mpango Kabambe wa kutatua changamoto za mazingira.

Meshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2022/2023 Serikali itaendelea kutekeleza mikakati ya kuhifadhi mazingira kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, mpango wa kitaifa wa kuhimili mabadiliko ya tabia nchi, kutoa elimu ya hifadhi ya mazingira kwa umma na kuhamasisha kampeni ya upandaji miti. Vilevile itaendelea kusimamia mifumo ya

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

uzalishaji viwandani ili iweze kuzingatia hifadhi ya mazingira pamoja na kutumia teknolojia rafiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, utawala bora; katika kuimarisha masuala ya utawala bora, Bunge lako Tukufu lilipitisha Miswada mbalimbali kuwa Sheria ikiwa ni pamoja na Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa mwaka 2021. Muswada huo ulihusisha Marekebisho ya Sheria ya Tafsiri ya Sheria iliyofanya lugha ya Kiswahili kuwa lugha rasmi ya Sheria na kutumika katika shughuli za Kimahakama. Hatua hii itawezesha mchakato wa utoaji haki kuwa na uwazi, usawa na wenye gharama nafuu. Aidha, Serikali imepanua wigo wa mfumo wa utoaji haki kwa kuwawezesha Mawakili kuanza kutoa huduma za uwakili katika Mahakama za Mwanzo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Nailbu Spika, Serikali katika mwaka 2022/2023 itaendelea kuimarisha utawala bora na utawala wa sheria ikiwa ni pamoja na kuimarisha mfumo wa utatuzi wa migogoro. Aidha, itaimarisha mifumo ya ushirikishaji wananchi katika maamuzi na mipango ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Muungano; Serikali imeendelea kudumisha Muungano wetu ambao ni tunu na mfano wa kuigwa Barani Afrika na dunia nzima. Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zimeendelea kushughulikia changamoto mbalimbali zinazojitokeza kwa lengo la kuulinda, kuuensi na kuudumisha Muungano wetu. Katika mwaka 2021/2022, kuititia vikao mbalimbali, hoja 11 zilifanyiwa kazi na kukamilika. Kati ya hizo, hoja tisa zimeandaliwa Hati za Makubaliano na kusainiwa na hoja mbili za kiutendaji zinaendelea kutekelezwa na mamlaka husika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2022/2023 Serikali itaendelea kuulinda, kuuensi na kuudumisha ushirikiano baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ili kuhakikisha kwamba mipango inayotekelzwa inanufaisha pande zote mbili za Muungano na Taifa kwa ujumla.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, uhusiano wa kimataifa; uhusiano kati ya Tanzania na Mataifa mengine umeendelea kuimarika. Uimara huo umechangiwa sana na ziara za viongozi wakuu wa kitaifa katika nchi mbalimbali sambamba na viongozi wakuu wa nchi hizo na Mashirika ya Kimataifa kuzuru hapa kwetu. Kupitia ziara hizo, nchi yetu imepata manufaa makubwa ikiwemo kuingia makubaliano ya ushirikiano katika maeneo mbalimbali kama vile miundombinu, nishati, elimu, teknolojia ya habari na mawasiliano, afya, michezo, kilimo, uwekezaji na kukuza lugha ya Kiswahili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2021/2022, Serikali imeshiriki katika mikutano mbalimbali ya Kimataifa na Kikanda ambapo Viongozi Wakuu wa nchi pamoja na masuala mengine, walipata fursa ya kuielezea dunia kuhusu sera na vipaumbele vya Serikali sambamba na kuimarisha uhusiano wa kidiplomasia, kisiasa na kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, aliongoza ujumbe wa Watanzania katika Mkutano wa 26 wa Umoja wa Mataifa kuhusu mabadiliko ya Tabianchi *COP26* uliofanyika *Glasgow* nchini Uingereza. Kupitia mkutano huo, Mheshimiwa Rais alipata fursa ya kuainisha vipaumbele vya nchi na Serikali anayoingoza katika majadiliano ya ajenda za mabadiliko ya tabia nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kulijulisha Bunge lako tukufu kuwa Serikali na Jumuiya ya Ulaya zimekubaliana kurejea kwenye mazungumzo ya Kitaalam kuhusu Mkataba wa Ushirikiano wa Kiuchumi unaojulikana kama *Economic Partnership Agreement*, na ninapenda kukuhakikishia kuwa majadiliano hayo yatazingatia maslahi mapana ya Taifa kwa lengo la kuinua uchumi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2022/2023 Serikali itaendelea kutekeleza Sera ya Mambo ya Nje, kuimarisha na kudumisha mahusiano ya kidiplomasia, kuongeza fursa za biashara na uvezeshaji kupitia utekelezaji

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

wa diplomasia ya uchumi, kuimarisha na kukuza uhusiano wa kiuchumi na mataifa, jumuiya na taasisi nyingine za kimataifa, kushiriki katika juhudhi za kuleta amani na usalama kwa Muungano kwa kuunga mkono Umoja wa Mataifa, Umoja wa Afrika na Jumuiya za Kikanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, itaendelea kuweka mazingira wezeshi, kuratibu na kuhamasisha ushiriki wa Watanzania waishio nje ya nchi kuchangia maendeleo ya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sanaa na michezo; Serikali ya Awamu ya Sita imeendelea kufanya jitihada mbalimbali kuhakikisha kwamba sekta hii nchini inapiga hatua kwenda mbele. Lengo ni kuimarisha michezo, sanaa na utamaduni ili ziweze kuchangia vema katika Pato la Taifa, sambamba na kuzalisha ajira kwa vijana, kutangaza utalii, kuimarisha umoja wa kitaifa na afya za Watanzania. Nyote mtakubaliana nami kwamba michezo na sanaa ni zaidi ya burudani kwani tumeshuhudia katika siku za hivi karibuni wanamichezo wetu wakinufaika kupitia sekta hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii kuwapongeza sana kwa dhati wanamichezo wote ambao wameiletea heshima nchi yetu kwa kupeperusha bendera ya nchi yetu. Tuna timu za mpira wa miguu, ngumi na wasanii mbalimbali, kwa upande wa michezo wa ngumi, niwapongeze sana wanamasumbwi Hassan Mwakinyo, Tonny Rashid, Twaha Kiduku na Ibrahim Class kwa ushindi mnono uliowawezesha kupata mikanda katika mashindano mbalimbali ya kimataifa waliyoshiriki. Lakini nitumie fursa hii pia kuzipongeza timu za mpira wa miguu za wanawake kwa ushindi wao katika mashindano mbalimbali ya kimataifa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee niwapongeze Timu ya Taifa ya Wanawake (*Twiga Stars*) kwa kutwaa ubingwa katika mashindano ya COSAFA mwaka 2021. Vilevile, niipongeze Timu ya Taifa ya Mpira wa Miguu ya Watu wenye Ulemavu '*Tembo Warriors*' kwa kufuzu kushiriki mashindano

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

ya dunia yatakayofanyika Oktoba mwaka huu nchini Uturuki. Hii ni mara ya kwanza Timu ya Taifa kushinda na kushiriki moja kwa moja mashindano ya dunia.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2021/2022, Serikali imekamilisha ujenzi wa Mfumo wa usajili na usimamizi wa wasanii na wadau wa sanaa na kuboresha mfumo wa usajili kwa njia ya kielektroniki. Mfumo huo, umewezesha wabunifu 485 na kazi zao 2,921 kusajiliwa. Aidha, Serikali imewezesha Wasanii wa fani ya muziki ambao kazi zao zimetumika kwenye vituo vya redio na televisheni kupata mirabaha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe wito kwa wasanii wote nchini kujisajili katika mfumo huo ili kupata manufaa tarajiwa. Katika mwaka 2022/2023, Serikali itaendelea kujenga mazingira wezeshi kwa wadau wa michezo, sanaa na utamaduni ili kuifanya Tanzania kuweza kung'ara katika medani za Kimataifa. Sambamba na hilo, Serikali itajenga shule maalum 56 za kukuza vipaji vya michezo katika maeneo mbambali hapa nchini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho; katika mwaka wa fedha 2022/2023 Ofisi ya Waziri Mkuu itaendelea kuimarisha uratibu wa shughuli za Serikali ili kuongeza tija na ufanisi katika matumizi ya rasilimali fedha. Aidha, maeneo yatakayopewa kipaumbele ni pamoja na kuratibu utekelezaji wa Sera za Taifa ili kuendana na mabadiliko ya kiuchumi na kijamii, kuratibu shughuli za maafa, kuboresha utendaji wa Baraza la Taifa la Biashara, uratibu wa shughuli za Serikali Bungeni, ufuatiliaji, tathmini na uratibu wa usimamizi wa shughuli za Serikali. Nitumie fursa hii kuwataka wadau wote waendelee kushirikiana na Serikali ili kurahisisha utekelezaji wa shughuli za Serikali kwa tija na ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeeleza kwa muhtasari baadhi ya shughuli ambazo Serikali imetekeleza kwa kipindi kilichopita. Aidha, nimetoa mwelekeo wa kazi zitakazofanyika kwa mwaka 2022/2023. Kwa kuhitimisha, ninapenda kusisitiza mambo muhimu yafuatayo: -

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Moja; Serikali ya Awamu ya Sita imepanga kufanya Sensa ya Watu na Makazi ifikapo mwaka 2022. Zoezi hili ambalo limeshaanza katika hatua za awali lina umuhimu wa kipekee katika kuisaidia Serikali kupata taarifa za msingi katika utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya mwaka 2025 na mipango mingine ya kitaifa na kimataifa. Taarifa za idadi ya watu husaidia mamlaka za ngazi ya Wilaya kutekeleza mipango ya maendeleo kwa kuweka uwiano wa mgawanyo wa rasilimali. Aidha, sensa hiyo itasaidia Serikali kupata taarifa za msingi za kidemografija, kijamii na kiuchumi. Hivyo, sote tuna wajibu wa kuhamasisha jamii kushiriki katika sensa, na kutoa taarifa na takwimu sahihi wakati makarani wa sensa ambaao watakuwa na vitambulisho maalum vyta Serikali watakapopita katika kaya zetu.

Mbili; Jitihada za Serikali ya Awamu ya Sita katika kuvutia uwekezaji zimeleta mwamko na matumaini makubwa kwa wawekezaji. Azma ya Serikali yetu ni kuona kwamba wawekezaji wakubwa wakiwemo wafanyabiashara na wakulima wanashirikiana kwa karibu na wawekezaji wa Kitanzania ili kuinua kipato cha Watanzania ikiwa ni pamoja na kuondoka kwenye kilimo cha kujikumu na kuingia katika kilimo cha kibiashara cha kisasa na chenye tija na ambacho pia kitawanufaisha wanaojishughulisha na Kilimo. Niwahakikishie Watanzania wote kwamba, upatikanaji wa ardhi iliyopimwa kwa ajili ya uwekezaji utaendelea kuwa moja ya vipaumbele vyta Serikali ili kuvutia wawekezaji wa ndani na nje ya nchi.

Tatu; Amani na usalama uliopo nchini umetujengea heshima kubwa katika Bara la Afrika na duniani kote. Sote tuna wajibu wa kuenzi na kusimamia visitoweke. Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mama yetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan itahakikisha kwamba amani, usalama na umoja wa Kitaifa vinadumishwa ili kuwawezesha wananchi kuendelea kufanya shughuli zao za maendeleo bila hofu. Serikali haitavumilia kuona mtu au kikundi cha watu wenye dhamira mbaya wakivuruga amani, usalama, umoja na mshikamano uliopo nchini kwetu kwa kisingizio chochote kile. Nitumie nafasi hii kuwaomba viongozi wa dini kuendelea

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

kuhubiri juu ya wajibu wa kuheshimu utawala bora na utawala wa Sheria, Kanuni na Taratibu zilizopo ili kudumisha amani, usalama na mshikamano wa Kitaifa.

Nne, ili kujiletea maendeleo endelevu kwa haraka, ni vema wote tuwajibike kwa vitendo na kufanya kazi kwa bidii, ubunifu, ufanisi na umakini ili kufikia malengo tuliojiwekea. Tunazo fursa nyingi za kukuza uchumi na kupunguza umaskini. Tujitahidi kuongeza tija na thamani katika bidhaa na mazao yetu ili kuwa na uchumi wa kisasa unaohimili ushindani katika masoko ya kikanda na kitaifa.

Tano, mpango wa muda wa kati wa Serikali ni kuendelea kutoa msukumo katika kutekeleza vipaumbele vyta Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/2022 – 2025/2026). Vipaumbele hivyo vinajumuisha kuchochaea uchumi shindani na shirikishi; kuimarisha uwezo wa uzalishaji viwandani na utoaji huduma; kukuza biashara na uwekezaji; kuchochaea maendeleo ya watu na kuendeleza rasilimali watu.

Sita, Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Uongozi wa Rais wetu, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, imeonesha dhamira ya dhati katika kukuza sekta binafsi pamoja na kuimarisha ushirikiano kati ya sekta ya Umma na sekta binafsi. Napenda kuuhakikisha Umma wa Tanzania kuwa Serikali yetu itaendelea kutambua, kuthamini na kushirikiana na sekta binafsi katika kukuza uchumi wa Taifa hili na jamii kwa ujumla. (*Makofii*)

Saba, Serikali itaendelea kushirikiana kwa karibu na Jumuiya za Kimataifa katika kukabiliana na kutockomeza maambukizi ya virusi vyta UVIKO-19. Vilevile itaendelea kuhimiza Watanzania kufuata maelekezo yanayotolewa na wataalam kuhusu kujikinga na kudhibiti ugonjwa wa UVIKO - 19. Aidha, Serikali itahakikisha kuwa chanjo inaendelea kupatikana katika vituo vyta kutolea huduma ya afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nane, hivi karibuni kumekuwepo na taarifa za uhaba na upandaji wa bei

usioendana na uhalisia wa soko kwenye bidhaa za ujenzi, vyakula, nishati na pembejeo za kilimo. Kufuatilia taarifa hizo, nililelekeza Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara kuunda jopo la wataalamu ili kufuatilia taarifa hizo. Wizara hiyo kwa kushirikiana na Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Tume ya Ushindani ilifanya ufuatilaji na tathmini ya mwenendo wa bei za bidhaa muhimu zinazozalishwa nchini na zile zinazotumia malighafi kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imechukua hatua mbalimbali ili kukabiliana na upandaji huo wa bidhaa muhimu. Hatua hizo ni pamoja na usimamiaji wa Sheria ya Ushindani Na. 8 ya mwaka 2003 ambayo inazuia kupanga bei. Hatua nyingine ni Serikali kutafuta vyanzo mbadala vya upatikanaji wa bidhaa na kuweka mifumo ya kusimamia masoko ya awali na minada.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inawaelekeza wazalishaji na wasambazaji wa bidhaa muhimu kushusha mara moja bei za bidhaa walizopandisha pasipo kuendana na uhalisia wa soko ikiwa ni pamoja na kutotumia kipindi hiki cha mfungo wa Ramadhani na Kwaresma kupandisha bei bila sababu yoyote ile. Nawasihi wazalishaji na wafanyabiashara wa bidhaa muhimu kuuza bidhaa husika kwa kuzingatia gharama halisi za uingizaji, uzalishaji na usambazaji. Wale watakaobainika kupandisha bei bidhaa muhimu bila taratibu, hatua kali zitachukuliwa dhidi yao. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa wito kwa viongozi wenzangu wote kuendelea kuunga mkono jitihada kubwa zinazofanywa na Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi chini ya uongozi mahiri na thabiti wa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kufanya kazi kwa bidii, weledi, uadilifu, tija na ufanisi, uaminifu na kupiga vita rushwa. Ni dhahiri kwamba, matokeo ya utendaji huu yatapunguza umasikini kwa Watanzania na kuwaletea maendeleo. (Makofii)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii pia kuendelea kusisitiza umuhimu wa Watanzania kujihusisha na mazoezi ya viungo ili kupata afya. Nitumie nafasi hii kuvipongeza vilabu vyetu vya mpira wa miguu vinavyoshiriki kwenye mashindano ya Ligi Kuu Tanzania Bara (*NBC Premier League*) na Ligi Kuu Zanzibar (*PBZ Premier League*). (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, hakika kwa mpira mzuri wanaocheza wanakonga miyo yetu washabiki wa mchezo wa mpira wa miguu nchini. Kipekee niipongeze timu ya *Simba Sports Club* kwa kupeperusha bendera ya Taifa letu katika mashindano ya Shirikisho la Klabu Bingwa Afrika. Mwenye macho haambiwi tazama, sote tumeshuhudia wakiendelea kuupiga mwingu na kutuwakilisha vema katika medani za kimataifa. (Makofi/Vigelegele)

Mheshimiwa Naibu Spika, niwapongeze pia wachezaji mahiri wa vilabu mbalimbali vya mpira wa miguu vikiwemo Yanga - Timu ya Wananchi; *Simba Sports Club* - Wekundu wa Msimbazi; Namungo - Wauaji wa Kusini; Azam - Wazee wa Lambalamba; Blashara *United* - Wanajeshi wa Mpakani; Dodoma Jiji - Walima Zabibu; Tanzania Prison - Wajelajela na bila kuwasahau Mtibwa *Sugar* - Wakata Miwa na Kagera *Sugar* - Wanankurukumbi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, nivipongeze vilabu vya Zanzibar vikiwemo KMKM, Mlandege, Malindi na vilabu vinginevyo. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha za Ofisi ya Waziri Mkuu na Ofisi ya Bunge kwa Mwaka 2022/2023; kwa mwaka 2022/2023, Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zilizo chini yake inaliomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya shilingi 148,892,553,000.00. Kati ya fedha hizo shilingi 101,365,398,000.00 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi 47,527,155,000.00 ni kwa ajili Matumizi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile naliomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya shilingi 132,728,638,000.00 kwa ajili

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

ya Mfuko wa Bunge. Kati ya fedha hizo shilingi 127,328,638,000.00 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi 5,400,000,000.00 ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.
(*Makofii*)

WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:
Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba nzuri ambayo imegusa maeneo yote ya nchi yetu. Hongera sana na hoja imeungwa mkono.

Sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria, atuwasilishie taarifa ya Kamati yake. (*Makofii*)

MHE. JOSEPH K. MHAGAMA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naomba taarifa yote iingizwe katika Taarifa Rasmi za Bunge kama ilivyowasilishwa Mezani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa kanuni 118(9) ya kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Juni, 2020, naomba kuwasilisha taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka wa fedha 2021/2022 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa ya Kamati kuhusu makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu, inagusa maeneo makuu mawili ambayo ni Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu) pamoja na Ofisi ya Waziri Mkuu, (Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu).

Mheshimiwa Naibu Spika, katika uchambuzi wake kuhusu bajeti hiyo, Kamati ilipitia jumla ya mafungu sita

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

ambayo ni Fungu Na. 24 - Ofisi Binafsi ya Waziri Mkuu, Fungu Na. 37 - Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, Fungu Na. 27 - Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa, Fungu Na. 61 - Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Fungu Na. 65 - Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu na Fungu 15 - Tume ya Usuluhishi na Uamuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uchambuzi na Tathmini ya Utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2021/2022. Katika mwaka wa fedha 2021/2022 Ofisi ya Waziri Mkuu ililenga kukusanya maduhuli ya jumla ya shilingi bilioni 35,085. Kati ya fedha hizo, fedha ya Ofisi ya Waziri Mkuu, (Sera, Bunge na Uratibu) ilipata kukusanya shilingi bilioni 5,085 na Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, iliidhinishiwa kukusanya shilingi bilioni 30. Mchanganuo wa kiasi cha maduhuli kwa kila fungu inaoneshwa katika Jedwali Na. 1.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa mwenendo wa ukusanyaji wa maduhuli unaonesha kama ifuatavyo: jumla ya shilingi 755,407,997,000 sawa na asilimia 15 ya makusanyo yote ya Ofisi ya Waziri Mkuu, (Bunge, Sera na Uratibu) yalikusanywa katika kipindi hicho. Aidha, jumla ya shilingi 20,682,200,000 sawa na asilimia 68.94 ya makusanyo ya Ofisi ya Waziri Mkuu, (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu) yalikusanywa katika kipindi hicho pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Ofisi ya Waziri Mkuu iliidhinishwa jumla ya shilingi 75,360,457,000 kwa matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo, shilingi 57,810,426,000 sawa na asilimia 76.71 na matumizi ya upande wa Sera, Bunge na Uratibu na shilingi 17,550,031,000 sawa na asilimia 23.29 upande wa Kazi, Ajira, Vijana na Watu Wenye Ulemavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia Februari, 2022 Ofisi ya Waziri ilipata jumla ya shilingi 63,118,348,817.88. Kati ya fedha hizo, shilingi 51,509,495,262.30, sawa na asilimia 81.2 ya fedha iliopatikana ni kwa matumizi ya ofisi Waziri Mkuu, (Sera, Bunge na Uratibu) na shilingi 11,908,853,595.58 sawa

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

na asilimia 18.78 ni kwa ajili ya Ofisi ya Waziri Mkuu, (Kazi, Ajira, Vijana na Wenyewe Ulemavu). (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mchanganuo wa fedha hizo kwa taasisi za Ofisi ya Waziri Mkuu ni kama ilivyo katika jedwali Na. 2.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa uchambuzi huo, Kamati ina maoni kwamba mwenendo wa upatikanaji wa fedha kwa ujumla ni wa kuridhisha. Hata hivyo, kiasi cha fedha kilichosalia kinahitajika kutolewa chote kwa taasisi zote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Waziri Mkuu alipowasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya ofisi yake kwa mwaka Fedha 2021/2022 aliomba jumla ya shilingi 21,335,344,030 kwa miradi ya maendeleo katika sekta zinazosimamiwa na Kamati. Kati ya kiasi hicho, shilingi 9,521,444,000 iliombe kwa ajili ya miradi chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, (Sera, Uratibu na Bunge) na shilingi 11,814,000,000 ziliombwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, (Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenyewe Ulemavu). Mchanganuo wa fedha hizo unaonekana katika jedwali Na.3.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imebaini kwamba kati ya fedha zilizotengwa na kutolewa ili kutekeleza miradi hiyo, fedha za nje zilitolewa kwa asilimia 42.23 ya makisio, wakati fedha za ndani zilitolewa asilimia 59.38 ya fedha iliyotengwa. Ni maoni ya Kamati kwamba mwenendo wa mapokezi ya fedha za nje, kutekeleza miradi ya maendeleo uko chini ukillinganisha na bajeti ya fedha za ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilifuatilia na kuchambua utekelezaji wa miradi hiyo. Baadhi ya miradi hiyo ni kama ifuatavyo: Mradi Na. 4937- ujenzi wa kiwanda cha uchapaji nyaraka za Serikali. Mradi huu unalenga kuboresha shughuli za uchapishaji wa nyaraka za Serikali lengo hilo lingeboresha azma ya Serikali inayotekelze wa kuititia kwa Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali. Jumla ya shilingi 2,500,000,000 zilitengwa katika mwaka wa fedha, 2021/2022 kwa ajili hiyo.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, mradi huo haujapata kiasi chochote cha fedha iliyopangwa kufikia Februari, 2022. Hali hiyo kwa maoni ya Kamati halioneshi mkazo wa Serikali katika shughuli za uchapishaji wa nyaraka zake. Uchambuzi huu unasisitiza umuhimu wa Serikali kuzingatia nafasi ya shughuli za uchapishaji wa nyaraka katika dhana ya utawala bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi Na. 6581 - *Program ya Kukuza Ujuzi Nchini*. Hadi kufikia Februari, 2022 programu hii ili kuwa imepokea shilingi bilioni sita kati ya shilingi bilioni tisa kutekeleza majukumu mbalimbali yakiwemo yafuatayo: kutoa mafunzo ya ujuzi na stadi za kazi kwa njia ya uanagenzi wa vijana na kujenga vitalu nyumba kwa maana ya *greenhouses* katika Halmashauri 36 za mikoa mitano.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi namba 4552 - Mfuko wa Maendeleo ya Vijana, mradi huu ni kwa ajili ya kutoa mkopo kwa vijana na unatekelezwa kwa fedha za ndani. Hadi kufikia Februari, 2022 jumla ya shilingi bilioni moja zilikuwa zimepokelewa ikiwa ni asilimia 100 ya fedha iliyotengwa. Taarifa za utekelezaji wa mradi zinaonesha kuwa maombi yaliyopokelewa na kukidhi vigezo hadi Februari, 2022 ni shilingi milioni 205 sawa na asilimia 20.5 tu. Kwa kiasi hicho, asilimia 79.5 ya fedha iliyotolewa imeendelea kubaki bila kupata walengwa waliokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali hiyo inaweza kutafsiriwa kuwa, Mfuko wa Maendeleo kwa Vijana haueleweki kwa walengwa au masharti yaliyowekwa hayana uhalisia. Kamati ina maoni kuwa, ili kufanikisha azma ya mradi huo, kuna umuhimu wa kutangaza Mfuko wa Maendeleo ya Vijana na kutathmini vigezo vilivyowekwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya tatu, ni uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2022/2023, sehemu ya kwanza ni maduhuli.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2022/2023 Ofisi ya Waziri Mkuu inaomba kuidhinishwa

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

kukusanya jumla ya shilingi 51,110,000,000/=, hii ni sawa na ongezeko la asilimia 45 ukilinganisha na makadirio ya makusanyo ya maduhuli kwa mwaka unaoisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ina maoni kwamba ongezeko la makadirio ya makusanyo ya maduhuli kwa mwaka wa fedha 2022/2023 linaakisi azma ya Serikali kuongeza wigo wa mapato yake. (Makoti)

Mheshimiwa Naibu Spika, matumizi ya kawaida, katika mwaka wa fedha, 2022/2023 - Ofisi ya Waziri Mkuu pamoja na taasisi zilizo chini yake inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi 85,411,679,000 ikiwa ni fedha za matumizi ya kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi ya maendeleo, katika mwaka wa fedha 2022/2023, Ofisi ya Waziri Mkuu inaomba kuidhinishwa shilingi 39,524,949,000 kwa ajili ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo. Kati ya fedha hizo shilingi 21,760,000,000 ni fedha za ndani na shilingi 17,764,949,000 ni fedha nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti ya maendeleo katika mwaka wa fedha 2022/2023 imeongezeka ukilinganisha na bajeti ya mwaka wa fedha unaoisha. Hata hivyo, baadhi ya miradi ambayo haikuwemo katika bajeti ya mwaka 2021/2022 inaombewa fedha katika mwaka wa fedha 2022/2023 kama ambavyo Jedwali Na. 6 limeainisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni na ushauri wa Kamati, maoni na ushauri wa jumla, kwa kuzingatia majadiliano ya kina kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Kamati inatoa maoni, ushauri na mapendekezo ya jumla kwa mafungu yote kama ifuatavyo: -

(i) Kamati ilibaini kuwa ni asilimia 15 tu ya maduhuli yaliyopangwa kukusanya na Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu) yalikusanya hadi kufikia tarehe 28 Februari, 2022. Kamati inaishauri Serikali kuongeza ubunifu na

kasi ya ukusanyaji maduhuli na ijiwekee malengo ya ukusanyaji maduhuli ambayo yanaakisi uwezo wa ukusanyaji na hali halisi ya vyanzo veya mapato. Aidha, Serikali iandae mpango mkakati wa ukusanyaji ambao utaiwezesha kuandaa taarifa ya kila mwezi ya makusanyo na tathmini ya uwezo wa ukusanyaji maduhuli.

(ii) Kamati ilibaini kwamba ni asilimia 42.23 tu ya fedha za nje na asilimia 59.38 ya fedha za ndani zilizotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo katika Ofisi ya Waziri Mkuu ndizo zilipatikana. Kamati inashauri kwamba Serikali ihakikishe kwamba inatoa kwa wakati fedha za maendeleo na matumizi mengine ili kuziwezesha taasisi na idara za Serikali kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Aidha, Serikali ijielekeze zaidi kwenye kutumia vyanzo veya ndani katika kutekeleza Miradi mbalimbali ya Maendeleo nchini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni na ushauri mahsus; katika Fungu Namba 37 - Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu Serikali iharakishe mpango wa ujenzi wa Kiwanda cha Uchapishaji Dodoma kwa kutoa fedha kiasi cha shilingi bilioni 2.5 zilizotengwa kutekeleza mradi huo katika mwaka wa fedha 2021/2022 na kutenga fedha za kutosha katika mwaka wa fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, Fungu 65; Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu; Serikali ihakikishe kwamba, inamrahisishia mwananchi kupata taarifa kuhusu fursa zinazopatikana katika programu mbalimbali ambazo zinaweza kumsaidia kuijendeleza kujipatia maendeleo. Aidha, Serikali itengeneze mazingira wezeshi na ya kisera, kisheria na kiutekelezaji kwa lengo la kumpunguzia mwananchi huyo gharama zisizo za lazima wakati wa kufuutilia fursa hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbili, ili kuongeza ufanisi katika masuala yanayohusu mafunzo kwa vitendo na uanagenzi, Ofisi ya Waziri Mkuu ishirikiane na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ili kufanya mabadiliko katika mitaala kwa lengo la kuwapa vijana mafunzo wanapokuwa

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

masomoni ili kupunguza gharama za mafunzo hayo baada ya kumaliza masomo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti; hitimisho; napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha taarifa hii. Aidha, napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria ambao maoni na ushauri ushirikiano wao umeiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na hatimaye kukamilika kwa taarifa hii. Naomba majina yao yaingie kwenye kumbukumbu za Kudumu za Bunge kama yalivyowasilishwa katika taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati naomba nichukue fursa hii kumpongeza Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Mbunge kwa uongozi wake wa Shughuli za Serikali Bungeni na kwa kuwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya ofisi yake kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, naomba nichukue fursa hii kuwashukuru Mawaziri na Naibu Mawaziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu ambao wamemsaidia kwa karibu Mheshimiwa Waziri Mkuu kutekeleza majukumu yake katika Ofisi hiyo. Kwa umuhimu wao naomba niwatambue kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa George Boniface Simbachawene, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu; Mheshimiwa Profesa Joyce Lazaro Ndalichako, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu; Mheshimiwa Ummy Hamisi Nderiananga, Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu; na Mheshimiwa Paschal Patrobass Katambi, Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia niwashukuru watendaji wote wa Ofisi ya Waziri Mkuu pamoja na taasisi zake kwa ushirikiano waliotupatia Kamati wakiongozwa na

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Makatibu Wakuu wa Ofisi hiyo Dkt. John Anthony Jingu - Sera, Bunge na Uratibu na Dkt. Jamal Adam Katundu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho lakini sio kwa umuhimu, napenda kuwashukuru watumishi wote wa Bunge chini ya uongozi thabit wa Katibu wa Bunge Ndugu Nenelwa Mwihambi (*ndc*), kwa kuratibu vema shughuli za Kamati na Bunge hadi kukamilika taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 kama yalivyowasilishwa na mtoha hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. (*Makofii*)

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA
SHERIA KUHSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA OFISI YA WAZIRI
MKUU KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022 PAMOJA NA
MAONI YA KAMATI KUHSU MAKADIRIO YA MAPATO NA
MATUMIZI YA OFISI HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023
KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

1.0 UTANGULIZI

1.1 Maelezo ya Awali

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa **Kanuni ya 118 (9)** ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria Kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, ili kukidhi mantiki iliyokusudiwa na Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Bunge, Taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu zifuatazo: -

- a) Sehemu ya Kwanza inatoa maelezo ya jumla kuonesha msingi na Muundo wa Taarifa pamoja na namna Kamati ilivyofanya kaz;
- b) Sehemu ya Pili ni uchambuzi wa utekelezaji wa bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 kwa kuangalia makusanyo ya maduhuli, mwenendo wa upatikanaji wa fedha za matumizi ya kawaida, utekelezaji wa miradi ya maendeleo na uzingatiaji wa ushauri wa Kamati Bungeni;
- c) Sehemu ya Tatu ni uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2022/2023;
- d) Sehemu ya Nne inahusu majumuisho ya maoni na ushauri wa Kamati; na
- e) Sehemu ya Tano ni maoni ni hitimisho.

1.2 Msingi wa Uchambuzi wa Kamati

Mheshimiwa Spika, Msingi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Ofisi ya Waziri Mkuu ni Masharti ya Kanuni za Bunge. Kifungu cha 6 (2)(a) kikisomwa kwa pamoja na Kifungu cha 7 (1)(a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge, kinatambua jukumu la Kamati hii kufanya uchambuzi huo. Aidha, Kanuni ya 117 (4) ya Kanuni za Bunge imeweka masharti yanayotaka Taarifa ya Utekelezaji na Makadirio ya Ofisi hii kuchambuliwa na Kamati kabla ya kujadiliwa Bungeni. Naomba kulijulisha Bunge lako tukufu kuwa masharti hayo yamezingatiwa na kwamba naliomba Bunge hili lijadili hoja ya Ofisi ya Waziri Mkuu pamoja na Taarifa hii.

1.3 Mawanda ya Uchambuzi

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hii, inagusa maeneo makuu mawili ambayo ni **Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu)** pamoja na **Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenyewe Ulemavu)**. Naomba kutoa taarifa

kuwa Kamati ilichambua taarifa na Makadirio ya Sehemu zote mbili zilizozitajwa kuanzia tarehe 21 hadi 24 Machi, 2022

Mheshimiwa Spika, Katika uchambuzi huo, Kamati ilipitia jumla ya mafungu 6 ambayo ni: -

- a) **Fungu 25** - Ofisi Binafsi ya Waziri Mkuu
- b) **Fungu 37** - Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu)
- c) **Fungu 27** - Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa
- d) **Fungu 61** - Tume ya Taifa ya Uchaguzi
- e) **Fungu 65** – Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu)
- f) **Fungu 15** – Tume ya Usuluhishi na Uamuzi

2.0 UCHAMBUZI NA TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

2.1 Ufafanuzi wa Jumla

Mheshimiwa Spika, matokeo ya uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Mapato na Matumizi yanaweka msingi wa ushauri wa Kamati kuhusu Hoja hii ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Kwa sababu hiyo, ili kuwezesha ufuatililaji mzuri wa wasilisho hili, naomba kubainisha mambo makuu manne yaliyochambuliwa. Mambo hayo ni;:-

- (a) Makusanyo ya maduhuli;
- (b) Mwenendo wa Upatikanaji wa fedha za Bajeti ya kawaida;
- (c) Taarifa ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu; na
- (d) Uzingatiaji wa Ushauri wa Kamati Bungeni.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

2.2 Uchambuzi wa Makusanyo ya Maduhuli

Mheshimiwa Spika, Katika mwaka wa Fedha 2021/22, Ofisi ya Waziri Mkuu ililenga kukusanya maduhuli ya jumla ya **Sh. 35,086,000,000**. Kati ya fedha hizo Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu) ilipanga kukusanya **Sh. 5,086,000,000**. na Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu) illidhinishiwa kukusanya **Sh. 30,000,000,000**. Mchanganuo wa kiasi cha maduhuli kwa kila fungu unaoneshwa katika Jedwali Na. 1.

JEDWALI NA. 1 – Makusanyo ya Maduhuli 2021/2022

FUNGU	MAKISIO YA MADUHULI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022	MAKUSANYO KUFIKIA FEBRUARI 2022	ASILIMIA YA MAKUSANYO
Fungu 27 – Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa	36,000,000	2,000,000	5.56%
Fungu 37 – Ofisi ya Waziri Mkuu	5,000,000,000	692,213,707	13.84%
Fungu 61 – Tume ya Taifa ya Uchaguzi	50,000,000	61,194,290.47	122.39%
Fungu 65 - Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu)	30,000,000,000	Sh. 20,682,002,180	68.94%
JUMLA KUU	35,086,000,000	21,437,410,177.47	61.09%

Chanzo: Randama za Ofisi ya Waziri Mkuu na Usanifu wa Kamati

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa mwenendo wa ukusanyaji wa maduhuli unaonesha yafuatayo: -

- (a) Jumla ya **Sh. 755,407,997.47** sawa na **asilimia 15** ya makusanyo yote ya Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu) yalikusanywa katika kipindi hicho.

(b) Aidha, Jumla ya **Sh. 20,682,002,180** sawa na **asilimia 68.94.** ya makusanyo yote ya Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu) yalikusanya katika kipindi hicho pia.

(c) Fungu 61 - Tume ya Taifa ya Uchaguzi imevuka lengo la makusanyo kwa kufikia **asilimia 122.39** ya lengo. Sababu ya kiasi hicho cha juu cha makusanyo ni kupokewa kwa bakaa ya fedha za uchaguzi zilizovuka mwaka wa fedha kutoka katika halmashauri.

(d) Fungu 27 - Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa bado hajakaribia lengo la makusanyo kwa kuwa hadi tarehe 28 Februari 2022 ilikuwa imekusanya **asilimia 5.56** ya lengo. Kiasi hicho kinaweza kuwa kimetokana na upangaji wa lengo usio na uhalsia au juhudhi hafifu za ukusanyaji.

Mheshimiwa Spika, kwa uchambuzi huo, Kamati ina maoni kuwa, makusanyo haya hafifu ya baadhi ya taasisi chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, yanaweza kutafsiriwa kwamba au malengo ya ukusanyaji yaliyowekwa hayakuwa halisi; au jitihada za ukusanyaji zilikuwa hafifu, au vyanzo vya maduhuli vilivyoanishwa havikuwa vya uhakika.

2.3 Uchambuzi wa Matumizi ya Kawaida

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Ofisi ya Waziri Mkuu ilidhinishiwa jumla ya **Sh. 75,360,457,000** kwa matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo **Sh. 57,810,426,000** sawa na **asilimia 76.71** ni matumizi upande wa Sera, Bunge na Uratibu na **Sh. 17,550,031,000** sawa na **asimilia 23.29** upande wa Kazi, Ajira, Vijana na Watu Wenye Ulemavu.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Februari, 2022 Ofisi ya Waziri Mkuu ilipata jumla ya **Sh. 63,418,348,817.88.** Kati ya fedha hizo, **Sh. 51,509,495,262.30** sawa na **asilimia 81.22** ya fedha iliopatikana ni kwa matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu), na **Sh. 11,908,853,555.58** sawa na **asilimia 18.78** ni kwa ajili ya Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu). Mchanganuo wa fedha hizo kwa taasisi

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

za Ofisi ya Waziri Mkuu ni kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 2.

JEDWALI NA. 2 – Mapokezi ya Fedhza Matumizi ya Kawaida 2021/2022

FUNGU	FEDHA YA MATUMIZI YA KAWAIDA ILIYOTENGWA KWA MWAKA 2021/2022	MAPOKEZI YA FEDHA KUFIKIA FEBRUARI 2021	ASILIMIA YA MAPOKEZI
Fungu 25 – Ofisi Binafsi ya Waziri Mkuu	11,090,619,000	9,728,804,882.22	87.72%
Fungu 37 – Ofisi ya Waziri Mkuu (SBU)	17,932,260,000	14,603,896,499.12	81.44%
Fungu 27 – Ofisi ya M sajili wa Vyama vya Siasa	19,999,196,000	13,802,927,827.92	69.02%
Fungu 61 – Tume ya Taifa ya Uchaguzi	8,788,351,000	13,373,866,053.04	152.18%
Fungu 65 – Ofisi ya Waziri Mkuu (KVAWU)	13,676,606,000	9,341,657,579	68.30%
Fungu 15 – Tume ya Usuluhishi na Uamuzi	3,873,425,000	2,567,195,976.58	66.28%
JUMLA KUU	75,360,457,000	63,418,348,817.88	84.15%

Chanzo: Randama za Ofisi ya Waziri Mkuu na Usanifu wa Kamati

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa upatikanaji wa fedha hizo unaonesha kwamba: -

(a) Kwa ujumla, Ofisi ya Waziri Mkuu imepokea jumla ya **Sh. 63,418,348,817.88** sawa na **asilimia 84.15%** ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya matumizi ya kwaida.

(b) Taasisi nne (4) zimeweza kupata kiasi ambacho ni pungufu ya asilimia ya jumla ya upatikanaji wa fedha ikilinganishwa na kiasi cha jumla kilichopatikana.

(c) Katika uwiano wa makadirio ya fedha yaliyoidhinishwa **Fungu 15 – Tume ya Usuluhishi na Uamuzi** ilidhinishiwa **asilimia tano** ya bajeti yote ya Ofisi ya Waziri Mkuu lakini katika upatikanaji, taasisi hiyo ilipata **asilimia 4** ya kiasi cha jumla ya fedha zilizopokewa na Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, kwa uchambuzi huo, Kamati ina maoni kwamba, mwenendo wa upatikanaji wa fedha kwa ujumla

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

ni wa kuridhisha. Hata hivo, kiasi cha fedha kilichosalia kinahitaji kutolewa chote kwa taasisi zote. Haitapendeza lwapo baadhi ya taasisi za Ofisi ya Waziri Mkuu zitapata bajeti yote kama ilivyoidhinishwa na nyingine zipate pungufu ya bajeti iliyoidhinishwa.

2.4 Tathmini ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo

Mheshimiwa Spika, wakati Waziri Mkuu alipowasilisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi yake kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 aliomba jumla ya **Sh 21,335,344,030** kwa Miradi ya Maendeleo katika Sekta zinazosimamiwa na Kamati. Kati ya kiasi hicho **Sh. 9,521,344,000** ziliombwa kwa ajili ya miradi chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Uratibu na Bunge) na **Sh. 11,814,000,030** ziliombwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya Maendeleo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye ulemavu. Mchanganuo wa fedha hizo unaoneshwa katika Jedwali Na. 3

JEDWALI NA. 3 – Miradi ya Maendeleo Iliyotengewa Fedha 2021/2022

FUNGU	NAMBA NA JINA LA MRADI	BAJETI ILIYOTENGWA 2021/2022		MAPOTEZI YA FEDHA KUFIKIA FEBRUARI 2022	
		FEDHA ZA NDANI	FEDHA ZA NJE	FEDHA ZA NDANI	FEDHA ZA NJE
Fungu 27 - Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Slasa	Na. 6389 Ujenzi wa Jengo la Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Slasa Dodoma	2,000,000,000	0.00	2,048,182,864	0.00
Fungu 37 - OWM (SBU)	Na. 6351 Ujenzi wa Makazi ya Waziri Mkuu Milim - Dodoma	1,500,000,000	0.00	453,673,155	0.00
Fungu 37 - OWM (SBU)	Na. 4429 Programu ya Kuendeleza Kilimo na Uvuvi	0.00	3,521,344,000	0.00	1,543,552,200
Fungu 37 - OWM (SBU)	Na. 4937 Ujenzi wa Kiwanda cha Uchapaji Nyaraka za Serikali	2,500,000,000	0.00	0.00	0.00
Fungu 65 - OWM (KVAWU)	Na. 6205 Programu ya Kukuza Kazi za Staha	0.00	1,814,000,030		709,831,927
Fungu 65 - OWM (KVAWU)	Na. 6581 Programu ya Kukuza Ujuzi Nchini	9,000,000,000	0.00	6,000,000,000	0.00
Fungu 65 - OWM (KVAWU)	Na. 4952 Mfuko wa Maendeleo ya Vijana	1,000,000,000	0.00	1,000,000,000	0.00
Jumla Ndogo		16,000,000,000	5,335,344,030	9,501,856,019	2,253,384,127
JUMLA KUU		21,335,344,030		11,755,240,146	

Chanzo: Randama za Ofisi ya Waziri Mkuu na Usanifu wa Kamati

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kwamba, kati ya fedha zilizotengwa na kutolewa ili kutekeleza miradi hiyo, fedha za nje zilitolewa kwa **asilimia 42.23** ya makisio wakati fedha za ndani zilitolewa **asilimia 59.38** ya fedha iliyotengwa. Ni maoni ya Kamati kwamba, mwenendo wa mapokezi wa fedha za nje kutekeleza miradi ya maendeleo uko nchini ukilinganisha na bajeti ya fedha za ndani.

Mheshimiwa Spika, jumla ya miradi saba ilitekelezwa na Ofisi ya Waziri Mkuu. Miradi minne kati ya hiyo inatekelezwa na Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Uratibu na Bunge) na miradi mitatu inatekelezwa na Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Ajira, Vijana na Watu wenye Ulemavu). Kamati ilifuatilia na kuchambua utekelezaji wa miradi hiyo kama ifuatavyo: -

2.4.1 Mradi Na. 6389 Ujenzi wa Jengo la Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa Dodoma

Mradi huu ulikusudia kuiwezesha ofisi ya msajili wa vyama vya siasa kuwa na jengo la Ofisi katika makao makuu ya nchi Dodoma. Taarifa zinaonyesha kuwa, fedha zilizotumika kwa utekelezaji wa mradi huu ni fedha za ndani kwa asilimia mia moja. Aidha, hadi kufikia mwezi Februari 2022, mradi ulipokea fedha zoite zilizoidhinishwa. Kamati ina maoni kuwa, upatikanji wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi kwa kiwango cha kutosha unafanikisha tija ya mipango ya maendeleo. Kwa msingi huo, Kamati inalpongeza Serikali kwa kufanikisha mradi huu kwa kiwango hicho.

2.4.2 Mradi Na. 6351 Ujenzi wa Makazi ya Waziri Mkuu Mlimwa – Dodoma

Kamati ilitaarifiwa kwamba kiasi cha shilingi **milioni 453** kilichopatikana kufikia Februari, 2022 kati ya **shilingi bilioni 1.5** kimeiwezesha Serikali kukamilisha miundombinu ya nishati ya umeme na ulinzi katika ukuta unaozunguka Ofisi na Makazi ya Waziri Mkuu. Ni maoni ya Kamati kwamba, viwango stahiki vinapaswa kuzingatiwa ili kuendana na hadhi ya makazi na ofisi ya kiongozi wa kitaifa.

2.4.3 Mradi Na. 4429 Programu ya Kuendeleza Kilimo na Uvuvi

Mheshimiwa Spika, taarifa zilizointyesha kwamba hadi kufikia Februari 2022 Ofisi imepokea takriban **shilingi bilioni 1.54** kati ya **shilingi bilioni 3.52** zilizotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha 2021/2022. Fedha hizo ni za nje. Kamati ilitaarifiwa kwamba, kazi zinazoendelea Tanzania Bara na Zanzibar ni pamoja na maandalizi ya *baseline study*, upembuzi yakinifu, kuandaa mfumo wa uhasibu wa mradi, na tathmini ya athari za mazingira hususan kwa ajili ya uvuvi na usimamizi wa mradi ikiwa ni takriban asilimia 10 ya utekelezaji.

2.4.4 Mradi Na. 4937 Ujenzi wa Kiwanda cha Uchapaji Nyaraka za Serikali

Mradi huu unalenga kuboresha shughuli za uchapishaji wa nyaraka za Serikali. Lengo hilo lingeboresha azma ya Serikali inayotekelizwa kupitia kwa Mpigachapa Mkuu wa Serikali. Jumla ya **Sh. 2,500,000,000** zilitengwa katika Mwaka wa Fedha 2021/2022 kwa ajili hiyo. Hata hivyo, mradi huu haujapata kiasi chochote cha fedha iliyopangwa kufikia Februari, 2022. Hali hiyo, kwa maoni ya Kamati, haioneshi mkazo wa Serikali katika shughuli za uchapishaji wa nyaraka zake. Uchambuzi huo unasisitiza umuhimu wa Serikali kuzingatia nafasi ya shughuli za uchapishaji wa nyaraka zake katika dhana ya utawala bora.

2.4.5 Mradi Na. 6205 Programu ya Kukuza Kazi za Staha (*Decent Work Country Program*)

Mradi huu unahusu kujenga stadi za Maisha kwa vijana kupitia programu ya kazi za staha. Jumla ya **Sh. 1,814,000,030** zilitengwa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu. Bajeti yote iliyotengwa ni fedha za nje. Taarifa iliyoenyesha kuwa, hadi Februari 2022, mradi ulipokea **Sh. 709,831,927**. Kamati ilijulishwa kuwa, fedha hizo zilitumika kufanya kazi kuu tatu mbazo ni:-

- a) Tathmini na mapitio ya sera ya vijana ya 2007
- b) Utafiti na maboresho ya muongozo wa stadi za Maisha kwa vijana; na
- c) Mapitio ya programu ya kazi za staha.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, kwa hatua hiyo ya utekelezaji, tija ya mradi haijaanza kuonekana licha ya kiwango hicho cha fedha kupokewa. Kamati ina maoni kuwa taasisi za umma, zinapaswa kuzingatia thamani halisi ya pesa inayopatikana kwa ajili ya utekelezaji wa miradi kwa hatua zinazofikiwa.

2.4.6 Mradi Na. 6581 Programu ya Kukuza Ujuzi Nchini

Hadi kufikia Februari, 2022 programu hii ilikuwa imepokea **shilingi bilioni 6** kati ya **shilingi bilioni 9** kutekeleza majukumu mbalimbali ikiwemo yafuatayo: -

- a) Kutoa mafunzo ya ujuzi na stadi za kazi kwa njia ya uanagenzi kwa vijana; na
- b) Kujenga Vitalu Nyumba (*Greenhouses*) katika Halmashauri 36 za Mikoa mitano (5).

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipotembelea Kitalu Nyumba katika Halmashauri ya Wilaya ya Meru, ilibaini kwamba Ofisi ya Waziri Mkuu iliweka vigezo vya namna ya kuwapata vijana katika maeneo yao. Hata hivyo, ilibainika kuwa vigezo hivyo havizingatiwi ipasavyo na kuathiri upatikanaji wa makundi maalum. Aidha, udadisi wa Kamati ulidhihirisha kuwa vijana wanaonufaika na mafunzo haya hupata ujuzi wenye manufaa, lakini inakuwa vigumu kwa ujuzi huo kuwasaidia katika Maisha halisi. Sababu ya ugumu huo ni gharama kubwa ya kujenga vitalu nyumba ikiunganishwa na ombwe la upatikanaji wa mitaji kwa vijana wanaohusika. Kwa mfano, Kamati ilibaini kwamba, ujenzi wa kitalu nyumba kimoja hugharimu wastani wa **Sh. 14,000,000** na **Sh. 8,000,000** iwapo kwa malighafi za asili. Hata hivyo, gharama zote hizi ni ngumu kwa vijana hawa kuzimudu. Kwa maoni ya Kamati, hali hiyo isipofanyiwa kazi, programu ya kukuza ujuzi nchini halitakuwa na tija.

2.4.7 Mradi Na. 4952 Mfuko wa Maendeleo ya Vijana

Mradi huu ni kwa ajili ya kutoa mikopo kwa vijana na unatekelezwa kwa fedha za ndani. Hadi kufikia Februari 2022,

jumlah ya **Sh. 1,000,000,000** zilikuwa zimepokelewa ikiwa ni **asilimia mia moja** (100%) ya fedha iliyotengwa. Taarifa za utekelezaji wa mradi zinaonyesha kuwa maombi yaliyopokewa na kukudhi vigezo hadi Februari 2022 ni **Sh. 205,000,000** sawa na **asilimia 20.5**. Kwa kiasi hicho, **asilimia 79.5** ya fedha iliyopokewa imeendelea kubaki bila kupata walengwa waliokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, hali hiyo inaweza kutafsiriwa kuwa, mfuko wa maendeleo kwa vijana haueleweki kwa walengwa, au masharti yaliyowekwa hayana uhalisia. Kamati ina maoni kuwa, ili kufanikisha azma ya mradi huu kuna umuhimu wa kuutangaza mfuko wa maendeleo ya vijana na kutathmini vigezo vilivyowekwa.

2.5 Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati

Mheshimiwa Spika, wakati wa uchambuzi wa Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, Kamati ilitoa maoni, ushauri na mapendekezo mbalimbali ili kuboresha utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi hiyo. Naomba kulitaarifu Bunge lako tukufu kwamba kwa sehemu kubwa Serikali imizingatia maoni na ushauri wa Kamati. Hata hivyo, kuna baadhi ya maoni na ushauri ambayo yamezingatiwa kwa sehemu na machache kutozingatiwa kabisa.

Mfano wa ushauri uliozingatiwa kikamilifu ni pamoja na ushauri juu ya muundo wa bajeti ya matumizi ya kawaida ambapo Kamati ilishauri Ofisi ya Waziri Mkuu kuandaa bajeti ya mwaka 2022/2023 yenye kuendana na uhalisia wa mahitaji ya utekelezaji wa vipaumbele na majukumu ya Ofisi hiyo. Kamati imebaini kwamba Ofisi ya Waziri Mkuu imeongeza bajeti ya Matumizi ya Kawaida (OC) sawa na ushauri wa Kamati.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia ilishauri Serikali kuhakikisha kwamba inatoa fedha za kutosha na kwa wakati kutekeleza miradi ya maendeleo. Ushauri huu umezingatiwa kwa sehemu kwa sababu hadi Februari, 2022 wastani wa **asilimia 55.09** ya fedha za maendeleo zilikuwa zimepokelewa. Kamati

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

inaendelea kusitiza Serikali kuendelea kutenga fedha za utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa kutumia fedha za ndani kwa kuwa mwenendo wa upatikanaji wa fedha za nje ni wa kusuasua.

3.0 UCHAMBUZI WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

3.1 Maduhuli

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 Ofisi ya Waziri Mkuu inaomba kuidhinishiwa kukusanya jumla ya Sh. **51,110,000,000** ikilinganishwa na **Sh. 35,086,000,000** katika Mwaka wa Fedha 2021/2022 kama ambavyo imeainishwa katika Jedwali Na. 4. Hii ni na sawa na ongezeko la **asilimia 45** ukilinganisha na makadirio ya makusanyo ya maduhuli kwa mwaka unaoisha.

JEDWALI NA. 4 – Maduhuli kwa Mwaka 2022/2023

FUNGU	MADUHULI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022	MADUHULI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023
Fungu 37 – Ofisi ya Waziri Mkuu (SBU)	5,000,000,000	6,000,000,000
Fungu 27 – Ofisi ya Majili wa Vyama vya Siasa	36,000,000	10,000,000
Fungu 61 – Tume ya Taifa ya Uchaguzi	50,000,000	100,000,000
Fungu 65 – Ofisi ya Waziri Mkuu (KVAWU)	30,000,000,000	45,000,000,000
JUMLA KUU	35,086,000,000	51,110,000,000

Chanzo: Randama za Ofisi ya Waziri Mkuu na Usanifu wa Kamati

Mheshimiwa Spika, Kamati ina maoni kwamba, ongezeko la makadirio ya makusanyo ya maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 linaakisi azma ya Serikali kuongeza wigo wa mapato yake.

3.2 Matumizi ya Kawaida

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 Ofisi ya Waziri Mkuu pamoja na taasisi zilizo chini yake inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Sh. 86,411,679,000** ikiwa ni Fedha za Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, **Sh. 20,101,214,761** ni mishahara, **Sh. 20,508,752,239** ni ruzuku na **Sh. 45,801,712,000** ni matumizi mengineyo (OC) kama ambavyo imechanganuliwa katika Jedwali Na. 5.

Jedwali Na. 5 – Matumizi ya Kawaida 2022/203

FUNGU	MISHAHARA	MATUMIZI MENGINEYO (OC)	RUZUKU	JUMLA MATUMIZI YA KAWAIDA
Fungu 25 – Ofisi Binafsi ya Waziri Mkuu	1,475,412,000	14,000,000,000	0.00	15,475,412,000
Fungu 37 – Ofisi ya Waziri Mkuu (SBU)	4,915,064,000	15,309,525,000	0.00	20,224,589,000
Fungu 27 – Ofisi ya Majili wa Vyama ya Siasa	953,044,000	2,517,370,000	17,563,000,000	21,033,414,000
Fungu 61 – Tume ya Taifa ya Uchaguzi	4,502,983,000	4,970,031,000	0.00	9,473,014,000
Fungu 65 – Ofisi ya Waziri Mkuu (KVAWU)	5,880,648,761	7,084,636,000	2,945,752,239	15,911,037,000
Fungu 15 – Tume ya Usuluhishi na Uamuzi	2,374,063,000	1,920,150,000	0.00	4,294,213,000
JUMLA KUU	20,101,214,761	45,801,712,000	20,508,752,239	86,411,679,000

***Chanzo:** Randama za Ofisi ya Waziri Mkuu na Usanifu wa Kamati*

Mheshimiwa Spika, Bajeti ya Matumizi ya Kawaida katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 imeongezeka kwa **asilimia 14.66** ukilinganisha na Mwaka wa Fedha unaoisha ambapo bajeti ya Matumizi ya kawaida ilikuwa **Sh. 75,360,457,000**. Kamati imebaini kwamba, moja kati ya sababu ya ongezeko hili ni maoni ya Kamati kwamba Serikali ipange bajeti kulingana na mahitaji halisi. Aidha, ongezeko hilo linaakisi mahitaji ya kifedha kulingana na sababu mbalimbali za kiuchumi ikiwemo kupanda bei kwa bidhaa na huduma.

Hata hivyo, Kamati inashauri Serikali kuhakikisha kwamba fedha zinazoombwa zinatumika vizuri. Na ili kuhakikisha hili

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

linatekelezwa ipasavyo, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba inawasilisha mbele ya kamati taarifa mbalimbali za utekelezaji wa bajeti kwa mujibu wa Sheria. Taarifa hizo zibainishe na kuainisha matumizi ya kila fedha ili kuweka uwazi katika matumizi ya Serikali kwa wawakilishi wa wananchi.

3.3 Miradi ya Maendeleo

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 Ofisi ya Waziri Mkuu inaomba kuidhinishiwa **Sh. 39,524,949,000** kwa ajili ya Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Sh. 21,760,000,000** ni fedha za ndani, na **Sh. 17,764,949,000** ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, bajeti ya maendeleo katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 imepungua kwa takriban **shilingi bilioni 1.66** ukilinganisha na bajeti ya Mwaka wa Fedha unaoisha kwa sababu baadhi ya miradi haikutengewa fedha kwa kuwa ilikuwa katika hatua za mwisho, na baadhi ilitengewa fedha pungufu. Hata hivyo, baadhi ya miradi ambayo haikuwemo katika bajeti ya Mwaka 2021/2022 inaombewa fedha katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 kama ambavyo Jedwali Na. 6 linaainisha.

Jedwali Na. 6 – Bajeti ya Maendeleo 2022/2023

FUNGU	NAMBA NA JINA LA MRADI	BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023	
		FEDHA ZA NDANI	FEDHA ZA NJE
Fungu 27 – Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa	Mradi Na. 6389 Ujenzi wa Jengo la Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa Dodoma	940,000,000	0.00
Fungu 37 – Ofisi ya Waziri Mkuu (SBU)	Mradi Na. 4429 Programu ya Kuendeleza Kilimo na Uvuvi	0.00	4,108,560,000
Fungu 37 – Ofisi ya Waziri Mkuu (SBU)	Mradi Na. 4937 Mradi wa Ujenzi wa Kiwanda cha Uchaguzi Nyaraka za Serikali	1,880,000,000	0.00
Fungu 61 – Tume ya Taifa ya Uchaguzi	Mradi Na. 6583 Programu ya Kusaidia Uchaguzi Tanzania	940,000,000	0.00
Fungu 65 – Ofisi ya Waziri Mkuu (KVAWU)	Mradi Na. 6205 Programu mu ya Kukiza Kazia za Staha	0.00	13,656,389,000
	Mradi Na. 6581 Programu ya Kukiza Ujuzini chini	12,000,000,000	0.00
	Mradi Na. 4952 Mfuko wa Maendeleo ya Vijana	1,000,000,000	0.00
Fungu 15 – Tume ya Usulu hishi na Uamuzi	Mradi Na. 5505 Kuboresha Shughuli za Taasisi Kuwa za Kisasa	1,000,000,000	0.00
JUMLA Ndogo		21,760,000,000	17,764,949,000
JUMLA KUU		39,524,949,000	

Chanzo: Randama za Ofisi ya Waziri Mkuu na Usanifu wa Kamati

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kwamba, bado kiwango cha fedha ambacho kinatengwa kwa kutumia fedha za nje ni kikubwa ukililinganisha na kile kilichotengwa kwa fedha za ndani.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 Serikali imetenga takriban **shilingi bilioni 1.88** ili kutekeleza **Mradi Na. 4937** - Ujenzi wa Kiwanda cha Uchapaji Nyaraka za Serikali. Katika Mwaka wa Fedha unaoisha, mradi huo ultiengewa **shilingi bilioni 2.5** ambazo kama ilivyoelezwa hapo awali, hakuna fedha iliyopokelewa kutekeleza mradi huo kufikia Februari, 2022.

4.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

4.1 Maoni na Ushauri wa Jumla

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia majadiliano ya kina kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 Kamati inatoa maoni, ushauri na mapendekezo ya jumla kwa mafungu yote kama ifuatavyo: -

i) Kamati ilibaini kuwa ni **asilimia 15** tu ya maduhuli yaliyopangwa kukusanya na ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu) yalikusanywa hadi kufikia tarehe 28 Februari 2022; Kamati inaishauri Serikali kuongeza ubunifu na kasi ya ukusanyaji maduhuli na ijiwekee malengo ya ukusanyaji maduhuli ambao yanaakisi uwezo wa ukusanyaji, na hali halisi ya vyanzo vya mapato. Aidha, Serikali iandae mpango mkakati wa makusanyo ambao utaiwezesha kuandaa taarifa ya kila mwezi ya makusanyo na tathmini ya uwezo wa ukusanyaji maduhuli.

ii) Kamati ilibaini kwamba ni asilimia **42.23** tu ya fedha za nje na na **asilimia 59.38** ya fedha za ndani zilizotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo katika Ofisi ya Waziri Mkuu ndizo zilipatikana. Kamati ina shauri kwamba Serikali ihakikishe kwamba inatoa kwa wakati Fedha za Maendeleo na Matumizi Mengineyo ili kuziwezesha taasisi na idara za Serikali

kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Aidha, Serikali ijielekeze zaidi kwenye kutumia vyanzo vyta ndani katika kutekeleza Miradi mbalimbali ya Maendeleo nchini.

iii) Fedha zinazotengwa kwa ajili ya mafunzo ya watumishi zinaweza kusaidia kukuza weledi, kuongeza ufanisi na motisha kwa watumishi iwapo fedha hizo zitatolewa na kutumika inavyostahili. Serikali itumie fedha za mafunzo na matumizi mengineyo kuwapatia watumishi mafunzo ya ndani na nje ya nchi ili kuwawezesha kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi.

iv) Serikali iweke mkakati wa muda mrefu kuhusu namna ya kutekeleza miradi yake yote ya maendeleo ili kuhakikisha miradi hiyo inakamilika kwa wakati. Mkakati huo uainishe kila mradi na kipindi ambacho kinatarajiwa kukamilisha miradi hiyo. Aldha, katika mkakati huo, Serikali iainishe namna ambavyo miradi iliyokamilika itatunzwa na kufanyiwa ukarabati wa mara kwa mara (*routine maintenance*) ili kuitunza miradi hiyo.

4.2 Maoni na Ushauri Mahsusini

4.2.1 Fungu 37 – Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu)

i) Lengo la Serikali kubadilisha Idara ya Mpiga Chapa kuwa Wakala wa Upigaji Chapa, linaweza kuwa na tija likitekelezwa ipasavyo. Hata hivyo, lengo hilo litakosa maana halisi kiutekelezaji iwapo Serikali haitaajiri wataalamu na kuwzesha utekelezaji wa mradi wa Ujenzi wa Kiwanda cha Uchapaji.

ii) Serikali iharakishe mpango wa ujenzi wa Kiwanda cha Uchapishaji Dodoma kwa kutoa fedha kiasi cha **shilingi bilioni 2.5** zilizotengwa kutekeleza mradi huo katika Mwaka wa Fedha 2021/2022 na kutenga fedha za kutosha katika Mwaka wa Fedha 2022/2023. Aidha, Kamati inashauri Serikali kufanya usanifu wa kiwanda hicho kwa kuzingatia masuala yafuatayo: -

- a) Uwezo wa kiwanda kuchapisha nyaraka za idara na taasisi nyingi za Serikali kwa kadri iwezekanavyo;
 - b) Urahisi wa wizara, idara na taasisi zote za Serikali kufika eneo ambapo kiwanda hicho kitajengwa;
 - c) Mifumo ya kiulinzi na kiusalama ili kuhakikisha kwamba nyaraka za Serikali zinazochapishwa hazivuji, kuharibika wala kughushiwa kirahisi; na
 - d) Mahitaji halisi ya mifumo ya teknolojia ya kisasa ambayo itarahisisha utendaji wa kiwanda hicho na kuongeza ufanisi.
- iii) Serikali iandae mpango kazi wa kuajiri wataalamu na kuwapa mafunzo watumishi waliopo katika Idara ya Mpigachapa Mkuu wa Serikali ili Kiwanda Kipyra cha Uchapishaji kitakapojengwa, kihudumiwe na watumishi wenye sifa na weledi. Kwa kufanya hivyo, Serikali itaokoa fedha nyingi na kuzalisha ajira za kudumu kwa vijana wetu wenye ujuzi wa masuala ya uchapishaji na kuondokana na mazoea ya kuchapisha nyaraka za Serikali kwa watu na makampuni binafsi.

4.2.2 Fungu 65 – Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu)

- i) Serikali ihakikishe kwamba, inamrahisishia mwananchi kupata taarifa kuhusu fursa zinazopatikana katika programu mbalimbali ambazo zinaweza kumsaidia kujieleta maendeleo. Aidha, Serikali itengeneze mazingira wezeshi na ya kisera, kisheria na kiutekelezaji kwa lengo la kumpunguzia mwananchi huyo gharama sizizo za lazima wakati akizitafuta fursa hizo.
- ii) Uwekaji wa vigezo na viwango vya upatikanaji wa watu wenye mahitaji maalumu kwa lengo la kuwawezesha, unapoteza maana iwapo vigezo hivyo havitazingatiwa. Aidha, vigezo vinavyowekwa visipokuwa na uhalisia, vitaathiri mafanikio na ufikiaji wa lengo la Programu ya Maendeleo

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

kwa vijana. Serikali izingatie vigezo vilivyowekwa ili kutoa fursa sawa kwa watu wenye ulemavu.

iii) Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, ihakikishe kwamba inachangamkia fursa za ajira zinazopatikana katika nchi nyingine. Aidha, Serikali iweke mifumo thabiti ya kuhakikisha kwamba, watanzania watakaopata fursa ya ajira hizo, haki zao za msingi na kisheria zinalindwa ikwemo uhifadhi wa utu wao. Vilevile Serikali ifanye tafiti za kujuu madhara yanayoweza kuambatana na ajira hizo ili kupima iwapo kuna ulazima kwa wananchi wake kwenda kufanya kazi hizo nje ya nchi.

iv) Serikali itathmini vigezo vilivyowekwa katika **Mradi Na. 4952 - Mfuko wa Maendeleo ya Vijana** ili vijana wengi zaidi ambao wanastahili kupatiwa mikopo kupata mikopo hiyo bila kikwazo. Aidha, Serikali ihakikishe kwamba inatengeneza mfumo madhubuti ambao utawezesha mikopo hiyo kurejea kwa wakati ili vijana wengi zaidi waweze kunufaika na mradi huu.

v) Katika **Mradi Na. 6581 Programu ya Kukuza Ujuzi Nchini**, Serikali ihakikishe kwamba ujuzi unaopatikana katika vitalu nyumba (*greenhouses*) na uanagenzi (*apprenticeship*) haupotei. Aidha, Serikali ione umuhimu wa kutoa ruzuku ya vifaa vya ujenzi na malighafi kwa vijana wanaoshiriki katika programu hii ili vijana hao waweze kumudu gharama muhimu kama vile kujenga vitalu nyumba kwa gharama nafuu.

vi) Ili kuongeza ufanisi katika masuala yanayohusu mafunzo kwa vitendo (*internship*) na uanagenzi (*apprenticeship*), Ofisi ya Waziri Mkuu ishirikiane na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ili kufanya mabadiliko katika mitaala kwa lengo la kuwapatia vijana mafunzo na kupunguza gharama za mafunzo hayo baada ya kumaliza masomo.

vii) Serikali ione namna ambayo mikopo itokanayo na Mfuko wa Maendeleo ya Vijana inawanufaisha vijana ambao tayari wana mafunzo mbalimbali yanayotolewa na programu hii.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Aidha, kamati inashauri kwamba Serikali isimamie kikamilifu upatikanaji wa vijana wanaoshiriki programu hii ili makundi maalum yawakilishwe kikamilifu.

viii) Serikali ione umuhimu wa kuunganisha mifuko na programu mbalimbali zinazohusu uwezeshaji wa vijana ili kuwe na sera, na utaratibu wa kitaifa wa wa kuwawezesha vijana. Sambamba na hilo, Serikali iandae mfumo Madhubuti wa marejesho ya fedha zinazotolewa kwa vijana ziwanufaishe vijana wengine.

4.2.3 Fungu 61 – Tume ya Taifa ya Uchaguzi

- i) Ili kupanua wigo wa wapiga kura, Serikali itoe elimu ya mpiga kura nchini na kuwaeleimisha wananchi kuhusu umuhimu wa kujitokeza kwa wingi siku ya kupiga kura. Elimu hii itolewe kwa ubunifu ambao utawezesha hadhira kubwa zaidi ya Watanzania kuelimishwa kuhusu haki hii ya msingi ya kikatiba.
- ii) Tume ya Taifa ya Uchaguzi ihuishe daftari la mpiga kura ili kila Mtanzania mwenye sifa zakupiga kura aweze kuandikishwa bila kubaguliwa kwa misingi yoyote.

4.2.4 Fungu 27 - Ofisi ya Msajili wa Vyama vy'a Siasa

- i) Ofisi ya Msajili wa Vyama vy'a Siasa itoe elimu ya kutosha kwa wasimamizi, wasaidizi wa uchaguzi, vyama vy'a siasa na wagombea kuhusu Sheria zinazosimia uchaguzi zinazoratibiwa na Ofisi ya Msajili wa Vyama vy'a Siasa. Elimu hii itolewe kabla na baada ya uchaguzi.
- ii) Taarifa za vyama vy'a siasa katika rejista za kisheria zihuishwe ipasavyo na kwa wakati ili kuwawezesha watumiaji na wadau mbalimbali wa taarifa hizo kuwa na taarifa sahihi na kwa wakati.

5.0 HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha taarifa hii. Aidha, napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na hatimaye kukamilika kwa taarifa hii. Naomba majina yao yaingie kwenye kumbukumbu za kudumu za Bunge kama yalivyo wasilishwa katika taarifa hii; nayo ni kama ifuatavyo: -

1. Mhe. Dkt. Joseph Kizito Mhagama, Mb. – Mwenyekiti
2. Mhe. Najma Murtaza Giga, Mb. – Makamu Mwenyekiti
3. Mhe. Abdullah Ali Mwinyi, Mb.
4. Mhe. Emmanuel Adamson Mwakasaka, Mb.
5. Mhe. Wanu Hafidh Ameir, Mb.
6. Mhe. Joseph Anania Tadayo, Mb.
7. Mhe. Edward Olelekaita Kisau, Mb.
8. Mhe. Zainabu Athumanji Katimba, Mb.
9. Mhe. Ng'wasi Damas Kamani, Mb.
10. Mhe. Lemburis Saputu Mollel Noah, Mb.
11. Mhe. Asha Abdallah Juma, Mb.
12. Mhe. Elibariki Immanuel Kingu, Mb.
13. Mhe. Omar Ali Omar, Mb.
14. Mhe. Suma Ikenda Fyandomo, Mb.
15. Mhe. Salum Mohammed Shaafi, Mb.
16. Mhe. Ahmed Juma Ngwali Dedi, Mb.
17. Mhe. Agnesta Lambert Kaiza, Mb.
18. Mhe. Yahaya Omari Massare, Mb.
19. Mhe. Jacqueline Ngonyani Msongozi, Mb.
20. Mhe. Hussein Nassor Amar, Mb.
21. Mhe. Khadija Shaaban Taya, Mb.
22. Mhe. Agnes Elias Hokororo, Mb.
23. Mhe. Luhaga Joelson Mpina, Mb.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati naomba nichukue fursa hii kumpongeza Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb) kwa uongozi wake wa Shughuli za Serikali bungeni na kwa kuwasilisha makadirio ya mapato na

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

matumizi ya Ofisi yake kwa ufanisi. Aidha, naomba nichukue fursa hii kuwashukuru mawaziri na naibu mawaziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, ambao wanamsaidia kwa karibu Mheshimiwa Waziri Mkuu kutekeleza majumu yake katika ofisi hiyo. Kwa umuhimu wao, naomba niwatambue kama ifuatavyo: -

1. Mhe. George Boniface Simbachawene, Mb. – Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu)
2. Mhe. Prof. Joyce Lazaro Ndalichako, Mb. – Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu)
3. Mhe. Ummy Hamisi Nderiananga, Mb. – Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu)
4. Mhe. Paschal Patrobass Katambi, Mb – Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu)

Mheshimiwa Spika, naomba pia niwashukuru watendaji wote wa Ofisi ya Waziri Mkuu pamoja na taasisi zake kwa ushirikiaono walioupatia Kamati wakiongozwa na makatibu wakuu wa Ofisi hiyo Dkt. John Anthony Jingu – (Sera, Bunge na Uratibu) na Dkt. Jamal Adam Katundu – (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu) wakisaidiwa na naibu katibu mkuu Ndg. Kaspar Kaspar Mmuya (Sera, Bunge na Uratibu).

Mheshimiwa Spika, mwisho lakini sio kwa umuhimu, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Nenelwa Mwihambi, *ndc* kwa kuratibu vema shughuli za Kamati na Bunge kwa mujibu wa Katiba ya Nchi. Aidha, nawashukuru Mkurugenzi wa Idara ya kamati za Bunge Ndg. Athuman Hussein, Mkurugenzi Msaidizi Ndg. Gerald Magili na Makatibu wa Kamati hii Ndg. Yona Kirumbi na Ndg. Elihaika Mtui wakisaidiwa na Bi. Theresia Jacob, kwa kuratibu shughuli za Kamati na kufanikisha kukamilika kwa taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 kama yalivyowasilishwa na mto hoja.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

Dkt. Joseph Kizito Mhagama, Mb

MWENYEKITI

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria

06 Aprili, 2022

NAIBU SPIKA: Ahsante. Sasa namwita Mwenyekiti Kamati ya Bajeti.

MHE. DANIEL B. SILLO – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGUE YA BAJETI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bajeti, kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Bunge - Fungu 42 kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba taarifa yetu hii yote iingie kwenye kumbukumbu Rasmi za Bunge kama ambavyo imewasilisha leo asubuhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kifungu cha 9(1)(c) cha Sheria ya Bajeti Namba 11 ya Mwaka 2015, Kamati ilikutana na Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchomba, Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Balozi Pindi Chana Mbunge, aliyekuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Uratibu na Bunge, Mheshimiwa Hamad Hassan Chande Mbunge, Naibu Waziri wa Fedha na Mipango pamoja na Katibu wa Bunge Bi. Nenelwa Mwihambi, (*ndc*) ili kupitia utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 pamoja na kufanya mashauriano kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha wa 2022/2023.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa hii inatoa mrejesho kwa Bunge lako Tukufu kuhusu utekelezaji wa Bajeti na majukumu ya Mfuko wa Bunge hadi kufikia tarehe 15 Machi, 2022, pamoja na vipaumbele na masuala muhimu yanayopendekezwa katika Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapitio ya utekelezaji wa Bajeti ya mwaka wa fedha 2021/2022; katika kuwezesha Ofisi ya Bunge kutekeleza majukumu yake, Kifungu cha 32 cha Sheria ya Uendeshaji wa Bunge kama ilivyofanyiwa rejea mwaka 2015 kilanzisha Mfuko wa Bunge. Hivyo, Mfuko wa Bunge hutengewa fedha kwa ajili ya kugharamia mahitaji mbalimbali, ambapo asilimia 85 ya mahitaji hayo ya fedha hutumika kugharamia Mikutano ya Bunge pamoja na Kamati, Posho ya Jimbo na Usafiri wa Wabunge, Matibabu kwa Wabunge na sehemu inayobaki asilimia 15 hutumika kutekeleza shughuli za utawala, uendeshaji na miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Bunge inatekeleza Bajeti yake kwa kuzingatia Sheria ya Bajeti Sura ya 439, Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma Sura 348 pamoja na Mpango Mkakati wa Ofisi ya Bunge yaani *Strategic Plan 2021/2022-2025/2026* na Mpango wa Muda wa Kati (*Medium Term Expenditure Framework*) wenyewe lengo la kuweka bayana mahitaji ya fedha za Mfuko wa Bunge kwa kuzingatia malengo yanayotarajiwa kutekelezwa katika vipindi husika vya makadirio hayo. Vilevile Utekelezaji wa Bajeti umezingatia malengo yaliyotarajiwa kutekelezwa katika vipindi husika na makisio ya Bajeti yamezingatia kuboresha na kutoa huduma mbalimbali kulingana na mahitaji halisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bajeti ya Mfuko wa Bunge iliyoidhinishwa kwa mwaka 2021/2022; katika mwaka wa fedha 2021/2022 Mfuko wa Bunge uliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 128.8 sawa na ongezeko la asilimia 5.8 ikilinganishwa na bajeti ya mwaka 2020/2021. Kati ya fedha hizo, kiasi cha shilingi bilioni 23.2 ni fedha za mishahara, shilingi bilioni 98.6 ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na shilingi bilioni

6.9 kwa ajili ya Mpango wa Maendeleo. Katika fedha za maendeleo, shilingi bilioni 5.0 ni fedha za ndani na Shilingi Bilioni 1.9 ni fedha za nje. Aidha, Mfuko wa Bunge uliidhinishiwa kukusanya maduhuli ya kiasi cha shilingi 124,002,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia tarehe 15 Machi, 2022 Fungu 42 ilikuwa limepokea jumla ya shilingi bilioni 80.6 sawa na asilimia 62.57 ya Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge katika fedha hizo shilingi bilioni 5.0 ilikuwa ni mishahara; bilioni 6.8 ilikuwa ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi milioni 759.2. Kwa upande wa maduhuli, Ofisi ya Bunge iliweza kukusanya jumla 112 sawa na asilimia 90 ya lengo la kukusanya Shilingi Bilioni 124.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mafanikio ya Utekelezaji wa Majukumu ya Mfuko wa Bunge kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ni kama ilivyoonyeshwa katika taarifa yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfuko wa Bunge umeweza kufanikisha uratibu na usimamizi wa uendeshaji wa Mikutano Mitatu ya Bunge na Mikutano Minne ya Kamati za Bunge kama ifuatavyo:-

(i) Kuratibu kuulizwa kwa jumla ya maswali ya kawaida 388 na ya nyongeza 1,052 yaliyoulizwa Bungeni na kujibiwa na Serikali;

(ii) Kuratibu jumla ya maswali 30 ya papo kwa papo yaliyoulizwa moja kwa moja kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu na kujibiwa;

(iii) Kupokea, kuhariri na kuwasilisha Serikalini maswali 1,242 ya Wabunge kwa ajili ya kupatiwa majibu;

(iv) Kuratibu shughuli za Miswada tisa na maazimio mawili (2) ya kimataifa yanayotokana na Kamati za Kudumu za Bunge yaliyojadiliwa na kupitishwa au kuridhiwa na Bunge na kuwasilishwa Serikalini kwa utekelezaji;

(v) Kuratibu shughuli za Kamati ambazo zilifanya uchambuzi wa Miswada ya Sheria, Sheria Ndogo, Taarifa za Uwekezaji wa Mitaji ya Umma, Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Taarifa za Utendaji wa Wizara na Taasisi za Serikali na ufuatiliaji wa utekelezaji wa Afua za UKIMWI;

(vi) Kuratibu ziara za ukaguzi wa miradi ya maendeleo mbalimbali ya Kamati 13 za Kudumu za Bunge kama inavyoelekezwa na Kanuni za Kudumu za Bunge. Aidha Mfuko wa Bunge iliwezesha ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyofanyika katika nchi ya DRC pamoja na Ethiopia;

(vii) Kuchambua Mwongozo wa Maandalizi ya Bajeti kwa Mwaka 2022/2023 na kuwasilisha Bungeni;

(viii) Bunge kupitia Kamati ya Kudumu ya Bunge la Bajeti ilipitia na kutoa ushauri juu ya mapendekezo ya matumizi ya fedha za Mkopo wa *IBF* ya shilingi 1.3 Triliioni za UVIKO-19; na

(ix) Kuwezesha Bunge kujadili Bungeni Taarifa ya Hali ya Uchumi kwa mwaka 2021/2022, Mapendekezo ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2022/2023 na Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2022/2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kuwezesha Ushiriki wa Bunge katika Mikutano ya Kimataifa; katika medani za Kimataifa Mfuko wa Bunge umeweza kufanikisha yafuatayo:-

(i) Kuratibu ushiriki wa Bunge la Tanzania katika Mkutano Mkuu wa Hamsini (50) wa Jukwaa la Mabunge ya *SADC* uliofanyika Afrika Kusini;

(ii) Kuratibu ushiriki wa Mheshimiwa Spika, Katibu wa Bunge na wa wawakilishi wengine watano katika mikutano ya 143 na 144 ya Umoja wa Mabunge yaani *IPU*; na

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

(iii) Kuratibu ushiriki wa vikao vya Kamati Tendaji ya CPA Kanda ya Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kuratibu Ofisi za Viongozi hadi kufikia tarehe 15 Machi 2022, Mfuko wa Bunge umeweza kufanikisha utekelezaji wa majukumu mbalimbali ya Ofisi ya Spika; Ofisi ya Naibu Spika na Ofisi ya Katibu wa Bunge na kuwezesha kusimamia uendeshaji shughuli zinazohusu Ofisi ya Bunge kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutolewa kwa Huduma za Matibabu; Mfuko wa Bunge - Fungu 42 umewezesha Waheshimiwa Wabunge na familia zao kupatiwa huduma ya matibabu kupitia utaratibu wa Bima ya Afya. Aidha, Mfuko wa Bunge umeendelea kuimarisha Kituo cha Afya cha Bunge kwa kununua vifaa tiba pamoja na madawa mbalimbali kwa ajili ya kuwahudumia Waheshimiwa Wabunge pamoja na Watumishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ukarabati wa Majengo ya Ofisi pamoja na Ujenzi wa Makazi ya Viongozi; hadi kufikia tarehe 15 Machi, 2022 Mfuko wa Bunge Fungu 42 umeweza kusimamia na kuratibu kazi za maendeleo zifuatazo:-

(a) Kuendelea na ukarabati wa majengo ya Ofisi ambapo matengenezo mbalimbali yamefanyika katika kumbi za Bunge kama ifuatavyo:-

(i) Kuboresha muonekano wa ndani wa Ukumbi wa Bunge na majengo ya Bunge;

(ii) Kufanya ukarabati katika Ukumbi wa Msekwa ikiwa ni pamoja na kuweka zulia jipya;

(iii) Kukamilisha ujenzi wa ghorofa ya tano;

(iv) Kufanya maandalizi ya Ujenzi wa nyumba za viongozi wa Bunge - Dodoma ikiwa ni kuandaa michoro, kufanya makadirio ya gharama za ujenzi pamoja na taratibu za kumpata Mkandarasi; na

(v) Kuratibu na kusimamia mafunzo mbalimbali kwa Wabunge na Watumishi kuititia mradi wa kulijengea uwezo Bunge (LSP II) na mradi wa maboresho wa usimamizi wa kifedha ambapo mafunzo kwa Waheshimiwa Wabunge pamoja na Watumishi yalitolewa katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa majukumu mengine; hadi kufikia tarehe 15 Machi, 2022, Mfuko wa Bunge umeweza kufanikisha utekelezaji wa majukumu mbalimbali kama inavyoonekana katika taarifa yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo ya makadirio ya Bajeti ya Mfuko wa Bunge kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Bajeti ya Mfuko wa Bunge kwa mwaka wa fedha 2022/2023; katika mwaka wa fedha 2022/2023, Mfuko wa Bunge unaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi billioni 132.7 sawa na ongezeko la asilimia 2.98 ikilinganishwa na bajeti ya mwaka 2021/2022. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 23.6 zimepangwa kwa ajili ya mishahara ya Wabunge na Watumishi, shilingi bilioni 103.6 zimepangwa kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na shilingi bilioni 5.4 zimepangwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo, ambapo Shilingi Bilioni 4.7 ni fedha za ndani na shilingi millioni 700 ni fedha za nje. Aidha, hadi kufikia 30 Juni, 2023 Ofisi imepanga kukusanya maduhuli yenyе jumla ya shilingi millioni 131.7.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla Makadirio ya Bajeti ya Mfuko wa kwa mwaka wa fedha 2022/2023 yameongezeka kwa takribani shilingi bilioni 3.8. Ongezeko hilo limetokana na shughuli zifuatazo:-

(i) Ununuzi wa magari matatu ya viongozi wapya wa Bunge;

(ii) Mafunzo kwa Waheshimiwa Wabunge, Kamati za Bunge na Tume ya Utumishi wa Bunge;

(iii) Kuboresha Bima ya Afya kwa Wabunge kulingana na masharti ya Mkataba;

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

(iv) Ushiriki katika michezo ya Mabunge ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa Wabunge na Watumishi nje ya nchi; na

(v) Ushiriki katika Mikutano ya Kimataifa na vyama vya Kibunge ambavyo Bunge ni Mwanachama pamoja na kuimarishwa kwa shughuli za uendeshaji wa Ofisi ya Bunge Dodoma, Dar es Salaam na Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa Kamati katika ulinganiso wa Bajeti ya Mfuko wa Bunge kwa mwaka 2021/2022 na 2022/2023 umebaini kwamba, fedha za mishahara zimeongezeka kwa asilimia 1.9, fedha za matumizi mengineyo zimeongezeka kwa asilimia 5.0, fedha za maendeleo zimepungua kwa asilimia 23 kutokana na kupungua kwa fedha za wafadhili na kukamilika kwa baadhi ya miradi ya mwaka wa fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, Maandalizi ya Bajeti kwa mwaka wa fedha 2022/2023 yamezingatia mahitaji ya msingi yakiwemo mahitaji ya shughuli za Bunge kwa maana Mikutano ya Bunge na Kamati za Bunge na uendeshaji wa Ofisi. Hivyo, fedha zimegawanywa katika Mafungu makuu matatu ambayo ni Programu 10 ambayo ni Utawala na Uendeshaji), Programu 20 Shughuli za Bunge na Programu 30 Ofisi ya Katibu wa Bunge. Katika mwaka wa fedha 2022/2023 Mfuko wa Bunge unatarajia kutekeleza shughuli mbalimbali kama zinavyoonekana kwenye taarifa ya Kamati ukurasa 13 na ukurasa 14.

Mheshimiwa Naibu Spika, Maoni na Ushauri wa Kamati; Ofisi za Wabunge Majimboni, Kamati inaendelea kusisitizia kuhusu suala la ujenzi wa Ofisi za Wabunge majimboni na kuziwekea samani kwa utekelezaji wa majukumu yao kwa ufanisi pindi wanapokuwa majimboni.

Aidha, kwa kuwa suala hili walikasimiwa Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa ajili ya utekelezaji wake, ni vema Bunge likapata mrejesho wa utekelezaji wa ujenzi wa Ofisi hizi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuongeza eneo la Bunge; kwa kuwa Ofisi ya Bunge imezungukwa na maeneo mengine ya Serikali yakiwemo maghala yaani *warehouses* ni vema sasa Bunge likaona uwezekano wa kutafuta namna ya kuyamiliki maeneo haya kwa lengo la kupanua wigo wa maeneo yanayozunguka Ofisi ya Bunge. Hii itasaidia kuongeza ujenzi wa majengo mengine ya ofisi, eneo la maegesho ya magari ya viongozi pamoja na kuimarisha usalama.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushiriki wa Bunge kwenye Vyama vya Kibunge; kwa kuwa Bunge ni Mwanachama wa Vyama vya Kibunge mbalimbali kuna umuhimu wa kuongeza bajeti ya Bunge ili kuliwezesha Bunge kushiriki kikamilifu katika Mkutano wa Vyama hivyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, michezo kwa Waheshimiwa Wajumbe; kwa kuzingatia kwamba wewe ni mwanamichezo na Mheshimiwa Spika pia ni mwanamichezo na Bunge linashiriki kwenye mashindano mbalimbali ya michezo ya Afrika Mashariki. Hata hivyo, tumeshuhudia Waheshimiwa Wabunge wakikosa maeneo ya kufanya mazoezi. Hivyo ni wakati muafaka kwa Serikali kupitia Mfuko wa Bunge kutenga bajeti ili kufanikisha azma ya kujenga uwanja wa kufanya mazoezi yaani *Sports Arena*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho; naomba nihitimishe kwa kukushukuru wewe binafsi na kumshukuru pia Mheshimiwa Spika kwa kuongoza vema mashauriano kati ya Kamati ya Bajeti na Serikali. Pia naomba kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchomba, Waziri wa Fedha na Mipango na Mheshimiwa Hamad Hassan Chande, Naibu Waziri wa Fedha na Mipango kwa ushirikiano wao kwa Kamati. Aidha, kipekee nimshukuru Mheshimiwa Balozi Dkt. Pindi Chana, aliyekuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Bunge kwa kushirikiana na Kamati wakati wa majadiliano kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumshukuru Mheshimiwa Omary Kigua Mbunge, Makamu Mwenyekiti wa

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Kamati ya Bunge ya Bajeti kwa ushirikiano wake katika kuiongoza Kamati. Vile vile napenda kuwashukuru wajumbe wa Kamati hii kwa umakini wao mkubwa katika kujadili na kutoa maoni na mapendekezo mbalimbali kuhusu Bajeti ya Mfuko wa Bunge. Naomba majina yao yaingie kwenye Taarifa Rasmi za Bunge yaani *Hansard*.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii, kumshukuru Ndugu Nenelwa Mwihambi (*ndc*), Katibu wa Bunge kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Aidha, napenda kuipongeza na kuishukuru Sekretarieti ya Kamati ikiongozwa na Mkurugenzi wa Idara ya Bajeti Ndugu Michael Kadebe kwa uratibu na kutoa ushauri wa kitaalam ambao umesaidia Kamati katika kukamilisha taarifa hii.

Mheshimiwa Nailbu Spika, baada ya maelezo hayo naliomba Bunge lako Tukufu sasa Ilijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mfuko wa Bunge Fungu 42, kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 kama yalivyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

MAONI YA KAMATI KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MFUKO WA BUNGE KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022 PAMOJA NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

1.0. UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bajeti, kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Bunge (Fungu 42) kwa Mwaka wa Fedha 2021/22 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2022/23.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kifungu cha 9 (1) (c) cha Sheria ya Bajeti Na.11 ya Mwaka 2015, Kamati ilikutana na Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba (Mb), Waziri wa Fedha na Mipango, Mhe. Balozi Pindi Chana (Mb), aliyekuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Uratibu na Bunge, Mheshimiwa Hamad Hassan Chande, (Mb) Naibu Waziri wa Fedha na Mipango pamoja na Katibu wa Bunge Ndg. Nenelwa Mwihambi, *ndc* ili kuitia utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2021/22 pamoja na kufanya mashauriano kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha wa 2022/23.

Mheshimiwa Spika, taarifa hii inatoa mrejesho kwa Bunge lako Tukufu kuhusu utekelezaji wa Bajeti na majukumu ya Mfuko wa Bunge hadi kufikia tarehe 15 Machi, 2022, pamoja na vipaumbele na masuala muhimu yanayopendekezwa katika Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa fedha 2022/2023.

2.0. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

Mheshimiwa Spika, katika kuwezesha Ofisi ya Bunge kutekeleza majukumu yake, Kifungu cha 32 cha Sheria ya Uendeshaji wa Bunge kama ilivyofanyiwa rejea mwaka 2015 kilianzisha Mfuko wa Bunge. Hivyo, Mfuko wa Bunge hutengewa fedha kwa ajili ya kugharamia mahitaji mbalimbali, ambapo asilimia 85 ya mahitaji hayo ya fedha hutumika kugharamia Mikutano ya Bunge pamoja na Kamati, Posho ya Jimbo na Usafiri kwa Wabunge, Matibabu kwa Wabunge na sehemu iliyobaki asilimia 15 hutumika kutekeleza shughuli za utawala, uendeshaji na miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Bunge inatekeleza Bajeti yake kwa kuzingatia Sheria ya Bajeti Sura ya 439, Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma Sura 348 pamoja na Mpango Mkakati wa Ofisi ya Bunge (Strategic Plan 2021/2022-2025/2026) na Mpango wa Muda wa Kati (Medium Term Expenditure Framework) wenyewe lengo la kuweka bayana mahitaji ya fedha za Mfuko wa Bunge kwa kuzingatia malengo yanayotarajiwa kutekelezwa katika vipindi husika vya

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

makadirio hayo. Vilevile Utekelezaji wa Bajeti umezingatia malengo yaliyotarajiwa kutekelezwa katika vipindi husika na makisio ya Bajeti yamezingatia kuboresha na kutoa huduma mbalimbali kulingana na mahitaji halisi.

2.1. Bajeti ya Mfuko wa Bunge iliyoidhinishwa kwa mwaka 2021/2022

Mheshimiwa Spika, Katika mwaka wa fedha 2021/2022 Mfuko wa Bunge uliidhinishiwa jumla ya kiasi cha **Shilingi 128,873,377,000** sawa na ongezeko la asilimia 5.8 ikilinganishwa na bajeti ya mwaka 2020/21. Kati ya fedha hizo, kiasi cha **Shilingi 23,205,762,000** ni fedha za Mishahara, **Shilingi 98,670,144,000** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo, (OC) na **Shilingi 6,997,471,000** kwa ajili ya Mpango wa Maendeleo. Katika fedha za maendeleo, **Shilingi 5,000,000,000** ni fedha za ndani na **Shilingi 1,997,471,000** ni fedha za nje. Aldha, Mfuko wa Bunge uliidhinishiwa kukusanya maduhuli ya kiasi cha **Shilingi 124,002,000**.

2.2. Fedha zilizopokelewa hadi kufikia tarehe 15 Machi, 2022

Mheshimiwa Spika, Utekelezaji wa Bajeti ya Fungu 42 uliwezekana kupitia upatikanaji wa fedha kutoka Hazina uliozingatia mgao wa kila mwezi wa Matumizi Mengineyo, fedha za Miradi ya Maendeleo na mahitaji ya Mishahara. Hivyo basi mtiririko wa fedha ulikuwa kama ifuatavyo:-

2.2.1. Mishahara

Mheshimiwa Spika. Hadi kufikia tarehe 15 Machi 2022, Mfuko wa Bunge umepokea kiasi cha **Shilingi 15,049,164,000.00** ambazo ni sawa na asilimia 65 ya fedha zote za mishahara zilizoidhinishwa na Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022. Kiasi hiki kimeongezeka toka asilimia 46 ya mwaka 2020/21.

2.2.2. Matumizi Mengineyo

Mheshimiwa Spika. Fedha za Matumizi Mengineyo (OC) zilizopokelewa hadi kufikia tarehe 15 Machi, 2022 zilifikia jumla

ya **Shilingi 64,833,560,000.00** ambazo ni sawa na asilimia 66 ya fedha zote za matumizi mengineyo zilizoidhinishwa na Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022. Kiasi hiki kimeongezeka toka asilimia 55 ukilinganisha na mwaka wa fedha 2020/21

2.2.3. Fedha za Miradi ya Maendeleo

Mheshimiwa Spika. Hadi kufikia tarehe 15 Machi, 2022 kiasi cha **Shilingi 759,239,000.00** ikiwa ni fedha za nje zilipokelewa sawa na asilimia 38 ya fedha za nje kupitia Mradi wa Kulijengea Uwezo Bunge (LSP II) pamoja na Programu ya Maboresho ya Usimamizi Bora wa Fedha za Umma (PFMRP). Hata hivyo, hadi kufikia tarehe 15 Machi, 2022 hakuna fedha za ndani zilizopokelewa kwa kuwa shughuli zinazo husisha miradi ya Ukarabati wa Majengo ya Bunge na Ujenzi wa Miundombinu ya Bunge bado hazjiaflikia hatua ya kutolewa *Certificate*.

2.2.4. Maduhuli

Mheshimiwa Spika. Katika Mwaka wa Fedha 2021/2022 Mfuko wa Bunge uliidhinishiwa kukusanya kiasi cha Maduhuli ya **Shilingi 124,002,000**. Hadi kufikia tarehe 15 Machi, 2022 kiasi cha **Shilingi 112,002,515** kimekusanya sawa na asilimia 90. Makusanyo ya maduhuli haya yametokana na Kodi ya Pango, kukodisha kumbi za Mikutano na malipo ya umeme na maji kutoka kwa mto huduma anayeendesha mgahawa wa Bunge.

3.0. MAFANIKIO YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA MFUKO WA BUNGE KWA MWAKA WA FEDHA 2021/22.

3.1. Mapitio ya utekelezaji wa shughuli za Mfuko wa Bunge zilizopangwa kufanyika katika kipindi cha mwaka 2021/2022

Mheshimiwa Spika, Katika kipindi cha Julai, 2021 hadi tarehe 15 Machi, 2022 Mfuko wa Bunge (Fungu – 42) umefanikisha kutekeleza shughuli mbalimbali zikiwemo za uratibu wa shughuli za Bunge kwa kuzingatia Mpango Mkakati wa Ofisi

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

(Strategic Plan 2021/2022-2025/2026), Maelekezo ya Serikali katika Mwongozo wa Bajeti (Budget Guidelines) pamoja na Mpango wa Muda wa Kati (Medium Term Expenditure Framework). Utekelezaji wa shughuli hizo ulikuwa kama ifuatavyo: -

3.2. Utekelezaji wa Mfumo wa Bunge Mtandao (e-Parliament)

Mheshimiwa Spika. Mfuko wa Bunge ulisimamia uendeshaji wa shughuli za Bunge kwa kutumia TEHAMA kupitia Mfumo wa Bunge Mtandao (e-parliament) na kufanya maboresho ya miundombinu ya mfumo kwa kuongeza madirisha (module) ya mfumo kutoka matatu hadi kumi ikiwemo kuwezesha mfumo kutuma nyaraka za Bunge kwa Wabunge na wadau wengine; mfumo kupatikana nje ya maeneo ya Bunge kwa kutumia mfumo wa VPN; madirisha (module) ya mfumo yameongezeka kutoka matatu hadi kufikia kumi; na Mbunge kutaarifiwa (notification) kwenye kishikwambi (Tablet) chake punde nyaraka inapotumwa;

3.3. Uratibu wa shughuli za Mikutano ya Bunge pamoja na Kamati za Bunge

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Bunge umeweza kufanikisha uratibu na usimamizi wa uendeshaji wa Mikutano Mitatu ya Bunge na Mikutano Minne ya Kamati za Bunge, kama ifuatavyo:-

- (i) Kuratibu kuulizwa kwa jumla ya maswali ya kawaida 388 na ya nyongeza 1,052 yaliyoulizwa Bungeni na kujibiwa na Serikali;
- (ii) Kuratibu jumla ya maswali 30 ya papo kwa papo yaliyoulizwa moja kwa moja kwa Mhe. Waziri Mkuu na kujibiwa;
- (iii) Kupokea, kuhariri na kuwasilisha Serikalini maswali 1,242 ya Wabunge kwa ajili ya kupatiwa majibu;

- (iv) Kuratibu shughuli za Miswada tisa (9) na maazimio mawili (2) ya kimataifa yanayotokana na Kamati za Kudumu za Bunge yallyojadiliwa na kuditishwa/kuridhiwa na Bunge na kuwasilishwa Serikalini kwa utekelezaji;
- (v) Kuratibu shughuli za Kamati ambazo zilifanya uchambuzi wa Miswada ya Sheria, Sheria Ndogo, Taarifa za Uwekezaji wa Mitaji ya Umma, Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali, Taarifa za Utendaji wa Wizara na Taasisi za Serikali na ufuutiliaji wa utekelezaji wa Afua za UKIMWI;
- (vi) Kuratibu ziara za ukaguzi wa miradi ya maendeleo mbalimbali ya Kamati Kumi na tatu (13) za Kudumu za Bunge kama inavyoelekezwa na Kanuni za Kudumu za Bunge, aidha Mfuko wa Bunge iliwezesha ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyofanyika nje ya nchi, DRC (Kinshasa) na Ethiopia;
- (vii) Mafunzo maalumu kwa Wenyeviti, Makamu Wenyeviti, Makamishna na Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge ndani ya nchi yalifanyika.
- (viii) Kuchambua Mwongozo wa Maandalizi ya Bajeti kwa Mwaka 2022/23 na kuwasilisha Bungeni;
- (ix) Bunge kupitia Kamati ya Kudumu ya Bajeti lilipitia na kutoa ushauri juu ya mapendekezo ya matumizi ya fedha za Mkopo wa Sh. 1.3 Trillioni za UVJKO-19; na
- (x) Kuwezesha Bunge kujadili Bungeni Taarifa ya Hali ya Uchumi kwa Mwaka 2021/22, Mapendekezo ya Mpango na Bajeti ya Taifa wa Mwaka 2022/23 na Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2022/23.

3.4. Kuwezesha ushiriki wa Bunge katika Mikutano ya Kimataifa

Mheshimiwa Spika, katika medani za Kimataifa Mfuko wa Bunge umeweza kufanikisha yafuatayo;

- (i) Kuratibu ushiriki wa Bunge la Tanzania katika mikutano mkuu wa hamsini (50) wa Jukwaa la Mabunge ya SADC uliofanyika Afrika Kusini;
- (ii) Kuratibu ushiriki wa Mhe. Spika, Katibu wa Bunge na wa wakilishi wengine watano (5) katika mikutano ya 143 na 144 ya umoja wa Mabunge IPU; na
- (iii) Kuratibu ushiriki wa vikao vya Kamati Tendaji ya CPA Kanda ya Afrika.

3.5. Uratibu wa Ofisi za Viongozi

Mheshimiwa Spika, Hadi kufika tarehe 15 Machi 2022, Mfuko wa Bunge umeweza kufanikisha utekelezaji wa majukumu mbalimbali ya Ofisi ya Spika; Ofisi ya Naibu Spika na Ofisi ya Katibu wa Bunge na kuwezesha kusimamia uendeshaji shughuli zinazohusu Ofisi ya Bunge kwa ujumla.

3.6. Kutolewa kwa huduma za Matibabu

Mheshimiwa Spika. Mfuko wa Bunge (Fungu – 42) umewezesha Waheshimiwa Wabunge na familia zao kupatiwa huduma ya matibabu kwa utaratibu wa Bima ya Afya. Aidha, Mfuko wa Bunge umeendelea kuimarisha Kituo cha Afya cha Bunge kwa kununua vifaa tiba pamoja na madawa mbalimbali kwa ajili ya kuwahudumia Waheshimiwa Wabunge pamoja na Watumishi.

3.7. Ukarabati wa Majengo ya Ofisi pamoja na Ujenzi wa Makazi ya Viongozi

Mheshimiwa Spika, Hadi kufikia tarehe 15 Machi 2022, Mfuko wa Bunge (Fungu – 42) umeweza kusimamia na kuratibu kazi za maendeleo zifuatazo: -

- a. Kuendelea na ukarabati wa majengo ya Ofisi ambapo matengenezo mbalimbali yamefanyika katika kumbi za Bunge kama ifuatavyo:

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

- (i) Kuboresha muonekano wa ndani wa Ukumbi wa Bunge na majengo ya Bunge;
 - (ii) Kufanya ukarabati katika Ukumbi wa Msekwa ikiwa ni Pamoja na kuweka zulia jipya
 - (iii) Kukamilisha ujenzi wa ghorofa ya tano.
 - (iv) Kufanya maandalizi ya Ujenzi wa nyumba za viongozi wa Bunge – Dodoma ikiwa ni kuandaa michoro, kufanya makadirio ya gharama za ujenzi pamoja na taratibu za kumpata Mkandarasi
- b. Kuratibu na kusimamia mafunzo mbalimbali kwa Wabunge na Watumishi kupidia mradi wa kulijengea uwezo Bunge (LSP II) ambapo mafunzo kwa Waheshimiwa Wabunge pamoja na Watumishi katika maeneo ya usimamizi wa bajeti, utungaji wa sheria na namna bora ya kuhuisha shughuli za Bunge kwa kuzingatia jinsia yalifanyika; na
- c. Kuratibu Mradi wa Moboresho ya Usimamizi wa fedha za Umma (PFMRP)

3.8. Kutoa Elimu kwa Umma

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Bunge (Fungu – 42) umeweza kufanikisha utoaji wa Elimu kwa Umma kwa wadau na wageni mbalimbali waliotembelea Bunge. Aidha Watumishi wameweza kushiriki katika maonesho ya Kitaifa ya Saba saba na Nane Nane ambapo wananchi waliotembelea Banda letu walipata ufanuzi wa kina kuhusu shughuli za Bunge. Vilevile, Ofisi ya Bunge iliweza kuendesha na kutoa elimu kwa umma kwa shule 66 za msingi na sekondari katika mikoa mitatu (3) ya Morogoro, Iringa na Dodoma.

3.9. Utekelezaji wa Majukumu Mengine

Mheshimiwa Spika, Hadi kufikia tarehe 15 Machi 2022, Mfuko wa Bunge (Fungu – 42) umeweza kufanikisha utekelezaji wa majukumu mbalimbali ikiwa ni pamoja na:-

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

- (i) kuratibu shughuli za Ulinzi na Usalama kwa Waheshimiwa Wabunge, Watumishi pamoja na Wageni mbalimbali wanaoingia maeneo ya Bunge au kushiriki safari za kibunge;
- (ii) kusimamia utekelezaji wa Mpango wa Manunuzi ya Bajeti ya mwaka wa fedha 2021/2022 pamoja na Kuandaa taarifa za manunuzi na kuwasilishwa kwenye Menejimenti ya Mamlaka ya Udhibiti na Ununuzi wa Umma (PPRA), Bodi ya Zabuni na Wakala wa Huduma ya manunuzi Serikalini (GPSA);
- (iii) Kuratibu Shughuli za Muungano zinazohusiana na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na kutoa huduma za kiofisi kwenye Ofisi ndogo ya Bunge Zanzibar;
- (iv) Kuratibu maandalizi ya Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Bunge kwa kipindi cha Robo mwaka na Nusu mwaka 2021/2022 na kuwasilishwa Hazina; na
- (v) Usimamizi wa matumizi ya fedha zilizokasimiwa kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ulifanyika kwa kuzingatia Sheria za Fedha na Manunuzi ya Umma (PFA na PPRA).
- (vi) Ushiriki katika michezo ya Mabunge ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa Wabunge na Watumishi;

4.0. MAELEZO YA MAKADIRIO YA BAJETI YA MFUKO WA BUNGE KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023.

4.1. Bajeti ya Mfuko wa Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2022/23

Mheshimiwa Spika, Katika mwaka wa fedha 2022/2023 Mfuko wa Bunge unaomba kuidhinishiwa jumla ya **Shilingi 132,728,638,000** sawa na ongezeko la asilimia 2.98 ikilinganishwa na bajeti ya mwaka 2021/22. Kati ya kiasi hicho, **Shilingi 23,658,494,000** zimepangwa kwa ajili ya Mishahara ya Wabunge na Watumishi, **Shilingi 103,670,144,000** zimepangwa kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na **Shilingi 5,400,000,000** zimepangwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ambapo **Sh. 4,700,000,000.00** ni fedha za ndani na **Shilingi**

700,000,000 ni fedha za nje. Aidha, hadi kufikia Juni 30, 2023 Ofisi imepanga kukusanya maduhuli yenyé jumla ya **Shilingi 131,766,000**.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla Makadirio ya Bajeti ya Mfuko wa Bunge (Fungu 42) kwa mwaka wa fedha 2022/2023 yameongezeka kwa takribani **shilingi bilioni 3.8**. Ongezeko hilo limetokana na shughuli zifuatazo:-

- (i) Ununuzi wa magari matatu ya viongozi wapya wa Bunge;
- (ii) Mafunzo kwa Waheshimiwa Wabunge, Kamati za Bunge na Tume ya Utumishi wa Bunge;
- (iii) Kuboresha Bima ya Afya kwa Wabunge kulingana na masharti ya Mkataba;
- (iv) Ushiriki katika michezo ya Mabunge ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa Wabunge na Watumishi nje ya nchi; na
- (v) Ushiriki katika Mikutano ya Kimataifa na vyama vya Kibunge ambavyo Bunge ni Mwanachama pamoja na kuimarishwa kwa shughuli za uendeshaji wa Ofisi ya Bunge Dodoma, Dar es salaam na Zanzibar

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati katika ulinganisho wa Bajeti ya mfuko wa Bunge kwa mwaka 2021/2022 na 2022/2023 umebaini kwamba fedha za mishahara zimeongezeka kwa asilimia 1.9, fedha za matumizi mengineyo zimeongezeka kwa asilimia 5, fedha za maendeleo zimepungua kwa asilimia 23 kutokana na kupungua kwa fedha za wafadhili na kukamilika kwa baadhi ya miradi ya mwaka wa fedha 2021/22.

Mheshimiwa Spika, Maandalizi ya Bajeti kwa mwaka wa fedha 2022/2023 yamezingatia mahitaji ya msingi yakiwemo mahitaji ya shughuli za Bunge (Mikutano ya Bunge na Kamati za Bunge) na uendeshaji wa Ofisi. Hivyo, fedha zimegawanywa katika Mafungu makubwa matatu (3) ambayo ni Programu 10 (Utawala na Uendeshaji), Programu

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

20 (Shughuli za Bunge) na Programu 30 (Ofisi ya Katibu wa Bunge). Katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 Mfuko wa Bunge unatarajia kutekeleza shughuli zifuatazo:-

- (i) Kugharamia shughuli za mikutano minne (4) ya Bunge;
- (ii) Kugharamia shughuli za mikutano minne (4) ya Kamati za Bunge;
- (iii) Kugharamia posho ya Jimbo na usafiri wa Wabunge;
- (iv) Kugharamia matibabu ya Wabunge na familia zao ndani na nje ya nchi;
- (v) Kugharamia ushiriki wa Wabunge katika Mikutano ya Kimataifa kama SADC-PF, EALA, Maziwa Makuu, Umoja wa Mabunge - IPU, Mabunge ya Jumuiya ya Madola, ACP-EU n.k;
- (vi) Kuwezesha Bunge kushiriki katika michezo ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na Watumishi kushiriki katika michezo ya SHIMIWI;
- (vii) Kuratibu na kuchapisha Taarifa rasmi za Bunge (Hansrad) pamoja na nyaraka mbalimbali za Bunge;
- (viii) Kuratibu na kusimamia kazi na majukumu ya Tume ya Utumishi wa Bunge;
- (ix) Kugharamia ununuzi wa magari matatu (3) mapya kwa ajili ya Viongozi;
- (x) Kugharamia ujenzi wa Makumbusho ya Bunge (Museums);
- (xi) Kugharamia ununuzi na usimikaji wa mitambo ya ulinzi na usalama;
- (xii) Kuwajenyea Wabunge uwezo ili waweze kutekeleza majukumu yao kikatiba;

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

- (xiii) Kugharamia kuendesha Ofisi, kama Umeme, Maji, Shajala nk;
- (xiv) Kugharamia Masuala mbalimbali yanayohusu uendeshaji wa Ofisi kwa ujumla;
- (xv) Kuwezesha Watumishi kushiriki mafunzo ya muda mfupi na mrefu ndani na nje ya nchi;
- (xvi) Kusimamia uendeshaji wa Ukumbi wa Bunge, mitambo na mashine;
- (xvii) Kuratibu kazi ya kukarabati Jengo la ukumbi wa Bunge na majengo ya Ofisi ya Bunge;
- (xviii) Kuandaa vipindi vyta televisheni na kurusha matangazo ya Bunge;
- (xix) Kuratibu utoaji wa habari kwa wananchi kuhusu shughuli za Bunge na Kamati;
- (xx) Kufuatilia utekelezaji wa hoja za ukaguzi zilizotolewa kabla ya Mwaka wa Fedha 2022/23;
- (xxi) Kufanya ukaguzi wa matumizi ya kawaida na maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2022/23 na kutoa taarifa;
- (xxii) Kuandaa taarifa ya ukaguzi ya mwaka (Annual Audit report) kwa Mwaka wa Fedha 2021/22;

5.0. MAONI NA USHAURI WA KAMATI

5.1. Ofisi za Wabunge Majimboni

Mheshimiwa Spika, Kamati inaendelea kusisitizia kuhusu suala la ujenzi wa Ofisi za Wabunge majimboni na kuziwekea samani kwa utekelezaji wa majukumu yao kwa ufanisi pindi wanapokuwa majimboni. Aidha, kwa kuwa suala hili walikasimiwa OR-TAMISEMI kwa ajili ya utelekezaji wake, ni

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

vema Bunge likapata mrejesho wa utekelezaji wa ujenzi wa Ofisi hizi.

5.2. Kuongeza eneo la Bunge

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Ofisi ya Bunge imezungukwa na maeneo mengine ya Serikali yakiwemo maghala (warehouses) ni vema sasa Bunge likaona uwezekano wa kutafuta namna ya kuyamiliki maeneo haya kwa lengo la kupanua wigo wa maeneo yanayozunguka Ofisi ya Bunge. Hii itasaidia kuongeza ujenzi wa majengo mengine ya ofisi, eneo la maegesho ya magari ya viongozi pamoja na kuimarisha usalama.

5.3. Ushiriki wa Bunge kwenye Vyama vyta Kibunge

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Bunge ni Mwanachama wa vyama vyta Kibunge mbalimbali kwani kuna umuhimu wa kuongeza bajeti ya Bunge ili kuliwezesha Bunge kushiriki kikamilifu katika Mkutano wa Vyama hivyo.

5.4. Michezo Kwa Waheshimiwa Wajumbe

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia kwamba wewe ni mwanamichezo na Bunge lako linashiriki mashindano mbalimbali ya michezo ya Afrika Mashariki. Lakini tumeshuhudia Waheshimiwa Wabunge wakikosa maeneo ya kufanya mazoezi. Hivyo ni wakati muafaka kwa Serikali kuitia mfuko wa Bunge kutenga bajeti ili kufanikisha azma ya kujenga uwanja wa kufanya mazoezi (Sports Arena).

6.0. HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, naomba nihitimishe kwa kukushukuru wewe Mheshimiwa Spika na Naibu Spika kwa kuongoza vema mashauriano kati ya Kamati ya Bajeti na Serikali. Pia naomba kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba (Mb), Waziri wa Fedha na Mipango na Mheshimiwa Hamad Hassan Chande Naibu Waziri wa Fedha na Mipango kwa ushirikiano wao kwa Kamati. Aidha, kipekee nimshukuru

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Balozi Pindi Chana (Mb), aliyekuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Uratibu na Bunge) kwa kushirikiana na Kamati wakati wa majadiliano kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru wajumbe wa Kamati hii kwa umakini wao katika kujadili na kutoa maoni na mapendekezo mbalimbali kuhusu Bajeti ya Mfuko wa Bunge. Naomba kuwatambua Wajumbe hao kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Daniel Baran Sillo, Mb	Mwenyekiti
2. Mhe. Omari Mohamed Kigua, Mb	M/Mwenyekiti
3. Mhe. Ali Hassan Omar King, Mb	Mjumbe
4. Mhe. Issa Jumanne Mtemvu, Mb	Mjumbe
5. Mhe. Oran Manase Njeza, Mb	Mjumbe
6. Mhe. Josephat Sinkamba Kandege, Mb	Mjumbe
7. Mhe. Leah Jeremiah Komanya, Mb	Mjumbe
8. Mhe. Joseph George Kakunda, Mb	Mjumbe
9. Mhe. Shally Josephha Raymond, Mb	Mjumbe
10. Mhe. Subira Khamis Mgatu, Mb	Mjumbe
11. Mhe. Esther Nicholas Matiko, Mb	Mjumbe
12. Mhe. Jonas William Mbunda, Mb	Mjumbe
13. Mhe. Mariam Madalu Nyoka, Mb	Mjumbe
14. Mhe. Juma Hamad Omar, Mb	Mjumbe
15. Mhe. Kwagilwa Reuben Nhamanilo, Mb	Mjumbe
16. Mhe. Tarimba Gulam Abbas, Mb	Mjumbe
17. Mhe. Amina Iddi Mabrouk, Mb	Mjumbe
18. Mhe. Riziki Said Lulida, Mb	Mjumbe
19. Mhe. Halima James Mdee, Mb	Mjumbe
20. Mhe. Zaytun Seif Swai, Mb	Mjumbe
21. Mhe. Mariam Kisangi, Mb	Mjumbe
22. Mhe. Dkt. Charles Kimei, Mb	Mjumbe

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii, kumshukuru Ndg. Nenelwa Mwihambi, *ndc*, Katibu wa Bunge kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Aidha, napenda kuipongeza na kuishukuru Sekretarieti ya Kamati ikiongozwa na Mkurugenzi wa Idara ya Bajeti Ndugu

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Michael Kadebe kwa kuratibu na kutoa ushauri wa kitaalamu ambao umesaidia Kamati katika kukamilisha Taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo naliomba Bunge lako tukufu sasa lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mfuko wa Bunge – Fungu 42, kwa Mwaka wa Fedha 2022/23 kama yalivyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

Daniel Baran Sillo (Mb)

MWENYEKITI

KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI

06 Aprili, 2022

NAIBU SPIKA: Ahsante. Sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Masuala ya Ukimwi na kwa mamlaka ya kititunaongeza mpaka shughuli yake itakapokwisha. (*Makof*)

MHE. FATMA H. TOUFIQ – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MASUALA YA UKIMWI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Yafuatayo ni maoni ya kamati kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Tume ya kudhibiti UKIMWI Tanzania na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Madawa za Kulevyta kwa mwaka wa fedha 2021/2022 na makadirio ya matumizi kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba taarifa hii iingie katika *Hansard* za Bunge kama ilivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, utangulizi; awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema, kwa kutujalia afya njema na kutukutanisha kwa mara nyingine katika Bunge hili Tukufu katika Mkutano huu wa Saba wa Bunge la Kumi na Mbili, kwa lengo la kutekeleza masharti ya Kanuni ya 118(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 118(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni 2020, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI, Kifua Kikuu, Dawa za Kulevyta na Magonjwa Yasiyoambukiza kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevyta – Fungu 91 na Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (*TACAIDS*) – Fungu 92 kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mafungu hayo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 10(e) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, kimeipa Kamati ya Masuala ya UKIMWI jukumu la kushughulikia Bajeti za Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevyta. Kamati inachambua Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 na kufanya ulinganisho kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fungu 92 - Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (*TACAIDS*) na Fungu 91 – Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevyta kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na jukumu hilo, kwa kuzingatia masharti ya Kifungu cha 10 (b), cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni ya Bunge ya Kudumu, Toleo la Juni, 2020, kinachoruhusu jukumu la kufuatilia utekelezaji wa Sera na Mipango ya Serikali kuhusu UKIMWI na Udhibiti wa Dawa za Kulevyta, Kamati ilifanya ziara ya kutembelea, kukagua utekelezaji wa afua za UKIMWI, Kifua Kikuu na Dawa za Kulevyta zinazotekelze wa Wizara, Taasisi na Mamlaka za Serikali katika mwitikio wa mapambano dhidi ya UKIMWI, Kifua Kikuu pamoja na biashara na matumizi ya Dawa za Kulevyta katika Mikoa ya Geita, Mara na Mwanza. Katika ziara hiyo masuala mbalimbali yalibainika kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, **Ongezeko la Maambukizi ya Ugonjwa wa UKIMWI**. Kamati imebaini kuwa hali ya Maambukizi ya VVU bado ipo juu katika Mkao wa Geita asilimia 6.4 na Mkao wa Mwanza imeongezeka kutoka asilimia

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

4.7 mwaka 2011/2012 hadi asilimia 7.2 mwaka 2016/2017; ukilinganisha na hali ya maambukizi Kitaifa ya asilimia 4.7. Kamati inaona ipo haja ya Mamlaka husika kuweka nguvu katika Mikoa hii ili kupunguza maambukizi mapya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna baadhi ya mialo ambayo Kamati iliitembelea elimu kuhusu UKIMWI bado hajjawafikia ipasavyo na hivyo watu wengi hawachukui tahadhari kwa maradhi haya. Kwa muktadha huu suala la kufikia 95 – 95 – 95 ifikapo mwaka 2030 litakuwa ni changamoto. Hivyo, Kamati inaziomba mamlaka husika kuhakikisha inatoa elimu ya UKIMWI katika maeneo haya na si kusubiri ujio wa Kamati ya Bunge ndipo watembelee maeneo husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imebaini kuwa baadhi ya Mikoa ina kiwango kikubwa cha wagonjwa wa Kifua Kikuu. Kwa Mfano, Mkoa wa Mara mwaka 2021 kati ya watu 100,000, watu 146 waligundulika kuwa na ugonjwa wa Kifua Kikuu. Pamoja na jitihada zinazochukuliwa na Serikali lakini bado kumekuwa na changamoto zifuatazo katika Mikoa yote ambayo Kamati iliitembelea:-

- (i) Upungufu wa mashine za *X-Ray na Gene Expert*;
- (ii) Ukosefu wa makopo au vifaa vya kuchukulia sampuli ya makohozi na vitendanishi vya maabara;
- (iii) Ukosefu wa fedha za kuwahudumia wagonjwa wa Kifua Kikuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni rai ya Kamati kuwa changamoto hizi zifanyiwe kazi ili kupunguza maambukizi ya Kifua Kikuu nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati pia ilibaini wafungwa na mahabusu wanapewa chakula cha aina moja tu yaani ugali na maharagwe. Hivyo, ipo haja Serikali kuhakikisha chakula bora kinatolewa kwa WAVIU waliopo magerezani ili kuimarisha hali yao ya lishe. (*Makofii*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo Kamati ilielezwa uwepo wa changamoto ya Magereza kudaiwa kulipia gharama za matibabu inapotokea wafungwa na mahabusu wanapokwenda kupata matibabu katika vituo vya afya. Kamati inaona jambo hili siyo sahihi hivyo mamlaka husika zichukue hatua ikiwemo kuhakikisha kuwa wafungwa wanapata huduma za matibabu bila gharama yoyote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mojawapo ya changamoto katika Magereza zetu ni msongamano wa wafungwa na mahabusu ambao kwa kiasi kikubwa imekuwa unachangia maambukizi kuenea kwa kasi. Kamati inashauri Mamlaka husika zione namna ya kuhakikisha msongamano unapungua magerezani ili kupunguza kuenea kwa Ugonjwa wa Kifua Kikuu.

Mheshimimiwa Naibu Spika, katika magonjwa yasiyoambukiza, Kamati inashauri elimu zaidi kuhusu magonjwa yasiyoambukiza inahitajika katika ngazi kuanzia elimu ya awali mpaka vyuo vikuu. Aidha, Serikali kwa kushirikiana na sekta husika wahakikishe kunakuwa na elimu ya kutosha kwa jamii juu ya magonjwa yasiyoambukiza kwani imekuwa ni tatizo kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi kuhusu uzingatiaji wa maoni ya Kamati, uzingatiaji wa maoni kuhusu Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (*TACA/DS*).

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni yaliyokuwa yametolewa na Kamati kwa mwaka wa fedha 2020/2021 yalikuwa yanahu maeneo matano ikiwemo suala la upatikanaji wa fedha za ndani kwa ajili ya afua za UKIMWI.

Kwa hiyo maelezo yako pale ukurasa wa Sita, lakini jambo kubwa sisi Kamati tumezungumzia kwamba, ni ushauri wa Kamati kupewa fedha zilizopitishwa na Bunge kwa ajili ya mwitikio wa UKIMWI zitolewe kwa wakati ili kutokwamisha utekelezaji wa shughuli zinazopangwa kwa kipindi husika.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati pia ilitoa ushauri wa hoja tatu kwa upande wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevyaa katika mwaka wa fedha 2021/2022 kama ilivyoonekana kwenye taarifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa Kamati unaona kwamba upo umuhimu wa kutenga bajeti ya maendeleo kwa mamlaka ili kusaidia utekelezaji wa miradi ya uzalishaji itakayowasaidia waraibu wa dawa za kulevyaa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (Fungu 92) iliiidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 4.3. Kati ya Fedha hizo, shilingi bilioni 2.9 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi bilioni 1.3 kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo ambapo shillingi billioni moja ni fedha za ndani na shilingi milioni 389 ni fedha za nje. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, kufikia mwezi Februari 2022, Tume ilikuwa imepokea kiasi cha shilingi bilioni 2.04 sawa na asilimia 47 ya Bajeti yake yote kama inavyoonekana katika Kielelezo Na. 1. Kwa hiyo, Tume haikupata kiasi chochote cha fedha za maendeleo ya ndani kama ilivyokuwa katika Bajeti iliyopita. (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaendelea kushauri kuwa Serikali ihakikishe upatikanaji wa fedha za matumizi ya maendeleo ili kuimarisha mapambano dhidi ya UKIMWI kwa mustakabali wa Taifa ili kufikia hiyo 95 – 95 – 95. Lakini sambamba na hilo, Serikali itengete fedha za ndani kwa ajili ya utekelezaji wa afua za UKIMWI na kupunguza utegemezi wa wafadhili.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2021/2022, Bunge liliidhinisha shilingi bilioni 8.5 zenye kujumuisha mishahara shilingi bilioni 6.1 na Matumizi mengineyo shilingi bilioni 2.3 na hakuna fedha yoyote iliyotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, kufikia Februari, 2022 jumla ya shilingi bilioni

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

6.2 sawa na asilimia 72.8 zilikuwa zimepokelewa kama inavyoonekana katika Kielelezo Na. 2. Hapa Kamati inaipongeza Serikali kwa utoaji wa fedha unaoridhisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania - Fungu 92, inaombewa jumla ya shilingi bilioni 14.9. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 2.9 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi bilioni 12 kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ambapo shilingi bilioni 1.8 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 10 ni fedha za nje kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Na. 3.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini ongezeka la Bajeti kwa asilimia 246.9 na zaidi kwenye fedha za Maendeleo, kadhalika, kutoka nje asilimia 2,498.97. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa kuongeza fedha kwenye miradi ya maendeleo na kusisitiza kuwa fedha hizi zitolewe kwa wakati ili shughuli zilizokusudiwa ziweze kufanyika kikamilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Fungu 91. Katika mwaka wa fedha 2022/2023 Fungu 91- Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevyia lilaombewa jumla ya shilingi bilioni 11 sawa na ongezo la asilimia 40.39. Sehemu ya fedha hizo, Shilingi Bilioni 2.1 ni Mshahara na shilingi bilioni 9.8 ni Matumizi Mengineyo kama inavyoonesha katika Kielelezo Na. 4. Kamati imeipongeza pia Serikali na kuomba fedha hizi zitumike kutekeleza majukumu yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, afua za lishe Magerezani, haya ni maoni ya jumla ya Kamati. Kwanza Mamlaka husika zihakikishe afua za lishe gerezani hususani kwa watu wenye mahitaji maalum zipewe kipaumbele. Pia ni vyema wakatafutwa wadau watakaosaidi kuwapatia wafungwa na mahabusu lishe bora kama wanavyofanya kwenye maeneo mengine kwa mfano kwenye UKIMWI kuwapatia dawa WAVIU. Kwenye magonjwa yasiyoambukiza, Kamati inaishukuru sana Serikali kwa kuendelea kuchukua hatua mbalimbali ili kukabiliana na Magonjwa Yasiyoambukiza.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaendelea kusisitiza yafuatayo:-

(i) Serikali ione umuhimu wa kutenga fedha zake za ndani kwa ajili ya udhibiti wa UKIMWI na kupunguza utegemezi wa fedha za wafadhili kutoka nje kwa ajili ya mwitikio endelevu wa mapambano dhidi ya UKIMWI hasa ukizingatia kwamba baadhi ya wafadhili wameanza kupunguza kiwango cha ufadhili wa fedha za UKIMWI Tanzania; na

(ii) Serikali iweke mipango madhubuti kwa kupata vyanzo vingine vya mapato vitakavyosaidia kupata fedha zaidi kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfuko wa *AIDS Trust Fund*; pamoja na Serikali kuendelea kutenga fedha kwa ajili ya *ATF* bado Kamati inaona umuhimu wa kutafutiwa vyanzo vingine ili iweze kujiendesha yenye badala ya kutegemea wafadhili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Utekelezaji wa Afua za UKIMWI. Kamati imebaini kuwa utekelezaji wa Afua za UKIMWI bado siyo wa kuridhisha sana katika maeneo mengi, hivyo kunatia shaka hasa kufikia malengo ya 95-95-95 ifikapo 2030, kwa hiyo mapendekezo yametolewa na Kamati kwamba lazima elimu iendelee kutolewa, kampeni maalum iendelee katika Mikoa yote, ufuatiliaji wa WAVIU watoro ufanyike lakini pia elimu kuhusu unyanyapaa na ukatili iweze kutolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kukabiliana na Ugonjwa wa Kifua Kikuu;

(i) Kwa kuwa msongamano wa Mahabusu unachangia kuongezeka kwa wagonjwa wa Kifua Kikuu kwenye Magereza, Serikali ione namna ya kuharakisha mashauri ya mahabusu ili kupunguza msongamano katika Magereza nchini kote;

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

(ii) Adhabu za wafungwa kama utoaji wa huduma za jamii (*Service Community*) uanze kutumika ili kupunguza msongamano wa wafungwa katika mahabusu katika Magereza; pia

(iii) Serikali isimamie kusisitiza Halmashauri kuendelea kutenga bajeti kwa ajili ya utekelezaji wa afua za Kifua Kikuu;

(iv) Elimu iendelee kutolewa; lakini pia

(v) Wizara ya Afya kwa kushirikiana na wadau ihakikishe upatikanaji wa kutosha wa vifaa mbalimbali kwa ajili ya kupima Kifua Kikuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa tangu kuanzishwa kwa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevy, Mamlaka imekuwa haitengewi bajeti ya Miradi ya Maendeleo. Serikali haina budi kutenga fedha za maendeleo ili kuwezesha waraibu kiuchumi kwa kuwapa mbinu za ujasiriamali, mikopo nafuu ya biashara, kilimo, ushonaji, ufugaji na stadi za Maisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, waraibu wa dawa za kulevy, Serikali iongeze vituo vya kutolea huduma angalau kila hospitali ya Mkaoa kuwepo na kituo kimoja ili kuondoa changamoto za umbali ambazo zimekuwa zikichochea baadhi ya waraibu kushindwa kuhuduria kliniki na kupata huduma. Maelezo mengine yako pale katika ukurasa wa 15.

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho. Napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha Taarifa ya Kamati mbele ya Bunge lako Tukufu. Napenda kukupongeza kwa namna unavyoliongoza Bunge letu kwa umahiri mkubwa. Vilevile, nawashukuru na kuwapongeza Mheshimiwa Spika na Wenyeleviti wote wa Bunge kwa utekelezaji mzuri wa majukumu yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia kutoa shukrani kwa aliyekuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge na Watu wenye Ulemavu, Mheshimiwa Pindi Hazara

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Chana Mbunge, Mheshimiwa Boniphace Simbachawene - Waziri mpya wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, pamoja na Naibu Mawaziri Mheshimiwa Ummy Nderiananga Mbunge na Mheshimiwa Patrobas Katambi Mbunge. Vilevile namshukuru Mheshimiwa Ummy Mwalimu Waziri wa Afya, Mheshimiwa Godwin Mollel kwa ushirikiano mkubwa alioupatia Kamati wakati wanapohitajika katika kutekeleza majukumu ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile napenda kuwashukuru Makatibu Wakuu, Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Watu Watu wenye Ulemavu, Ofisi ya Waziri Mkuu Dkt. John Jingu pamoja na Maafisa wote Waandamizi kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia namshukuru Mkurugenzi Mtendaji Dkt. Leonard Maboko, Kamishna Jenerali wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevyta Ndugu Jenerali Gerald Kusaya na Watendaji wote, kwa ushirikiano walioutoa kwa Kamati hii katika kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nafasi ya kipekee naomba niwashukuru sana Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI, kwa kazi nzuri waliyoifanya kwa kujadili na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevyta kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na ufinyu wa muda, Wajumbe hawa walikuwa tayari kutekeleza majukumu yao haya makubwa na kwa wakati. Kwa heshima kubwa, naomba orodha yao iingie katika *Hansard*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwashukuru kwa dhati Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge wakiongozwa na Ndugu Nenelwa Mwihambi - Katibu wa Bunge, Ndugu Athuman Hussein -Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge na Ndugu Gerald Magili - Mkurugenzi Msaidizi, kwa

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

kuiwezesha Kamati hii kutekeleza majukumu yake bila kukwama. Kipekee, Nawashukuru Katibu Ndugu Happiness Ndalu, Ndugu Asia Msangi na Ndugu Pamela Pallangyo kwa kuratibu vyema kazi za Kamati na kuhakikisha taarifa hii inakamilika kwa wakati mwafaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevy - Fungu 91 kiasi cha Shilingi Bilioni 11.9 na Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania - Fungu 92 kiasi cha Shilingi Bilioni 14.9.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. (*Makofii*)

**MAONI YA KAMATI KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA OFISI
YA WAZIRI MKUU TUME YA KUDHIBITI UKIMWI TANZANIA NA
MAMLAKA YA KUDHIBITI NA KUPAMBANA NA DAWA ZA
KULEVYA KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022 NA MAKADIRIO
YA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023 – KAMA
YALIVYOWASILISHWA MEZANI**

SEHEMU YA KWANZA

1.0 UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, kwa kutujalia afya njema na kutukutanisha kwa mara nyininge katika Bunge hili Tukufu katika Mkutano huu wa Saba wa Bunge la Kumi na Mbili, kwa lengo la kutekeleza masharti ya Kanuni ya 118 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni 2020, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI, Kifua Kikuu, Dawa za Kulevy na Magonjwa Yasiyoambukiza kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya

Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevyta – **Fungu 91** na Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (*TACAIDS*) – **Fungu 92** kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mafungu hayo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 10 (e) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, kimeipa Kamati ya Masuala ya UKIMWI jukumu la kushughulikia Bajeti za Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevyta. Katika kutekeleza jukumu hilo, mnamo tarehe 31 Machi, 2022, Kamati ilichambua Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 na kufanya ulinganisho kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya **Fungu 92** – Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (*TACAIDS*) na **Fungu 91** – Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevyta kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, baada ya uchambuzi wa kina wa Taarifa na Makadirio ya (**Fungu 92 & 91**), naomba kutoa taarifa ya Kamati inayofafanua mambo makubwa matano (5) yafuatayo: -

- (a) Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (*TACAIDS*) kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022;
- (b) Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevyta kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022;
- (c) Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (*TACAIDS*) kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023;
- (d) Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mamlaka ya Kupambana na Kudhibiti Dawa za Kulevyta Tanzania kwa Mwaka wa Fedha wa 2022/2023; na
- (e) Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati kwa Fungu 91 na Fungu 92.

Mheshimiwa Spika, pamoja na jukumu hilo, kwa kuzingatia masharti ya Kifungu cha 10 (b), cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, kinachohusu jukumu la kufuatilia utekelezaji wa Sera na Mipango ya Serikali kuhusu UKIMWI na Udhibiti wa Dawa za Kulevyta, Kamati ilifanya ziara kati ya tarehe 28 Februati – 9 Machi 2022, kutembelea na kukagua utekelezaji wa afua ya UKIMWI, Kifua Kikuu na Dawa za Kulevyta zinazotekelezwa na Wizara, Taasisi na Mamlaka za Serikali katika mwitikio wa mapambano dhidi ya UKIMWI, Kifua Kikuu pamoja na biashara na matumizi ya Dawa za Kulevyta katika Mikoa ya Geita, Mara na Mwanza. Ufuatilaji huo ulifanyika kwa kukagua maeneo ya migodi, vituo vinavyotoa huduma ya CTC, magerezani, vituo vinavyotoa huduma ya methadone kwa waraibu na kwenye konga. Katika Ziara hiyo masuala mbalimbali yalibainika kama inavyoonekana katika Taarifa hii.

1.1 Uchambuzi wa yaliyobainika wakati wa Ziara ya Kamati

Mheshimiwa Spika, katika ziara hiyo ya Kamati katika Mkao wa Geita, Mara na Mwanza, pamoja na kazi nzuri ambayo inafanywa, Kamati ilielezwa changamoto mbalimbali. Miongoni mwa changamoto hizo ni kama ifuatavyo: -

1.1.1 Ongezeko la Maambukizi ya Ugonjwa wa UKIMWI

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwa hali ya Maambukizi ya VVU bado ipo juu kwa Mkao wa Geita (**asilimia 6.4**) na Mkao wa Mwanza imekuwa imeongezeka kutoka **asilimia 4.7** mwaka 2011/2012 hadi **asilimia 7.2** mwaka 2016/2017; ukilinganisha na hali ya maambukizi Kitaifa ya **asilimia 4.7**. **Kamati inaona ipo haja ya Mamlaka husika kuweka nguvu zaidi katika Mikoa hii ili kupunguza maambukizi mapya.**

1.1.2 Ukosefu wa Elimu kuhusu UKIMWI katika Maeneo ya Mialo

Mheshimiwa Spika, Katika baadhi ya mialo ambayo Kamati iliitembelea elimu kuhusu UKIMWI bado haijawafikia ipasavyo na hivyo watu wengi hawachukui tahadhari ya kujikinga na

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

maradhi haya. Kwa muktadha huu suala la kufikia 95 – 95 – 95 ifikapo mwaka 2030 litakuwa ni changamotoo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na changamoto hiyo, Kamati ilielezwa changamoto zifuatazo katika mapambano dhidi ya UKIMWI na Kifua Kikuu kwa wavuvi:-

- i) Kiwango kidogo cha upimaji wa VVU katika mialo na kambi za wavuvi kutokana na ugumu wa mazingira ya shughuli za uvuvi;
- ii) Upatikanaji duni wa Kondomu katika maeneo ya mialo;
- iii) Kiwango kidogo cha uelewa kuhusu Sera, Sheria na wajibu kwa waathirika; na
- iv) Uhaba wa rasilimali za kuwasaldia waathirika wa VVU katika maeneo ya Uvusi.

Kamati inaziomba mamlaka husika kuhakikisha zinatoa elimu ya UKIMWI katika maeneo haya na si kusubiri ujio wa Kamati ya Bunge ndipo watembelee maeneo husika.

1.1.3 Ugonjwa wa Kifua Kikuu

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini bado baadhi ya Mikoa ina kiwango kikubwa cha wagonjwa wa Kifua Kikuu. Kwa Mfano, Mkoa wa Mara kwa Mwaka 2021 kati ya **watu 100,000, watu 146** waligundulika kuwa na ugonjwa wa Kifua Kikuu (Chanzo: DHIS2-ETL) na Mkoa wa Mwanza kati ya **watu 100,000, watu 145** ni wagonjwa wa Kifua Kikuu. Pamoja na jitihada zinazochukuliwa na Serikali lakini bado kumekuwa na changamoto zifuatazo katika mikoa yote ambayo Kamati iliitembelea:-

- (i) Upungufu wa mashine za X- Ray na Gene Expert
- (ii) Ukosefu wa makopo au vifaa vya kuchukulia sampuli za makohozni na vitendanishi vya maabara;

(iii) Ukosefu wa fedha za kuwahudumia wagonjwa wa Kifua Kikuu;

Ni rai ya Kamati kuwa changamoto hizi zifanyiwe kazi ili kupunguza maambukizi ya Kifua Kikuu nchini.

1.1.4 Ukosefu wa Lishe katika Magereza

Mheshimiwa Spika, Hali nzuri ya Lishe ni muhimu kwa watu Wanaoishi na Virusi vya UKIMWI kwani inawasaidia kuweka afya vizuri wanapokuwa wanatumia dawa za kufubaza virusi (*ARVs*). Kamati imebaini ya kwamba wafungwa na mahabusu wanapewa chakula cha aina moja tu ambacho ni ugali na maharagwe kila siku hali ambayo inafanya wazidi kudhoofika kiafya kwani dawa wanazotumia ni kali na zina nguvu sana. **Ipo haja ya Serikali ya kuhakikisha chakula bora kinatolewa kwa WAVIU waliopo magerezani ili kuimarisha hali yao ya lishe.**

1.1.5 Wafungwa na mahabusu kujilipia gharama za matibabu

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa uwepo wa changamoto ya Magereza kudaiwa kulipia gharama za matibabu inapotokea wafungwa na mahabusu wanapokwenda kupata matibabu katika vituo vya afya. **Kamati inaona jambo hili siyo sahihi hivyo Mamlaka husika zichukue hatua ikiwemo kuhakikisha kuwa wafungwa wanapata huduma za matibabu bila kulipia gharama.**

1.1.6 Maambukizi ya Kifua Kifuu katika Magereza

Mheshimiwa Spika, Moja ya changamoto katika Magereza zetu nchini ni msongamano wa wafungwa na mahabusu. Kamati ilielezwa kuwa wapo baadhi ya wafungwa na mahabusu ambaao wanaingia magerezani wakiwa wameambukizwa Kifua Kikuu. Magereza huwapima wanapoingia lakini ipo changamoto ya maeneo ya kuwatenga ili wasiambukize wenzao kutokana na msongamano uliopo ambaao kwa kiasi kikubwa umekuwa

unachangia maambukizi kuenea kwa kasi. **Mamlaka husika zione namna ya kuhakikisha msongamano unapungua magerezani ili kupunguza kuenea kwa Ugonjwa wa Kifua Kikuu**

1.1.7 Magonjwa Yasiyoambukiza

Mheshimiwa Spika, Magonjwa Yasiyoambukiza yanaeendelea kulitikisa Taifa hivi sasa. Kamati imebaini kuwa wapo wananchi wa kawaida, wafungwa na mahabusu wanaokabiliwa na magonjwa kama kisukari, kansa, shinikizo la damu, moyo na mengineyo. **Elimu zaidi kuhusu magonjwa yasiyoambukiza inahitajika katika ngazi kuanzia elimu ya awali mpaka vyuo vya elimu ya juu.** Aidha, Serikali kwa kushirikiana na sekta husika wahakikishe kunakuwa na elimu ya kutosha kwa jamii juu ya magonjwa haya.

SEHEMU YA PILI

2.0 UCHAMBUZI WA KAMATI

Mheshimiwa Spika, ili kuliwezesha Bunge kufuatilia utekelezaji wa bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 na kushauri ipasavyo kuhusu makadirio ya matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, Kamati illifanya uchambuzi wa wasilisho la Serikali kuhusu mambo makuu matatu ambayo ni:

- a) Utekelezaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati;
- b) Taarifa ya Utekelezaji wa bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022; na
- c) Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 yanatokana na Kamati kufanya mapitio ya mambo makuu yafuatayo: -

- a) Uzingatiaji wa maoni na ushauri uliotolewa na Kamati Bungeni wakati wa kujadili Makadirio ya Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu: **Fungu 91** – Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana

na Dawa za Kulevyaa na **Fungu 92** - Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS) kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022;

b) Hali ya upatikanaji wa Fedha hadi kufikia mwezi Februari, 2022; na

c) Utekelezaji wa malengo yaliyokuwa yamewekwa kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi huo ulilenga kuliwezesha Bunge kujiridhisha na utoshelevu wa utekelezaji wa mipango na mwenendo wa matumizi, ikilinganishwa na madhumuni ya Bunge kuidhinisha bajeti inayohusika.

2.2 Uchambuzi kuhusu Uzingatiaji wa Maoni ya Kamati

Mheshimiwa Spika, Ili kujiridhisha na namna Serikali inavyozingatia ushauri wa Kamati unaotolewa na Bunge lako Tukufu, Kamati ilichambua taarifa iliowasilihwa kuhusu utekelezaji wa Maoni na Ushauri uliotolewa wakati wa kujadili Makadirio ya Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu: Fungu 91 – Mamlaka ya Kupambana na Dawa za Kulevyaa na Fungu 92 – Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS). Uchambuzi wa Kamati ulibaini yafuatayo:-

2.2.1 Uzingatiaji wa Maoni kuhusu Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS)

Mheshimiwa Spika, Maoni yaliyokuwa yametolewa na Kamati kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 yalihusu maeneo makuu matano ambayo ni:

i) Upatikanaji wa fedha za ndani kwa ajili ya afua za UKIMWI;

ii) Kuanzisha vyanzo vya Mfuko wa Udhaminii wa Kudhibiti UKIMWI (*AIDS Trust Fund – ATF*);

iii) Elimu ya lishe kwa Watu Wanaoishi na Virusi vya UKIMWI;

iv) Upimaji wa VVU na Tohara ya Hiari ya Kitabibu kwa Wanaume; na

v) Kuimarisha ukusanyaji, uhifadhi na matumizi ya takwimu za UKIMWI na Kifua Kikuu kwa Watu Wenyewe Ulemavu.

Mheshimiwa Spika, naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa, ushauri wa Kamati umezingatiwa na kutekelezwa kwa kiasi kikubwa. Hata hivyo, Kamati ilibaini kuwa kwa ujumla hali ya upatikanaji wa fedha ilikuwa ni wastani wa **asilimia 47.5** badala ya **asilimia 66.6** inayopaswa kuwa imepatikana kufikia Februari 2022. Aidha, katika Mwaka wa Fedha 2021/2022 Tume ilitengewa kiasi **Shilingi 1,000,000,000.00** fedha za ndani kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo, Kiasi ambacho mpaka siku ambayo Kamati inakutana na Tume kilikuwa hakijatolewa kabisa na Hazina. **Ni ushauri wa Kamati** kuwa, pesa zinazopitishwa na Bunge kwa ajili ya mwitikio wa UKIMWI zitolewe kwa wakati ili kutokwamisha utekelezaji wa shughuli zilizopangwa kwa kipindi husika.

2.2.2 Uzingatiaji wa Maoni kuhusu Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevyta Tanzania

Mheshimiwa Spika, Kamati ilitoa ushauri wa Hoja tatu kwa upande Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevyta katika Mwaka wa Fedha 2021/2022. Hoja hizo zilihusu yafuatayo:

- i) Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevyta itenye Bajeti kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo;
- ii) Huduma za *Sobber Houses* zinatolewa na Sekta Binafsi kulingana na Miongozo ya Kitaifa ambapo wagonjwa hulipia gharama kulingana na makubaliano na watoa huduma na pia kulingana na muda ambaao mgonjwa ataishi katika nyumba hiyo na hivyo wakati umefika kuanzishwa *Sobber Houses* za Serikali ambazo zitapunguza mzigo wa gharama za kuwatunza; na
- iii) Serikali ihimize wadau mbalimbali kuiga mfano wa Asasi ya Walter Reed Program ili kurahisisha kuwatambua, kuwashirikisha na kuwasaidia waraibu wa dawa za kulevyta.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati unaona bado upo umuhimu wa kutenga bajeti ya maendeleo kwa Mamlaka itakayosaidia utekelezaji wa miradi mbalimbali ya uzalishaji itakayowasaidia waraibu wa dawa za kulevyia nchini. Vilevile Kamati inasisitiza uhamasishaji wa wadau uendelee ili kuweza kuwafikia waraibu wengi zaidi katika mikoa yote Tanzania Bara.

2.3 Uchambuzi kuhusu Upatikanaji wa Fedha

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifanya uchambuzi wa Upatikanaji wa fedha za Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS) - Fungu 92 na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevyia (DCEA) - Fungu 91 kama ifuatavyo:-

2.3.1 Upatikanaji wa Fedha za Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS) - Fungu 92

Mheshimiwa Spika, Kamati ilichambua taarifa ya hali ya upatikanaji wa fedha kwa lengo la kujiridhisha ni kwa kiwango gani fedha hizo zilizoidhinishwa na Bunge lako Tukufu zimetolewa ili kuwezesha utekelezaji wa malengo na vipaumbele veya Tume.


Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2021/2022 Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (**Fungu 92**) iliidhinishwa jumla ya **Shilingi 4,317,818,000.00**. Kati ya Fedha hizo, **Shilingi 2,928,348,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida yenyе kujumuisha Mishahara Shilingi **1,715,602,000.00** na Matumizi mengineyo **Shilingi 1,212,746,000.00**; na Shilingi **1,389,470,000** kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo ambapo **Shilingi 1,000,000,000** ni fedha za ndani na **Shilingi 389,470,000** ni fedha za nje. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, kufikia mwezi Februari 2022, Tume ilikuwa imepokea kiasi cha Shilingi **2,049,837,057.00** sawa na asilimia **47.0** ya Bajeti yake yote kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Na. 1. Kati ya fedha hizo mishahara ni **Shilingi 693,272,557.12** sawa na **asilimia 57.2** ya lengo na Matumizi mengineyo **Shilingi 967,094,500.00** sawa na **asilimia 56.4**. Aidha, kiasi cha **Shilingi 389,470,000** fedha za nje kimepokelewa sawa na **asilimia 100** ya fedha za nje

zilizoidhinishwa na Bunge. Tume haikupata kiasi chochote cha fedha za ndani za maendeleo kama ilivyokuwa katika bajeti ya mwaka uliopita. Hali hii inaonesha kwa kiasi kikubwa bado tunategemea fedha za wafadhili katika kutekeleza miradi ya maendeleo inayohusu mapambano dhidi ya UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaendelea kushauri kuwa

- i) Serikali ihakikishe upatikanaji wa fedha za matumizi ya maendeleo ili kuimarisha mapambano dhidi ya janga la UKIMWI kwa mustakabali wa taifa wa kufikia 95 – 95 – 95 ifikapo mwaka 2030.
- ii) Serikali kuhakikisha inatenga fedha za ndani kwa ajili ya utekelezaji wa afua ya UKIMWI na kupunguza utegemezi wa wafadhili.
- iii) Fedha zinazopitishwa na Bunge zitolewe kwa wakati ili utekelezaji wa shughuli zilizopangwa ufanyike kama mpango kazi wa Tume unavyojeleza.

Kielelezo Na. 1: UPATIKANAJI WA FEDHA KUFIKIA FEBRUARI, 2022




Chanzo: Taarifa ya TACAIDS kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Mwaka 2022/2023

2.3.2 Upatikanaji wa Fedha za Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevyaa (DCEA) - Fungu 91

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/2022, Bunge liliidhinisha **Shilingi 8,529,797,000** kwa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevyaa (Fungu 91) ili kuwezesha mapambano na udhibiti wa dawa za kulevyaa. Fedha hizo zinajumuisha Mishahara **Shilingi 6,167,415,000.00** sawa na **asilimia 72.3** na Matumizi mengineyo **Shilingi 2,362,382,000.00** sawa na **asilimia 23.7** na hakuna fedha yoyote iliyotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, kufikia Februari, 2022 jumla ya **Shilingi 6,210,679,332.38** sawa na **asilimia 72.8** zilikua zimepokelewa. Kati ya fedha hizo Mishahara ni **Shilingi 4,790,648,476.38** sawa na **asilimia 77.7** ya bajeti na Matumizi mengineyo **Shilingi 1,420,030,856.00** sawa na **asilimia 60.1** kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Na. 2. Kamati inaipongeza Serikali kwa utoaji wa fedha unaoridhisha.

Kielelezo Na. 2: UPATIKANAJI WA FEDHA KUFIKIA FEBRUARI, 2022



Chanzo: Taarifa ya TACAIDS kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Mwaka 2022/2023

SEHEMU YA TATU

3.0 UCHAMBUZI WA MPANGO WA MAKADIRIO YA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA WA 2022/2023

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipokea na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu – Fungu 91 (Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevy) na Fungu 92 (Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania) kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023. Uchambuzi ulilenga pamoja na mambo mengine kuhakiki kama Mpango na Makadirio haya vimezingatia llani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2020 – 2025, Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano na Mwongozo wa Mpango wa Bajeti uliotolewa na Wizara ya Fedha na Mipango. Uchambuzi unaonesha kuwa maeneo ya vipaumbele katika makadirio hayo yamezingatia miongozo inayotakiwa ikiwemo llani ya Uchaguzi.

3.1 Mapitio ya Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa fedha 2022/2023

3.1.1 Tume ya Kudhibiti UKIMWI – Fungu 92

Mheshimiwa Spika, Kwa Mwaka wa Fedha wa 2022/2023 Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania - **Fungu 92** inaombewa jumla ya **Shilingi 14,981,224,000.00**. Kati ya fedha hizo, Shilingi **2,979,018,000** sawa na **asilimia 20** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 12,002,206,000** sawa na **asilimia 80** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ambapo **Shilingi 1,880,000,000** ni fedha za ndani na Shilingi **10,122,206,000** ni fedha za nje kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Na. 3.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi umebaini ya kuwa bajeti ya Tume imeongezeka kwa asilimia **asilimia 246.9** kutoka **Shilingi 4,317,818,000.00** mwaka 2021/2022 hadi kufikia **Shilingi 14,981,224,000** mwaka 2022/2023. Ongezeko zaidi ni kwenye fedha za Maendeleo nje kwa **asilimia 2,498.97** na maendeleo ndani kwa **asilimia 88**. Kamati inapongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa kuongeza fedha kwenye miradi ya maendeleo

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

na kusitiza kuwa fedha hizi zitolewe kwa wakati ili shughuli zilizokusudiwa ziweze kutekelezwa kikamilifu.

Kielelezo Na. 3: ULINGANISHO WA BAJETI YA KWA MWAKA 2021/2022 NA 2022/2023

AINA	2021/2022	2022/2023	ONGEZKO/PUNGUFU	ASILIMIA
OC	1,212,746,000.00	1,212,746,000.00	-	-
MISHAHARA	1,715,602,000.00	1,766,271,000.00	50,669,000.00	295
MAENDELEO NDANI	1,000,000,000.00	1,880,000,000.00	880,000,000.00	88.00
MAENDELEO NJE	389,470,000.00	10,122,206,000.00	9,732,736,000.00	2,498.97
JUMLA	4,317,818,000.00	14,981,223,000.00	10,663,405,000.00	246.96

Chanzo: Taarifa ya Bajeti ya TACAIDS 2022/2023

3.1.2 Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevy - Fungu 91

Mheshimiwa Spika, Katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 Fungu 91- Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevy linaombewa kiasi cha **Shilingi 11,974,701,000.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 2,127,286,000.00** ni Mishahara ya watumishi na **Shilingi 9,847,415,000.00** ni fedha za Matumizi Mengineyo.

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi umefanyika kwa kulinganisha Bajeti ya Mamlaka kwa Mwaka 2021/2022 na 2022/2023 kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Na. 4 na kubaini ongezeko la bajeti kwa **asilimia 40.39**. Ongezeko zaidi ni kwenye Matumizi mengineyo (OC) kwa **asilimia 59.7** na hususan Kasma 31121 ya Vyombo vya Usafiri kutoka **Shilingi 1,000,000.00** hadi **Shilingi 660,000,000.00** sawa na ongezeko la **asilimia 65,900**; na Kasma 31122 ya Mashine na Vifaa visivyo vya usafiri kama vifaa vya kisayansi vya utambuzi wa dawa za kulevy kutoka **Shilingi 187,650,000.00** Mwaka 2021/2022 hadi kufikia **Shilingi 411,049,000.00** Mwaka 2022/2023 sawa

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

na ongezeko la **asilimia 119**. Kamati inapongeza ongezeko hili na kuomba zitumike kutekeleza majukumu yaliyokusudiwa ikiwemo Serikali kuhakikisha fedha hizi zinatoka kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi pia umebaini kuwa mishahara imepungua kwa **asilimia 9.9** na hususan katika Kasma 21111 - Idara ya Utawala kutoka **Shilingi 2,362,382,000.00** mwaka 2021/2022 hadi kufikia **Shilingi 2,127,286,000.00** sawa na upungufu wa **asilimia 9.95**. Kamati ilihoj sababu ya kupungua kwa mishahara na ilielezwa kuwa ni kutokana na mahitaji halisi ya mwaka huu wa fedha.

Kielelezo Na. 4: ULINGANISHO WA BAJETI YA KWA MWAKA 2021/2022 NA 2022/2023

AINA	2021/2022	2022/2023	ONGEZEO/UPUNGUFU	ASILIMIA
OC	6,167,415,000.00	9,847,415,000.00	3,680,000,000.0	59.67
MISHAHARA	2,362,382,000.00	2,127,286,000.00	- 235,096,000.0	- 9.95
JUMLA	8,529,797,000.00	11,974,701,000	3,444,904,000.0	40.39

Chanzo: Taarifa ya Bajeti ya Mamlaka ya Kudhibiti Dawa za Kulevyaa 2022/2023

SEHEMU YA NNE

4.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

Mheshimiwa Spika, baada ya uchambuzi wa Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha wa 2021/2022 na Makadirio ya Matumzi kwa Mwaka wa Fedha wa 2022/2023 kwa Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (*TACA/DS*) – Fungu 92 na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevyaa – Fungu 91, Sasa naomba kutoa maoni na ushauri kwa Mafungu yote mawili kama ifuatavyo:

4.1 Maoni ya Jumla

4.1.1 Afua za Lishe Magerezani

i) Kamati inasisistiza Mamlaka husika zihakikishe afua za lishe magerezani na hususan kwa watu wenyewe mahitaji maalum zipewe kipaumbele.

ii) Ni vyema pia wakatafutwa wadau watakaosaidia kuwapatia wafungwa na mahabusu lishe bora kama wanavyofanya kwenye maeneo mengine kwa mfano kwenye UKIMWI kuwapatia dawa WAVIU.

4.1.2 Magonjwa Yasiyoambukiza

Mheshimiwi Spika, Kamati inaishukuru Serikali kwa kuendelea kuchukua hatua mbalimbali ili kukabiliana na Magonjwa Yasiyoambukiza. Hata hivyo, Kamati inaona bado ipo haja ya Serikali kufanya yafuatayo:-

i) Kuendelea kutoa Elimu kwa jamii ya namna ya kujikinga na magonjwa haya; na

ii) Kuendelea kutenga bajeti ya kutosha kwa ajili ya kutibu magonjwa haya

4.2 Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania

4.2.1 Upatikanaji wa fedha za ndani kwa ajili ya afua za UKIMWI

Mheshimiwi Spika, Kamati inaendelea kusisitiza yafuatayo:-

(i) Serikali ione umuhimu wa kutenga fedha zake za ndani kwa ajili ya udhibiti wa UKIMWI na kupunguza utegemezi wa fedha za wafadhili kutoka nje kwa ajili ya mwitikio endelevu wa mapambano dhidi ya UKIMWI hasa tukizingatia kwamba baadhi ya wafadhili wameanza kupunguza kiwango cha ufadhili wa fedha za UKIMWI kwa Tanzania na wakati mwingine wanatoa masharti magumu; na

(ii) Serikali iweke Mipango madhubuti ya kupata vyanzo vingine vya mapato vitakavyosaidia kupata fedha zaidi kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Ni jambo jema bajeti ya UKIMWI kwa kiasi kikubwa itokane na fedha zetu za ndani.

4.2.2 Mfuko wa UKIMWI wa Taifa (*AIDS Trust Fund - ATF*)

Mheshimiwa Spika, Pamoja na Serikali kuendelea kutenga fedha kwa ajili ya *ATF*bado Kamati inaona upo umuhimu wa kutafutiwa vyanzo iweze kujidesha yenye badala ya kutegemea fedha za wafadhilli. Hivi sasa kuna mlipuko wa Ugonjwa wa UVIKO 19 na mlipuko wa vita vya Rusia na Ukraine ambavyo kwa pamoja vimetikisa uchumi na kuhamisha masikio ya watu wengi kwenye maeneo hayo. Hivyo basi, ni vema kama nchi tukatafuta namna ya kuisaidia *ATF* iweze kujidesha kwani hata ikitokea baadhi ya wafadhilli kuhamishia ufadhilli wao kwenye majanga hayo basi Mfuko huu uendelee kujidesha bila kutetereka.

4.2.3 Utekelezaji wa Afua za UKIMWI

Kamati imebaini kuwa utekelezaji wa Afua za UKIMWI bado siyo wa kuridhisha sana katika maeneo mengi na hivyo kunatia shaka hasa kufikia malengo ya 95 95 95 ifikapo 2030, Kamati inashauri yafuatayo:-

- i) Elimu iendelee kutolewa kwa jamii kuhusu umuhimu wa kupima Virusi vya UKIMWI kwani bado wanaojitokeza ni wachache na hususan wanaume ili wanapobainika waanzishiwe dawa mapema kwa lengo la kufikia 95 95 95 ifikapo 2030;
- ii) Kampeni Maalum zianze kwenye Mikoa ambayo ina maambukizi zaidi ya kiwango cha Kitaifa cha **asilimia 4.7**;
- iii) Ufuatiliaji wa WAVIU watoro ufanyike ili kuhakikisha hawakatishi matumizi ya dawa za kufubaza kiwango cha Virusi mwilini;

- iv) Elimu kuhusu unyanyapaa na ukatili wa kijinsia iendelee kutolewa kwa jamii ili kuondoa hofu ya upimaji lakini pia kupunguza maambukizi kutokana na vitendo vya ukatili wa kijinsia hawa kwa wanawake;
- v) Kamati za UKIMWI za Vijiji zinategemewa sana katika kusaidia katika mapambano dhidi ya UKIMWI. Hata hivyo, imebainika kuwa, Kamati hizi katika maeneo mengi zinalegalega katika utendaji kazi wake. Kamati inashauri Wizara ya Afya, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) ione namna ya kuziwezesha Kamati hizi ili ziweze kusaidia katika mapambano na hivyo kupunguza maambukizi; na
- vi) Elimu kuhusu umuhimu wa kufanya Tohara kwa wanaume iendelee kutolewa kwa jamii na kadhalika.

4.2.4 Kukabiliana na Ugonjwa wa Kifua Kikuu

- (i) Kwa kuwa Msongamano wa Mahabusu unachangia kuongezeka kwa wagonjwa wa Kifua Kikuu kwenye Magereza, Serikali ione namna ya kuharakisha mashauri ya mahabusu ili kupunguza msongamano katika Magereza zetu nchini;
- (ii) Adhabu kwa wafungwa kama utoaji wa huduma za jamii (*Community Service*) uanze kutumika ili kupunguza msongamano wa Wafungwa na Mahabusu katika Magereza;
- (iii) Serikali isimamie na kusisitiza Halmashauri kuendelea kutenga bajeti kwa ajili ya utekelezaji wa afua za Kifua Kikuu;
- (iv) Jamii ishirikishwe vya kutosha ili kuweza kuibua wagonjwa wa Kifua Kikuu;
- (v) Elimu iendelee kutolewa kwa jamii kuhusu Kifua Kikuu ili tahadhari ziweze kuchukuliwa na jamii ikiwa ni pamoja na kupima na kuanza matumizi ya dawa pale wanapobainika kuwa na maambukizi; na

(vi) Wizara ya Afya kwa kushirikiana na wadau ihakikishe upatikanaji wa kutosha wa vifaa mbalimbali kwa ajili ya kupima na kutibu Kifua kikuu nchini.

4.3 Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya

4.3.1 Bajeti ya Miradi ya Maendeleo

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa tangu kuanzishwa kwa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, Mamlaka imekuwa haitengewi bajeti kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Mojawapo ya athari za kutotengewa fedha za maendeleo ni kuwepo kwa changamoto ya vituo vichache vya kliniki za kutolea dawa ya *methadone* kwa waraibu wa dawa za kulevya ambapo huduma hiyo ya tiba inatolewa katika hospitali za wilaya tu.

Mheshimiwa Spika, ajenda ya kupambana na dawa za kulevya ni kubwa na inapaswa kuangaliwa kwa uzito wa pekee. Kamati inaona kuwa Miradi ya Maendeleo inayoweza kutekelezwa kwa fedha za maendeleo ni pamoja na kuwawezesha waraibu kiuchumi kwa kuwapa mbinu za ujasiriamali, mikopo nafuu ya biashara, kilimo, ushonaji, ufugaji na stadi za maisha. Fedha hizo zikitengwa zinaweza kusaidia uongezaji wa vituo vya upataji nafuu kwa waathirika wa dawa za kulevya pamoja na kufanya uraghbishi kwa jamii wa namna ya kupambana na kudhibiti dawa za kulevya pamoja na kuanzisha ujenzi wa vituo vya ofisi za kanda katika maeneo ambayo yana viashiria vya matumizi makubwa ya dawa za kulevya. Kwa mfano, hivi sasa Ofisi ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini iliyopo Mkoani Mbeya inahudumia Mikoa ya Njombe, Iringa na Mbeya.

4.3.2 Waraibu wa Dawa za Kulevya

i) Ili kukabiliana na changamoto ya uchache wa Vituo vya kutoa huduma kwa waraibu wa dawa za kulevya, Serikali iongeze vituo hivi angalau katika kila Hospitali ya Mkoa kuwepo na kituo moja ili kuondoa changamoto ya umbali ambayo imekuwa ikichochea baadhi ya waraibu kushindwa

kuhudhuria kliniki kwa ajili ya kupata huduma; Aidha, Serikali ione umuhimu wa kuanzisha *Multi Satelite Clinics* kwenye maeneo ambayo ni hatarishi zaidi kama kwenye Migodi, Maeneo ya Wavivu n.k

- ii) Vituo vya kujifunza elimu ya kujitegemea vianzishwe katika maeneo mbalimbali nchini ikiwa ni pamoja na kupelekwa jeshini au VETA ili kuwasaidia Waraibu wanaohitimu kujifunza ujuzi mbalimbali utakaowasaidia kujidesha kimaisha;
- iii) Mikopo ya asilimia 10 itolewe kwa Waraibu wahitimu ili iwaezeshwe kuanzisha shughuli za kujingizia kipato na hivyo kutorudi tena kwenye matumizi ya dawa za kulevya;
- iv) Elimu itolewe kwenye jamii ili kubaini watumiaji wa madawa wa kulevya na kuwaanzishia dawa mapema.

5.0 HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha Taarifa ya Kamati mbele ya Bunge lako Tukufu. Napenda kukupongeza kwa namna unavyoliongoza Bunge letu kwa umahiri mkubwa. Vilevile nawashukuru na kuwapongeza Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa utekelezaji mzuri wa majukumu yao.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani kwa aliyekuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge na Watu wenyе Ulemavu, Mhe. Pindi Hazara Chana (Mb), Mheshimiwa Boniphace Simbachawene - Waziri mpya wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge, na Watu wenyе Ulemavu, pamoja na Manaibu Waziri; Mheshimiwa Ummy Nderiananga (Mb) na Mheshimiwa Patrobas Katambi (Mb). Vilevile namshukuru Waziri wa Afya - Mhe. Ummy Mwalimu na Naibu Waziri - Mhe. Godwin Mollel kwa ushirikiano wao mkubwa walioupatia Kamati wakati wote walipohitajika katika kutekeleza majukumu ya Kamati. Vilevile napenda kuwashukuru Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Watu Watu wenyе Ulemavu, Ofisi ya Waziri Mkuu – Dkt. John Jingu pamoja na Maafisa Waandamizi wa Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mhesimiwa Spika, napenda kumshukuru Mkurugenzi Mtendaji wa Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania - Dkt. Leonard Maboko na Kamishna Jenerali wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevy - Kamishna Jenerali Gerald Kusaya Musabila na Watendaji wote, kwa ushirikiano walioutoa kwa Kamati hii ili kutekeleza majukumu yake.

Mhesimiwa Spika, kwa nafasi ya kipekee kabisa naomba niwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI, kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kujadili na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevy kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023. Pamoja na ufinyu wa muda, Wajumbe hawa walikuwa tayari kutekeleza jukumu hili kubwa na kwa wakati. Kwa heshima kubwa, naomba kuwatambua kwa majina Waheshimiwa wafuataa:-

1. Mhe. Fatma Hassan Toufiq, Mb	-	Mwenyekiti
2. Mhe. Dkt. Alice Karungi Kaijage, Mb	-	M/Mwenyekiti
3. Mhe. Amandus Julius Chinguile, Mb	-	Mjumbe
4. Mhe. Tecla Mohamedi Ungele, Mb	-	Mjumbe
5. Mhe. Dkt. Christine Christopher Mnzava, Mb	-	Mjumbe
6. Mhe. Neema Gerald Mwandabila, Mb	-	Mjumbe
7. Mhe. Stanslaus Haroon Nyongo, Mb	-	Mjumbe
8. Mhe. Justin Lazaro Nyamoga, Mb	-	Mjumbe
9. Mhe. Dkt. Pius Stephen Chaya, Mb	-	Mjumbe
10. Mhe. Francis Leonard Mtega, Mb	-	Mjumbe
11. Mhe. Oliver D. Semuguruka, Mb	-	Mjumbe
12. Mhe. Grace Victor Tendega, Mb	-	Mjumbe
13. Mhe. Kassim Hassan Haji, Mb	-	Mjumbe
14. Mhe. Hawa Mchafu Chakoma, Mb	-	Mjumbe
15. Mhe. Neema Kichiki Lugangira, Mb	-	Mjumbe
16. Mhe. Jacqueline N. Msongozi, Mb	-	Mjumbe
17. Mhe. Juma Usonge Hamad, Mb	-	Mjumbe
18. Mhe. Antipas Zeno Mgungusi, Mb	-	Mjumbe
19. Mhe. Abdul-Hafar Idrissa Juma, Mb	-	Mjumbe
20. Mhe. Asha Abdallah Juma, Mb	-	Mjumbe
21. Mhe. Yahaya Omary Massare, Mb	-	Mjumbe
22. Mhe. Khalifa Mohamed Issa, Mb	-	Mjumbe

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

- | | | |
|--|---|--------|
| 23. Mhe. Ester Amos Bulaya, Mb | - | Mjumbe |
| 24. Mhe. Munde Tambwe Abdallah, Mb | - | Mjumbe |
| 25. Mhe. Catherine Valentine Magige, Mb | - | Mjumbe |
| 26. Mhe. Esther Edwin Malleko, Mb | - | Mjumbe |
| 27. Mhe. Neema William Mgaya, Mb | - | Mjumbe |
| 28. Mhe. Rose Cyprian Tweve, Mb | - | Mjumbe |
| 29. Mhe. Juliana Daniel Shonza, Mb | - | Mjumbe |
| 30. Mhe. Asia Abdulkarim Halamga, Mb | - | Mjumbe |
| 31. Mhe. Agnes Mathew Marwa, Mb | - | Mjumbe |
| 32. Mhe. Dkt. Faustine Engelbert Ndugulile, Mb | - | Mjumbe |

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru kwa dhati Watumishi wa Ofisi ya Bunge wakiongozwa na Ndugu Nenelwa Joyce Mwihambi - Katibu wa Bunge, Ndg. Athuman Hussein - Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge na Ndg. Gerald Magili - Mkurugenzi Msaidizi kwa kuiwezesha Kamati hili kutekeleza majukumu yake bila kukwama. Kipekee, Nawashukuru Makatibu wa Kamati Ndg. Happiness Ndalu, Ndg. Asia Msangi na Ndg. Pamela Pallangyo kwa kuratibu vyema kazi za Kamati na kuhakikisha Taarifa hii inakamilika kwa wakati mwafaka.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Matumizi ya Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevyta - **Fungu 91** kiasi cha **Shilingi 11,974,701,000.00** ambapo kiasi cha **Shilingi 2,127,286,000** ni mishahara na **shilingi 9,847,415,000** kwa ajili ya matumizi mengineyo na Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania - **Fungu 92** kiasi cha **Shilingi 14,981,224,000.00**, ambapo kiasi cha **shilingi 12,002,206,000** zinaombwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo na **shilingi 2,979,018,000** kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

Fatma H. Toufiq, (Mb)

MWENYEKITI

KAMATI YA BUNGE YA MASUALA YA UKIMWI

6 Aprili, 2022

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mwenyekiti. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge kuna tangazo, Wenyeviti na Makatibu wa Kamati ya Kisekta ya Chama cha Mapinduzi wanakumbushwa Kikao cha pamoja na Sekretarieti ya *Party Caucus* ya Wabunge ya CCM mara baada ya kuahirishwa shughuli za Bunge Ukumbi wa Msekwa C. Kwa hiyo, Katibu wa *Caucus* Mheshimiwa Rashid Shangazi MNEC ndiyo ametoa tangazo hili.

Waheshimiwa Wabunge, sasa jioni tutaanza na Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani Msongozi atafuatia Mheshimiwa Anna Richard Lupembe na tutaendelea na Mheshimiwa Ahmed Shabiby. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge, nasitisha shughuli za Bunge mpaka 10.00 Jioni.

(*Saa 7.15 Mchana Bunge Lilisitishwa Mpaka Saa 10:00 Jioni*)

(*Saa 10.00 Jioni Bunge lilitrudia*)

NAIBU SPIKA: Tukae. Katibu.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na mjadala wa Ofisi ya Waziri Mkuu, tulishamtaja Mheshimiwa Ngonyani, ajiandae Mheshimiwa Lupembe na Mheshimiwa Shabiby.

MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa fursa hii ili nami niweze kuchangia bajeti ya mwaka 2020/2022 na 2020/2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa mimi nimchangiaji wa kwanza kabisa katika bajeti hii ya mwaka nilioutaja, ambayo inakadiliwa kuwa na thamani ya pesa za Kitanzania shilingi triliuni 41, naomba nichukuwe nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu na niseme rasmi kwamba sasa naliamsisha dude. (*Kicheko/Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakwenda moja kwa moja kwenye suala la kilimo. Suala la kilimo niseme kwamba sasa kimepata Waziri ambaye anaendana na kasi ya sasa ya kwenda kufungamanisha masuala ya kilimo na viwanda. Ni matumaini yangu kwamba akipewa bajeti itakayotosha, basi atakwenda kufanya vizuri zaidi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia Bunge hili naomba niwajulische Watanzania kwamba wasiwe na hofu kuhusiana na suala la kilimo, tayari linakwenda kupata tiba na ndugu zangu wa Mkoa wa Ruvuma sasa wanakwenda kupata tiba ya kile kilio cha mbolea kwa maana ya bei kubwa ya pembejeo zilizokuwa zimebekwa. Kwa mujibu wa taarifa ambayo juzi imetolewa na Waziri mwenye dhamana, anasema kwamba ana uhakika wa kuweka ruzuku kwenye mbolea na hatimaye mbolea hii itakuja ikiwa na bei ambayo inanunulika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii pia kuomba taasisi mbalimbali za fedha kujitokeza kusaidia kwenye Mkoa wa Ruvuma walete pesa za mikopo ili wananchi wa Mkoa wa Ruvuma weweze kukopa waende kuwekeza kwenye kilimo. Naomba sana taasisi hizo zitukopeshe kwa *style* ya *single digit* ili kila mkulima aweze kukopa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Mkoa wa Ruvuma ni bingwa kabisa na umeshika namba moja miongo minne mfululizo kwa uzalishaji wa mazao ya nafaka nchini, ni matumaini yangu kwamba Serikali itaona umuhimu pia wa kupeleka Benki ya Kilimo ili wananchi waweze kukopa kwa ukaribu. Hata mtoto akifanya vizuri, anapewa zawadi. Kwa hiyo, nitoe wito kwa Serikali kwenda kuweka Benki ya Kilimo katika Mkoa wa Ruvuma. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na suala la *EPZ* kuchukua maeneo mbalimbali na kuwafanya wananchi kuendelea kuwa masikini kwenye maeneo husika bila kuwapa riba. Miiongoni mwa maeneo hayo naomba nitaje Kata ya Mwengemshindo iliyoko katika Manispaa ya Songea.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Hivi ninavyozungumza, kutokana na zoezi la anuani ya makazi, Mwengemshindo imetengwa na wananchi wana tafrani, hawaelewi mwisho wao, hawaelewi mwelekeo, kwenye eneo la makazi hawajahesabiwa nyumba zao. Kwa misingi hiyo, wanapata mashaka kwamba inawezekana wanaondolewa kwenye duru ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia EPZwamechukua eneo la Mwengemshindo tangu mwaka 2008, mpaka sasa hivi ninavyozungumza ni takribani miaka 12 wananchi hawa hawajapewa fidia na wamedumaa kiuchumi. Serikali inachukua hatua gani ya haraka ya kuwawezesha hawa wananchi ili waweze kuondoka kwenye maeneo haya na waende kwenye maeneo mengine ambayo wataweza kwenda kufanya uwekezaji? (*Makofii*)

Mheshimiwa Nailbu Spika, pesa wanayoidai mpaka sasa hivi kutokana na eneo hilo ni shilingi bilioni 3.5. Naomba Serikali iniambie ni lini watawezesha wananchi hawa wa Kata ya Mwengemshindo ili waweze kuondoka maeneo hayo na kwenda kuwekeza maeneo wanayokwenda kutarajia kufanya shughuli zao? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni muda mrefu sasa imekuwa ikitajwa barabara ya Njombe Songea ambayo hajafanyiwa ukarabati kwa muda mrefu na inahitaji ifanyiwe upanuzi. Naomba Serikali jje na majibu, ni lini itanza kufanya ukarabati huo? Pia tunayo barabara ya kimkakati Likuyufusi - Mkenda inayokwenda kuunganisha Tanzania na Mozambique, ina urefu wa kilometra mia 124; ni barabara ya kimkakati. Tunaomba kujua ni lini Serikali itanza kujenga kwa kiwango cha lami? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la barabara ya Mtwara - Pachani kwenda Lusewa na Rasi mpaka Tunduru pia ni barabara ya mkakati, tunaomba sasa ianzwe kujengwa kwa kiwango cha lami. Lumecha - Londo kwenda kwa Mpapo, yaani inaunganisha Mkoa wa Ruvuma na Mkoa wa Morogoro, tunataka ianzwe kujengwa kwa kiwango cha lami. (*Makofii*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo cha Afya Msindo ni kituo cha muda mrefu sana. Wananchi sasa wamejitokeza kujenga jengo la upasuaji kwa kutumia pesa zao. Sasa Serikali ni lini itapeleka pesa ili iweze kuhakikisha kwamba lile jengo la upasuaji linakamilika na waweze kupata huduma?

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni suala la utawala bora. Nichukue nafasi hii kumpongeza sana kipenzi chetu Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan, mwanamke shupavu ambaye amejipambanua ndani ya nchi na nje ya nchi, anafanya vizuri sana; na kwamba anafanya kazi zake kwa kuzingatia misingi ya utawala bora na anakwenda vizuri mno. Tuna imani naye, hatuna mashaka naye, mama yetu atatuvusha vizuri sana. Tunamwombea kwa Mwenyezi Mungu amjalie kila la kheri na kila atakapoona kwamba kuna jambo ambalo linakuwa ni kikwazo katika kutimiza majukumu yake kupitia masuala ya sheria, shime atuletee sheria hapa Bungeni tuzirekebishe na mambo yake yasikwame. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema kuhusiana na suala la utawala bora. Mheshimiwa Mama Samia anakwenda mwendo kasi, lakini wako baadhi ya watendaji wanamkwamisha. Tunaomba watendaji wote wa nchi hii wafanye kazi kwa uadilifu na uaminifu ili mama yetu asikwame mahali popote pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nataka nizungumzie suala la *LTRA*. Nchi yetu ni nchi ambayo hiko katika hali ya usalama kabisa, lakini pia tunatakiwa tuweke mazingira mazuri ya wananchi kufanya shughuli zao ikiwemo wajasiliamali waweze kusafiri muda wote, wasafiri mchana, wasafiri usiku. *LTRA* wana mpango gani wa kuhakikisha jambo hili linatekelezeka ili wananchi waweze kusafiri?

Mheshimiwa Naibu Spika, wako baadhi ya Watendaji Wakuu ambao ni tatizo kuhusiana na suala hili hili la utawala bora. Unampigia simu Mtendaji Mkuu unajitambulisha kwamba mimi ni fulani bin fulani. Sasa kama mimi kiongozi ninaweza nikajitambulisha na bado asirudi kwangu, asijibuu

message, hao ni watu ambao ni majipu yanatakiwa yatumbuliwe haraka sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii pasipo shaka yoyote na nina ushahidi wa kutosha, ninaomba kama kanuni inaruhusu nimirage Mtendaji wa LATRA ni jipu. Mtendaji Mkuu wa LATRA ni jipu. Hapokea simu, hajibu *message*, watu wanapata ajali maeneo mbalimbali, wafanyabiashara wana shida mbalimbali ya kujua ABCD, maelekezo mengi anapata lakini hawesi kuyatekeleza. Sasa huyu ni mtu wa aina gani? Ingekuwa ni amri yangu ningesema apishe uchunguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia niende kwenye suala la mpango mzima unahusiana na masuala ya vijana. Ofisi ya Waziri Mkuu kupitia bajeti yake, ameeleza namna ambavyo vijana wamewezeshwa kwenye maeneo mbalimbali na tumeona vijana, mimi ni Mjumbe wa Kamati hiyo, tumeona vijana wamewezeshwa vitalu nyumba kwenye maeneo yao, lakini je mrejesho ukoje? Tathmini ikoje? Hawa vijana kupitia hivyo vitalu nyumba vimewasaidia kwa kiasi gani? Wame-achieve nini? Kwa hiyo, tunataka kujua.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumepata taarifa maeneo mengine unakuta Madiwani wanaingilia katika wanapoka vile vitalunyumba vya vijana. Kwa hiyo, naomba sana Serikali yangu iende kule, Wakurugenzi wa maeneo husika waende wakakague na tupate majibu, vimesaidia kwa kiasi gani na vijana wamenufaika kiasi gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine la mwisho, naomba sana wanawake wa Mkoa wa Ruvuma wana uhitaji sana wa kuwekeza katika kilimo. Naomba sana uwepo mpango mzuri; wakati mwagine unaweza kuwakopesha vikundi mbalimbali wakafanya biashara, lakini hawana utaalamu wa mambo ya biashara, lakini tukiangalia maeneo mbalimbali kulingana na jiografia zao na mila zilizopo, unaweza kuwasaidia vikundi hivyo ukawapa mbegu, ukawawezesha katika masuala ya kilimo na wakafanya vizuri zaidi na wakawa na tija zaidi.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maneno haya, naomba kuwasilisha. Ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante. Sasa namwita Mheshimwa Lupembe, jiandae Mheshimiwa Shabiby na Mheshimiwa Nusrat Shaaban Hanje.

MHE. ANNA R. LUPEMBE: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa naomba nimshukuru Mungu ambaye ametupa uzima na uhai hatimaye ametupa kibali tuko katika eneo hili la Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwamba kabisa naomba nimshukuru Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mama yetu mpPENDWA Mheshimiwa Samia Suluhu kwa kazi kubwa ambayo anaifanya kwa Watanzania. Naomba nimpongeze sana. Vile vile naomba nimpongeze Waziri Mkuu kwa kazi kubwa ya kuendelea kuisimamia Serikali. Anafanya kazi nzuri, tunaona anahangaika katika Mikoa mbalimbali kuhakikisha nchi yetu inasonga mbele. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niipongeze Serikali kwa ujumla kwa kazi kubwa kupitia mama yetu Mheshimiwa Samia; tulipewa fedha nydingi kupitia fedha za UVICO ambazo zimekuja katika Majimbo yetu, zimetuwezesha kujenga Zahanati, Vituo vya Afya, Shule Shikizi na Shule za Sekondari. Naomba niipongeze sana Serikali kwa kazi kubwa ambayo wameifanya. Kusema kweli sisi Wabunge wa Majimbo tunajivunia sana kwa sababu kazi imeonekana na bajeti imeonekana. Naomba tuipe pongezi kubwa sana Serikali ya Awamu ya Sita kwa kazi kubwa ambayo wameifanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kazi kubwa imefanyika, tumeona kwenye majengo ya Shule Shikizi na Shule za Sekondari tumeweka vifaa kama madawati na kadhalika, pia tumejenga Vituo vya Afya na Zahanati, lakini mpaka leo bado hatujapata vifaa. Tumeanza kujenga majengo mengine mwezi wa Tatu mwaka 2021, mengine tumepewa

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

fedha mwezi wa Kumi mwaka 2021, tayari yamekamilika lakini mpaka leo vifaa tiba hatujapata. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jimbo langu nimepewa fedha za Hospitali ya Wilaya, nimejenga Hospitali ya Wilaya lakini mpaka leo hatujaweza kuifungua kwa sababu hatuna vifaatiba. Tunaiomba Serikali sasa ijielekeze kwenye vifaatiba ili majengo yale yaweze kufanya kazi vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tulikuwa tuna kero kubwa sana ya watendaji wa kazi amba ni walimu, manesi na madaktari. Leo naomba nimshukuru sana Waziri mwenye dhamana ambaye ni Waziri wa Utumishi, ametuambia kutakuwa na ajira kama 30,000 ambapo atakuja kwenye bajeti yake kuisema. Naomba tuipongeze sana Serikali kwa kazi kubwa ambayo wanaendelea kutuonyesha sisi Watanzania. Tulikuwa tunapata kero kubwa kwa ajili ya watumishi, lakini leo tunatarajia sasa watumishi watapatikana katika maeneo yetu kwa sababu tumejenga Shule na Zahanati lakini hakuna watumishi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini bado kidogo kuna changamoto kwa ajili ya walimu wenye madai yao, bado hatujaweza kuwafikia wote, wengine hawajapata madai yao, wanadai malimbikizo ya madeni yao. Tunaomba hilo tulifanyile kazi kwa sababu wanafanya kazi kubwa, wanakaa katika mazingira magumu. Naiomba sana Serikali yangu sikivu iwaangalie hawa walimu wanaodai madai yao limbikizi waweze kulipwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niipongeze sana mifuko ya kijamii pamoja na mashirika. Hii mifuko inajitegemea na vilevile kuna vikwazo kuititia mashirika yetu haya, yana uwezo wa kuajiri, sasa tumewawekea vikwazo wasiajiri mpaka kibali kitoke Utumishi. Nilikuwa naomba haya mashirika kwenye ngazi labda kuanzia vibarua, makarani na wengineo hapa tumewapa fursa waajiri wenyewe, lakini kuititia ngazi ya Mameneja na Wakurugenzi iende Utumishi ili waweze kuajiri. Kwa sababu kuna vikwazo, unakuta wanatamani

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

kuajiri watu, lakini kuna vikwazo lazima wapate vibali ili kazi ziweze kusonga mbele. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naiomba Serikali yangu kupitia utumishi tuwape ruhusa waajiri kuanzia ngazi ya vibarua mpaka makarani, zile kazi ambazo ni za kawaida, waajiri wenyewe ili kazi zile nyepesi na rahisi zaidi waweze kuzifanya ili majukumu yao yaweze kwenda vizuri zaidi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakuja *TARURA*. Naomba niipongeze Serikali yangu; na kupitia Rais wetu, Mheshimiwa Mama Samia, najua bajeti iliyopita kila Mbunge wa Jimbo alipata shilingi bilioni 1,500. Zile fedha zimetusaidia sana, zimefungua barabara, kazi kubwa imefanyika, inaonekana; barabara za vijiji na vitongoji sasa hivi zimeunganika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, ndani ya maeneo yetu ya vijijini kuna madaraja makubwa. Tumeona Mheshimiwa Waziri Mkuu hapa wakati akiwasilisha bajeti yake, ameonesha madaraja makubwa yaliyojengwa na mama yetu Mheshimiwa Samia kwa fedha nyingi.

Naomba Serikali sasa iongeze bajeti kwenye *TARURA* ili sasa madaraja yote ya vijijini, kuunganisha vijiji na vitongoji yaweze kujengwa kwa ajili ya usalama wa wananchi wetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia kipingi hiki cha mvua, leo hii mvua zikinyesha katika maeneo yetu, vitongoji na vijiji watoto wa shule katika mito yetu wanashindwa kuvuka kabisa. Ina maana mvua zikianza kunyesha watoto wengi hawaendi kwenye masomo inavyotakiwa katika muhula.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naomba sana, sasa ifike kipindi *TARURA* tuiongezee bajeti. Madaraja yote makubwa ndani ya vijiji na vitongoji vyetu, yajengwe na *TARURA* yenyewe. *TANROADS* inashughulika na barabara kubwa na madaraja makubwa, sasa naomba *TARURA* tuiongezee fedha ili iweze kufanya kazi vizuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, najua kuna vitu vingi tunavyovifanya katika nchi yetu, tunajenga vituo vyatupu polisi katika maeneo yetu na tunaendelea kuchangia na wananchi wanaendelea kuchangia, kuna maboma, lakini naomba ndani ya kata zetu unakuta polisi anakaa kwenye Ofisi ya Mtendaji anakuwa yeye polisi peke yake. Sasa kama kuna uhalifu ndani ya maeneo yetu au kuna kitu chochote kimefanyika katika maeneo yetu ya kata, ina maana wale wahalifu wanachukuliwa wanapelekwa katika Ofisi ya Mtendaji maana yake hana sehemu ya kuwatunza. Nilikuwa naomba kupitia Serikali yetu siki. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ufile muafaka katika kila kata tujenge vituo vidogo vidogo vyatupu polisi ili wajitegembe. Ukiangalia sasa hivi katika maeneo yetu kuna uhalifu mwingu. Watu wako mbali unakuta kilometra 20, kilometra 30, kilometra 60, kilometra 70 hawana kituo cha polisi. Naomba sana tujielekeze sasa kuhakikisha tunajenga vituo vidogo vidogo kwenye kata zetu kwa ajili ya ulinzi na usalama wa Watanzania tunaendelea kuwatumikia. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, najua kuna mengi ambayo yamefanyika katika nchi yetu na ni mazuri, sasa hivi hatuna hata la kusema, kazi kubwa imefanyika. Tumeomba pesa tumeletewa, kero nydingi kusema kweli zimepungua hata leo Wabunge sidhani kama tutaongea sana kwa sababu tunaona pesa tunaletewa miradi inafanyika, kero kubwa tu tuliyokuwa nayo sisi Wabunge, watendaji kazi hatuna, tunaomba sasa ajira ya watendaji kwa sababu tayari tumeshaambiwaa watendaji wataajiriwa au kuna ajira zinakuja. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba niseme ahsanteni sana. Naomba niunge mkono bajeti hii ya Waziri Mkuu kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Shabiby, jiandae Mheshimiwa Nusrat.

MHE. AHMED M. SHABIBY: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii, lakini kabla sijaongea masuala yangu ya bei za mafuta, kwanza nataka nitoe kabisa tahadhari kwa Mawaziri wa Wizara ya Maji kwamba nitachangia kwenye Wizara yake kuhusu habari ya mpango wa maji yale ya kutoka Changongwe kwenda Kata ya Lubeho, Kata ya Msingisi, Kata ya Gairo, Kata ya Kibedia na Kata ya Chakwale. Kwa hiyo najua bajeti iwekwe mapema. Vile vile kwenye TAMISEMI, Mheshimiwa Waziri Mkuu ni shahidi, Mheshimiwa Rais alipita pale Gairo na tulimwambia ile shida yetu ya kuhusu ule mfereji ambao unazuia mafuriko pale Gairo, lakini mpaka leo hatujawekewa bajeti kwa ajili ya ule mfereji ya kuzuia maji pale Gairo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, nataka niseme tu kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mawaziri wanafanya kazi nzuri na tunataka wafanye kazi bila woga illi waweze kumsaidia Mheshimiwa Rais. Nia ya Mheshimiwa Rais ni nzuri na tunaona kwenye majimbo yetu mambo yanavyokwenda, mimi ni Mbunge wa kipindi kirefu kidogo, lakini naona fedha zinazokwenda kwenye majimbo. Tunashuhudia barabara, tunashuhudia minara ya simu, tunashuhudia hospitali, tunashuhudia kila tu, ila nao wasibaki kusema tu mama kaupiga mwangi, huyu mama nilivyomsoma soma mimi hataki sifa sana, anataka kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mama kaupiga mwangi iendane na ufanyaji kazi wenu Mawaziri na kumsaidia kazi, wasije wakajidanganya kwamba mama anaupiga mwangi kwamba mwenzenu anapenda sifa sana mimi nilivyomsoma soma huyu sifa hataki, anataka kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachotaka kusema Watanzania kila kinachofanyika kama kuna wizi sehemu unakuja au wizi unafanyika, Watanzania wa sasa hivi wana akili wanajua kwamba hapa pana wizi umefanyika au wizi unakuja. Pakiwa na chochote kinachopitishwa kikiwa cha *dea*/Watanzania wanajua kabisa, hili hapa ni *dea*, si hawa Watanzania wa sasa hivi ni wale Watanzania wa zamani. Hapa niliongea miaka minne *nili-spendsana* kuongea habari

ya mafuta, lakini imebidi tena na leo niongee, lakini miaka minne akina Ole-Sendeka ni mashahidi hawa, nilikuwa nazungumzia habari ya mafuta ya taa kufanywa malighafi kuchanganywa na *diesel* na *petrol*, akina mama Kilango wote walikuwepo hapa, miaka minne ndiyo Serikali imekuja kuchukua hatua za kuweka kodi kwenye mafuta ya taa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo mmeshuhudia wenyewe robo ya yale mafuta ya taa yaliyokuwa yanatumika hayatumiki, Serikali imepata mapato mengi imefanya vitu vingi sana. Hili suala tumechangia sana kwamba itakuja kuleta athari kubwa sana za kupanda kwa bei ya mafuta. Ule mpango wa *bulk procurement* wakati unakuja. Kuwa na vita Urusi na Ukraine kwa Tanzania ni fursa na kwa nchi zingine ni fursa ya kupata mafuta kwa bei rahisi, lakini kwetu sisi sasa imekuja ni moto. Tulishasema na narudia kusema kipindi kile imekuja kampuni ya *Lilanceya* tajiri mmoja wa India anaitwa Ambani mwaka 2007 ilipokuja hapa *Reliance* iliponunua *GAPCO* na *GAPWAY* kwa ajili ya kuendesha biashara ya mafuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, *Reliance* ndiyo wenye *refine* kubwa sana duniani kipindi kile ndiyo ya kwanza hata hao Urusi hata Saudi Arabia hawana. Wao wana meli zao walipokuja hapa wakati wameanza kuleta mafuta, mafuta yalishuka zaidi ya shilingi 400 au 500 kwa lita kwa makampuni mengine yote walikuwa hawapati nafasi ya kuuza mafuta. Haya makampuni makubwa ya kizungu yanashirikiana na baadhi ya Wabunge wengine wapo upande wetu na mwingine alikuwa kiongozi kabisa wa chama fulani kule upinzani naye alikuwemo. Wakapiga *deal* kule, wale wajamaa wakawaambia bwana hebu sasa tunafanyaaje huyu *Reliance* anashusha bei, na nini wakawaambia nyie hebu anzisheni mgomo hapo, msiuze mafuta hata siku mbili jifanyeni bei ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema vile vituo vilivyogoma kidogo wakaja huku, twendeni kule kwenye *depots*, sijui twendeni wapi, mbwebwe tu, kumbe wenzetu kuna ulaji. Baadaye tukaleta hoja maalum tujadili. Baada

ya kujadili tukasema hakuna mtu binafsi kuleta mafuta, tununue kwa *bulk procurement*, matokeo yake ni nini? Ukiishanunua mafuta kwa pamoja, sasa nani maana wote mnanunua bei hii halafu wote mnaleta mnapangiwa bei hii, sasa atakayeshusha nani, wote mnakuwa na bei moja, hakuna tena ushindani wa mafuta. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, yule bwana akaamua kuza kabisa, akawauzia *TOTAL* ile *GAPCO* na *GAPWAY*, maana yeye alitegemea ataleta mafuta yake atauza kwa ushindani kama alivyokuwa anafanya atashusha bei, lakini mnawambia sasa bwana tunaenda kununua wote kwa pamoja, sasa ushindani uko wapi? Hebu kumbukeni angalieni kuanzia ile miaka ile kuna makampuni mpaka ya Watanzania *World Oil* ni ya Mtanzania, mtu wa Kigoma; hawa akina Vedasto Manyinyi huyu Mbunge wa hapa wa Musoma hawa nao walikuwa na kampuni yao; wako akina Barongo, watu wa Bukoba huko walikuwa na makampuni yao, watu kibao walikuwa na makampuni yao. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi ninavyokwambia kule *deep sea* kuna meli zinauza robo ya bei ya dunia yanatoka huko Urusi mengine yanatoka nchi zilizoweke kwa vikwanzo yako pale yanauza robo ya bei ya dunia, ukimruhusu mfanyabiashara wa binafsi yeye kazi yake anachokwenda pale *ship to ship* anachukua mafuta, meli kwa meli anapakia mzigo anakuja, ninyi watu wa huku wa *EWURA*, watu sijui wa Serikali, watu wa *TBS*, kazi yenu ilikuwa panga bei bwana, mafuta haya kwa bei ya dunia yasizidi hapa na *TBS* kiwango chetu tunataka hiki, yanatimiza kiwango basi, kwisha lakini unataka tu kupanga. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naangalieni kwenye hiyo *bulk procurement*, watu wanakula pesa siyo mchezo, nchi hii inatumia lita milioni mia nne kwa mwezi. Sasa fanya tu wale kwenye ile Kamati wanachosema kwamba fulani nikupe *tenderya* kwenda kununua wakiweka dola tano tano wana shilingi ngapi? Hata dola mbili mbili wana bei gani? Tunachokizungumza hatukizungumzi kwa kukisia, lakini ukiongea sana hapa ukishika mishiko ya watu unasilika huyu

Shabiby atakuwa mwizi wa mafuta huyu yaani nyie mnajua wa wizi wizi tu. Wakati wezi wako huko huko, ndio majambazi halafu wanatengeneza na nataka niseme kwamba kila kitu sasa hivi ni *deal* na kuna watu wachache ambao kazi yao ni kupanga *deal* kwenye hii nchi, sisi huku tunapelekeshwa tu, tunapitisha sheria kumbe sheria hakuna. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii mkiruhusu kampuni binafsi ziagize mafuta na kama mtu anaona kuna unafuu kama mnavyodai *bulk procurement* nayo iwepo, kama ataona kuna nafuu aende huko, kama ataona hamna nafuu alete yeye, Serikali kazi yake iwe kuangalia tu kiwango inachokitaka na bei inayotakiwa, lakini vitu vingine wanatunga tu utasikia ukileta mafuta mtu mmoja mmoja yatakuwa yanakwepa ushuru, meli zote zinashusha kwenye mita, zinashushia wapi? Hii kazi waachieni *TRA*, *TRA* ya nchi hii inafanya kazi nzuri, waaminini *TRA* lakini wao wanawapa kazi *TRA* wanakula *deal*. Sasa hivi tukiangalia toka ile *bulk procurement* mpaka sasa hivi ile mita imekufa mara ngapi? Imekufa mara nyigi kuliko wakati wanaleta watu binafsi ile mita ya bandarini. Naombeni sana turuhusu hayo bei ya mafuta itashuka kuliko tulivyotegemea na wala tusidanganyane na tusiwedanganye watu na watu wengine hata waliopo huko nje wasiwedanganye kwamba Serikali inaweza ikatoa kodi ya kwenye mafuta, ukitoa kodi nchini, hii mishahara haipo wala hakuna madawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunategemea hiyo kodi ya *petro/tusidanganyane* eti kodi sijui elfu moja na ngapi? Kodi yetu ndio inayotulisha sisi Serikali wala tusiwedanganye watu kama tunaweza kutoa kodi, kodi hatuwezi kutoa tunachotakiwa kufanya ni kupata mafuta kwa bei rahisi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine, dakika yangu moja imepotea kwa ajili ya makofi, naomba uilinde. Serikali imeleta matrekta yale matrekta yapo pale Kibaha yanaitwa *Alice* sijui *Ursus* yanaitwa nini? Serikali imewaletea wakulima kuja kuwaua, imeleta matrekta mabovu mimi sijawahi kuona toka

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

nizaliwe, mimi ni mkulima nina trekta zaidi ya ishirini sijawahi kuona trekta inakatika katikati kichwa kinaenda peke yake matairi ya nyuma yanabaki peke yake. Haya matrekta yote ni mabovu, leo wamewatia watu umaskini hawa, huko yalikonunuliwa wapo wapi wale watu, hawajatoa *guarantee*? Yale matrekta leo wanasumbua wakulima wetu wanawadai wanataka kuwanyang'anya matrekta wao walikuwa hawana *guarantee* na yule aliyeagiza yale matrekta naye ashtakiwe, huwezi kuleta trekta kwanza ina jina la mama linaitwa *Alice*, halafu inakuja inasumbua, nenda unakuta dereva yupo mbele matairi yamebakii nyuma, kiuno kimekatika karibu matrekta yote hamna hata moja mikoa yote Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu leo hii wanaandikiwa barua usipolipa tutakunyang'anya trekta. Mtu unamda milioni 20, ukimnyang'anya trekta unaenda kulipiga mnada kwa milioni mbili kwa hiyo hapa pana kila aina ya njia ya wizi. Serikali iangalie namna ya kuwasaidia kuyatengeneza yale matrekta na wawasadie namna ya kuwaongeza muda ili waweze kulipa yale madeni wanayodai. Vilevile wachunguze haya matrekta nani kaleta na yana mkataba gani na yana *guarantee* gani, maana yake trekta haiwezi kuwa na *guarantee* ya mwaka mmoja kama lori au kama basi au kama gari ndogo, linatakiwa liwe na muda mrefu. Kwa hiyo...

NAIBU SPIKA: Ahsante.

MHE. AHMED M. SHABIBY: Kwa hiyo naomba wayafuatilie hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Nusrat Shaaban Hanje, wajiandae Mheshimiwa Hasunga na Mheshimiwa Abdul-Hafar Idrissa Juma.

MHE. NUSRAT S. HANJE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi ili niweze kuchangia. Kwenye

bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu na nitachangia Fungu 65 - Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitachangia *specific* kwenye eneo moja sana kwenye maendeleo ya vijana kwa sababu pamoja na kwamba tunafanya sensa mwaka huu lakini sensa ya mwisho kufanyika bado imeonesha kwamba nguvu kazi ya Taifa sehemu kubwa sana ni vijana na hatuwezi kuzungumza maendeleo ya vijana bila kuangalia mambo ambayo yanawakibili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasikitika kwamba baadhi ya Mawaziri na Mawaziri wengi sana hawapo hapa na kuna vitu ambavyo tunaongea vingine vinaingia kwao moja kwa moja. Kwa hiyo niseme hivyo, lakini kwenye kitengo na *segment* kuu ya maendeleo ya vijana kwenye Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwenye upande wa Sera ya Maendeleo ya Vijana. Mwaka 2019 vijana wa nchi wallitwa kutoka maeneo mbalimbali wakakaa wakajadili na wakapitisha kwa kutoa mapendekezo yao kuhusu namna ambavyo tunaweza tukawa na Sera ya Maendeleo ya Vijana yenye tija. Mpaka sasa ni miaka minne Sera ya Maendeleo ya Vijana ambayo kimsingi ndiyo inayotoa dira ya shughuli za vijana kwenye nchi, sera inatoa dira kwenye masuala ya Maendeleo ya Vijana.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tunafahamu wote kwamba *life span* yaani umri wa kuishi sera ni miaka 10. Kwa hiyo mpaka sasa hivi katika miaka 10 ya sera ya vijana tumeshakula miaka minne mpaka sasa hivi hatujui nini kitakachofuata, lakini kimsingi watu wanatakiwa wajue. Kwa hiyo wakati sera inakuja tayari imeshakula miaka minne bila kutekelezwa na kimsingi nina sera hapa ambayo kuna baadhi ya vitu tayari vimeshakuwa *outdated*, vimeshapitwa na wakati ambapo pia inatakiwa irudishwe ikapitiwe upya ndiyo iende tena kutekelezwa, *four years. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hatuwezi kuzungumzia Maendeleo ya Vijana bila kuzungumza uwezeshaji wa vijana kiuchumi. Kamati imetoa mapendekezo yao na nimekuwa

nikisoma taarifa za Kamati miaka kadhaa ya nyuma siyo mwaka tu wa leo na leo pia wamezungumza kuhusu Mfuko wa Maendeleo ya Vijana. Mfuko huu umekuwa ni kichomi na kimsingi nilikuwa nasoma pia llani ya Chama cha Mapinduzi hapa kuanzia ukurasa wa 26 mpaka ukurasa wa 30 wanazungumzia masuala ya vijana, lakini mwelekeo wao umejiwekeza katika kutoa semina, kufanya warsha, kufanya makongamano na kujengea uwezo vijana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, imetosha kujengea uwezo vijana, tunataka Mfuko usaidie vijana kujidoresha kiuchumi. Serikali haiwezi kuajiri vijana wote, soko la ajira linatoa watu wengi sana, haiwezekani, kwa hiyo lazima Mfuko huu usaidie vijana kujitegemea kujajiri na kulipa kodi kuchangia maendeleo ya nchi hii. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeangalia pia taarifa hata Kitengo cha Ofisi ya Waziri Mkuu pia na wao wanazungumza ni semina, makongamano, warsha na kujengea uwezo, inavunja moyo kwa sababu sasa hivi kuna kitu kinaitwa *startups* mmekuwa mkisikia, inawezekana watu hawaelewi nitafafanua *startups business* ni biashara ambazo ni za Watanzania zimebuniwa humu, yaani vijana wetu wa Kitanzania wanabangua bongo zao wanaandaa biashara kwa kutumia sayansi, teknolojia na ubunifu kuitikia mabadiliko ya sayansi na teknolojia duniani, lakini kuitikia maendeleo ya viwanda yaani mapinduzi ya nne ya viwanda. Sasa vijana hawa kuna vitu wanahitaji kufanyiwa hawahitaji warsha na makongamano, walishatoka huko. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, *startups* za Tanzania kuna kitu kinaitwa Tanzania *Startups Association* ambayo ndiyo imeunganisha *startups* za Tanzania ambazo zipo 587. Waheshimiwa wana vishikwambi, wachukue *tabulates* zao, wa-google Tanzania *Startups Association* wataona jinsi ambavyo vijana wetu wanabuni vitu vikubwa ambavyo wengine wanashinda mpaka tuzo Afrika. Kuna *startup* inaitwa *Agree Info* wameshinda katika nchi 19 Afrika, lakini sisi tunajadili warsha na makongamano yaani *irrelevant*

kabisa, yaani tunakuwa hatulingani na jinsi vijana wanataka twende. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vijana hawa wanabuni vitu ambavyo ni vya kielektroniki, wengine wanahitaji vitu vidogo vidogo kwa mfano, badala ya kujadili warsha na makongamano, tujadili ni namna gani tunatunga sheria kwa ajili ya kuzilinda *startup business*. Tutunge sheria, sasa hivi ninavyozungumza nilikuwa napitia Kenya, Kenya mwaka 2020 mwezi wa Tisa wamepeleka Bungeni Muswada wa *startups* Kenya kwa ajili ya kuzilinda biashara za kiteknolojia ndogo ambazo zinaanzishwa na vijana wa Kenya. Sasa si kitu kibaya kuiga kwa wenzetu kama kuna kitu kizuri kinafanyika, si mpaka tuchelewe sana, tuje mwisho. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kitu kingine mfano mzuri wa *startup* ya Tanzania ni ile gari ya juzi ya Masoud Kipanya ile ni ya ndani, Masoud ameanzisha kile kitu *from the scratch* ameagiza mitambo kutoka nje. Sasa kama vijana wetu wapo wengine ambaao wanaagiza mitambo kutoka nchi mbalimbali kwa maana ya kuja kuhakikisha wanakuja kutengeneza vifaa vyao vya kielektroniki basi tuwaondolee VAT kwa ajili ya kuwa-*support* na kuhakikisha kwamba tunakuza ubunifu katika nchi yetu. Sasa haiwezekani Wizara ambayo ita-*deal* na masuala ya Vijana inajadili warsha na makongamano. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu nydingine ambayo ninawe nikazungumza, sasa hivi ni miaka saba tangu Bunge hili litunge Sheria ya Baraza la Vijana la Taifa, na ni miezi saba tangu Mheshimiwa Rais aongee na Vijana wa Tanzania kupitia Jukwaa la Vijana wa Tanzania kupitia jukwaa la Vijana wa Mkoa wa Mwanza kutoa maelekezo tuunde Baraza la Vijana wa Taifa. Sasa sitazungumza faida yake lakini nataka tu muone *double standard*, Zanzibar kuna Baraza la Vijana la Taifa, hawawezi kupata kitu chochote kwenye kuiwakilisha nchi kwa sababu Zanzibar siyo nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapozungumza kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki wameanza mchakato wa

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

kuanzisha Baraza la Vijana la Jumuiya ya Afrika Mashariki lakini Vijana wa Tanzania hawatashiriki kwa sababu sisi tunaendekeza siasa mpaka kwenye mambo ya msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna fursa mbalimbali ambazo Vijana wa Tanzania wanaweza kuzipata, sasa labda tuulize Serikali hivi ni kweli mnataka kuwanyima vijana wa Tanzania fursa za kushirika katika Jumuiya ya Afrika Mashariki na Vijana wenzao?

MHE. MOHAMED SAID ISSA: Mheshimiwa Naibu Spika taarifa.

NAIBU SPIKA: Taarifa!

T A A R I F A

MHE. MOHAMED SAID ISSA: Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimpe taarifa ndugu yangu Nusrat Hanje, kwa kusema kwamba Zanzibar siyo nchi. Kwa hiyo naomba atufafanulie hapa. Ahsante sana. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Hebu zungumza tena hoja yako.

MHE. MOHAMED SAID ISSA: Hoja yangu nataka nimpe taarifa Mheshimiwa Nusrat Hanje kwamba Zanzibar ni nchi, kwa hiyo naomba aipokee hiyo taarifa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Nusrat.

MHE. NUSRAT S. HANJE: Mheshimiwa Naibu Spika nashukuru na ninalewa *concern* ya ndugu yangu hapa, lakini katika *representation* katika uwakilishi wa nchi kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki *haiwi-considered* kama nchi, sitazungumza hapo zaidi lakini ninajua *concern* yake na ninafahamu na ninaheshimu masuala yote ya Muungano. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka sasa hatuna Baraza ambalo lingeweza kuwa chombo kiunganishi, kimsingi hata

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Rais anajua hilo Ndiyo maana hata yeye ndiye aliyezindua Baraza la Vijana la Zanzibar akiwa Makamu wa Rais. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya Nne ambayo ndiyo ya mwisho nitazungumza leo ni katika maendeleo ya vijana kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu kuna kitu kinaitwa Mbio za Mwenge wa Kitaifa.

Ninafahamu, ninaheshimu na ninatambua umuhimu wa mbio za Mwenge za Kitaifa kwa maana ya Mwenge wa Uhuru. Ni kitu ambacho tumeki-*respect* na tunakiheshimu sana, ni kitu ambacho kimefanya vitu vikubwa kwenye hii nchi. Lakini kama Mfuko wa Vijana kwa mwaka unatengewa bilioni moja haipelekwi kwa sababu hakuna pesa na tunakimbiza Mwenge nchi nzima kwa ajili ya kumulikia umoja, amani, upendo na mshikamano, tunaviheshimu sana na tunavihitaji sana kwenye nchi, lakini mimi nafikiri tufikiri kuna haja ya kuendelea kutumia gharama kubwa ambayo kimsingi hatuzijui, kwa sababu labda mimi ni mgeni, lakini sijawahi kuona Bungeni inajadiliwa Bajeti ya mbio za Mwenge za Kitaifa, hatujui wala sijawahi kusoma ripoti ya CAGimejadili kuhusiana na gharama za Mwenge na tunaheshimu na naomba ielewewe hivyo. Lakini hivi hatuwezi kutumia ubunifu mwingine kwa ajili ya kuenzi na kuheshimu Mwenge huu ambao kimsingi Luteni Kanali Alexander Nyerenda alianza yeye kwa kwenda kuweka pale juu na tunaheshimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tunaweza kukosa Bima za Afya kwa wote kwenye nchi lakini tusikose pesa ya kukimbiza Mwenge tunakuwa hatutendei haki Vijana wa Taifa hili. Ninasema hivi ili Vijana waelewe mbio za Mwenge kwenye Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu zipo upande wa maendeleo ya Vijana. Kwa hiyo, vijana wajue kwamba kama kuna mambo yanashhindikana maana yake ni kwa sababu tunakimbiza Mwenge! Yaani hajjawahi kukosekana pesa ya kukimbiza Mwenge kwenye nchi hii. (*Makofî*)

MHE. JOSEPH K. MHAGAMA: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

NAIBU SPIKA: Taarifa!

TAARIFA

MHE. JOSEPH K. MHAGAMA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumpa taarifa Mheshimiwa Mbunge kwamba katika hoja yake ameeleza kwamba ameshangaa kuona Mfuko wa Vijana haujatengewa fedha. Mfuko wa vijana ilitengewa Bilioni Moja na fedha zote Bilioni Moja zilipatikana kwenye Mfuko wa Vijana, isipokuwa Vijana wengine hawakukidhi vigezo, Milioni Mia Mbili na Tano zilishatolewa kwa ajili ya Vijana hao na fedha zilizobaki zinawasubiri Vijana kuziomba kwa kuzingatia vigezo. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Ahsante, Mheshimiwa Nusrat.

MHE. NUSRAT S. HANJE: Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru na ni ufanuzi mzuri lakini kwa vijana kule hazifiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda hoja yangu hajanielewa, yaani hivi hakuna namna ambazo sisi kama nchi na *machinery* zote ambazo tunazo, *Ma-Professor*, Waatalam, hivi hatuwezi kufikiri namna bora tunaweza tukauenzi na kuuheshimu huu Mwenge zaidi ya kuuzungusha kutumia gharama ambazo hatuzijui? (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe Mbuge hili, labda ifike muda tuletewe bajeti ili tuone *value for money*. Mwenge unaweza ukakimbizwa kwa Shilingi Bilioni Mia Tisa ukaenda kukagua miradi ya Shilingi Milioni Mia Nne au Shilingi Bilioni Moja, yaani *value for money* katika kujenga.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu sisi hii ni awamu ya kwanza kuna watu wana awamu nydingi humu, labda tusaidiane na ni katika kujenga tusaidine hivi hamna namna nydingine tunaweza tukafanya. Kwa sababu kama Vijana wanakosa pesa, Vijana wenyewe kazi yao ni kwenda kufunga majukwaa, tunahitaji pesa tuende tukafanye miradi ya maendeleo, tunahitaji pesa kwa ajili ya kwenda kujenge

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

barabara. Waheshimiwa Wabunge jana walikuwa wanadai vituo vya Polisi hapa.

MHE. HUSNA J. SEKIBOKO: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

NAIBU SPIKA: Taarifa!

T A A R I F A

MHE. HUSNA J. SEKIBOKO: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumpa taarifa mzungumzaji kwamba Mwenge wa Uhuru ni nembo ya nchi, tunapokuwa tunapozungumzia nembo tunazungumzia *culture* kwa maana ya utamaduni wa Taifa huwa hatuwezi kuangalia *value for money* kwenye mambo yanayohusu utamaduni na alama ya nchi. Utamaduni huu wa *National Torch* siyo kwa Tanzania peke yake, Mataifa mengi yana tamaduni zao na wanatumia mbio za Mwenge kwa ajili ya kuhamasisha, kutia ari na kuweka nguvu katika kuhamasisha shughuli za maendeleo ya nchi husika. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Nusrat.

MHE. NUSRAT S. HANJE: Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2015 tulahirisha sherehe za Uhuru, Mwenge ulikuja baada ya kupata Uhuru kwa hiyo sidhani kama kuna kitu ni muhimu kuliko uhuru wa nchi. Kama tuliweza kuahirisha sherehe za uhuru tukapeleka pesa na Mheshimiwa Rais wa kipindi hiko alitoa maelekezo zifanyiwe nini. (*Makof*)

MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Ole-Sendeka.

T A A R I F A

MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kutoa taarifa.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

NAIBU SPIKA: Hebu tulieni.

MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA: Mheshimiwa Naibu Spika, chimbuko la falsala ya Mwenge wa Uhuru.

NAIBU SPIKA: Nakuruhusu utoe elimu kidogo. (*Kicheko*)

MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA: Mheshimiwa Naibu Spika, chimbuko la falsafa ya Mwenge wa Uhuru ilitolewa kabla ya Uhuru wa Tanganyika. Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alipokwenda kuhutubia Umoja wa Mataifa alisema sisi tunataka kuwashaa Mwenge na kuuweka juu ya Mlima Kilimanjaro, umulike hata nje ya mipaka ya nchi yetu, ulete matumaini pale ambapo hamna matumaini, ulete upendo pale ambapo hamna upendo na ulete heshima pale ambapo hakuna heshima.

Mheshimiwa Naibu Spika, Baba wa Taifa alikuwa anaendelea kuenzi misingi mikuu mitatu ya Chama cha TANU, Utu, Haki na Usawa. Hapo ndipo msingi wa Uhuru wa Tanganyika ulipoasisiwa na Hayati Baba wa Taifa. Naomba msubiri msikilize darasa la haki. (*Makofi*)

MHE. KUNTI Y. MAJALA: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa!

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Sendeka wamekuelewa vizuri sana, Ahsante. Mheshimiwa Nusrat aah kaa tu. Mwenge huu alivyosema pale Mheshimiwa ni *symbol* kwanza ukienda kwenye shughuli za Mwenge siyo kwamba watu wanakimbizana tu kuna kukagua miradi na kuna miradi inakataliwa kutokana na kutokutengenezwa kwa viwango, kwa hiyo *value for money* ipo.

Pili, Mwenge huu kuna risala inasomwa anasomewa Rais, kwa hiyo, yule atayekwenda pale anamuwakilisha Rais wa nchi. Ni njia ambayo tumeitumia kutafuta urahisi wa kipeleka maendeleo na taarifa zifike kwenye maeneo mbalimbali, kwa hiyo kwa kifupi habari ndiyo hiyo (*Makofi/ Kicheko*).

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Mheshimiwa Hasunga.

MHE. JAPHET N. HASUNGA: Mheshimiwa Naibu Spika...

NAIBU SPIKA: Jiandae Mheshimiwa Abdul-Hafar Idrissa Juma.

MHE. JAPHET N. HASUNGA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia katika bajeti ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Jambo la kwanza naomba...

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa tuwe na utulivu.

MHE. JAPHET N. HASUNGA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa namna anavyoiongoza nchi yetu, lakini kwa namna anavyoifungua nchi. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa upande huu tuwe na utulivu Ramadhan hii, Hasunga endelea.

MHE. JAPHET N. HASUNGA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa namna anavyoiongoza nchi yetu, lakini kwa namna anavyoifungua kiuchumi na kwa namna ambavyo ameamua kupanua demokrasia ya kweli, katika hatua hizi kwa kweli tunampongeza sana Mheshimiwa Rais. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nampongeza Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, nampongeza Makamu wa Rais pia, nampongeza pia Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi kubwa ambayo anaifanya, lakini zaidi ya hapo nazipongeza Kamati zote tatu kwa taarifa ambazo wameziwasilisha humu ndani na uchambuzi wa kina ambao wameufanya kwa kweli nazipongeza sana Kamati. (*Makof*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nimpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kweli hotuba alioitoa humu Bungeni *ime-set* viwango nya juu sana, kwa sababu *ime-covermaeneo* yote, imechambua kwa undani maeneo yote ambayo yamefanyiwa kazi. Hii ni ishara tu ya mwaka mmoja ya Serikali ya Awamu ya Sita mambo ambayo imeyatekeleza, tukiendelea hivi kwa muda wa miaka minne ijayo nchi yetu itapiga hatua kubwa sana. Kwa hiyo mimi nawapongeza sana, naipongeza sana Serikali kwa kazi kubwa ambayo wameifanyi hapa tulipofika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona miradi mingi ya vielelezo, tumeona miradi mbalimbali, huduma za jamii kila mahali, kila eneo limeguswa katika mwaka huu tunawapongeza sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo mambo ambayo yamebaki ni mambo makubwa ambayo ni ya muhimu katika maendeleo ya nchi yetu, ambayo naamini kwamba Serikali ya Awamu ya Sita inabidi itafute namna ambavyo tunaweza kufanya katika kutatua hizi changamoto. Changamoto ya kwanza ninayoiona ni tatizo la ajira kwa vijana wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi tuna tatizo kubwa la ajira, vijana wengi wamesoma katika vyuo vikuu, wamesoma katika vyuo nya kat, wengi wana elimu lakini ajira imekuwa ni changamoto. Hali hii tusipoichukulia hatua, tusipoitafakari tukaja na mikakati ya kutosha litakuja kuwa ni bomu kubwa ambalo halitaisaidia nchi hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nafikiri hiki ni kipindi pekee ambacho lazima tuangalie suala la ajira. Hili suala la ajira haliwezi kushughulikiwa na Serikali peke yake linahitaji sekta binafsi ambayo lazima iwe *very strong* ambayo ndiyo itaweza kuchukua vijana wengi wanaomaliza katika vyuo vyetu, tunahitaji kuwa na viwanda vingi na sekta mbalimbali zifanye vizuri ili ziweze kuajiri hawa vijana wengi ambao wamesoma katika taaluma mbalimbali.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali imeshasema tutatoa ajira zaidi ya 35,000, naipongeza sana Serikali kwa hatua hizo hongereni sana. Lakini hiyo itakuwa ni hatua moja, bado tunahitaji vijana wanaomaliza ni karibu takribani 90,000 mpaka 100,000 kwa mwaka, hiyo haitoshi. Pia sehemu wanayoenda kuajiri zaidi ni kwenye sekta ya Ualimu na Afya, zipo sehemu zingine, zipo taaluma zingine ambazo tunahitaji pia wawe na ajira, wanahitaji kutoa mchango mkubwa katika nchi yetu ambao bado ajira inaendelea kuwa tatizo. Kuna Wahasibu, kuna Wagavi, kuna Wahandisi, kuna Maafisa Utumishi na maeneo mengi kuna tatizo la ajira. Kwa hiyo, ninafikiri bado tunalo hilo tatizo ni lazima tulitafakari.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninashauri Serikali iangalie kwa namna ambavyo Mheshimiwa Waziri Mkuu ameratibu mambo mbalimbali, nashauri hata katika suala la ajira tuwe na mdahalo wa kitaifa wa kuzungumzia namna ya kutatua tatizo la ajira kwa vijana wetu ili kusudi Watanzania wote tushirikiane tuangalie kwa undani, tufanye nini ili kutoa ajira kwa Vijana wetu. Hiyo itatusaidia sana na tutaweza kujenga Taifa ambalo litakuwa linamanufaa na wataweza kufaidika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ambalo ningependa kuchangia ni mishahara kwa Watumishi wa Umma. Katika kipindi cha takribani cha miaka mitano au Sita Watumishi wa Umma hawakuweza kuongezewa mishahara kwa sababu Serikali ilikuwa haina na uwezo, naamini tumefika mahali ili Watumishi wa Umma hawa waweze kufanya kazi yao vizuri, waweze kutekeleza majukumu mbalimbali, waweze kusimamia mipango mbalimbali ambayo Serikali inatakiwa kutekeleza wanahitaji pia kupewa motisha ya kutosha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo, Serikali sasa hivi iangalie namna itakavyoboresha maslahi ya Watumishi wa Umma. Ninalisema hivyo kwa sababu maslahi ya Watumishi wa Umma yakiboreshwa, wakiwa na mapato ya kutosha hawa pia watatoa ajira, kwa sababu hela wanazopipata

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

wanaenda kuwekeza. Watawekeza kwenye kilimo, watawekeza kwenye miradi mbalimbali na ile miradi itatoa ajira kwa vijana mbalimbali. Kwa hiyo, zile pesa watakazipata maslahi yakiboreshw Watumishi wa Umma yataisaidia nchi katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Serikali sasa ifike mahali katika Bajeti hii iwafikirie Watumishi wa Umma wote kuongezewa mishahara yao na nyongeza zile zinazotakiwa na maeneo mbalimbali ili maslahi na mazingira ya kazi yawe mazuri, yakiboreshw mazingira ya kazi utendaji utakuwa mzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili ni la msingi kwa sababu sasa hivi huko nyuma tulikuwa tunasema mteja ndiyo mfalme, sasa hivi wanasema rasilimali watu ndiyo mfalme katika Taasisi. Kwa hiyo, ukiimarissha hawa Watumishi wa Umma ukawapa motisha vizuri watakafanya kazi vizuri, watatekeleza malengo vizuri na nchi itapiga hatua kubwa. Kwa hiyo, napendekeza tuliangalie kwa makini suala hili la maslahi ya Watumishi wa Umma katika ngazi zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napendekeza tunapoangalia maslahi ya Watumishi wa Umma tuangalie na sekta binafsi, sekta binafsi sasa hivi tuna takribani miaka zaidi ya 13, kile kima cha chini cha mshahara havijawahi kurekebishwa kile cha kisheria. kisheria kima cha chini sekta zote hakijawahi kurekebishwa. Toka kimerekebishwa wakati huo kumetokea mabadiliko mengi, mfumuko wa bei, *inflation rate* imepanda sana, ukiangalia *exchange rate*, maisha yamebadilika. Fedha ambazo wanalipwa wafanyakazi wanaofanya sekta binafsi ni kidogo sana haziwawezeshi kuchangia katika Pato la Taifa vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri ni vizuri Serikali sasa ikaangalia wafanyakazi wa sekta binafsi, na hasa kima cha chini cha sekta binafsi iwe ni kwenye kilimo, iwe ni kwenye uvuvi, iwe ni kwenye maeneo gani, maeneo yote ya sekta binafsi. Zipo sekta zaidi ya 12 ambazo tulipanga kima cha chini vya mishahara, sasa hivi kima cha chini sehemu nyingine

tulisema ni shilingi laki moja toka mwaka 2013, tulisema Laki Moja mpaka leo wanalipa shilingi 100,000, hadi shilingi 150,000 ni nani anayeweza kuishi kwa kwango hicho cha fedha? Ni wazi kabisa hawawezi katika kwango hicho cha fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ni vizuri Serikali sasa ikaliangalia hili ili hawa maslahi yao yakiimarika sekta binafsi ndipo uchumi wetu utaimarika, hawa watakuwa na uwezo wa kununua bidhaa zetu na wakinunua bidhaa zetu uchumi utakua.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi kunaweza kukawa na bidhaa, kunaweza kukawa na huduma lakini watu hawawezi ku-access hivyo kwa sababu hawana uwezo wa kumudu namna ya kununua hivyo vitu. Kwa hiyo, ni vizuri Serikali ikaliangalia hili suala la watumishi wa sekta binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo ningependa kulizingumzia ni kule Mkoani Songwe. Sasa hivi tunasema, bandari yetu hii, nchi nydingi zinatamani kuwa na Bandari kama ya Tanzania, lakini hazina hizo bandari. Sisi tunayo bandari na tuna maeneo mengi yenye bandari.

Mheshimiwa Naibu Spika, zaidi ya hapo, nchi ya Congo imeingia kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki. Nchi zote za Afrika Mashariki zinajialandaa sasa kufanya biashara ya *DRC*. Sehemu pekee ambayo tunaweza tukafanya biashara yetu vizuri ni kuangalia uwezekano wa kufungua Bandari Kavu pale Tunduma. Tukifungua Bandari Kavu pale Tunduma, itasaidia wale wa Congo, Zambia, Zimbabwe na nchi nydingine waweze kusafirishea mizigo yao kupitia *TAZARA* mpaka pale Tunduma halifu wanakuja kuchukua mizigo pale. Watafanya vizuri sana na uchumi wetu utaimarika vizuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nashauri Serikali, ni vizuri ikaangalia uwezekano wa kufungua Bandari Kavu lakini sambamba na hilo iimarishe *TAZARA* yetu. Sasa hivi *TAZARA* inafanya vibaya; na inafanya vibaya kwa sababu hatujaiipa uzito unaostahili. Hili shirika toka limeanzishwa ni la

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

nchi mbili; wenzetu upande mwingine inawezekana wasione manufaa ya kuimarisha hii *TAZARA*, lakini kwa nchi kama ya kwetu ambayo uzalishaji mkubwa upo kwenye Nyanda za Juu Kusini...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante kwa mchango mzuri, ahsante.

MHE. JAPHET N. HASUNGA: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, naipongeza Serikali kwa hatua zote hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Sasa namwita Mheshimiwa Mheshimiwa Abdul-Hafar Idrissa Juma, jilandae Mheshimiwa Ndaisaba na Mheshimiwa Deo Sanga.

MHE. ABDUL-HAFAR IDRISSA JUMA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuzungumza katika Bunge siku ya leo kuchangia bajeti hii ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuipongeza bajeti hii. Bajeti hii imeakisi mwelekeo wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi na inavyokwenda kutekelezeka kabla ya mwaka 2025. Ilani yetu imemelekeza kuendelea kutafuta ahueni katika kila nyanja katika Taifa letu. Yale ambayo yamesemwa na Waziri Mkuu, kuanzia yale yaliyotekelizwa na yale ambayo yamepangwa kutekelezwa katika bajeti hii, sina mashaka yoyote chini ya Mama Samia, mwaka 2025 Ilani ya Chama cha Mapinduzi itakuwa imetekelizuka sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuyasema hayo, yaliyozungumzwa katika bajeti hii, naomba nichangie kuhusiana suala la *TASAF*. Katika Jimbo langu la Mtoni, mimi ni mnufaika wa *TASAF* katika Shehia zote. Hivi karibuni Shehia mbili ambazo zilikuwa hazipo; Shehia ya Kwagoa na Shehia ya Sharifu Mussa zimeingizwa katika mradi huu

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda niishauri Serikali. Zipo changamoto katika kupata wanufaika wa *TASAF* katika maeneo yetu kwa sababu ya klijografia. Umaskini wa Zanzibar haufanani na umasikini wa mtu wa Kigoma. Umaskini wa Zanzibar haufanani na umasikini wa Tanga na maeneo mengine. Umasikini unapishana kutokana na mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa wasaidizi wetu katika *TASAF* kama watatafsiri mtu kumiliki *tvy*a chogo kule Zanzibar hafai kuwa katika *TASAF*, wanaweza wakakuta Wazanzibar wengi hawana sifa hiyo, lakini ni watu masikini ambao wanastahiki kusaidiwa na Mfuko wa *TASAF*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika jimbo langu, japo mchakato wa rufaa za *TASAF* unaendelea, lakini wapo ambao wameenguliwa kwa sababu vyoo vyao wamekuta kuna masinki.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda niwakumbushe wenzetu, sisi kule Zanzibar unaweza ukununua *TV* mpya, badala ya kuuza *TV* uliyokuwa nayo ukamgawia mtu ambaye unadhani anastahiki kugawiwa. Sasa mimi niwakumbushe wenzetu, umasikini huu unapishana. Nashauri wenzetu katika *TASAF*, wakiwa wanafanya tathmini ya kutafuta watu wenye kustahiki kusaidiwa na mfuko huu wa *TASAF*, waugawe umasikini kutokana na mazingira yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kwetu Zanzibar hatulimi. Ukimkuta mtu masikini hasa katika jimbo langu ni masikini kweli kweli, anahitaji msaada wa Serikali. Hatuna ardhi ya kulima, jimbo langu kwa ardhi ni ndogo. Ukikuta hana uwezo wa kufanya biashara, huyo anastahiki na *TASAF*.

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kushauri kwamba pamoja na mambo mazuri, wamechukuliwa baadhi yao, wanaendelea kupewa na wanufaika na msaada huu wa *TASAF* lakini mgawanyo wa masuala ya kuutafsiri umasikini, watafsiri umasikini kwa mazingira yake. Mazingira yanatofautisha umasikini wetu. (*Makofi*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia nizungumzie suala la UKIMWI katika bajeti ya Waziri Mkuu. Kwanza naipongeza Serikali yetu chini ya Mheshimiwa Mama Samia, wameendelea kuhakikisha upatikanaji wa *ARV* nchi nzima. Mimi ni Mjumbe wa Kamati inayoshughulikia masuala ya UKIMWI, hakuna mahali tulipokwenda tumekuwa *ARV* hazipatikani, zinapatikana kwa asilimia 100.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda katika bajeti hii tuendelee kuiboresha tuhakikishe zinapatikana mashine za kupima *viral load* katika maeneo yale ambayo yanatoa huduma *CTC*. Ili kupima ufanisi wa *ARV* katika mwili wa mtu ambaye anatumia vidonge hivi, ni lazima tupime virusi kwa kutumia *viral load*.

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo maeneo tumeyaona hayana mashine zenyeye uwezo wa kupima *viral load*. Katika bajeti hii ya Waziri Mkuu, mambo yake mazuri sana, lakini yaongeze nyama kwa kuhakikisha mashine za *viral load* zinapatikana. Tunatambua Tanzania wapo waathirika wa virusi vya UKIMWI takribani milioni 1.7, sasa kwa nini tusihakikishe tunakuwa na *viral load* zitakazowafanya wasihame kutoka eneo moja kwenda eneo lingine ili kupata huduma hii kwa ajili ya kusaidia wananchi wetu?

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naipongeza Ofisi ya Waziri Mkuu kwa dhamira ya kuongeza bajeti katika fungu la maendeleo kwa fedha za ndani. Hata hivyo naomba dhamira hii iendane na kutekelezwa. Mwaka wa fedha unaokwisha huu walitenge shilingi bilioni moja, mwaka huu wametenga shilingi 1,880,000,000, lakini shilingi bilioni moja iliyopita, changamoto ipo, hazijatoka zote. Sasa dhamira ni nzuri ya kuongeza bajeti, lakini dhamira iende ikatekelezeke ili wenzetu wa Tume ya Taifa ya Kupambana na Virusi vya UKIMWI wawe na uwezo wa kuhakikisha tunafikia zile 95 tano kufikia mwaka 2030. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie kwa kuzungumzia maradhi yasiyoambukiza. Nashauri tena jambo hili kuititia bajeti ya Waziri Mkuu. Maradhi yasiyoambukiza

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

kwa sasa ndiyo yanayoongoza kuua Watanzania. Maradhi yasiyoambukiza ndiyo maradhi ambayo yanafilisi familia zetu, maradhi yasiyoambukiza ndiyo yanayoleta unyonge kwa ndugu zetu. Sasa basi, ninaishauri sana Serikali yetu ione tunavyoweza kuanzisha Tume ya Kupambana na Maradhi Yasiyoambukiza kama ambavyo tumeanzisha Tume ya UKIMWI.

Mheshimiwa Naibu Spika, shilingi ngapi tunazipoteza kila siku kuhakikisha watu wenyewe maradhi ya figo wanasafishwa damu. Shilingi ngapi zinapotea kila siku watu kwa ajili ya kuchukua vidongo vya *pressure*? Maradhi yasiyoambukiza ni tabia zetu tu, namna tunavyoishi, namna tunavyokaa muda mrefu na kupigwa na viyoyozi mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiweza kuanzisha Tume inaleta hamasa na kuleta uelewa mkubwa kama Tume ya Kupambana na UKIMWI. Leo wote humu ndani tunajua namna gani virusi ya UKIMWI vinaambukizwa, lakini tukibainika tuna virusi vya UKIMWI, tuna amani na tunatumaini kwa sababu tunajua Serikali imeandaa dawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba Tume hii ianzishwe ili kuongeza hamasa na kutambua maradhi yasiyoambukiza.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya haya, naunga mkono hoja hii. Nashukuru sana (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Mheshimiwa Ndaisaba, jiandae Mheshimiwa Sanga.

MHE. NDAISABA G. RUHORO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa ya kuchangia hotuba ya bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakumbuka mara ya mwisho kuchangia kwenye Bunge hili ilikuwa ni siku mbili kabla wewe Mwenyewe Mheshimiwa Naibu Spika hujagombea na tukakuchagua kuwa Naibu Spika wa Bunge letu la Jamhuri

ya Muungano wa Tanzania. Hivyo nimeona ni budi niweze kusimama hapa nikupongeze wewe mwenyewe kwa ushindi mzito ulioupata pamoja na Spika wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hongera sana kwa ushindi mnono. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na pongezi hiso, naomba pia niweze kuchukua fursa hii kwenye dakika zangu za kuchangia kuweza kumpongeza Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutenga muda na kufika Mkoa wa Kagera siku chache zilizopita ambapo alitoa maelekezo mahususi yenye lengo la kuwasaidia wakulima wa kahawa kwenye Mkoa wa Kagera.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Kagera ni mionganini mwa mikoa ambayo wakulima wamekuwa wakidhulimiwa sana hasa wakulima wa kahawa. Kulikuwa na utitiri wa tozo mbalimbali ambapo mkulima wa kahawa anatozwa tozo 47; na matokeo ya tozo hizi ni kwamba mkulima alikuwa hanufaiki kabisa na zao lake la kahawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu alifika Kagera kwa maelekezo ya Mheshimiwa Rais, akafuta tozo 42 kati ya 47 na kubakisha tozo tano tu. Hongereni sana Waziri Mkuu na Mheshimiwa Mama Samia. Wakulima wa Kahawa Mkoa wa Kagera na Tanzania kwa ujumla tunaahidi kuiunga mkono Serikali ya Mheshimiwa Mama Samia, tunaipenda na tunaomba iendeleee kutuhudumia wakulima wa kahawa na kuhakikisha kwamba wakulima tunaendelea kunufaika na zao letu la kahawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbali na kuondoa tozo 42 kati ya 47, Mheshimiwa Waziri Mkuu alitoa maelekezo mahususi kwa Vyama vya Ushirika kuacha kwenda kuchukua mikopo ambapo mikopo ile mwisho wa siku inakwenda kulipwa na mkulima mwenyewe. Wakulima wa kahawa wanachokita, wanapoandaa mashamba yao, wanapopanda kahawa, zinakuja kutoa matunda baada ya miaka mitatu. Wakulima wanakuwa wamehenya kweli kweli, wanakuwa wameumia kweli kweli. Mkulima anachokitaka, anapovuna kahawa

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

yake, aende kuiuza kwa bei nzuri. Naendelea kuipongeza Serikali ya Mheshimiwa Mama Samia, imetujali sisi wakulima kwa kuondoa tozo hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na kuondoa tozo hizi ambazo zilikuwa zinawakandamiza wakulima, Serikali imeelekeza Vyama nya Ushirika viache kwenda kuchukua mikopo kwa lengo la kwamba mikopo hiyo ilipwe na mkulima ambaye anapolima kahawa yake wala hajui kwamba kuna mtu atakwenda kuchukua mkopo ili kahawa yake ndiyo ilipe ule mkopo. Maelekezo haya yametolewa, naomba Ofisi ya Waziri Mkuu iendelee kusimama maelekezo haya kuhakikisha kwamba wakulima wetu hawarudi kule walikotoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Mheshimiwa Waziri Mkuu ametoa maelekezo kwamba Vyama nya Msingi ndivyo viweze kusimamia uuzaaji wa kahawa; na vyama vyote nya Ushirika...

MHE. HUSSEIN N. AMAR: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

NAIBU SPIKA: Taarifa.

TAARIFA

MHE. HUSSEIN N. AMAR: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpe taarifa mzungumzaji kwamba Serikali hii ni ya Chama cha Mapinduzi chini ya Mheshimiwa Rais, Samia Suluhu Hassan. (*Makof!*)

MHE. NDAISABA G. RUHORO: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa nimeipokea na ndiyo maana nimeendelea kumpongeza Mama yetu tokea nianze kuchangia. Nakushukuru sana kwa taarifa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nielekeze mchango wangu kwenye Fungu Na. 65 ambalo linahusu Mfuko wa kuwezesha vijana na hasa kwenye mchakato mzima wa kuwezesha vijana kiuchumi.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi hii kwa mwaka, vijana wanaohitimu Vyuo Vikuu...

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa tuwe na utulivu kidogo ndani.

MHE. NDAISABA G. RUHORO: Mheshimiwa Naibu Spika, narudia tena.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. NDAISABA G. RUHORO: Najua ni kengele ya kwanza.

NAIBU SPIKA: Wewe endelea tu.

MHE. NDAISABA G. RUHORO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Vijana wanaohitimu Vyuo Vikuu kwa mwaka wengine wamesema ni 90,000 lakini wale wanaomaliza *Degree* peke yake ni 48,000 na matokeo yake ni kwamba namba yote hii inapomaliza Vyuo Vikuu inarudi mtaani bila ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona juhudzi nzuri za Ofisi ya Waziri Mkuu za kuhakikisha kwamba vijana hawa wanapotoka Vyuo Vikuu wanapatiwa ajira. Nimeomna ushirikiano baina ya Ofisi ya Waziri Mkuu pamoja na Vyuo Vikuu ambapo tumezemewa kwamba wahitimu zaidi ya 2,000 wameweza kupatiwa mafunzo mbalimbali ya ujasiliamali na hivyo kuwawezesha kuanzisha miradi mbalimbali ya kujajiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, natambua kwamba jukumu la Ofisi ya Waziri Mkuu ni pamoja na kutambua Makampuni ya Vijana na kushirikiana na PPRA na kusaidia makampuni haya kuyaunganisha na wazabuni wakubwa ili *tender* zinapokuwa zinatolewa vijana hawa na wenyewe waweze kunufaika na *tender* za nchi hii.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Manunuzi ya Mwaka 2011 imeelekeza kwamba makundi maalum wakiwepo vijana, wanufaika na asilimia 30 ya fedha zote za zabuni, lakini katika uhalisia wake ni kwamba vijana wanaojua mambo haya au waliofahamishwa juu ya fursa hizi ni wachache sana na matokeo yake vijana wengi hawana ajira, *tender* za nchi hii zinaendelea kutolewa kwenye makampuni ya nje na mengine ya ndani makubwa, vijana wengi wameachwa pembedi kwenye utaratibu huu na kwenye mfumo huu wa zabuni za nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama mfumo ukiwekwa vizuri na sheria hii ikasimamamiwa, tutawasaidia vijana wengi sana waweze kujajiri kwenye mfumo wa *tender*, yaani zabuni na wengine wataweza kufanya shughuli za kandarasi. Sasa hivi tumewaachia vijana wako mtaani, wanashinda *club house*, wanaikosoa Serikali na kukosoa chama chetu na kusema maneno yanayohusiana na mambo ya kupingapinga, lakini zipo fursa za *ku-drain* vijana wengi tukawaingiza kwenye zabuni baada ya kuwatoa mitaani na tukawawezesha vijana wetu kujajiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto kubwa iliyopo ni utekelezaji wa sheria ya kutoa fursa kwenye makundi maalum nchi hii. Naomba kuishauri Serikali na hususan Ofisi ya Waziri Mkuu, iweke utaratibu mzuri wa kwenda kusimamia sheria zinazolinda maslahi ya makundi maalum ili kila *tender* inayotolewa nchi hii, kuwe na utaratibu wa *tenderer* kutoa taarifa ni kikundi gani amekihuisha kwenye zabuni yake na amekilipaje? Hii itahakikisha vijana wetu nchi hii wananaufaika na zabuni zote zinatolewa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine, naomba Ofisi ya Waziri Mkuu iweke utaratibu maalum wa kukusanya taarifa na makampuni yote ya vijana kuhakikisha kwamba kila kampuni ya kijana iliyopo nchini hii inapata fursa hizi. Haya mambo hayafahamiki, vijana wetu hawanufaiki na hizi fursa, wapo kimya utadhani fursa hazipo, lakini zipo hazitangazwi.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante kwa mchango mzuri.

MHE. NDAISABA G. RUHORO: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Deo Sanga, jiandae Mheshimiwa Kunti.

MHE. DEO K. SANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia. Kwanza nianze sana kwa kumpongeza Rais wetu, Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri anayoifanya kuwaleta Watanzania maendeleo; akiwemo Mtendaji Mkuu, Waziri Mkuu, Makamu wa Rais, ni kazi nzuri sana ambayo inafanya kuwaleta maendeleo Watanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tuwe wakweli Waheshimiwa Wabunge, katika awamu zote ambazo nimekaa hapa Bungeni, hakuna kipindi tulichopata fedha nyingi katika Halmashauri zetu kama hiki. Tumepata fedha nyingi sana maendeleo. Ombi langu, sasa Waziri Mkuu yupo hapa, tumwambie Rais aende akakope tena fedha ili ziweze kujenga vyoo katika mashule yetu, ziweze kujenga nyumba za walimu katika maeneo yetu. Tumekosa nyumba na vyoo katika shule zetu na pia vifaatiba, Waheshimiwa Wabunge wamesema hapa, katika Vituo vya Afya, Zahanati na Hospitali ambazo zimejengwa. Sasa tukope fedha ili tutimize haya, shughuli ziweze kwenda vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ndugu zangu niwaambie, maendeleo yoyote hayawezi kwenda bila kukopa. Hayawezi kwenda. Hata mimi hapa mjasiriamali, nimekopa mabilioni ya fedha. Lazima ukope ndiyo shughuli zinakwenda. Kwa hiyo, lazima akope ili kusudi ziweze kufanya kazi za maendeleo katika maeneo yetu. (*Makofii*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na kazi nzuri inayofanywa na Rais, Waheshimiwa Wabunge hawa na Waheshimiwa Madiwani wetu imebidi tuunge mkono jitihada za Rais. Katika maeneo yetu na sisi tumefanya maendeleo katika majimbo yetu. Nikianza na mimi mwenyewe, nimeunga mkono kwa kujenga madarasa tisa hivi sasa ambapo sasa mengine wanapiga ripu, mengine wanaezeka na mengine yamekwisha. Madarasa tisa kwa pamoja. Madarasa hayo ni kama ifuatavyo: Shule ya Kitisi, madarasa mawili; Shule ya Mwembetogwa, madarasa mawili na ofisi; Shule ya Uhuru, madarasa mawili; Shule ya Ilangamoto, darasa moja; Shule la Kifumbe, madarasa mawili. Jumla madarasa tisa. Madarasa hayo yote yatafunguliwa mwezi wa Sita mwaka huu 2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, atakayefungua madarasa haya, wa Kwanza namwomba Mheshimiwa Bashungwa, Waziri wa TAMISEMI, aje afungue madarasa mawili na ofisi; Mkuu wa Mkoa, madarasa mawil; Mkuu wa Wilaya, madarasa mawili; Mwenyekiti wa TASAF wa Zanzibar, madarasa mawili ili Muungano uende vizuri. (*Makofi/Vigelegele*)

Mheshimiwa Naibu Spika, si hao tu, ASAS wa Iringa kutokana na jitihada za Rais ameunga mkono kwenye Jimbo la Makambako kujenga darasa moja katika Shule ya Magegere. Pia Mbunge mstaafu Haroun Mwambalali ameunga mkono kujenga darasa moja Majengo (Kilimahewa). Kwa hiyo, nawapongeza naomba kuititia kikao hiki Waziri mwenye dhamana wa TAMISEMI peleka barua kwa ASAS na Haroun kuwashukuru kwa kazi nzuri ambayo wameunga mkono jitihada za Rais. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niende kwenye changamoto kwenye Jimbo la Makambako. Changamoto ya kwanza, kuna tatizo la fidia katika eneo la Polisi, kuna wananchi pale wanapata shida sana, fedha zilikuja wakasema ni kidogo, tukaomba ziongezwe, fedha zile zikahamishwa zikapelekwa Wanging'ombe. Tunaomba wapewe ili kusudi waondokane na tatizo hili. Fidia ya pili, Idofu

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

kunatakiwa kujengwa *one stop center* wameshalipwa fidia shilingi milioni 800 bado sh.3,100,000,000/=. Ombi langu, tunaiomba Serikali ilete fedha ili waweze kulipwa wananchi hawa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha za kujenga mradi mkubwa wa *One stop center* zipo tayari, Benki ya Dunia ilikwishatoa muda mrefu zili-expire wamerudia tena. Tatizo la tatu ni fidia umeme wa upepo Makambako, wananchi wale walishalipwa bado ambao hawajalipwa, tunaomba kupitia *TANESCO* waweze kulipa ili wananchi wale waweze kuondoka maeneo ambayo yanahitajika. La mwisho, la nne, soko la Kimataifa, Serikali ilishalipa fidia bado wananchi 18. Kwa hiyo, tunaomba waweze kulipwa ili kusudi kero hii iweze kuondoka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la tano, wananchi wa Makambako wana matumaini makubwa juu ya miradi ile ya Miji 28. Tunaomba miradi hii imezungumzwa kwa muda mrefu sana. Ombi letu Wabunge tulioipitiwa na miradi hii ya Miji 28, tunaiomba Serikali sasa ifike mwisho miradi hii ianze ili wananchi waweze ku... (*Makofi*)

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante.

MHE. DEO K. SANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo lingine....

NAIBU SPIKA: Ahsante sana muda wako umekwisha.

MHE. DEO K. SANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, sekunde.

NAIBU SPIKA: Haya sekunde moja.

MHE. DEO. K. SANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho. Posho za Madiwani tunaomba ziongezwe. Madiwani

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

wanafanya kazi nzuri sana za maendeleo katika maeneo yetu, tunaomba posho zao ziongezwe. (*Makofî*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana.

MHE. DEO K. SANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, Liganga na Mchuchuma tunaomba pia liweze kushughulikiwa. (*Makofî*)

NAIBU SPIKA: Haya.

MHE. DEO K. SANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. (*Makofî*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kunti, jiandae Mheshimiwa Vita Kawawa.

MHE. KUNTI Y. MAJALA: Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipatia nafasi ili niweze kutoa mchango wangu kwa bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu ya mwaka 2022/2023.

Kwanza kabisa nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uhai na hatimaye leo tumekutana katika ukumbi huu tukizungumza maslahi mapana ya Taifa letu. Kwenye mchango wangu leo naomba kwanza nitajielekeza kwenye migogoro ya ardhi ndani ya Taifa letu. Nimshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu kwenye hotuba yake. Ukurasa wa 45(75) Ardhi, ametuambia naomba kunukuu: "*Ardhi ni rasilimali muhimu katika kukuza uchumi na kuondoa umasikini.*" Naomba niishie hapo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu kutambua kwamba ardhi ni rasilimali muhimu, lakini rasilimali hiyo muhimu inaweza ikuontoa kwenye wimbi kubwa la umaskini wa Watanzania tulionao. Hata hivyo, napata shida kidogo kama Serikali inatambua kwamba ardhi ni rasilimali muhimu na ndio kichocheo cha uchumi katika Taifa letu, ni kwa nini Serikali imekuwa na kigugumizi cha kutatua migogoro ya ardhi ndani ya Taifa letu? (*Makofî*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu imekuwa na migogoro mingi sana ya aina tofauti tofauti. Tumekuwa na migogoro ya mipaka, ya vijiji kwa vijiji, wilaya kwa wilaya, mikoa kwa mikoa, migogoro baina ya hifadhi na wafugaji, wakulima na wafugaji, wakulima na wahifadhi. Migogoro hii tumekuwa tukiisema kila siku. Tangu nimeingia Bunge la 11 nimekuwa nikisema suala zima la migogoro hii. Lakini nakumbuka bajeti ya mwaka 2017/2018 tuliambiwa Wabunge wote, tuainishe migogoro yetu tuliyonayo ndani ya majimbo yetu na ndani ya maeneo yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tuliorodhesha migogoro tukaletewa kitabu kimoja kikubwa sana kila Mbunge akapewa zaidi ya kurasa 1,000, tukijua kwamba Serikali imekwenda kutambua migogoro hiyo na inakwenda kuifanyia kazi. Sio hilo tu, baada ya hilo ikaundwa Tume ya Mawaziri Nane, Bunge lilllopita wakatumla hellkopta, kodi za Watanzania wakazunguka nchi hii nzima kwenye maeneo mbalimbali kupitia ile ripoti tuliyowapa. Mpaka leo ile ripoti iko chini ya uvungu, hajjawahi kutoka hadharani, hivi shida ni nini kwa Serikali Sikivu, inayowapenda Watanzania wake, kwenda kuwaondolea wananchi hawa migogoro ili twende tukakuze uchumi wa Taifa? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini sio hicho tu mwaka jana pia Tume hiyo hiyo ya Mawaziri Nane, wamezunguka tena nchi nzima kwenda kukagua migogoro. Walikotoka leo moto umewaka kuliko ilivyokuwa. Watu wanaauawa kisa ni mpaka wewe upo Wilaya A na mimi nipo Wilaya B yaani utafikiri sijui tupo Taifa gani hata Ukraine haipo hivyo. Hajjafikia namna hiyo katika suala zima la migogoro katika Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna Tume ya Matumizi Bora ya Ardhi ina zaidi ya miaka 10, lakini Tume hii hivi inafanya kazi gani? Ukija kwenye bajeti wanapewa mishahara, lakini tunaambiwa Tume hii kazi yake, ni kuratibu na kutoa mafunzo kwa Halmashauri zetu ili Halmashauri ziweze kutekeleza. (*Makofi/Kicheko*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, huwezi ukawa unatengea watu fedha kwa ajili ya kutoa mafunzo ya kwenda kutatua migogoro, badala ya kwenda kutoa fedha ya kwenda kupima ardhi ya kupanga, kupima na kumilikisha. Leo tunavyozungumza kuna ardhi ya wawekezaji wanatajwa sana. Mkulima leo ardhi yake hajulikani, mfugaji leo ardhi yake hajulikani iko wapi lakini maliasili (wanyama) ardhi yao inajulikana mahali ilipo. Leo mfugaji wa nchi hii mwenye ng'ombe 100, ng'ombe 200 hana tofauti na mtu anayemiliki bangi au madawa ya kulevya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo mfugaji wa Taifa letu ambapo pia kwenye hotuba ya Waziri Mkuu amekiri kwamba, tumeongeza pato kwa kusafirisha nyama nje ya nchi, maziwa pamoja na ngozi, lakini ukija kuangalia hali ya mfugaji wa Tanzania malisho anajitafutia mwenyewe, majosho anatafuta mwenyewe, madawa anatafuta mwenyewe, kila kitu anajitafutia mwenyewe. Leo ng'ombe wakitoka wamechunga kwenye Hifadhi, huyo mfugaji hataweza kumiliki chochote kwenye ile mifugo. Tulizungumza Bunge lililopita hata mwaka jana nilisema namna mfugaji wanavyomfanya katika Taifa hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mfugaji huyo huyo tukija hata kwenye shughuli zetu mbalimbali hata za Mwenge tu hizi Mheshimiwa Nusrat amesema, mfugaji huyu tunamfuata aweze kutuchangia kitoweo, lakini pili atoe na mchango wa mafuta ili Mwenge uweze kuzunguka ndani ya nchi yetu; na wakati Ole Sendeka anasema suala la Mwenge kwamba ulikuwepo na Mwalimu alisema kwamba utawashwa na nimsaidie tu hiyo nyingine ya kuzunguka ni ya kwake. Mwalimu alisema tutauwasha Mwenge na kuweka juu ya Mlima Kilimanjaro na sio kuukimbiza kuzunguka nao barabarani. (*Makofii/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mifugo ambayo wanachanga vitoweo kwa ajili ya kuzungusha Mwenge barabarani *brother pole* sana. Ahakikishe apambane apate hati miliki ya kuweza kumiliki ardhi yako ya kuchunga mifugo na ili aweze kupata tija ya mazao yake na mifugo na kujenga

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

uchumi wa familia yake na kipato chake na sio kutetea suala zima la kuzungusha Mwenge, anasema eti ni Mwalimu alisema. (*Makof/Kicheko*)

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, WENYE ULEMAVU (MHE PASCAL P. KATAMBI): Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

NAIBU SPIKA: Taarifa. Kaa chini kuna taarifa.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, WENYE ULEMAVU (MHE. PASCAL P. KATAMBI): Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumpa Taarifa mzungumzaji Mheshimiwa Kunti kwamba, Mwenge wa Uhuru katika azma yake ya kuanzishwa ilikuwa mwaka 1958 na katika azma ile ile ya yale yaliyoelezwa ni katika kuhakikisha kwamba kunakuwa na umoja, amani, upendo na mshikamano. Baada ya Uhuru mwaka 1961 tullyopata Uhuru Mwenge ule uliwekwa Mlima Kilimanjaro na baada ya hapo *purpose* yake tulipoingia katika Mfumo wa Vyama Vingi vya Siasa ulirithiwa na kuasiwiwa chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, kwa maana ya kwamba ukawa na jukumu sasa la kusimamia masilahi ya nchi. Mojawapo la kwanza, ni kuhakikisha unamulika masuala yote ya rushwa katika miradi ya maendeleo, unakwenda kufanya usimamizi kwa kufanya *monitoring* na *evaluation* katika miradi mikubwa ya maendeleo ya nchi hii. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha zote zinazotolewa katika bajeti ya Serikali hii pamoja na kuwa na Mfumo wa Kiserikali wa kiutawala kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, inahitaji kuwa na *overseeing body* au *institution*nyingine ambayo inakwenda ikiwa *independent* kama Mwenge wa Uhuru ambao wajibu wake unapokwenda katika maeneo hayo ni kuhakikisha kwamba, kama kwa mwaka wa jana tu Mwenge wa Uhuru uligundua miradi zaidi ya 46 yenye thamani ya fedha zaidi ya shilingi bilioni 40 na haya mambo yapo kwenye uchunguzi *PCCB* watachukua hatua. Kwa hiyo, kilichopo kwenye hii dhana... (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Ahsante amekuelewa. Haya Mheshimiwa Kunti, malizia dakika yako moja.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

MHE. KUNTI Y. MAJALA: Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri alikuwa na muda wa kuja kujibu hoja za Wabunge na huu haukuwa wakati wake. Pili, kwenye suala la ufisadi hiyo hiyo miradi tunayokwenda kuzindua na Mwenge bado tunakutana na ufisadi 150 kidogo. Kwa hiyo, naomba tu Mheshimiwa Waziri atulia muda wake utafika atajibu hoja za Wabunge wala asitake kupata kuwa na haraka. Naomba niendelee na mchango wangu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye suala la migogoro ya ardhi tuliyonayo leo viongozi wa Chama cha Mapinduzi ambaao wamepewa dhamana na Taifa hili; na watu wanaendelea kuumia na kupoteza maisha na mali zao kwa sababu ya kushindwa kufanya maamuzi ya kutatua migogoro kwa kwenda kusema kwamba wewe eneo lako ni hili na wewe eneo lako ni hili. Hawataki kuweka bayana hizo, hakika Mwenyezi Mungu atakuja kuwahesabu siku ya hukumu. Naomba niwashauri kwenye migogoro ya ardhi, cha kwanza Sheria ya Tume ya Mipango ya Ardhi imepitwa na wakati. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaiomba Sheria hiyo ije hapa tufanyie marekebisho ili Tume hii tuipe mamlaka ya kuweza kusimamia mpaka chini kwenye halmashauri zetu na kuweza kwenda kutatua hiyo migogoro. La pili, mamlaka zetu za halmashauri ambazo na zenyewe zinahusika kwenye suala zima la upimaji na upangaji na umilikishaji, twende sasa TAMISEMI tunawaomba sasa, waende wakatenge Mafungu kwa ajili ya suala zima la upimaji na umilikishaji wa ardhi kwa wananchi wetu na kwenda kuondoa migogoro. Suala la tatu...

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

NAIBU SPIKA: Kaa chini Kunti, muda wako umekwisha. Mheshimiwa Kawawa. (*Makof*)

MHE. VITA R. KAWAWA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa fursa hii ili niweze kutoa mchango wangu katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na Wizara zilizo

chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuwasilisha vyema Hotuba yake lakini pia, nawapongeza Mawaziri wote walio katika Ofisi ya Waziri Mkuu, Waziri wa Nchi, Sera, Uratibu na Bunge na Waziri wa Nchi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu, nawapongeza sana. Nchi yetu imekuwa ikifanya vizuri katika hatua za maendeleo pamoja na changamoto zinazotukabili za ndani ya nchi na nje ya nchi. Lakini bajeti hii iliyowasilishwa leo naamini itatuvusha. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Raymond utajiandaa, samahani nilikuwa sijakwambia.

MHE. VITA R. KAWAWA:itatusha na kutufikisha mahali pazuri. Kuna maeneo ya huduma za jamii tumepeiga hatua nzuri, lakini napenda kutoa ushauri pia kuna maeneo tunahitaji kuongeza juhudhi za kutosha, ili kuweza kusaldia mahitaji ya kufanikisha kwa ufanisi maendeleo ya huduma za jamii kwa wananchi wetu kama tulivyokusudia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, dunia imebadilika inakabiliana sasa hivi na changamoto kubwa ambazo na sisi zinatuathiri kiuchumi na kijamii. Hivyo, sisi kama nchi hatuna budi na sisi kukaza mkanda ili tuendelee kuwaendeleza wananchi wetu kiuchumi na kijamii. Katika kipindi hiki cha Serikali ya CCM Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan tumeona Serikali ikifanya mambo makubwa ya kuendeleza hasa miradi ile mkakati iliyoanzishwa, lakini kuanzisha miradi mipyä ya huduma za jamii. Shule zimeejengwa, vituo vya afya vimeejengwa, hospitali za wilaya na mikoa zimeejengwa na zinaendelea kujengwa. Miradi ya maji inaendelea kujengwa na kazi zingine zinaendelea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie fursa hii pia pamoja na miradi hiyo inayojengwa inahitaji watu wa kwenda kuifanya kazi. Kwa hiyo, naomba niishukuru Serikali kwa kauli yake leo iliyotoa hapa Bungeni kupitia Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama ya kuwa Serikali inategemea kutangaza ajira

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

32,000. Hii ni taarifa njema ni taarifa muhimu na yenyeye afya, kwani katika maeneo ya afya na elimu sasa hivi tunahitaji sana watumishi. Kama nilivyoeleza hapo awali tumejenga majengo ya afya, vituo vya afya, zahanati, hospitali za wilaya tunahitaji watu wa kwenda kutoa huduma na hili likikamilika dhamira ya Serikali ya kwenda kuwahudumia wananchi katika maeneo haya ya elimu na afya itakuwa imetimia. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ya afya ina unyeti wake inahitaji pia kufanyika uchambuzi wa kina ili kuangalia madaktari na madaktari bingwa, manesi na manesi bingwa wa maeneo yote, tunahitaji wangapi katika hospitali zetu na kwa sasa tunao wangapi? Ili kukidhi mahitaji hayo inatubidi tuchukue muda gani kuwapata hao wapya. Tukishajua hilo, tutaweza kupanga mkakati mahususi kabisa kwa ajili ya kuwatafuta na kuwapata hawa wataalam wetu. Wiki iliyopita nilisoma kwenye gazeti la Uhuru Mheshimiwa Waziri wa Afya alikuwa anaeleza kwamba tuna wataalam wa ubongo na wa mishipa ya fahamu 16 tu, lakini kwa *population* tuliyonayo sisi nchini takribani milioni 60 tunahitaji wataalam hao wawe kama 600. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tuna upungufu wa wataalam bingwa huo ni mfano tu. Kwa hiyo, hatuna budi tuweke mkakati mahususi wa kuona tunapataje wataalam bingwa kwa ajili ya kwenda kuhudumia wananchi wetu. Leo tumenunua vifaa vya kwenda katika hospitali za mikoa, hospitali za wilaya, tunahitaji watumishi ambao wataweza kuhudumia katika vifaa tiba hivyo. Pamoja na ajira mpya Serikali imetangaza leo, naomba iangalie pia na *replacement* za ajira za watu wanaokufa, wanaostaafu, wanaoacha kazi wenyewe, wanaofukuzwa kazi na *replacement* haiathiri *wage bill*. Kwa hiyo, Serikali iendelee kuangalia tunafanya *replacement* na eneo hili ndio tunalolipoteza sana la wataalam bingwa. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naishauri Serikali iangalie sana. Jana Profesa hapa wakati anauliza swali alitoa na pendekezo kwamba, wale wataalam/Madaktari Bingwa

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

tuwaongezee muda na tuna pengo kubwa la wataalam bingwa kama nilivyoeleza awali. Kwa sababu, pia tulisahau hii *replacement*. Kwa hiyo, tunaomba sana Serikali iangalie kundi hili pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la uzalishaji. Pamoja na kazi nzuri inayofanywa na Serikali hatuna budi kuedelea kuliangalia kwa karibu sana na kuliwezesha na kulipa fursa zaidi eneo la uzalishaji. Eneo hili tukiliangalia kwa karibu wananchi/wawekezaji watapata fedha na Serikali itapata fedha yake. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka jana nilitoa ushauri kwamba tunajenga *SGR Standard Gauge Railway*, lakini huko njiani kuna eneo kubwa sana ni porini. Nikasema sekta ya kilimo, sekta ya maliasili na sekta za viwanda zianze kufanya utafiti kuangalia maeneo gani inakopita hii reli kwenye mapori tunaweza tukapanda mazao ya miti. Pia, tunaweza tukaweka eneo la utafiti la kilimo. (*Makof!*)

NAIBU SPIKA: Malizia sekunde tano.

MHE. VITA R. KAWAWA: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. (*Makof!*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Raymond, tutamalizia Mheshimiwa Kiswaga.

MHE. SHALLY J. RAYMOND: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa nafasi hii. Kipekee namshukuru Mungu kwa zawadi ya uhai kwetu sote.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesimama hapa kuunga mkono hoja ya Waziri Mkuu na niseme kwamba, wasilisho lilikuwa makini na tumelielewa vizuri, ila kuna mambo machache. Niende moja kwa moja katika ule ukurasa wa 28 ambapo amezungumzia yale mazao ya kimkakati, katika zao mojawapo lilitotajwa pale ni zao la kahawa ambalo linalimwa Kilimanjaro na kwingineko. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nipayenda kusema kwamba, zao lile sasa ni kama halipo tena kwa sababu vitu vitatu ambapo kahawa inahitaji ni pamoja na maji ya kutosha, mbolea ya kutosha, lakini pia na ufanisi wa kusimamia. Ni bahati mbaya sana kwa ajili ya tabianchi ile mifereji ya asili sasa haipo tena na inahitaji ifufuliwe upya, lakini pia uoteshaji wa miti umekuwa hafifu ili maji yaendelee kutoka. Kwa hiyo, nimesimama kumuomba basi ili tunapoelekea kuweza kufufua tena kahawa wale Maafisa Ugani ambao wamepewa zile pikipiki juzi na Mheshimiwa Rais waweze kutembelea kaya kwa kaya ili waone kwamba, jambo hilo linafanyika. Nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa jambo hilo jema na zito, jambo la maendeleo, kwa kuwapa hao Maafisa Ugani pikipiki hizo ili waweze kuwatembelea wakulima hao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nikitoka hapo kwenye kilimo ningependa pia kuzungumzia mifugo. Toka niingie Bunge hili huwa kila nikisimama naomba wakati Marais wetu wanapokwenda nje waweze basi hata kutuombea sisi wanawake ambao tunafanya ufugaji wa *zero grazing* mitamba ambayo ni bora. Nakumbuka kabisa nikiwa mtoto Mwalimu Nyerere alikwenda huko Denmark, lakini pia Rais wa Kenya alikwenda na wa Uganda wote walikwenda safari mbalimbali, mitamba bora ikaja katika nchi zao tukaweza kupata *cross breeding* ya *high breed* kutoka katika ng'ombe wa jersey, phrasian, ng'ombe wakawa wanatoa maziwa bora sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati mbaya sana Kenya wanatoa maziwa mengi sasa hivi na wanauzia Tanzania, Uganda hali kadhalika, lakini Tanzania mazaiwa yetu ni kidogo pamoja na zile lita alizotuambia hapa leo asubuhi Waziri Mkuu katika ule ukurasa wa mifugo, lakini bado uzalishaji wa maziwa ni kidogo sana Tanzania. Kwa hiyo, ninaomba basi kwa wale ambao hawafugi ng'ombe wengi wa kuswaga wanawake wamekaa na wanawake wa Kilimanjaro wamenituma, ni lini watapatiwa mitamba bora kwa sababu, mtamba mmoja kutoka katika *ranch* ya Tanzania ni Shilingi Laki Nane, siyo rahisi kwa Mtanzania wa

kawaida kwenda kununua mtamba kwa Shilingi Laki Nane ni hela nyingi sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninaomba katika ule ukurasa wa kilimo wamezungumzia ushirika hiyo mitamba ipitishwe kwenye vyama vyetu nya ushirika kama zamani. Tukishapata ndama wakizalishwa ndama wazuri tunaambiwa kopa ng'ombe, lipa ndama kwa hiyo, tutarudi tena kule Mwalimu alikotuwezesha kulipa mitamba bora. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda pia kuzungumzia ule ugawaji wa ile asilimia 10. Tuna 4, 4, 2, lakini imekuwa ngumu sana kwa wale ambao wako kwenye vikundi kufaidika. Watu sasa Shilingi Laki Tano haitoshi kwa hiyo, kukopa kiasi cha Shilingi Milioni Mbili kwenye kikundi ni kitu kidogo, tumekiongea hapa, wenzangu wameongea kwa herufi kubwa, tulikuwa tunaomba sasa waruhusiwe kila mtu kukopa. Wakope na katika Wilaya ambazo zina hela za kutosha kama kule llala basi mtu aruhusiwe kukopa mwenyewe kutoka huko au agawiwe halafu arejeshe, kule ambako wapo wachache vikoba basi vipewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini imekuwa ni ngumu, wanawake hao wanapata mikopo kidogo sana. Makundi maalum, na ukikuta wenzetu ambao wana ulemavu wa viungo inakuwa ngumu, sasa wale wanakuaje kwenye kikundi? Tulikuwa tunaomba Serikali ikubali sasa watu wale wakopeshwe mmoja mmoja na arejeshe kama anavyopenda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna jambo moja ambalo linaniumiza kichwa na bahati nzuri niko kwenye Kamati ya Bajeti, zinaingia Wizara nyingi sana, lakini inaweza ikaingia Wizara wote ni suti, ni akina Baba tu mwanamke ni mmoja. Ninaiuliza Serikali ni lini italeta Muswada hapa Bungeni katika ajira za wanawake sasa ziwe hamsini kwa hamsini jumla? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, maana haiingii akilini tukianza chekechea tunaanza idadi moja wavulana na

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

wasichana, sekondari tunaenda pamoja, chuo kikuu tunaenda pamoja, inapokuja kwenye ajira wanaopata *promotion* au kuonekana wanaweza zaidi ni wanaume. Ni wapi hapo mnapotuacha? (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mkienda vitani, wanaume wakienda vitani wanakwenda na sisi tunabaki nyumbani tunachunga nyumba. Hata ile vita ya Iddi Amin tulioni, lakini wanaume wanakuja wanakuwa kwamba, wao ndio wawe kule kwenye, Wanajeshi wanasema *beret*, unapiga *beret*, sisi wanawake tuko tu chini. Imefika wakati sasa na ninamshukuru Mungu sana kwamba, tuna Rais mwanamke na tumeona wanawake wanaweza na wanaweza sana. Nasi sasa uletwe Muswada hapa waajiriwe hamsini kwa hamsini iwe ni kwenye ajira za Serikali... (*Makof!*)

NAIBU SPIKA: Malizia.

MHE. SHALLY J. RAYMOND: Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naona hilo jambo la hamsini kwa hamsini sasa lisiwe ni upendeleo ila lipite kisheria kabisa. *Fifty-fifty* ni wajibu wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (*Makof!*)

NAIBU SPIKA: Ahsante. Sasa mchangiaji wetu wa mwisho, Mheshimiwa Kiswaga.

MHE. BONVENTURA D. KISWAGA: Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi hii, ili niweze kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuipongeza Serikali inayoongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan pamoja na Mawaziri wake, lakini pia ninapojikita Ofisi ya Waziri Mkuu naomba nizungumzie uchumi kwa wananchi mmoja-mmoja wetu kwa sababu ndio tunaowategemea zaidi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi hii ardhi hatujaitumia kwa kilimo. Pamoja na jitihada mbalimbali ambazo zinafanywa na Wizara hii kubwa, tunapaswa tufikiri upya. Ardhi tuliyonayo yote inategemea mvua, lakini Mwenyezi

Mungu ametupa mito, ametupa maziwa, ametupa maji ya chini pia, lakini wananchi wetu wanakuwa na likizo ya miezi sita bila sababu, wakati Mtumishi wa Serikali anakuwa na likizo ya mwezi mmoja kwa mwaka. Ili kuinua uchumi wananchi hawa wanastahili kufanya kazi ikiwezekana miezi kumi ili wapumzike miezi miwili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tuna upungufu wa mafuta, lakini mazao ambayo yanasaababisha tupate mafuta yote tunategemea mvua, mfano michikichi, alizeti, pamba, yote inategemea mvua. Kwa hiyo, naomba ushauri wangu ni kwamba akili zetu zitumike, akili za watendaji zitumike na akili za viongozi zitumike.

Mheshimiwa Naibu Spika, mahali ambapo tuna mito, maji yatumike kwa ajili ya umwagiliaji ndiyo itakuwa mkombozi. Mahali ambapo hatuna mito tuna ziwa, millima itumike kutengeneza mabwawa juu ya mlima. Kama tunatengeneza matenki ya maji, tunashindwaje ku-pump maji kwenda mlimani na kushuka kwenye mashamba ambayo yako kwenye mwinuko hayo ya pamba, alizeti pamoja na michikichi, ili mwananchi aweze kuvuna mazao wakati wote? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo inapokosekana mvua mwananchi anapata hasara, Serikali inapata hasara, viwanda vinapata hasara kwa sababu vinakosa malighafi ya kuzalisha. Ajira inakufa, kodi inakosekana kwa hiyo, tufikiri upya kuona namna ya umwagiliaji tunaweza kuutumiaje? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mahali ambapo hakuna ziwa maji ya chini yatumike. Tunakwenda nchi za wenzetu zilizoendelea, mashamba yote kuna maji ya chini, maji yameelekezwa kwenye mashamba wananchi wanavuna masaa yote. Tubadilishe kilimo hiki kiwe kilimo ambacho wananchi kweli kinawasaidia, kwa sababu leo tunaweza kuwa tunalalamika mfumuko wa bei ni kwa sababu wananchi wetu hawana fedha, hawana kipato cha kukidhi kununua hayo mahitaji, kwa hiyo, tubadilike. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali hapa ije na mpango wa miaka mitano au miaka kumi kwa sababu jambo hili linahitaji fedha nyingi, lakini kama tutaendelea kutegemea mvua nataka nikuhakikishie hatutabadili kilimo chetu, tutapeleka pembejeo, tutapeleka mbolea, tutapeleka viuadudu, lakini kama hawana mvua ya kuivisha, hawana maji ya kuweza kuivisha, hawana maji ya kuweza kuivisha mazao, tunapiga kelele bure. Hatutakuwa tunasaidia wananchi. *Multisectoral/wenzangu sasa wafikiri hapa kwenye jambo hili ili waweze kuona nje ya box* kuhakikisha wakulima hawa tunawasaidia. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili. Serikali imewekeza kwenye vituo vya afya, lakini vifaa muhimu ambavyo vinahitajika bado hafijafika. Liangaliwe jambo hili kwenye bajeti hii ili tuweze kupeleka vifaa kuvipunguzia hospitali za Wilaya majukumu yake kwa sababu, kuna vitu ambavyo vinapaswa viishie tu kwenye vituo vya afya, kama Kituo changu cha Kisesa ambacho kwa kweli kinahudumia watu wengi ni kama hospitali ya Wilaya, Mheshimiwa Ummy ananua jambo hili, lakini kituo changu cha Rugeye, Mheshimiwa Ummy anajua jambo hili, kituo cha Kabilia, Mheshimiwa Ummy anajua jambo hili, Shishani kinachomalizika, Mheshimiwa Ummy anajua jambo hili. Kwa hiyo, Serikali ione namna ya kuweza kusaidia jambo hili liweze kwenda. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara zetu zitengenezwe. *TARURA* tuiongezee fedha kama ambavyo wengine wamependekeza. Huko huduma wanayohitaji wananchi ni kusafirisha mazao yao, kusafiri wakati wote. Uchumi tunaposema umekua siyo fedha mfukoni bali miundombinu ambayo inawawezesha kusafirisha bidhaa zao ndiyo inayohitajika kwa hiyo, kwa kazi ambayo mwaka jana tumeifanya na mwaka huu wa bajeti unaoendelea, tuongeze fedha kwenye *TARURA* ili tuweze kufungua barabara nyingi zaidi na wananchi wetu waweze kusafirisha mizigo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapohitaji kuendeleza nchi lazima sisi sote tuamue. Hili jambo si la Rais peke yake,

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

hili jambo ni la Watanzania wote. Kila mmoja mahali pake alipo tuamue kubadilisha mawazo yetu ili kuwahakikishia wananchi tunawasaidia kweli. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, wachangiaji wa leo wote wameisha. Kuna changamoto ya Ofisi ya Bunge kupokea majina ya wachangiaji Ofisi ya Waziri Mkuu na agizo lilitotoka ni la kuchangia kuitia mtandao. Mpaka sasa hivi Wajumbe ambao wamepitia kwenye mtandao ni wachache sana, niombe wote wenye azma ya kutaka kuchangia Ofisi ya Waziri Mkuu ambayo inaanza leo mpaka tarehe 13 waingie kwenye mtandao wa Bunge na muorodheshe majina yenu. Kwa idadi ambao wamechangia leo na tukichangia Ijumaa kwa idadi hili, bado ni Wabunge wachache sana. Kwa hiyo, tuombe wote ambao wana hoja za ofisi hii basi mchukue hiyo tahadhari.

Waheshimiwa Wabunge, ninawashukuru kwa michango mizuri. Ninawashukuru sana kwa kazi nzuri iliyofanywa na Serikali. Naahirisha Shughuli za Bunge mpaka siku ya Ijumaa, tarehe 08, Saa Tatu Asubuhi.

*(Saa 11.56 Jioni Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Ijumaa,
Tarehe 8 Aprili, 2022 Saa Tatu Asubuhi)*